Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 23 Mei, 2014

Mkutano Ulizana Saa TAtu Asubuhi

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):

Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa za "*LAPF Pensinon Fund*" kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 *(The Annual Report and Audited Accounts of Local Authorities Pension Fund for the Financial Year* 2011/2012).

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

NAIBU WAZIRI WA UCHUIKUZI:

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi, ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaanza na maswali na Ofisi ya Waziri Mkuu. Atakayeuliza swali letu la kwanza kwa leo ni Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa.

Na. 110

Tatizo La Maji Kata ya Mwabomba

MHE. RICHARD M. NDASSA aliuliza:-

Kata ya Mwabomba yenye Vijiji Vitano (5) vya Ngogo, Mwangika, Chamva, Mwabomba na Mhulula, haina hata kisima kimoja cha maji ya kunywa kinachofanya kazi, hali inayosababisha usumbufu mkubwa kwa Wananchi hao hasa ukizingatia uwezo wa Halmshauri ya Kwimba kuwa mdogo kutatua tatizo hilo.

Je, Serikali ina wasaidiaje wananchi wa Kata ya Mwabomba ili waondokane na adha hiyo ya ukosefu wa maji?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika ninakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kuwa hali ya upatikani wa huduma ya Maji Safi na Salama katika Kata ya Mwabomba, siyo ya kuridhisha. Takwimu zinaonyesha kuwa ni asilimia 24 tu ya Wakazi wa Kata hii, ndiyo wanaopata huduma ya Maji. Kwa kutambua tatizo hilo, Serikali imeanza kuchukua hatua zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014. Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba kwa kushirikiana na Taasisi ya *Rotary Club* ya Uholanzi, wamechimba na kujenga visima viwili vyenye dhamani ya Shilingi milioni 10,000,000/= katika kijijiji cha Mabomba.

Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Halmashauri kupitia vyanzo vyake vya ndani, imepanga kutumia shilingi milioni 8,000,000,000/= kwa ajili ya kuchimba visima viwili vifupi katika kijiji cha Ngogo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, kwa mwaka wa 2014/2015, imeidhinishiswa shilingi bilioni 2.5 kwa ajii ya utekelezaji wa Miradi ya maji kwa kuzingatia vipaumbele vilivyowekwa. Azma ya Serikali ni kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma ya maji karibu zaidi ili kuwaondolea adha ya kufuata huduma hiyo katika umbali mrefu.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, lakini inawezekana Mheshimiwa Waziri hakupata taarifa kamili kwa sababu mnapo sema asilimia 24 (24%) siyo kweli. Sasa ninaomba taarifa muende mzipate vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninaomba uniruhusu, niishukuru sana Serikali, kwa kukamilisha ile Miradi mitano ya uchimbaji wa visima katika Jimbo langu la Sumve, ninaipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ufumbuzi wa maji katika Wilaya ya Kwimba, hasa Jimbo la Sumve, ni maji kutoka Ziwa Victoria peke yake. Kwa sababu pesa hizi zilizotengwa hizi ni pesa kidogo, Shilingi milioni 8,000,000/=. Shilingi milioni 10,000,000/= ni pesa kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha kwamba vijii hivyo nilivyovitaja hivyo, vinapata maji ya kutosha kutoka Ziwa Victoria, kwa sababu mpango upo. Ninaomba Serikali itueleze ni mpango upi sasa, na pesa kiasi gani zimetengwa, kwa ajili ya mradi wa maji wa Ziwa Victoria?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Richard Ndassa, kama hivi ifutavyo.

Ni kweli mpango huo upo, na nia ya Serikali ni kufikisha maji ya kutoka Ziwa Victoria, kupitia Magu mpaka Kwimba, na zimetengwa shilingi 4,000,000,000/= katika mwaka huu wa fedha.

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Tanzania nzima tunayo matatizo makubwa sana ya maji. Lakini ninaomba nijielekeze kwenye Mradi wa Maji Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Serikali imejitahidi kuhakikisha kwamba wananchi wa Dar es Salaam wanapata maji. Lakini katika Mradi ule wa Ruvu Chini, mpaka sasa hivi wamesambaza mabomba kwa muda mrefu sana na wananchi wanasema mabomba yamesambazwa lakini bado hakuna maji hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini tatizo la maji, katika mkoa wa Dar es Salaam, hususan Wilaya ya Kinondoni, litapatiwa ufumbuzi na Serikali?

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, nafikiri utakubaliana na mimi hilo ni swali jipya kabisa? Mheshimiwa kwa sababu Dar es Salaam ni Dar es Salaam basi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Lyimo, kama hivi ifuatavyho. Ni kwei liko tatizo la maji. Lakini leo tutatoa taarifa hapa Bunge, kauli ya Waziri, kuhusu gatizo la maji Dar es Saam. Lakini pia ni kwamba ipo mipango ambayo inaendelea na ulazaji wa bomba umefika maeneo ya Tegeta.

Kwa hiyo, Mradi ule utakamilika mwezi Juni, 2014. Lakini Miradi mingine ya Ruvu Juu, inaendelea pamoja na kuchimba visima, ili kuondoa tatizo la maji kabisa katika Jiji la Dar es Salaam.

SPIKA: Ndiyo iko kauli ya Waziri wa Maji na imepangwa katika *Order Paper* ya leo.

Na. 111

Tatizo la Maji Tarafa ya Wang'ing'ombe

MHE. NEEMA HAMID MGAYA aliuliza:-

Je, ni lini tatizo la maji kwenye Tarafa ya Wang'ing'ombe litakwisha?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALAZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Hamid Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama hivi ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Wang'ing'ombe ina jumla ya vijiji 44 vyenye wakazi wapatao 65,226 kati yake ni wakazi 37,629 wanapata huduma ya Maji safi na salama ikiwa ni sawa na asilimia 57.

Wananchi hao wanapata huduma ya maji toka kwenye miradi ya msereereko inayotumia vyanzo viwili vya kutoka Mto unaoitwa Mtego wa Mbukwa na Mtitafu wa Visima virefu vyenye pampu za mikono miwili katika kijiji cha Uhenga.

Pia Mradi wa maji ya kusukuma na Mashine ipo mitatu (3) katika vijiji vya Makondo, Idenyimembe na Lyadembwe.

Mheshimiwa Spika, kwakutambua tatizo hili, Serikali, imeanza kuchukua hatua zifuatazo. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya shilingi 380,000,000/= zilitengwa kwa ajili ya uboeshaji wa miundombinu ya maji, katika mradi wa Wanging'ombe na Masaulwa. Shlingi milioni 100, zilitumika kukarabatai miradi ya Wanging'ombe na shilingi 280,000,000,000/= zilijenga Mradi wa maji wa Masaulwa.

Mheshimiwa Spika, Mradi mingine inayoendelea kutekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 ni ya vijiji vya Isimike, Igenge, Idenyimembe na Wangama yenye thamani ya shilingi 886,593,887.20. Miradi hiii imefikia hatua mbalimbali ya utekelezaji na inatarajiawa kukamilika mwezi Juni, 2014.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 jumla ya shilingi 418,233,000,000/= zimtengwa kwa ajili ya kuendeela kuboresha hudma za maji, katika Tarafa ya Wangiong'omb ambapo vijiji vya Malangali na Isindagosi vyenye jumla ya wakazi 3,309 vitanufaika.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine yaliyobaki, yayaendelea kujengewa miundombinu ya maji kwa kadiri rasilimali fedha itakavyokuwa inapatikana.

MHE. NEEMA HAMID MGAYA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri. Ninayo maswali mawili ya nyongeza.

(i) Wilaya yetu ya Wang'ing'ombe ni Wilaya mpya. Kwa kuwa Wilaya hii ni mpya na matatizo ya Maji yako kwa kipindi kirefu sasa, nilitaka kusikia sauti ya Serikali, kutaka kujua itasaidia vipi, Wang'ing'ombe kutatua tatizo la maji kwa kupitia mradi mkubwa wa kitaifa wa maji na Matokeo ya Haraka Sasa *(GRN)?*

(ii) Kuna Mradi ulioanzishwa mwaka 1976, na *UNICEF,* Mradi ule haujawahi kukarabatiwa, wala kupanuliwa miundombinu yake. Kwa sababu kadiri siku zinavyozidi kwenda watumiaji wa maji wanaongezeka. Kuna Kata mbili ambazo zina shida sana ya Maji. Kata ya Saja ya Kijombe. Kwa kuboreshwa kwa Mradi huu, tutaweza kuhudumia viiji vingi sana vilivyopo katika Kata hiyo. Kwa sababu shinda ya maji, hasa iko kwenye Tarafa ya Wang'ing'ombe.

Mheshimiwa Spika, naomba majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Neema Hamid Mgaya, kama hivi ifutavyo.

Mheshimiwa haya majina haya, wewe utakuwa unayafahamu, ni ya kule kwako waliko meguka ndiyo waliokwenda Wanging'ombe, kwa hiyo unayafahamu vizuri. Yananipa tabu hapa kuyatamka, ni majina magumu ya Kihehe.

Mheshimiwa Spika, lakini la kwanza ambalo nilitakakusema, ni hii, Mheshimwia Mbunge ana *underscore point* ya msingi, na asubuhi tumeii-*discuss.*

Mheshimiwa Spika, Wanging'ombe ni Wilaya mpya, imeanza juzi juzi tu. Bajeti yake hii iliyopia hapa walikuwa na shilingi 239,000,000/=. Hivi imepanda imekwenda kwenye milioni 418,000,000/=.

Lakini kuhusu mipango hii inayozungumzwa hapa wanayo barua na Halmashauri zote nchini, zimeandikiwa barua na Waziri wa Maji. Naibu Waziri yuko hapa anafahamu, zikielekezwa kwamba waende kwenye *commitments* zao kama walivyokuwa wame-*plan,* bila kujali kwamba hicho kiasi walicho nacho hawana.

Kwa maneno mengine sasa hivi, wanayo *commitment* ya shilingi 889,000,000/= kwa ajili ya Miradi mbalimbali, ambayo iko katika Halmashauri yao. Kwa hiyo ninamwomba Mheshimiwa Mgaya, afuatilie ile. Nina *appreciate,* ninakubaliana naye ya kwamba Halmashauri hizi changa unatakiwa uzibebe kama unavyobeba mototo wa mwisho pale nyumbani, mdogo unamwangalia. Ndicho anachokisema Mheshimiwa hapa. Ambaye mimi ninampongeza kwamba analiona hilo yeye na Mheshimiwa Lwenge, wanahangaikia katika hali hii. Sisi tutakwenda kuangalia.

Mheshimiwa Spika, ametaja huu mradi mwingine hapa ulioanza mwaka 1976 ninakuomba Mheshimiwa Spika, nitafutilia Mradi huu wa karibu. Kwa sababu amesema umekaa muda mrefu na hakuna jambo lolote ambalo limefanyika pale. Hili ni suala la *priorities.* Lakini tutakwenda kuangaia sisi na yeye ili tuone tatizo hili linaondolewa.

MHE. SAID M. MTANDA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nifahamu nikwka nini Bunge na Serikali linafanya maonyesho ya kumwaga maji hapo nje. Wakati Jimbo langu Mchinga, hasa kiiji cha Lihimilo hakina maji?*(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, wanamwaga waoi?

Mheshimiwa Mbunge rudia swali lako, sijalisikia vizuri.

MHE.SAID M. MTANDA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, nirudie tena swali dogo la nyongeza. Nilitaka kufahamu kila siku nikiingia hapa Bungeni. Bunge na Serikali, inafanya maonyesho ya kumwaga maji hapo nje.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nijue ni kwa nini Serikali inafanya maonyesho ya kumwaga maji pale nje, wakati Jimbo langu hasa kijiji cha Lihimilo na kijiji cha Kitohavi havina maji? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, basi na teknolojia hujui. Hayamwagiki, yanazunguka pale pale. *(Kicheko/Makofi)*.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, kijiji cha King'ombe, kimepata mradi wa kupelekewa maji, na kimepata pesa. Lakini kutokana na ushauri mbovu wa Mhandisi Mshauri, wananchi wamekwama kupata maji safi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba maji yanapelekwa katika Kijiji cha Kinng'ombe?

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, hicho kijiji cha King'ombe kiko wapi?

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, kiko Wlayani Nkasi.

SPIKA: Sasa mnafikiri kuuliza maswali namna hiyo, swali hilo lifanana na swali la msingi? Maana huyu alikuwa anauliza Wang'ing'ombe. Mheshimiwa Waziri kama unavijua vijiji hivyo jibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deusderius Mipata, kama hivi ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, hiki kitu anachokisema hapa. Yaani hapa wameingia mkenge hapa.Ndicho anachokisema hapa. Kwa sababu tatizo hili linatokana na mtu anayeitwa *Consultant*.

Mheshimiwa Spika, na kwamba wamefika mahali hakuna namna. Hela zimekwenda kulej, zimepelekwa kule hizo hela. Ninachotaka kusema hapa, na huyo *Consultant* na *who ever*. Aliyehusikanajambohilo, mimi tushiriiane na Mbunge hapa, aniambie kwamba ilikwendakwendaje. Haiwezikani tupeleke kule halaafu tunakuja hapa tuaambiwa kwamba kuna tatizo limetokea kwa sababu ya Mshauri aliye jitokeza pale.

Mheshimiwa Spika, mimi ninamwomba huyo anaye nisikiliza, nisemayo anisikilize vizuri. *We shall never live a stone un turned*. Kama pesa zilikwenda lazima tuhakikishe kwamba zilitumika kama zinavyotakiwa. Sauti hii ni msisitizo tu. *(Makofi)*

Na. 112

Hitaji la Umeme Mbeya

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA (K.n.y. MHE. JOSEPH O. MBILINYI) aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Kata za Iduda, Isyesye, Itende, Tembela, Mwansanga, Mwansekwa na Iziwa zilizoko Jijini Mbeya ambako Wananchi walishafanya *wiring* kwenye nyumba zao kwa zaidi ya miaka nane (8) sasa? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kazi ya kupeleka umeme katika Kata ya Isesye na Itende imetekelezwa kupitia mradi wa kusambaza umeme uliogharamiwa na Serikali kupitia *MCC*. Mradi huo umetekelezwa na Mkandarasi aitwaye *Symbion* na umekwishakamilika kwa asilimia 100.

Kazi zilizofanyika ni: Ujenzi wa nia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomia 2.4. Ujenzi wa njia ya umeme yenye msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 22.95, kusimika *transfoma 4* na kuwaunganisha wateja wa awali 1,076. Mradi umegharimu shilling milioni 803.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya kupeleka umeme Kata ya Idunda, Mwasekwa na Iziwa imejumuishwa katika Miradi ya *TANESCO* ya kupeleka umeme katika maeneo ya Idunda, Igawilo, Itagha, Hasanga, Iweambala, Itanji, Utukuyu, Mwasenga, Itengano na Iziwa.

Miradi hiyo inajumuisha; Ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 16.5; ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 11 yenye urefu wa kilomita 13; ujenzi wanjia ya umeme wa msongo wakilomita 0.4 yenye urefu wa kilomita 26; kufunga transfoma tano (5) na uwaunganisha wateja wa awali 2,335.

Gharama ya Mradi zinakadiriwa kuwa shilingi bilioni 1.299, utekelezaji wa Mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2014.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* imeanza kufanya upembuzi yakinifu mwezi Mei, 2014 katika Kata ya Tembela na Mwasanga, hususan mitaa ya reli na Tembela (Kata ya Tembela); na Isoso na Nduguya (Kata ya Mwasanga) ambayo haina umeme ili kupata gharama za utekelezaji wa Miradi wa Umeme katika Mitaa hiyo ili iweze kuombewa fedha mwaka wa fedha wa 2015.

MHE. MCH. PETER S. MSINGWA: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Wizara kwa kuwa imetekeleza maeneo mbalimbali na utendaji makiniwa Mheshimiwa Sugu katika Jiji la Mbeya.

Mheshimiwa Spika, ningeliomba nipate uhakika wa Wizara, haya maeneo ambayo wanesena yanafanyiwa umbembuzi yakinifu, ni lini hasa wakazi wa Jiji la Mbeya wategemee kwamba maeneo haya yatapata umeme. Maeneo ya Isoso, Kata ya Tembela na Kata ya Mwasaga?

Lakini la pili, maeneo haya yanafanana sana na Manispaa ya Iringa Kata ya Nduli, maeneo ya Kigonzile, Mtalagana na maeneo ya Sakalilo. Wananchi wamekuwa wanaomba umeme kwa muda mrefu sana, lakini hawajawekewa.

Ni lini sasa Serikali ukizingatia Jiji la Mbeya pamoja na Manispaa ya Iringa ni miji inayopanuka kwa haraka na yana wakazi wengi wasomi na wengine wanasoma pale. Yatapata umeme maeneo yote hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana!

SPIKA: Haya, majibu Naibu Waziri wa Nishati na Madini!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, kama ifuatavyo.

Kama nilivyojibu swali la msingi lini hasa katika Mji wa Mbeya ni kwamba tumesema tunafanya upembuzi yakinifu kuanzia Juni na tutahakikisha kwamba Bajeti ya *TANESCO* ambayo inaanza Januari, 2015 hadi Desemba, 2015 inayajumuisha maeneo hayo.

Lakini kuhusu Kata ya Nduli na Kigonzile katika Mji wa Iringa, nieleze tu kwamba *TANESCO* ina mpango maalum sasa hivi wa kupeleka umeme katika miji. Lakini changamoto inayotukumba maeneo mengi katika miji yetu hayakupimwa.

Kwa hiyo, tunashirikiana pamoja na TAMISEMI kuona ni kwa namna gani tunaweza kupeleka umeme katika maeneo hayo kwa sababu huwezi kutoa nyaya kutoka hapa ukapitisha juu ya nyumba ya mtu. Lakini kama tutashirikiana na wenzetu wa TAMISEMI tutahakikisha kwamba umeme umepelekwa sasa katika maeneo yote ya mijini. Tayari *TANESCO* imeshajipanga na imechukua mkopo wa shilingi bilioni 2,058 ili kuhakikisha kwamba tunapeleka umeme katika maeneo yote ya mijini.

SPIKA: Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale!

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa vijiji hivi vyote ambavyo vimetajwa katika swali la kwanza la msingi vinapakana na vijiji vilivyopo Mbeya Vijijini. Kwa mfano, kijiji cha Iduda kiko jirani na kijiji cha Ifiga na Nzongwe Juu. Ni kwa nini basi hata vijiji hivi vilivyopo Mbeya Vijijini visipewe umeme?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Nadhani umemwelewa Mehshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, jibu kwa kifupi!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri vijiji vya Mbeya Vijijini vipo katika mpango wa *REA*. Kwa hiyo, haya niliyozungumza ya Mbeya Mjini, ni kwa ajili ya miradi ya mjini. Lakini vijiji alivyovitaja vipo katika mpango wa *REA* na utatekelezwa katika mradi wa *REA* Namba Mbili.

SPIKA: Ahsante sana, tunaendelea na swali linalofuata Mheshimiwa Highness S. Kiwia!

Na. 113

Utekelezai wa Mradi wa Umeme wa MCC na REA

MHE. HIGHNESS SAMSON KIWIA aliuliza:-

Mradi wa umeme wa *MCC* ulipaswa uanze kutekelezwa katika Kata za Buswelo, Sangabuye na Kata ya Nyakato, lakini haujatekelezwa hadi sasa licha ya ahadi mbalimbali za Serikali za kutekeleza mradi huo.

(a) Je, ni lini utekelezaji wa Mradi huo kwenye Kata zilizotajwa utaanza kutekelezwa?

(b) Je, ni lini Mradi wa Umeme wa *REA* utaanza kutekelezwa kwenye maeneo ya Kata ya Bugongwa na vijiji vyake?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Highness Kiwia lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme Kangae, Kata ya Nyakato na kwenye Kata ya Buswelu ulifanyika chini ya miradi ya *MCC* na ulikamilika mwezi Agosti, 2013. Kazi za mradi huu zilihusisha ujenzi wa njia ya umeme wa kilovoti 11 yenye urefu wa kilomita 4.2, ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovolt 0.4 yenye urefu wa kilomita 19.36, ufungaji wa *transformer 3* na kuunganisha wateja wa awali wapatao 218. Gharama ya mradi huu ilikuwa ni dola za Kimarekani 481,625.13.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme kwenye Kata ya Sangabuye chini ya miradi ya *MCC* ulikamilika mwezi Aprili, 2013 na ulilenga kusambaza

umeme katika eneo la Kayenze na Kitongoji cha Lutongo. Kazi za mradi huu zilihusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovolt 33 yenye urefu wa kilomita 20, ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovolt 0.4 yenye urefu wa kilomita 4.6, ufungaji wa *transformer* 2 na kuunganisha wateja wa awali 67. Gharama za mradi huu zilikuwa ni dola za Marekani 7,049,643.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mradi wa kupeleka umeme katika Kata ya Bugongwa na Sangabuye kupitia mpango kabambe wa umeme vijijini awamu ya pili chini ya Wakala wa Nishati Vijiji *REA*. Mkandarasi anayetekeleza mradi huu ni *China Hanen International Cooperation Group Co. Ltd* ikishirikiana na *China National Electric Wire & Cable Imp/Exp. Corp.* Mradi huu ulioanza kutelekezwa mwezi Aprili, 2014 utanufaisha maeneo ya vijiji vya Kabangaja, Nyafula, Sekondari ya Bugongwa na Sangabuye na kituo cha Afya cha Sangabuye.

Mheshimiwa Spika, kazi za mradi zinazojumuisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovolt 33 yenye urefu wa kilomita 11, ujenzi wa njia ya umeme wa kilovolt 0.4 yenye urefu wa kilomita 12, ufungaji wa transformer 6 na kuwaunganishia umeme wateja wapatao 324. Miredi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2015 kwa gharama ya shilingi milioni 675,876,606.13.

Kwa sasa survey imekamilika na michoro kwa ajili ya ujenzi na njia ya umeme inaandaliwa. Uchimbaji wa mashimo pamoja na usimikaji wa nguzo utaanza kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2014.

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Highness Kiwia, swali lingine la nyongeza.

MHE. HIGHNESS SAMSON KIWIA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza niipongeze Serikali na Wizara kwa ujumla kwa kazi nzuri inayofanya katika Jimbo langu la Ilemela kusambaza umeme katika maeneo mengi ya Jimbo la Ilemela.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa umeme wa MCC kwa sehemu kubwa sana umefanyika katika Kata ya Sangabuye, Bugogogwa na Buselwa lakini hususani katika maeneo ya center ya Kata hizo na kuacha maeneo mengi ya pembezoni bila umeme hususani hususani huduma muhimu kama za afya na elimu.

Sasa naomba kujua kwamba Serikali na Wizara kwa ujumla, sasa iko tayari kushirikiana na *TANESCO* na kuingiza vijiji hivi na maeneo haya muhimu ya pembezoni ambako mrdi wa *MCC* umeishia katika *REA* awamu ya pili na kwa ajili ya kuhudumia wananchi wa maeneo hayo?

Pili, ninapenda kujua mradi huu wa *REA* unaotekelezwa kwenye Kata ya Sangabuye pamoja na Bugogwa na vijiji vyake ni lini utakamilika hasa kwa kuzingatia kwamba maeneo mengi tayari yamejiandaa na yako tayari kwa ajili ya huduma hiyo hasa maeneo ya Nyafra, Bugogwa, Ilalila, Masemele, Igogwe na Malinganya. Naomba kujua kwamba miradi hii ya *REA* itakamilika lini katika maeneo hayo husika?

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Highness Kiwia, kama ifuatavyo;

Kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi *REA* awamu ya pili itaangalia vijiji alivyovitaja ili tuone ni kwa namna gani na vyenyewe vinaweza kuuunganishwa ili na wenyewe waweze kupata umeme ndugu zangu wa Wilaya ya Ilemela.

REA Sangabuye na vijiji vingine ni lini, nimesema katika jimbu langu la msingi kwamba mradi huu utakamilika tarehe 30 Juni, 2015.

SPIKA: Mheshimiwa Suleiman Nchambi, swali lingine la nyongeza.

MHE. SULEIMAN MASOUD NCHAMBI SULEIMAN: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru sana Prof. Muhongo na Manaibu wake kwa kazi nzuri ya urekelezaji wa miradi ya umeme katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Kishapu inatekeleza mpango kabambe wa upelekaji wa umeme katika Kata ya Songwa, Mondo, Seke Bugolo, Bubiki, Shagihiru, Masanga mpaka Mwamalasa.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ananihakikishiaje kuwa vijiji vilivyosalia nilivyoviomba katika awamu hii ya pili vitaingia katika mpango huo na hatimaye Kishapu ing'are kama maeneo mengine yatakavyong'ara?

SPIKA: Huoni kama ni swali jipya kabisa hilo? Sasa usipojibiwa sawasawa ndivyo ilivyo. Mheshimiwa Naibu Waziri jaribu!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA): Mheshimiwa Spika, naomba ni mjibu Mheshimiwa Nchambi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli vijijij alivyovitaja viko katika mpango na tayari mkandarasi yuko kule na ameshaanza kufanya *survey* na kwa taarifa nilizozipata kwa asubuhi hii ni kwamb *surveyor* ameshamaliza na sasa hivi anafanya *design*.

Vijiji alivyoviomba vya ziada ni vijiji ambavyo havikuwepo kwenye awamu hii. Lakini tunamhakikishia tu kwamba Serikali inajipanga kuhakikisha kwamba Serikali inajipanga kuhakikisha kwamba vijiji vyote vinapata umeme Tanzania nzima, lakini itakuwa ni hatua kwa hatua.

Kwa hiyo, awe na subira pale ambapo pesa zitakuwa zimepatikana tutahakikisha vijiji hivyo vinahusishwa vilevile. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Dkt. David M. Mallole, atauliza kwa niaba yake Mheshimiwa Fatma Mikidadi.

Na. 114

Soko kwa Zao la Zabibu

MHE. FATMA MIKIDADI (K.n.y. MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE) aliuliza:-

Nchi ya Tanzania inawajali sana wakulima wake ikiwa ni pamoja na kuwatafutia masoko ya mazao yao na kuwatafutia wawekezaji katika Kilimo.

(a) Je, ni lini zao la Zabibu litatafutiwa soko la uhakika na kuwa miongoni mwa maao yenye tija katika uchumi wetu?

(b) Je, ile ahadi ya Waziri Mkuu ya kutafuta soko la uhakika la Zabibu na uwekezaji wa kutosha imefikiawapi?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mciwa Malolle, Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo ni kivutio kikubwa karika kuongeza uzalishaji wa mazao ikiwemo zao la Zabibu. Katika kuandaa mazingira ya soko la uhakika la Zabibu, Serikali itaendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kusindika Zabibu kupitia uwekezaji wa viwanda vidogovidogo vya wakulima yaani *Semi Refinery* na viwanda vikubwa yaani *Double Refinery* ili kuongeza usindikaji wa Zabibu na hivyo kuwepo kwa soko la uhakika kwa wakulima kwa Zabibu nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mikakati hiyo Wizara inashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino kuandaa mkakati wa kufungua kiwanda cha kusindika Zabibu katika Shamba la Chinangali namba mbili ili Zabibu zinazozalishwa katika eneo hilo pamoja na maeneo mengine Mkoani Dodoma ziweze kusindikwa na hivyo kuwezesha wakulima kupata bei zuri.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa *program* ya *ASDP* kiasi cha shilingi milioni 260 zilitolewa mwaka 2012/2013 na shilingi milioni 380 zimetengwa mwaka 2013/2014 kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kusindika Zabibu kinachokadiriwa kugharimu kati ya shilingi milioni 800 hadi bilioni moja.

Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino imeingia makubaliano yaani *MOU* na Benki ya Taifa ya Raslimali yaani *The Tanzania Investment Bank* kwa ajili ya kupata mkopo wa fedha za kukamilisha ujenzi wa kiwanda hicho.

(b) Mheshimiwa Spika, ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kutafuta soko la uhakika la Zabibu inaendelea kufanyiwa kazi kupitia mkakati wa kuanzisha viwanda vya kusindika Zabibu ghafi ili kuongeza thamani ambapo bei ya Zabibu iliyosindikwa yaani *Grapes Juice Concentrate* ni takribani mara tatu ya bei ya Zabibu ghafi. Hivyo, kukamilika kwa viwanda hivyo kutawezesha wakulima kupata soko la uhakika la zao la Zabibu na hivyo kuwaongezea wakulima kipato.

SPIKA: Mheshimiwa Fatma Mikidadi swali la nyongeza!

MHE. FATMA MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri watu wa Dodoma wanapenda sana wawe na viwanda. Lakini havipo, mazao yote usindikaji wa mazao ndiyo uvumbuzi pekee wa kuleta soko. Tulijaribu kuleta zao la Zabibu Lindi ikashindikana…..

SPIKA: ULiza swali Mheshimiwa!

MHE. FATMA MIKIDADI: Likabaki zao la Korosho.

Mheshimiwa Spika, naomba pamoja na mazao haya ya Zabibu Dodoma tunaomba na Lindi viletwe viwanda vya kusindika Korosho Lindi?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana! (*Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi tafadhali maana yake halihusiki!

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum Lindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubali tumepokea ombi lake tutalifanyia kazi kikamilifu sana. Ahsante sana! *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Chibulunje!

MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE: Mheshimiwa Spika, kwa kweli nakushukuru sana, usingenipa nafasi hii ningesikitika sana.

Nataka kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, jitihada zile ambazo tunazifanya Chamwino za kujenga kiwanda najua Serikali iko karibu sana.

Lakini swali langu ni kwamba hivi sasa wakati tunaendelea na ujenzi wa kiwanda cha usindikaji Zabibu Chinangali, mnunuzi wa sasa hivi wa Zabibu ambaye alikuja kwa jina la kununua Zabibu za Chinangali amekuwa na ukiritimba halipi wakulima mapema na wakati mwingine anakuwa na lugha ambazo hazifai.

Je, ni lini Serikali itakemea tabia za ukiritimba wa mnunuzi huyu?

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Majibu!

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chibulunje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana kwa kutukumbusha jambo hili lakini naomba niseme kwamba Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushiurika, Mheshimiwa Engineer Chiza alishatembelea eneo hili analolisema.

Lakini naomba naomba niseme kwamba kama mnunuzi huyu ana tabia ya ukiritimba, kama mnunuzi huyu ana tabia au lugha ya kiburi na kwa sababu hapa ni jirani mimi naomba nimwombe Mheshimiwa Chibulunje kwamba mimi na yeye tuko tayari wiki lijalo tutafute muda ili twende tukaonane na mnunuzi huyu. Tuzungumze naye ili tumwelimishe na aone umuhimu pia wa kukaa karibu na wakulima wa Zabibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana, tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla.

Na. 115

Wilaya ya Nzege Kuwekwa Kwenye Mpango wa SAGCOT

MHE. DKT. HAMISI ANDREA KIGWANGALLA aliuliza:-

Wilaya ya Nzega ni maarufu kwa kuzalisha mchele mzuri kama vile *Super,* Afaa, Tule na Bwana, Mbawa Mbili na kadhalika.

Je, ni kwa nini Wilaya hii isiwekwe kwenye mpango wa *SAGCOT* ili kuzalisha mbegu bora na kuziuza?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Chakula na Ushirika, naomba nijibu swali la Dkt. Hamis A. Kigwangalla, Mbunge wa Jimbo la Nzega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa kukuza kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania yaani *The Southern Agricultural Corridor of Tanzani (SAGCOT)* ni mpango wa ubia kati ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma yaani *Public Private Partneship* unaolenga kuongeza tija ya uzalishaji katika kilimo kwa kushirikisha zaidi Sekta Binafsi kuwekeza katika kilimo kwa kutumia zana bora na mnyororo wa thamani wa zao husika yaani *Value Chain Approach*.

Mheshimiwa Spika, mpango wa *SAGCOT* umeandaliwa kwa misingi ya utekelezaji wa dhana ya Kilimo Kwanza ambao unalenga kuleta mageuzi ya Kilimo kwa kubadilisha Kilimo kuwa cha Kibiashara. Wadau mbalimbali wakiwemo wakulima wadogo wa kati na wakubwa. Wafanyabiashara wa pembejeo na Zana za Kilimo, watoa huduma za ugani, wanunuzi wa mazao, wasindikaji, wasafirishaji na wadau wa maendeleo wanashiriki katika utekelezaji wa mpango huo.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa utekelezaji wa kilimo kwanza unakuwa na tija na maslahi mapana katika maendeleo ya kilimo nchini, wadau walikubaliana kutekeleza mpango huo kupitia mpango wa ukanda yaani *Corridor Approach* ambapo Kanda mbalimbali zimeainishwa ikiwemo Kanda ya Kati. Aidha, katika utekelezaji wadau walikubaliana kuanza na ukanda wa Kusini kutokana na sifa mbalimbali ikiwemo ardhi yenye rutuba na upatikanaji wa miundimbonu ya usafirishaji na masoko.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua fursa za maeneo ya uzalishaji wa Mpunga katika Wilaya ya Nzega ambapo kuna *scheme 12* zenye jumla ya hekta 4100 zinazotumia teknolojia ya umwagiliaji wa kuvuna maji ya mvua kwa njia ya mabanio na mabwawa zinazozalisha kiasi cha tani 11,150.

Aidha, Wilaya ya Nzega ni kati ya maeneo muhimu nchini yanayochangia katika utekelezaji wa malengo ya mpango wa matokeo makubwa sasa yaani *BRN* ya kuongeza tani 290,000 za Mpunga ifikapo mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Nzega ni mojawapo ya Wilaya Nzega ni mojawapo ya Wilaya zinazozalisha mpunga nchini na hivyo kuwa eneo la kimkakati katika kuongeza uzalishaji wa Mpunga nchini. Kwa kuzingatia fursa za kilimo zilizopo katika ukanda wa Kati, Serikali kwa kushirikiana na wadau itaandaa mpango wa maendeleo ya kilimo yaani ukanda wa wa kati, *(Central Agricultural Development Corridor)* unaohusisha Wilaya ya Nzega.

Aidha, uzoefu unaopatikana kupitia utekelezaji wa *SAGCOT* utasaidia katika maandalizi na utekelezaji wa mpango wa maendeleo ya Kilimo katika Kanda ya Kati. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla swali la nyongeza!

MHE. DKT. HAMISI ANDREA KIGWANGALA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwa kuwa raha ya kula wali inapatikana kwenye ladha. Lakini pia kwenye harufu nzuri ya mchele, na kwa kuwa Wilaya ya Nzega ina mbegu zenye sifa hizo za ladha nzuri, tamu.

Lakini pia harufu yenye kuvutia na kwa kuwa mbegu za asili ya Nzega kama Afaa, *Super*, Mbawa mbili, Tule na Bwana ni mbegu maarufu zenye ladha nzuri na harufu ya kuvutia, na sasa zinaingia katika hatari ya kupotea kutokana na ujio wa mbegu za kisasa zinazotoka nje ya nchi kama kule Thailand ambazo hazina ladha nzuri lakini zina tija katika uzalishaji.

Ni kwa nini Serikalikwa kuwa inaanza mpango wa maendeleo ya kilimo ya ukanda wa kati *(Central Agricultural Development Corridor)* isiifanye Nzega wakati inajiandaa na mpango ule kuwa ni eneo maalum la kuzalisha mbegu hizi za asili?

Swali langu la pili ni kwamba, ni kwanini Serikali isikitumie kituo cha Utafiti cha Mwanahala, kilichopo pale Nzega, kuzalisha mbegu hizi za asili ya Nzega, zenye ladha nzuri na harufu ya kuvutia. Ili mbegu hizi nazo ziweze kuwa na tija, kwa maana ya kupata mazao mengi kutokana na shina moja la mpunga. Kama zilivyo zile mbegu nyingine ambazo wakulima sasa wanazikimbilia kuzilima na badala yake wanaacha kulima mbegu za asili.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi ingawa swali lenyewe ni refu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Dkt. Hamisi Andrea Kigwangala, Mbunge wa Nzega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli wanazalisha mbegu zile alizozitaja kule Nzega na kwamba ni mchele ambao wameuzoea, lakini ni vizuri pia tukaondokana na mazoea. Vituo vyetu vya utafiti ambavyo viko nchini na hasa kituo chetu cha Katrinia ambacho kiko Ifakara kimefanikiwa kuzalisha mbegu bora sana inayoitwa *TXD306* au *Saro Five*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbegu hii inazalisha kwa wastani wa gunia kati ya 25 mpaka 40 kwa heka moja kama mtu akiitumia vizuri, tofauti na mbegu tulizozizoea ambazo Mheshimiwa Mbunge anazisema ambazo nyingi zinazalisha kati ya gunia 10 mpaka 20.

Kwa hiyo, tuwaombe Waheshimiwa Wabunge badala ya kuendelea na tabia ya mazoea ya kutumia mbegu za zamani zile, kwa sababu mbegu hizi ambazo tunazisema ikiwepo hiyo *Saro Five* pamoja na mbegu ya *Nerika One* ambazo zote zinazalishwa hapa nchini.

Basi nimwombe Mheshimiwa Mbunge pamoja na mambo mengine twende tutumie mbegu hizi ambazo zimetafitiwa na wataalam wetu hapa nchini ambazo tunafikiri zinatuletea tija zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuwaombe Waheshimiwa Wabunge, tuna chuo chetu cha Mkindo pale Mvomero ambacho kinatafiti pia mbegu nzuri sana. Lakini pia kinafundisha pia wakulima namna ya kulima vizuri zaidi mbegu hizi ambazo zinatafitiwa hapa nchini. Kwa maana hiyo kuwapa wananchi tija kubwa zaidi kwenye mpunga wanaolima pale mashambani.

Pia nimwombe Mheshimiwa Mbunge, kwamba chuo alichokisema pale Nzega tutakitembelea ili tuone kina uwezo gani na kama kinaweza kutumika pia kwa ajili ya shughuli za utafiti wa mbegu za mpunga.

SPIKA: Swali refu, majibu marefu, sasa tunaenda Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, atauliza swali hilo.

Na. 116

Fursa za kujiendeleza Kimasomo kwa Askari Polisi na Magereza

MHE. CONCHESTA LEONCE RWAMLAZA aliuliza:-

Askari Polisi na Magereza wamekuwa wakicheleweshewa ruhusa ya kwenda kujiendeleza kimasomo hasa kwa ngazi ya elimu ya juu na hivyo kuwanyima fursa ya kujiendeleza kimasomo:-

Je, askari anapoiingia anapaswa kutumikia ajira yake kwa muda gani ndipo aruhusiwe kujiendeleza masomo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta L. Rwamlaza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, majeshi ya Polisi na Magereza yana utaratibu wa kuruhusu askari kwenda masomoni nje ya jeshi kulingana na mahitaji ya jeshi ya wakati uliopo na siyo kucheleweshewa ruhusa ya kwenda kujiendeleza.

Mheshimiwa Spika, majeshi ya Polisi na Magereza yamekuwa yakitoa vibali kwenda kusoma kwa Maafisa na Askari wao kwa kuzingatia mahitaji ya wataalam katika jeshi na bila kuathiri shughuli zao za msingi. Askari hupata fursa ya kujiendeleza katika kozi mbalimbali katika vyuo vya ndani ya jeshi na hata nje ya jeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya wataalam ndaniya jeshi hufikiriwa sana kipindi cha ajira, hivyo jeshi huajiri wataalam kwa kuzingatia kazi za ulinzi.

Hata hivyo, pindi inapotokea upungufu wa wataalam katika fani mbalimbali za kazi, jeshi hutoa nafasi za askari wenye sifa kuhudhuria kozi mbalimbali kwa viwango tofauti vya taaluma ikiwemo elimu ya juu. Miongoni mwa sifa za mtu kuhudhuria kozi hizo ni lazima awe na rekodi nzuri ya utendaji kazini na sifa za kuweza kupata udahili katika chuo husika.

Mheshimiwa Spika, askari wa ngazi zote wanalazimika kuomba na kukubaliwa kwa nia ya kujiendeleza kielimu kwenye taaluma zinazohitajika ndani ya jeshi baada ya kumaliza muda usiopungua miaka mitatu.

SPIKA: Mheshimiwa Rwamlaza, swali la nyongeza.

MHE. CONCHESTA LEONCE RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi linahitaji ueledi na katika Bunge hili tumekuwa tukilalamika kwamba, wanajeshi hasa wa jeshi la Polisi hawawezi kutafsiri sheria vizuri, na kwa

kuwa kuna askari polisi ambao wako tayari kujiendeleza katika taaluma hiyo, na kwa kuzingatia kwamba Serikali haiwalipii pale wanapokwenda kusoma katika vyuo vikuu.

Ni kwanini Jeshi la Polisi linawachelewesha na kuwanyima vijana hawa nafasi ya kujiendeleza?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Askari wanaoajiriwa katika Jeshi la Polisi wanaokuwa wamehitimu katika kiwango cha shahada *(degree)* ajira zao zinaambatana na vyeo, lakini kwa wale waliojiendeleza wenyewe kwa gharama zao na kwa kusaidiana na wazazi wao, hawawezi kupewa vyeo.

Je, Serikali haioni kwamba inafanya upendeleo?,

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Conchesta L. Rwamlaza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, sheria ni elimu muhimu sana katika kazi za Jeshi la Polisi na hata wakati wa mafunzo ya awali *(recruit)* askari wote hawa huwa wanapewa elimu ya sheria. Elimu ya sheria pia ni sehemu ya elimu muhimu na kipaumbele ambacho katika jeshi hili zinaonekana.

Hata hivyo, niwakumbushe kwamba, jumla ya waajiriwa wa jeshi la Polisi ni 44,000 na pamoja na umuhimu wa sheria lakini kuna watu tofauti ambao taaluma zao zinahitajika pia. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile wote hawatasoma sheria kama sehemu ya matakwa waliyonayo isipokuwa ni sehemu ya kuliendeleza jeshi na kuhakikisha kwamba mara zote ulinzi na vitengo vingine vinapata wahudumu wenye weledi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyeo na kusoma *degree*. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la swali dogo la kwanza, ni kwamba watu wowote na idadi yoyote wakisoma degree siyo tatizo.

Lakini katika jeshi pamoja na kuwa elimu ni sehemu ya kupandisha vyeo, lakini jeshi ni lazima liwe na kitu kama *pyramid*. Wakiishasoma wote na siku moja wote wakapewa wakawa majenerali hakuna mtu ambaye ataenda kulinda benki na fedha zisiibiwe. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumechukua muda mrefu mno. Sasa nitamwita Mheshimiwa Kapt. John Zefania Chiligati.

Na. 117

Ujenzi wa Kituo cha Polisi Wilaya ya Manyoni

MHE.KAPT. JOHN Z. CHILIGATI aliuliza:-

Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Manyoni ni kidogo, chakavu na hakina hadhi ya kuwa kituo cha Wilaya. Kiwanja cha kujenga kituo kipya na cha kisasa kimepatikana na wananchi wameanza kufyatua matofali ya ujenzi na hasa ikizingatiwa kuwa *IGP* aliishatoa ahadi kwamba, Serikali itaunga mkono juhudi hizo.

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya kusaidia kuanzisha ujenzi wa kituo hicho?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kapt. John Zephania Chiligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako Tukufu nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Kapt. Mstaafu John Zefania Chiligati na wananchi wa Jimbo la Manyoni kwa ujumla kwa jitihada zao walizozionesha wakishirikiana na wadau mbalimbali kuanza hatua ya matayarisho ya ujenzi wa kituo cha Polisi cha Wilaya ya Manyoni.

Jeshi la Polisi liko tayari kuunga mkono juhudi hizi kama ilivyoahidiwa na Inspekta Jenerali wa Polisi mwaka uliopita.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwezo wa Serikali kuwa mdogo ninamwomba Mheshimiwa Mbunge kuendelea kutumia fursa aliyonayo ya Wadau Werevu kuchangia katika ujenzi wa kituo anachokisema. Hata hivyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mara hali ya kifedha itakaporuhusu basi itatoa mchango wake stahiki.

SPIKA: Mheshimiwa Kapt. John Chiligati.

MHE. KAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya kutia moyo ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili madogo tu ya nyongeza.

Swali la kwanza ni kwamba, je, mwaka huu wa fedha (unaoanza mwezi Julai) Serikali itatenga walau fedha kidogo ili ujenzi wa kituo hiki uendelee kwa wakishirikiana na Wananchi wa Wilaya ya Manyoni?

Polisi wa pale Manyoni wana shida kubwa sana ya nyumba kwa sababu zilizopo ni chache na chakavu. Je, katika mradi huu wa ujenzi wa kituo cha polisi tunaweza tukaunganisha na ujenzi wa nyumba za polisi ili kuwapa motisha Polisi wa Manyoni? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kapt. John Zephania Chiligati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni juzi tu tumepitisha Bajeti ya Jeshi la Polisi. Kwa mtazamo wa haraka haraka sikukiona kituo cha Manyoni. Hata hivyo, katika kujenga vituo vya polisi hatutegemei moja kwa moja, Bajeti ya Serikali ambayo ni finyu. Ninamwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutashirikiana na ikiwezekana katika mwaka unaoanza Julai, kupitia njia tofauti ambazo tunazo wakiwamo Wadau Werevu tunaweza kupata *resources* kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo hiki.

Swali la pili ni kwamba, kwetu sisi Jeshi la Polisi mara zote inavyowezekana kituo cha Polisi hasa cha Wilaya ni lazima kiwe na nyumba angalau ya *OCD* pale pale. Kwa hiyo, katika *package* hii ambayo tunajiandaa kuitayarisha kwa Manyoni basi suala la nyumba nalo tuanze kulifikiria ili iwe ni sehemu ya kituo tunachokizungumzia. *(Makofi)*

SPIKA: Tunaendelea, Mheshimiwa Joseph Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Rombo kwa kutambua umuhimu wa ulinzi na usalama wao na mali zao kwa kushirikiana na Mbunge wao wanajenga vituo vya polisi katika Kata za Mahida, Shimbi, Useri na Mengwe.

Je, Serikali iko tayari kushirikiana nao katika kukamilisha ujenzi wa vituo hivyo?

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Selasini, Mbunge wa Rombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze kwa hamasa ambayo ameijenga kule Rombo na kuweza kujenga vituo vya polisi na wala siyo kimoja. Nawaomba Wabunge wengine tuone hili linawezekana kama linavyowezekana kule Rombo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachoweza kumuahidi Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, tutaenda tuvione vituo, tutazame mahitaji na hapo tutatangaza tutakachoweza kuchangia. *(Makofi)*

SPIKA: Naomba tuendelee na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Masoud Adballa Salimu, atauliza swali hilo na kwa niaba yake Mheshimiwa Rashid Abdalla.

Na. 118

Mafao ya Wastaafu

MHE. RASHID ALI ABDALLAH K.n.y. (**MHE. MASOUD ABDALA SALIMU)** aliuliza:-

Imebainika kwamba, mafao ya Wastaafu wanayolipwa baada ya kustaafu sio sahihi na mara nyingi hulipwa pungufu kuliko inavyostahili:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kurekebisha kasoro hiyo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (**MHE. ADAM K. MALIMA**) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mtumishi wa Serikali anapostaafu, anakokotolewa mafao yake kwa mujibu wa Sheria ya Pensheni *(Public Sector Retirement Act,* ya mwaka 1999) kwa kuzingatia masharti ya ajira ya mtumishi anayestaafu, muda aliofanyakazi kuanzia tarehe ya ajira ya kwanza hadi tarehe yake ya kustaafu, mshahara wake wa mwisho kabla ya kustaafu kwa cheo chake cha mwisho. Baada ya taarifa hizo kupatikana, ukokotoaji hufanyika kwa kutumia fomula ya pensheni.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa fomula hiyo, nusu ya matokeo ya ukokotoaji, Mstaafu hulipwa kwa mkupuo mmoja (kiinua mgongo) ambapo nusu inayobaki hukokotolewa ili kupata kiwango cha pensheni anachostahili kulipwa kila mwezi kwa muda wote wa uhai wa Mstaafu. Mafao hayo yaani kiunua mgongo na pensheni ya kila mwezi, hulipwa kwa mstaafu baada ya nyaraka za ukokotoaji kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Hivyo, madai kuwa imebainika kuwa mafao yanayolipwa Wastaafu baada ya kustaafu sio sahihi si madai ya kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mafao yanayolipwa kwa Wastaafu baada ya kustaafu ukokotoaji wake unazingatia sheria ya pensheni niliyoitaja na hulipwa baada ya kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*, malipo hayo ni malipo sahihi na hakuna mkakati mahsusi wa kurekebisha utaratibu huo kwa sasa. Inapotokea kasoro kwa Mstaafu mmoja mmoja katika ukokotoaji, kasoro hiyo hurekebishwa kwa utaratibu pale inapogundulika. *(Makofi)*

SPIKA: Sasa Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Swali la nyongeza.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake, lakini pamoja na majibu hayo naomba niulize maswali mawili madogo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya CAG ya mwaka 2009/2010 kati majalada 4,960 ya Wastaafu yalikaguliwa, lakini majalada 137 yalionekana yana malipo pungufu.

Je, ni lini Mheshimiwa Waziri atayapitia majalada hayo na kulipa mapungufu hayo ambayo yalionekana na CAG.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Wastaafu wana hali mbaya na hakuna ambaye halifahamu hilo. Hali ya malipo hailingani na hali ya mabadiliko ya maisha tuliyo nayo sasa. Serikali ina utaratibu gani wa kuweza kufanya marekebisho ili kuwawezesha Wastaafu hao waweze kuishi vizuri.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (**MHE. ADAM K. MALIMA**): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kila ripoti ya CAG inapotokea inaonekana kweli kuna Wastaafu wengine ambao tunabaini matatizo kidogo. Lakini matatizo hayo yanajitokeza mara nyingi kwa sababu ya mambo mbalimbali. Kwa mfano tarehe ya ajira ya kwanza, mara nyingine inaonekana mwajiri yule anakuwa haja-*submit* tarehe ya ajira ya kwanza au saa nyingine yule Mstaafu anakuwa amepitia kwenye *promotions* mbalimbali na taarifa zile za *promotions* hazijaoneshwa kikamilifu.

Kwa hiyo, ni kweli suala hilo lipo, lakini kila linapobainika utaratibu uliokuwepo ni kwamba, Mstaafu huyu anatakiwa apeleke taarifa kwenye kituo chake cha mwisho cha kazi na wao wailete kwenye kitengo chetu cha Idara ya Pensheni, kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali na hilo linafanyiwa kazi. Inawezekana huo mchakato unakuwa na ucheleweshaji kidogo, lakini ndiyo utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili la pili la hali ya malipo kwamba, kuna watu ambao wako kwenye pensheni na hali zao ni ngumu ni kweli nalo. Kinachotokea ni kwamba, pensheni ni fomula inayotokana na mchango uliotoa kutokana na mishahara yako. Kwa hiyo, unaweza kukuta watu wawili wameajiriwa kwenye nafasi moja lakini vipindi tofauti, mmoja alikuwa Mhasibu kuanzia mwaka 1980 hadi 1985 na mwingine kuanzia mwaka 1980 hadi 1995, kwa sababu mishahara yao ilikuwa tofauti na uchangiaji ulikuwa tofauti na mafao yao pia yatakuwa tofauti.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna huo utaratibu wa harmonization unafanyiwa kazi kupitia utafiti wa kisayansi, ni mgumu kidogo lakini Serikali inaendelea nao kuangalia namna ambavyo tutajielekeza kwenye suala la kuboresha malipo ya Wastaafu ambao malipo yao yamekuwa ni ya zamani kidogo. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, muda unakwenda kinyume. Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Esther Amos Bulaya, atauliza swali hilo na kwa niaba Mheshimiwa Saidi Mohamed Mtanda.

Na. 119

Muswada wa Sheria ya Habari kuletwa Bungeni

MHE. SAID M. MTANDA (K.n.y. MHE. ESTER A. BULAYA) aliuliza:-

Mwaka 2007 Serikali iliitikia wito wa Wadau wa Habari na Haki za Binadamu wa kutaka kuwepo kwa Rasimu mbili tofauti za Muswada wa Sheria ya Uhuru wa Habari moja ya Sheria ya Haki ya Kupata Habari na nyingine ya Huduma za Vyombo vya Habari.

Je, Serikali italeta lini Miswada yote miwili Bungeni ijadiliwe na kupitishwa kuwa Sheria?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mwaka 2007 Serikali iliitikia wito wa wadau mbalimbali wa habari waliotaka kuwepo kwa rasimu mbili tofauti za Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari *(Media Service Law)* na Uhuru Wa Kupata Habari *(Right to Information)*. Serikali imepokea mapendekezo mbalimbali kutoka kwa wadau wakiwemo Waandishi wa Habari, Wamiliki wa vyombo vya habari, wanataaluma waliobobea katika tasnia ya habari, Taasisi au Mashirika yanayojishughulisha na masuala ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Muswada wa Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari *(Media Service Law)* umekamilika baada ya kupitia hatua zote muhimu za kuandaa Muswada na taratibu za kuleta Bungeni zinaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muswada wa Sheria ya Haki ya Kupata Habari *(Right to Information),* napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa utafiti wa uzoefu kutoka nchi zenye Sheria kama hiyo mfano, India umekamilika na sasa Muswada wa Sheria hiyo unaandaliwa na Wizara ya Katiba na Sheria. Endapo maamuzi yatafikiwa Muswada huo utawasilishwa katika Bunge lako Tukufu kwa kujadiliwa na hatimaye kupitishwa kuwa Sheria.

SPIKA: Mheshimiwa Mtanda swali la nyongeza.

MHE. MOHAMMED S. MTANDA: Mheshimiwa Spika, kwanza muuliza swali Mheshimiwa Ester Amos Bulaya alitaka kufahamu ni lini Muswada wa Sheria ya Uhuru wa Habari na siyo Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari, hilo mosi.

La pili, tulitaka sasa kufahamu ni lini Muswada huu utaletwa hapa Bungeni kwa sababu takribani miaka kumi na saba sasa Serikali imekuwa ikiahidi, lakini hadi leo mazingira ya Waandishi wa Habari, uhuru wa kupata habari katika nchi hii bado ni changamoto kubwa, ni lini sasa baada ya miaka kumi na saba kupita toka Serikali ilipoahidi, Muswada huu utaingia hapa Bungeni? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mtanda ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii ambayo pia inasimamia

Wizara ya Habari na anajua fika taratibu za kuleta Muswada zikoje. Kwa hiyo, nimwahidi tu kwamba, Muswada huo utaletwa wakati wowote kuanzia sasa.

SPIKA: Mheshimiwa Mkosamali swali la nyongeza.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, nimesimama kuuliza swali la nyongeza kuhusu danadana za Muswada huu kwa sababu toka tumefika kwenye Bunge hili na kabla hatujaja wanashindwa kusema lini. Naomba uwaagize waseme ni lini wataleta kwa sababu kama wao hawakandamizi Vyombo vya Habari hawa watu, kwa nini hawataki kusema ni lini wataleta huu Muswada? Alitudanganya hapa Makalla, Nchimbi alishatudanganya huyu naye anatudanganya ni lini wanaleta Muswada hapa?

SPIKA: Usinipigie hotuba hapa, uliza swali tu basi. *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, Mbunge aliyeuliza swali ni Waziri Kivuli na siamini Waziri au Serikali inaweza kudanganya hapa.

WABUNGE FULANI: Aaaah!

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Kwa hiyo hizi ni kauli tu za kutafuta vitu ambavyo siyo sahihi. Ninachosema ni kwamba, mimi ni mdau wa habari na ningependa sana kuona Waandishi wa Habari wa nchi hii wanapata haki wanayostahili. Kwa maana hiyo, Muswada huu utaletwa, lakini kila jambo lina taratibu zake, vuteni subira**.**

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa Waandishi wa Habari au vyombo vya Habari ndivyo vinavyotusaidia kupata habari mbalimbali nchini na kwa kuwa hakuna Sheria mpaka sasa hivi, je wanapokuwa wanaonekana kuwa wana hatia hatuoni kwamba hatuwatendei haki? Je, Waziri husika anaweza akatoa jibu sahihi hapa la kusema ni lini, tarehe, mwezi na mwaka?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Matitu ambaye pia ni Mwandishi wa Habari.

Mheshimiwa Spika, Bunge hili ni Bunge la Bajeti na sote humu ndani tunafahamu taratibu za uendeshaji wa Bunge zilivyo; kuna kalenda za wakati wa Miswada na kuna kalenda wakati wa Bunge la Bajeti, vuteni subira.

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa muda wa maswali umepita, sasa tuendelee na matangazo. Kwanza nitambue wageni tulionao nao leo:-

Wapo wageni 32 wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao ni Wahadhiri, Wakufunzi na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mkwawa wakiongozwa na Ndugu Thea M. Tala. Naomba hawa wote wasimame huko waliko, asante sana na karibuni sana.

Tunao wageni wengine 45 wa Mheshimiwa Hasnain Mohammed Murji ambao ni Maaskofu, Mapadri, Wachungaji, Makatekista na Waandishi wa Habari kutoka Mtwara. Naomba na wenyewe wasimame walipo. Ahsante sana na karibuni sana. Sitaweza kupiga picha na ninyi kwa sababu niko kazini.

Kuna wageni 10 wa Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro kutoka Kiteto ambao wako 10, lakini amewataja na wengine, yupo Mheshimiwa Maike Lemalili, ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, naomba asimame alipo kama yupo, nina mashaka pengine amekosa nafasi. Kuna Mheshimiwa Lairumbe, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto,

nafikiri hawa wamekosa nafasi wataingia baadaye. Kuna Mheshimiwa Leonard Kunamila Diwani Kata ya Engusero na yupo Mheshimiwa Bosco Ndunguru, ni *DED* Kiteto na wanafunzi sita kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, hawa wanafunzi nao wapo? Nadhani ni ukosefu wa nafasi wataingia baadaye.

Halafu kuna wageni wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ambao ni Mchungaji Alfonce Elias wa Kanisa la *TMC Methodist* Katoro na Mchungaji Silvanus Dome wa Kanisa la *TAG* Katoro, Bukwimba, hawa sijui kama wamepata nafasi. Naona leo tumekuwa na wageni wengi hawajafika. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Blandes ambao ni Mheshimiwa Saad Rwazo, Diwani wa Kata ya Kanoni na Ndugu Severine Sande, mfugaji kutoka Kata ya Kianga. Wale pale. Karibuni. *(Makofi)*

Tuna wageni nane wa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu kutoka Chama cha Makatibu Muhtasi Tanzania, wakiongozwa na Mrs Pili Mpenda, Mwenyekiti wa Chama hicho. Pili Mpenda yuko wapi, nina wasiwasi kutokana na nafasi, wote karibu wako sehemu ambayo hawaonekani, lakini watasikia tu hivyo hivyo, ahsanteni na karibuni.

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o ambaye ni Ndugu Peter Owaga, Mkurugenzi wa Taasisi inayoshughulikia idadi ya watu na elimu kwa vijana, huyu yuko wapi na yeye? Nafasi nafikiri leo zimejaa wageni.

Tuna wageni 15 wa Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi, Tabora. Hawa kama wamepata nafasi wasimame walipo, nafikiri nafasi haipo watafika baadaye.

Kuna wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo, ni wanafunzi 63 kutoka Chuo Cha Mipango, Dodoma; naomba wasimame walipo kama wapo. Ahsante sana, tunawatakia masomo mema. *(Makofi)*

Halafu kuna wanafunzi wengine 60 wa Shahada ya Uchumi, Kilimo na Biashara kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Morogoro na hawa wasimame walipo kama wapo. Ahsanteni sana na tunawatakia masomo mema. *(Makofi)*

Halafu kuna 60 kutoka Shule ya Msingi ya Ritaliza ya Rombo, Moshi; hawa nao wasimame walipo, nafikiri ni wa Mheshimiwa Selasini hawa, ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi wengine 32 kutoka Shule ya Msingi ya *Saint* Joseph ya Moshi na hawa wasimame walipo kama wapom asante sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, matangazo yanayofuata, nina tangazo moja tu, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu Mheshimiwa Peter Serukamba anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kuwa leo tarehe 23, saa nane na nusu kutakuwa na kikao cha Kamati katika ukumbi namba 229 uliopo katika jengo la Utawala, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Katibu!

MWONGOZO WA SPIKA

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Haiwezekani kuwa na miongozo yote, nachukua mmoja tu sijui nimwite nani? Mheshimiwa Mnyika kwa kifupi na siyo hotuba!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kwa Mujibu wa Kanuni ya 46(1), Waziri anayeulizwa swali anakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kikamilifu kama lilivyoulizwa, isipokuwa kama jibu hilo husika ni refu na lina takwimu nyingi na Kanuni ya (64)(1)(a)kwamba hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali la 119 Mheshimiwa Ester Bulaya aliuliza ni lini Miswada hii itawasilishwa, jambo hili la ni lini Miswada hii itawasilishwa, halijajibiwa kwa ukamilifu kwa sababu Waziri hakusema ni lini na badala yake Waziri ametoa maelezo yasiyokuwa ya kweli kwamba kwa kuwa tuko kwenye Bunge la Bajeti ndiyo sababu ya Waziri kutokujua Muswada huu utawasilishwa lini! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni muhimu jambo hili likatolewa taarifa za ukweli kwa sababu kwenye Bajeti iliyopita Serikali ilitoa kauli Bungeni humu kwamba Miswada hii itawasilishwa katika mwaka huu wa fedha na Mheshimiwa Rais ambaye ni kiongozi wa Serikali akiwa Uingereza, aliiahidi dunia kuwa ifikapo mwezi Machi, 2014 Sheria hiyo itakuwa imetungwa. Kwa hiyo, Rais alisema muda maalum, kwa hiyo, Serikali inatakiwa kusema muda maalum ni lini hasa Miswada hii italetwa ikizingatiwa kwamba kauli ya Rais haijatekelezwa mpaka hivi sasa mwezi Machi umepita.

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako.

SPIKA: Mheshimiwa Mnyika na wewe hapo umechemsha ni Mwongozo au ni nini? Basi kama alivyosema yeye hivyo hivyo, sasa ukiniuliza mimi ni lini na yeye amefanya vizuri kutokusema kwa sababu hajui tarehe, kwa hiyo, atajibu wakati wake.

WABUNGE FULANI: Aaah!

SPIKA: Waheshimiwa sikilizeni, Waziri anayekuja kujibu maswali hapa anaweza akawa hana uhakika, lakini lakini taratibu zetu zinamruhusu atakapopata uhakika anaweza kuja kutoa *statement* hapa, kama ninavyotaka kumwita sasa Waziri mwingine, kwa hiyo Mheshimiwa Katibu sasa tunaendelea!

KAULI ZA MAWAZIRI

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa Kauli ya Serikali kuhusu matatizo ya uzalishaji maji katika Mtambo wa Maji wa Ruvu Juu. Tarehe 12 Mei, 2014, Mheshimiwa John Mnyika aliomba Mwongozo wa Spika kuitaka Serikali itoe kauli Bungeni chini ya Kanuni ya 49 ya Bunge kueleza matatizo yanayoukabili mtambo unaozalisha na kutibu maji Ruvu Juu kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya *DAWASA* katika Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, mtambo wa maji wa Ruvu Juu uliopo Mlandizi, Wilaya ya Kibaha ulijengwa mwaka 1954 - 1956 kwa ajili ya kuupatia Mji wa Dar es Salaam na maeneo ya yaliyopo kando ya bomba maji kwa wananchi wake. Uwezo wa mtambo huo kuzalisha maji ni lita milioni themanini na mbili kwa siku.

Mheshimiwa Spika, mtambo wa Ruvu Juu unaendeshwa kwa kutumia seti tatu za pampu katika shughuli za uzalishaji. Seti ya kwanza ina pampu nne na hutumika kuchota maji kutoka

mtoni, eneo la Ruvu Darajani, mita ishirini na moja chini ya usawa wa ardhi kwa kiwango cha lita milioni moja nukta tisa kwa saa kwa kila pampu.

SPIKA: Naomba utulivu.

WAZIRI WA MAJI: Pampu mbili hadi tatu hutumika kwa wakati mmoja kulingana na wingi na kina cha maji kilichopo mtoni. Seti ya pili yenye pampu nne husukuma maji ghafi kutoka kwenye eneo la mto kwa kiwango cha lita milioni moja nukta nne kwa saa kwa kila pampu kwa mwinuko wa mita sitini na sita na umbali wa kilomita sita hadi Mlandizi kwenye mtambo wa kusafisha na kutibu maji, pampu tatu hutumika kwa wakati mmoja kwa kazi hiyo. Seti ya tatu ina pampu nne zinazosukuma maji safi kwenye mwinuko wa mita mia mbili na tano na umbali wa kilomita sitini na tano kutoka Mlandizi hadi Kimara, Jijini Dar es Salaam.

SPIKA: Waheshimiwa, tunaomba utulivu sasa.

WAZIRI WA MAJI: Pampu ina uwezo wa kusukuma lita milioni moja nukta mbili kwa saa. Ili kufikia uzalishaji halisi pampu tatu hupaswa kutembea kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, hali ya Mtambo; Mtambo wa Ruvu juu kwa sasa umeshindwa kukidhi uzalishaji wa kiwango cha maji kilichopangwa yaani lita themanini na mbili kwa siku kutokana na kuharibika kwa pampu mara kwa mara kunakosababishwa na uchakavu unaotokana na umri mkubwa au miaka sitini ya mtambo huo, kukatika kwa umeme mara kwa mara, maji kuwa na tope jingi sana wakati wa mvua na mafuriko. Hii hupunguza uwezo wa pampu kusukuma maji, husababisha kusagika vifaa na vipuri ndani ya pampu. Nne, ugumu wa upatikaji wa vipuri halisi yaani *genuine parts* huchangia katika kuchelewesha matengenezo.

Mheshimiwa Spika, changamoto za mtambo; kwa takribani siku sitini na saba kuanzia tarehe 1 Machi, 2014 na tarehe 6 Mei, 2014, mtambo ulizalisha maji chini ya kiwango kutokana na matukio yafuatayo:-

(1) Kuharibika mara nane kwa pampu tatu za maji ghafi *(raw water pumps)*.
(2) Kuharibika kwa pampu za maji safi *(treated water pumps)* mara mbili;

(3) Kukatika kwa umeme mara kumi na tano kwa jumla ya masaa tisa na dakika hamsini na nane;

(4) Mafuriko katika Bonde la Mto Ruvu siku tisa. Mafuriko hayo yalikuwa makubwa sana yaani kuanzia tarehe 12 Aprili, 2014 na tarehe 20 Aprili, 2014;

(5) Kukatika kwa bomba la maji ya kupooza pampu za maji ghafi kutoka eneo la mafuriko;

(6) Kuungua kwa *auto transformers* kulikosababishwa na hitilafu ya umeme kwa siku mbili yaani tarehe 25 Aprili na tarehe 26 Aprili, 2014; na

(7) Kiwango kikubwa cha tope katika maji yaani *very high turbidity* ambacho kiliongezeka kutoka *units* mia moja tisini na sita za *NTU* hadi *units* elfu moja, mia moja na mbili.

Mheshimiwa Spika, tatu, athari zilizojitokeza; kutokana na changamoto nilizokwishazieleza uzalishaji maji ulipungua na kufikia kati ya lita nane nukta mbili na lita milioni hamsini hamsini na saba nukta nne ikilinganishwa na lita milioni themanini na mbili kwa siku ambazo ndizo uwezo halisi wa mtambo huo.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji ulikuwa chini zaidi tarehe 18 Aprili, 2014 ambapo uzalishaji ulifikia lita milioni moja nukta tisa kutokana na mafuriko na hitilafu kubwa ya umeme. Kupungua kwa uzalishaji kuliathiri usambazaji maji na migao ya maji kwenye eneo lote linalohudumiwa na mtambo huo. Maji kidogo yaliyozalishwa yaliishia njiani katika ya Mlandizi na Kibaha, maeneo ya Tabata na Kimara yaliathirika sana.

Mheshimiwa Spika, jitihada za Serikali katika kukabiliana na changamoto za Mradi; Wizara katika kukabiliana na matukio hayo imechukua hatua zifuatazo:-

(1) Kuchonga vipuri na vifaa vya pampu katika karakana zilizopo hapa nchini kwa kuwatumia wataalam wa Jeshi la Wananchi;

(2) Kuagiza vipuri nje ya nchi; na

(3) Kutoa matangazo kwa wananchi kuhusu upungufu wa maji pale uzalishaji unapopungua au kusimama.

Mheshimiwa Spika, kwa wakati tofauti, matengenezo yalichukua muda mrefu kidogo kutokana na kutopatikana kwa wakati malighafi zinazohitajika. Mfano, chuma cha *high carbon steel* kwa ajili ya *shaft* za *pump* za *bearing housing cover*. Vifaa vilivyoagizwa nje ya nchi ni pamoja na *roller bearings*, pamoja na *valve* za kuzuia maji kurudi kwenye *pump au non-return valves* kwa ajili ya seti za *pump* za maji ghafi.

Bearings zote za akiba zilikwisha katika matengenezo hayo baada ya *pump number three* kuharibu *bearings* mbili na *pump number four* kuharibu *bearing* moja, *pump* zote hizi ni za maji ghafi.

Mheshimiwa Spika, *auto of transformers* nne zilizoagizwa kutoka Uswiss ziliwasili na kufungwa kwenye kituo cha Mlandizi. *Auto transformers* hutumika kupooza umeme kwa ajili ya *pumps* za maji safi.

Bomba la pili la maji la kupooza *pump* limeongezwa ili kuwepa utegemezi wa bomba moja tu ambalo lipo kwenye tindiga la maji lililopo kwenye mashamba ya JKT Ruvu, kati ya Ruvu na Mji wa Mlandizi. Lengo ni kuokoa muda wa kuzima *pump* endapo bomba mojawapo la maji ya kupooza *pump* litapata hitilafu.

Mheshimiwa Spika, baada ya jitihada kubwa zilizotajwa awali, uzalishaji wa maji wa mtambo wa Ruvu Juu unaendelea kurudi katika hali yake ya kawaida. Kwa mfano, tarehe 17 Mei, 2014, uzalishaji wa maji ulifikia lita 80.8 kwa siku na tarehe 18 Mei, 2014, uzalishaji ulikuwa lita milioni 80.3 kwa siku, lakini tarehe 19 Mei, 2014, uzalishaji ulishuka ukafikia lita milioni 70.8 kwa siku kutokana na kukatika kwa umeme kwa muda wa masaa matatu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuchukua hatua za dharura, vifaa na vipuri vya ziada viliagizwa kutoka nje na vingine kuchongwa katika karakana za ndani na kuvihifadhi kwa ajili ya dharura. Hivi sasa zipo seti mbili za *pump* kwa ajili ya dharura. Aidha, mtambo wa kuchotea maji mtoni, unafanyia ukarabati sasa na kama sehemu ya kazi hiyo, *DAWASA* wameagiza *pumps* mbili mpya kwa ajili ya kuchotea maji ghafi katika *intake*. *Pumps* hizi zitawasili hapa nchini mwezi Agosti mwaka jana. Mkandarasi amewasilisha tathimini ya ukarabati unaohitajika ili mtambo huo ufanye kazi katika kipindi chote cha mpito cha miezi kumi na nane wakati mtambo mpya unajengwa.

Mheshimiwa Spika, jitihada nyingine za Serikali; Serikali imeendelea na jitihada za kudhibiti wizi mkubwa na maji unaofanyika katika Jiji la Dar-es-Salaam yakiwemo maeneo ya

Kinondoni, Mwananyamala, Kigogo, Mabibo, Magomeni, Tegeta, Kiluvya, Kibamba, Mbezi na Kimara. Mwezi wa April, 2013, Serikali iliunda Kamati ya kufuatilia tatizo hilo la wizi wa maji katika Jiji la Dar-es-Salaam na Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, jumla ya watuhumiwa wa wizi wa maji 162 walikamatwa na kufikishwa Mahakamani. Hadi sasa watuhumiwa 23 walipatikana na hatia ambapo 19 waliamuriwa kulipa faini kati ya shilingi laki mbili hadi Sh. 2,316,400/= na watuhumiwa wanne walifungwa.

Mheshimiwa Spika, mpango uliopo sasa; kwa kutumia mkopo kutoka Serikali ya India, Serikali imemwajiri Mkandarasi Va Tech Wabag kutoka India kujenga upya na kupanua mtambo wa Ruvu Juu. Upanuzi huu utaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 82 hadi lita milioni 196 kwa siku. Gharama za Mradi huu ni dola za Marekani milioni 39.7.

Mheshimiwa Spika, kazi zitakazofanyika ni pamoja na kukarabati miundombinu yote iliyopo sasa; kujenga *intake bay* mpya; kujenga miundombinu ya kuondoa tope kabla ya kuchota maji; kujenga kituo kipya cha *pumps* za maji ghafi; kujenga bomba jipya la maji ghafi; kupanua na kuongeza chujio la maji eneo la Mlandizi; kujenga matanki ya kuhifadhi maji; kukarabati na kupanua mfumo wa umeme na kujenga kituo kipya cha *pump* za maji safi.

Mheshimiwa Spika, Mkandarasi alianza kazi tarehe 15 Februari, 2014 na ujenzi unatarajiwa kukamili tarehe 14 Agosti, 2015.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mkandarasi mwingine *Megha Engineering Limited,* pia kutoka India, ameanza kazi ya kulaza bomba jipya la kipenyo cha milimita 1,200; kutoka Mlandizi hadi Kibamba ambapo atajenga tenki lenye ujazo la mita milioni kumi.

Mheshimiwa Spika, pia Mkandarasi huyo atajenga bomba la kipenyo cha milimita 1,000 kutoka tanki la Kibamba hadi katika matenki ya Kimara. Mradi huu umeanza kutekelezwa tarehe 10 Machi, 2014 na unatarajiwa kukamilika tarehe 9 Septemba, 2015 na utagharimu dola za Kimarekani 59.3 milioni. Kazi zote hizi zitakapokamilika uhaba wa maji kwenye maeneo ya Mlandizi, Kibaha, Kiluvya, Mbezi, Kimara, Kibamba, Ubungo na Tabata utakakwisha.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na matukio mengi ya kufululiza kuathiri uzalishaji wa maji katika mtambo wa kusafisha maji wa Ruvu Juu. Matatizo hayo yamehusu kuharibika kwa *pump*, umeme kukatika mara kwa mara na kupasuka kwa mabomba. Wizara imeunda Kamati Maalum ya Watalam ambayo imeanza kufanya tathimini ya kina ili kujua chanzo cha matukio hayo ambayo yamekuwa yakifululiza.

Mheshimiwa Spika, Kamati hiyo, itafanya uchunguzi kubaini kama matatizo hayo yanatokana na mitambo yenyewe, mifumo ya kiufundi, kiuendeshaji au yanaweza kutokana na makosa ya kibinadamu. Kamati inatarajiwa kutoa taarifa yake katika kipindi cha mwezi mmoja na hatua zitaendelea kuchukuliwa ili kuhakikisha kwamba mtambo unarudi katika hali yake ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Katibu!

Taarifa ya Waziri, Mheshimiwa Susan nimekuona unasemaje!

TAARIFA

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nipo katika kuhusu utaratibu, kanuni namba 49(3). Inasomeka hivi: "Waziri mwenye kutoa kauli atawajibika kutoa nakala ya kauli yake kwa Wabunge wote wakati anapowasilisha.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Waziri wa Maji anatoa kauli mpaka anamaliza hakuna nakala iliyowasilishwa kwa maana hiyo, tumeshindwa kabisa kufuatilia na tunajua kwamba tatizo ni kubwa sana, lakini vile vile naomba Mwongozo wako kuhusu kifungu hiki hiki 49(2).

Mheshimiwa Spika, najua kwamba kauli za Mawaziri haziwezi kujadiliwa kama hazitazua mjadala, lakini utakubaliana nami kwamba kauli hii aliyotoa Mheshimiwa Waziri inazua mjadala kwa sababu inatokana na hoja ambayo aliitoa Mheshimiwa Mnyika toka mwaka jana na baadaye ikatolewa kauli na Serikali. Mpaka leo anapozungumza Mheshimiwa Waziri ni kwamba bado tatizo la Maji, Dar-es-Salaam ni kubwa sana na lengo lilikuwa ni kutoa lita 82.

SPIKA: Naomba usijadili, sema nini unachotaka kusema.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kauli hii ya Waziri ipelekwe kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge inayoshughulikia sekta hii ili iweze kujadiliwa kwa sababu bado ina utata mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Ahsante. Nadhani kumekuwa na tatizo katika ofisi yangu, kuna nakala mia nne ambazo zilipaswa ziwe zinasambazwa wakati Waziri anasoma. Wanadai zipo, sasa nataka nijue ofisini kwako zipo wapi? Kwa hiyo, naomba ninyi Makatibu hapo, zile nakala zipatikane.

Ya pili, kwa sababu hotuba ya Waziri wa Maji inakuja, hamwezi kujadili sasa hivi kwa sababu bado inakuja hotuba ya Waziri wa Maji, kwa hiyo, mtajadili. Katibu!

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2013/2014 – Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Ahsante. Mwenyekiti wa Kamati iliyohusika na Wizara hii kwa niaba yake Mheshimiwa! Naomba nakala zilizokuwa zimesomwa na Mwenyekiti zitafutwe na zigawiwe. *(Makofi)*

Taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Bajeti ya 2014/2015 ya Wizara ya Afrika Mashariki kama ilivyosomwa Bungeni

MHE. AMINA NASSORO MAKILAGI (K.n.y. MHE. PROF. PETER M. MSOLLA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI): Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya

Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ilikutana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi tarehe 14 na 15 Mei, 2014. Katika kikao hicho Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi alitoa maelezo kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ikiwa ni pamoja na changamoto za utekelezaji. Aidha, Waziri alitoa maelezo ya malengo na maeneo ya kipaumbele pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2013/2014, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa Serikali. Kwa ujumla wake Kamati haikuridhika na utekelezaji wa miradi mbalimbali. Hali hii imesababishwa na upungufu mkubwa wa fedha pamoja na ucheleweshaji wa fedha kidogo zilizopatikana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto; pamoja na jitihada kubwa zilizofanywa na Wizara katika kutekeleza majukumu yake, Wizara ilikumbana na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa ni kikwazo kikubwa katika kufikia malengo iliyojiwekea. Baadhi ya changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

(1) Wizara kutopata fedha zilizoidhinishwa na Bunge ili kutekeleza majukumu yaliyoainishwa kwenye mpango kazi, pili Uhaba wa maafisa ugani wa mifugo na uvuvi katika Halmashauri ikilinganishwa na mahitaji halisi ya wataalam hao;

(2) Upungufu wa madawa, mbegu bora za mifugo na samaki ikiwa ni pamoja na huduma hafifu ya uhimilishaji *(artificial insemination);*
(3) Kutokutumia fursa zilizopo ili kuuza mazao ya mifugo na uvuvi tuliyonayo;

(4) Ushiriki mdogo wa wadau katika kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya samaki na mazao ya uvuvi; hali hii imechangia kupungua kwa samaki katika maziwa, tano mito na bahari;

(5) Kuenea kwa magonjwa ya mifugo, hususan magonjwa ya milipuko, magonjwa yasiyo na mipaka, magonjwa yanayoenezwa na kupe na mbung'o; na

(6) Kasi ndogo katika kuainisha, kupima na kumilikisha maeneo ya wafugaji kunachangia kwa kiwango kikubwa kuhamahama kwa mifugo na hivyo kusababisha migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha na malengo ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi chini ya Fungu 99, inaomba jumla ya sh. 66,142,627,000/=. Kati ya fedha hizo, sh. 40,952,022,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na sh. 25,190, 605,000/= ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Kati ya fedha za matumizi ya kawaida, sh. 17,984,834,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na sh. 22,998,888,000/= ni kwa ajili ya mishahara. Aidha, kati ya fedha za maendeleo, sh. 23,000,000,000/= ni fedha za ndani na sh.120,000,605,000/= ni fedha za kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, maombi hayo ya fedha yatawezesha Wizara kutekeleza kazi mbalimbali ilizojipangia. Baadhi ya kazi hizo ni kama ifuatavyo:-

(1) Kuendeleza na kuboresha miundombinu ya mifugo na uvuvi na nyanda za malisho;

(2) Kuongeza upatikanaji wa pembejeo na zana za mifugo na uvuvi;
(3) Kuimarisha na kujenga ushirika wa Vyama vya Wafugaji na Wavuvi;

(4) Kutumia fursa za mazao zilizopo na kuongeza thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi;

(5) Kuimarisha uwezo wa taasisi na mifumo ya taarifa kwa ajili ya maendeleo na usimamizi wa sekta za mifugo na uvuvi;

(6) Kuiwezesha Kampuni ya Taifa ya Ranchi *(NARCO)* kuongeza idadi ya mifugo; na

(7) Kujenga mazingira mazuri kwa ajili ya kukuza uwekezaji wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati kwa Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015. Baada ya kueleza kazi zilizopangwa kutekelezwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla; upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo. Utakumbuka kuwa wakati wa Vikao vya Bunge la Bajeti ya mwaka 2013/2014, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, baada ya kujiridhisha kuwa bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi isingekidhi matarajio ya kuboresha huduma muhimu, ilipendekeza na Bunge likapitisha nyongeza ya shilingi bilioni 20 kwenye Fungu la Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Nyongeza hii ilifanya Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa fedha za vyanzo vya ndani kuongezeka kutoka sh. 3,488,270,000 iliyokuwa imetengwa awali hadi sh. 23,488,270,000.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2013/2014, iliyowasilishwa na Wizara mbele ya Kamati, upatikanaji wa fedha za maendeleo za ndani hauridhishi. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2014, hakuna fedha za nyongeza zilizotolewa ambazo Kamati hii iliziomba na kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaihoji Serikali kwa kuweka mikakati ya kufanya Modenaizesheni ya Sekta za Mifugo na Uvuvi kwa lengo la kuzifanya endelevu zenye uzalishaji bora na zinazoendeshwa kibiashara wakati haina nia thabiti ya kutekeleza mikakati hiyo.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi baina ya wakulima, wafugaji, hifadhi na wawekezaji. Migogoro ya ardhi kati ya watumiaji mbalimbali na hususan baina ya wakulima na wafugaji imekuwa sugu na kila siku migogoro mipya inaibuka. Hili ni tatizo ambalo lisipopata ufumbuzi mapema litasababisha maafa makubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri yafuatayo:-

Kitendo cha kutopima ardhi na kubainisha maeneo ya mifugo na matumizi mengine kimekuwa sababu kubwa ya migogoro ya ardhi. Kamati inatoa rai kwa Serikali kuharakisha zoezi hili kwa kulipa kipaumbele ili hatimaye migogoro hii imalizike mapema.

(1) Serikali ifanye tathmini ya maeneo ambayo yamepoteza sifa ya kuwa hifadhi, yapimwe upya na yatangazwe katika gazeti la Serikali ili yatumike kwa ufugaji na kilimo;

(2) Maeneo yatakayotengwa kwa ajili ya mifugo yapatiwe huduma muhimu za malisho, majosho na maji kwa kuchimba mabwawa, visima na malambo;

(3) Serikali itenge maeneo yasiyo na maradhi kwa ajili ya kusafirishia mifugo na mazao yake nje ya nchi; na

(4) Serikali ione umuhimu wa kusimamia Sheria namba 12 ya 2010 ya utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Uhaba wa Wataalam; tatizo la kutokuwa na wataalam wa kutosha katika sekta hii limeendelea kuathiri mchango wake katika Pato la Taifa. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuajiri wataalam wa kutosha ukizingatia kwamba wahitimu wengi wako sokoni.

Mheshimiwa Spika, Taasisi za Utafiti; Taasisi za Utafiti ni muhimu sana katika kuongeza tija katika uzalishaji na utoaji huduma ndani ya jamii. Kamati imebaini kuwa wataalam wengi kwenye Vituo vya Utafiti nchini ni wenye umri mkubwa ambao wamekaribia kustaafu. Kamati inaishauri Serikali kuandaa wataalam watakaochukua nafasi za watakaostaafu, na iendelee kuongeza bajeti kwa taasisi hizi ili ziweze kutekeleza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, Ruzuku ya Mifugo na Uvuvi; pamoja na kwamba Serikali inatoa ruzuku kwa Sekta hii ya Mifugo; Kamati imebaini kuwa wananchi wengi hasa walengwa wa ruzuku hii hawana elimu au taarifa juu ya uwepo wake. Kamati inaishauri Serikali kutoa elimu na kuhakikisha walengwa wanapata ruzuku. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kutoa ruzuku katika sekta ya uvuvi ikiwa ni pamoja na zana za uvuvi.

Mheshimia Spika, mgawanyo wa madaraka; Miradi mingi ya ufugaji na uvuvi ipo kwenye Halmashauri ambazo ndizo mamlaka za utekelezaji, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuimarisha mahusiano ya kikazi kati ya Wizara na TAMISEMI kwa maana ya Halmashauri ili kuleta ufanisi zaidi wa kazi katika kutekeleza miradi hiyo. Aidha, Sekta za Mifugo na Uvuvi pamoja na wataalam wake walioko katika Halmashauri zitenganishwe badala ya utaratibu wa sasa wa kuunganisha Idara hii pamoja na Idara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mifugo, Minada na Masoko ya Mipakani; kwa muda mrefu sasa tumekuwa na minada maeneo ya mipakani ambayo haitumiki kikamilifu. Kamati inatoa ushauri ufuatao kwa Serikali;

(a) Minada hii iboreshwe kwa kuwa na usimamizi mzuri;

(b) Mifugo iuzwe kwa kutumia mizani badala ya kuuza kwa kuitazama mifugo ambapo thamani halisi haipatikani; na

(c) Serikali ijenge machinjio maeneo ya mipakani ili kuweza kutoa ushindani kwa nchi jirani ambazo wana machinjio na hivyo hununua mifugo nchini kwetu kwa bei ndogo na kuchinja na baadaye kuja kuiuza nchini kwetu kwa bei kubwa hasa katika mahoteli.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ngozi; ngozi ni zao ambalo likitumiwa vizuri linaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika pato la Taifa. Ngozi za mifugo bado hazichangii ipasavyo ikilinganishwa na idadi ya mifugo tuliyonayo. Hii inatokana na ngozi kutokuwa na ubora unaokidhi viwango, kutokuwa na Viwanda vya Kusindika Ngozi hapa nchini, utoroshaji wa ngozi ghafi na ukosefu wa wataalam wa ngozi. Kamati inashauri Serikali kama ifuatavyo:-

(a) Elimu zaidi iendelee erikali itenge maeneo yasiyo na maradhi kwa ajili ya kusafirishia mifugo na mazao yake nje ya nchi; na

(b) Ili kukuza soko la ngozi nchini, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ijenge Viwanda vya Kuongeza Thamani ya Bidhaa za Ngozi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wafugaji; Sekta ya Mifugo imekuwa haipewi umuhimu stahiki katika bajeti ya Serikali kiasi kwamba miradi mingi ya sekta hii haitekelezwi. Kutokana na hali hii, Kamati inashauri Serikali kama yafuatayo:-

(i) Sekta hii iongezewe fedha ili kukidhi haja ya kuipatia mifugo mahitaji muhimu kama majosho, malisho na maji kwa njia ya malambo, mabwawa na visima.
(ii) Ranchi za Taifa ambazo walipewa Wawekezaji wakashindwa kuziendeleza zigawiwe kwa wafugaji wazalendo watakaoweza kuendeleza maeneo hayo;

(iii) Serikali iendelee kutoa elimu ya ufugaji wa kitaalam ili kuongeza thamani yake kabla ya kwenda sokoni; na

(iv) Elimu kuhusu umuhimu wa uvunaji wa mifugo itolewe ili kuongeza pato la mfugaji na la Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uvuvi; Uvuvi ni Sekta muhimu katika nchi hii kutokana na mchango wake mkubwa katika kuwapatia wananchi ajira, lishe, kipato na kuingizia nchi fedha za kigeni. Aidha, ufugaji wa samaki katika mabwawa haujatiliwa mkazo wa kutosha licha ya kwamba hii ni fursa nzuri ya lishe bora, kipato na ajira kwa wananchi. Pamoja na umuhimu wake, bado sekta hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali. Kamati inashauri kuwepo na mikakati maalum ya kukabiliana nazo.

Mheshimiwa Spika, ufugaji wa samaki kwenye mabwawa; Kamati inaishauri Serikali itenge na kutoa bajeti ya kutosha ili kutoa elimu kwa wafugaji, kuajiri wataalam wa kutosha na kuhamasisha vikundi mbalimbali vipate mikopo kutoka katika taasisi mbalimbali za fedha ikiwemo na Benki ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, Uvuvi Haramu; kwa muda mrefu sasa Kamati imekuwa ikitoa ushauri wa namna ya kupambana na uvuvi haramu. Ushauri huu haujatekelezwa kwa kuwa Serikali haijatenga bajeti ya kutosha. Ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kutokomeza uvuvi haramu kwa vitendo. Aidha, Serikali ifanye juhudi za makusudi kulinusuru Ziwa Tanganyika ambalo kina chake kinazidi kupungua.

Mheshimiwa Spika, Msimu wa Uvuvi; kama taratibu za uwindaji wa wanyama pori unavyozingatia msimu wa kuwinda na ule wa kuzaliana, ni dhahiri kuwa hata kwenye uvuvi

kuna msimu wa kuvuna na ule wa kuzaliana. Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu wa msimu wa kuvua samaki na hivyo kusitisha uvuvi wa samaki wa kibiashara kwa msimu huo.

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Uvuvi wa Kina kirefu; Bandari ya uvuvi ni muhimu sana kwa uboreshaji wa sekta hii. Manufaa ya bandari hii yatakuwa ni pamoja na kupata takwimu sahihi za uvuvi katika bandari Kuu ili wavuvi hao waweze kulipa ushuru unaostahiki. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha uanzishwaji wa bandari hii kwa kuweka Kanuni madhubuti za kuifanya iwe ya manufaa makubwa kwa jamii na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Uvuvi wa kina kirefu ukitiliwa mkazo, una manufaa makubwa kwa uchumi wa nchi yetu. Mavuno yanayopatikana kwenye uvuvi huu ni makubwa kuliko kiasi kinachoripotiwa. Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati madhubuti ili mavuno yanayopatikana yadhibitiwe na faida iweze kuonekana badala ya wachache kunufaika na uvuvi wa kina kirefu.

Mheshimiwa Spika, Wawekezaji katika sekta ya Uvuvi; Kamati inatambua kuwa ili sekta ya uvuvi ikue kwa kiwango cha kuridhisha na kuchangia kukua kwa pato la Taifa ni lazima kuwepo na uwekezaji wa kutosha. Kamati inaishauri Serikali iweke programu maalum na mipango mizuri ya kuwavutia wawekezaji wakubwa watakaofanya uvuvi wa kibiashara na kujenga Viwanda vya Kusindika Samaki.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa nafasi hii ili kuwasilisha Taarifa ya Kamati. Napenda pia kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo:-

SPIKA: Hakuna *time* ya kuwatambua.

MHE. AMINA A. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wachukuliwe kwenye *Hansard* kama walivyoorodheshwa katika ukurasa wa 22 mpaka ukurasa wa 23.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati napenda kuwapongeza Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani na Naibu Waziri, Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, kwa ushirikiano wao mzuri waliyoipa Kamati katika kipindi chote hiki.

Mheshimiwa Spika, aidha, nampongeza Katibu Mkuu Dkt. Charles Nyamrunda na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Yohana Budeba pamoja na wataalam wote wa Wizara kwa ushirikiano wao wakati wa kujadili na kuchambua bajeti ya Wizara kwa mwaka huu wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika…

SPIKA: Ahsante. Kengele imegonga. Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naomba yanukuliwe katika *Hansard* kama yanavyoonekana kuanzia ukurasa wa 24 mpaka 25.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Kengele ikigonga imegongwa.

Taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Bajeti ya 2014/2015 ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kama ilivyowasilishwa Mezani

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA FEDHA 2014/2015

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ilikutana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi tarehe 14 na 15 Mei, 2014. Katika kikao hicho Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi alitoa maelezo kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ikiwa ni pamoja na changamoto za utekelezaji. Aidha, Waziri alitoa maelezo ya malengo na maeneo ya kipaumbele pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

2.0 UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mheshimiwa Spika, wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2013/2014, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa Serikali. Kwa ujumla Kamati haikuridhika na utekelezaji wa miradi mbalimbali. Hali hii imesababishwa na upungufu mkubwa wa fedha pamoja na ucheleweshaji wa fedha kidogo zinazopatikana.

3.0 CHANGAMOTO

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada kubwa zilizofanywa na Wizara katika kutekeleza majukumu yake, Wizara ilikumbana na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa ni kikwazo kikubwa katika kufikia malengo iliyojiwekea. Baadhi ya changamoto hizo ni:-
Wizara kutopata fedha zilizoidhinishwa na Bunge ili kutekeleza majukumu yaliyoanishwa kwenye mpango kazi,

- Uhaba wa maafisa ugani wa mifugo na uvuvi katika Halmashauri ikilinganishwa na mahitaji halisi ya wataalam hao,

- Upungufu wa madawa, mbegu bora za mifugo na samaki ikiwa ni pamoja na huduma hafifu ya uhimilishaji *(artificial insemination),*

- Kutokutumia fursa zilizopo ili kuuza mazao ya mifugo na uvuvi tuliyonayo,

- Ushiriki mdogo wa wadau katika kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya samaki na mazao ya uvuvi; hali hii imechangia kupungua kwa samaki katika maziwa, mito na bahari,

- Kuenea kwa magonjwa ya mifugo, hususan magonjwa ya milipuko, magonjwa yasiyo na mipaka, magonjwa yanayoenezwa na kupe na mbung'o, na

- Kasi ndogo katika kuainisha, kupima na kumilikisha maeneo ya wafugaji kunachangia kwa kiwango kikubwa kuhamahama kwa mifugo na hivyo kusababisha migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

4.0 MAOMBI YA FEDHA NA MALENGO YA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi chini ya **Fungu 99,** inaomba jumla ya **shilingi 66,142,627,000/=**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 40,952,022,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 25,190, 605,000/=** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Kati ya fedha za matumizi ya kawaida, **shilingi 17,984,834,000/=** ni kwa ajili ya matumuzi mengineyo (OC) na **shilingi 22,968,188,000/=** ni kwa ajili ya mishahara (PE) ya Wizara. Aidha, kati ya fedha za maendeleo, **shilingi 23,000,000,000/=** ni fedha za ndani na shilingi **2,190,605,000/=** ni fedha kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, maombi hayo ya fedha yatawezesha Wizara kutekeleza kazi mbalimbali ilizojipangia. Baadhi ya kazi hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuendeleza na kuboresha miundombinu ya mifugo na uvuvi na nyanda za malisho,

(ii) Kuongeza upatikanaji wa pembejeo na zana za mifugo na uvuvi,

(iii) Kuimarisha na kujenga ushirika wa vyama vya wafugaji na wavuvi,

(iv) Kutumia fursa za mazao zilizopo na kuongeza thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi,

(v) Kuimarisha uwezo wa taasisi na mifumo ya taarifa kwa ajili ya maendeleo na usimamizi wa sekta za mifugo na uvuvi,

(vi) Kuiwezesha Kampuni ya Taifa ya ranchi (NARCO) kuongeza idadi ya mifugo, na

(vii) Kujenga mazingira mazuri kwa ajili ya kukuza uwekezaji wa sekta binafsi.

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2014/2015

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza kazi zilizopangwa kutekelezwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:

(a) Maoni ya Jumla

(i) Upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kuwa wakati wa Vikao vya Bunge la Bajeti ya mwaka 2013/2014, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, baada ya kujiridhisha kuwa bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi isingekidhi matarajio ya kuboresha huduma muhimu, ilipendekeza na Bunge likapitisha nyongeza ya **shilingi bilioni 20.0** kwenye fungu la Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Nyongeza hii ilifanya Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa fedha za vyanzo vya ndani kuongezeka kutoka **shilingi 3,488,270,000** iliyokuwa imetengwa awali hadi **shilingi 23,488,270,000.**

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2013/2014 iliyowasilishwa na Wizara mbele ya Kamati, upatikanaji wa fedha za maendeleo za ndani hauridhishi. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2014, hakuna fedha za nyongeza zilizotolewa ambazo Kamati hii iliziomba na kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa kwa kutokupatikana fedha hizo hadi sasa! Kamati inaihoji Serikali kwa kuweka mikakati ya kufanya Modenaizesheni ya Sekta za Mifugo na Uvuvi kwa lengo la kuzifanya endelevu zenye uzalishaji bora na zinazoendeshwa kibiashara wakati haina nia thabiti ya kutekeleza mikakati hiyo.

(ii) Migogoro ya ardhi baina ya wakulima, wafugaji, hifadhi na wawekezaji:

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi kati ya watumiaji mbalimbali na hususan baina ya wakulima na wafugaji imekuwa sugu na kila siku migogoro mipya inaibuka. Hili ni tatizo ambalo lisipopata ufumbuzi mapema litasababisha maafa makubwa zaidi.

Kamati inashauri yafuatayo:-

- Kitendo cha kutopima ardhi na kubainisha maeneo ya mifugo na matumizi mengine kimekuwa sababu kubwa ya migogoro ya ardhi. Kamati inatoa rai kwa Serikali kuharakisha zoezi hili kwa kulipa kipaumbele ili hatimae migogoro hii imalizike,

- Serikali ifanye tathmini ya maeneo ambayo yamepoteza sifa ya kuwa hifadhi, yapimwe upya na yatangazwe katika gazeti la Serikali ili yatumike kwa ufugaji na kilimo,
- Maeneo yatakayotengwa kwa ajili ya mifugo yapatiwe huduma muhimu za malisho, majosho na maji kwa kuchimba mabwawa, visima na malambo,

- Serikali itenge maeneo yasiyo na maradhi (*Disease Free zones*) kwa ajili ya kusafirishia mifugo na mazao yake nje ya nchi, na

- Serikali ione umuhimu wa kusimamia Sheria namba 12 ya 2010 ya utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo.

(iii) Uhaba wa Wataalam

Mheshimiwa Spika, tatizo la kutokuwa na wataalamu wa kutosha katika sekta hii limeendelea kuathiri mchango wake katika Pato la Taifa. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuajiri wataalam wa kutosha ukizingatia kwamba wahitimu wengi wako sokoni.

(iv) Taasisi za Utafiti

Mheshimiwa Spika, Taasisi za Utafiti ni muhimu sana katika kuongeza tija katika uzalishaji na utoaji huduma ndani ya jamii. Kamati imebaini kuwa wataalam wengi kwenye vituo vya utafiti nchini ni wenye umri mkubwa ambao wamekaribia kustaafu. Kamati inashauri Serikali:-

- Kuandaa wataalam watakaochukua nafasi za watakaostaafu, na

- Iendelee kuongeza bajeti kwa taasisi hizi ili ziweze kutekeleza wajibu wake.

(v) Ruzuku ya Mifugo na Uvuvi

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba serikali inatoa ruzuku kwa sekta hii ya mifugo, Kamati imebaini kuwa wananchi wengi hasa walengwa wa ruzuku hii hawana elimu au taarifa juu ya uwepo wake. Kamati inaishauri Serikali kutoa elimu na kuhakikisha walengwa wanapata ruzuku. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kutoa ruzuku katika sekta ya uvuvi ikiwa ni pamoja na zana za uvuvi.

(vi) Mgawanyo wa madaraka

Mheshimiwa Spika, miradi mingi ya ufugaji na uvuvi ipo kwenye Halmashauri ambazo ndizo mamlaka za utekelezaji, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuimarisha mahusiano ya kikazi kati ya Wizara na TAMISEMI (Halmashauri) ili kuleta ufanisi zaidi wa kazi katika kutekeleza miradi hiyo. Aidha, sekta za mifugo na uvuvi pamoja na wataalam wake walioko katika halmashauri zitenganishwe badala ya utaratibu wa sasa wa kuunganishwa na idara ya kilimo.

(b) Sekta ya Mifugo

(i) Minada na Masoko ya Mipakani

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa tumekuwa na minada maeneo ya mipakani ambayo haitumiki kikamilifu. Kamati inatoa ushauri ufuatao kwa Serikali:-

- Minada hii iboreshwe kwa kuwa na usimamizi mzuri,

- Mifugo iuzwe kwa kutumia mizani badala ya kuuza kwa kuitazama ambapo thamani halisi haipatikani, na

- Serikali ijenge machinjio maeneo ya mipakani ili kuweza kutoa ushindani kwa nchi jirani ambazo wana machinjio na hivyo hununua mifugo nchini kwa bei ndogo na kuchinja na baadae kuja kuiuza nchini kama nyama kwa bei kubwa zaidi.

(ii) Ngozi

Mheshimiwa Spika, Ngozi ni zao ambalo likitumiwa vizuri linaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika pato la Taifa. Ngozi za mifugo bado hazichangii ipasavyo ikilinganishwa na idadi ya mifugo tuliyonayo. Hii inatokana na ngozi kutokuwa na ubora unaokidhi viwango, kutokuwa na viwanda vya kusindika ngozi hapa nchini, utoroshaji wa ngozi ghafi na ukosefu wa wataalam wa ngozi. Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Elimu zaidi iendelee kutolewa kwa wafugaji kuhusu umuhimu wa kutunza mifugo yao.

b) Ili kukuza soko la ngozi nchini, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ijenge viwanda vya kuongeza thamani ya bidhaa za ngozi.

(a) Wafugaji

Mheshimiwa Spika, sekta ya mifugo imekuwa haipewi umuhimu stahiki katika bajeti ya Serikali kiasi kwamba miradi mingi ya sekta hii haitekelezwi. Kutokana na hali hii, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Sekta hii iongezewe fedha ili kukidhi haja ya kuipatia mifugo mahitaji muhimu kama majosho, malisho na maji kwa njia ya malambo, mabwawa na visima

(ii) Ranchi za taifa ambazo walipewa wawekezaji wakashindwa kuziendeleza zigawiwe kwa wafugaji wazalendo watakaoweza kuendeleza maeneo hayo,

(iii) Serikali iendelee kutoa elimu juu ya ufugaji wa kitaalam ili kuongeza thamani yake kabla ya kwenda sokoni, na

(iv) Elimu kuhusu umuhimu wa uvunaji wa mifugo itolewe ili kuongeza pato la mfugaji na la Taifa kwa ujumla.

(c) Sekta ya Uvuvi

Mheshimiwa Spika, Uvuvi ni sekta muhimu katika nchi hii kutokana na mchango wake mkubwa katika kuwapatia wananchi ajira, lishe, kipato na kuingizia nchi fedha za kigeni. Aidha ufugaji wa samaki katika mabwawa (aquaculture) haujatiliwa mkazo wa kutosha licha ya kwamba hii ni fursa nzuri ya lishe bora, kipato na ajira kwa wananchi. Pamoja na umuhimu wake, bado sekta hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali. Kamati inashauri kuwepo na mikakati maalum ya kukabiliana nazo.

(i) Ufugaji wa samaki kwenye mabwawa

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali itenge na kutoa bajeti ya kutosha ili kutoa elimu kwa wavuvi, kuajiri wataalam wa kutosha na kuhamasisha vikundi vipate mikopo kutoka taasisi za fedha kama vile benki ya kilimo.

(ii) Uvuvi Haramu

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa Kamati imekuwa ikitoa ushauri wa namna ya kupambana na uvuvi haramu. Ushauri huu haujatekelezwa kwa kuwa Serikali haijatenga bajeti ya kutosha. Ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kutokomeza uvuvi haramu kwa vitendo. Aidha, Serikali ifanye juhudi za makusudi kulinusuru Ziwa Tanganyika ambalo kina chake kinazidi kupungua.

(iii) Msimu wa Uvuvi

Mheshimiwa Spika, kama taratibu za uwindaji wa wanyama pori unavyozingatia msimu wa kuwinda na ule wa kuzaliana, ni dhairi kuwa hata kwenye uvuvi kuna msimu wa kuvuna na ule wa kuzaliana. Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu wa msimu wa kuvua samaki na hivyo kusitisha uvuvi wa samaki wa biashara kwa msimu huo.

(iv) Bandari ya Uvuvi na Uvuvi wa Kina kirefu *(Deep Sea Fishing)*

Mheshimiwa Spika, Bandari ya uvuvi ni muhimu sana kwa uboreshaji wa sekta hii. Manufaa ya bandari hii yatakuwa ni pamoja na kupata takwimu sahihi za uvuvi katika bahari kuu ili wavuvi hao waweze kulipa ushuru stahiki. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha uanzishwaji wa bandari hii kwa kuweka Kanuni madhubuti za kuifanya iwe ya manufaa makubwa kwa jamii na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Uvuvi wa kina kirefu ukitiliwa mkazo una manufaa makubwa kwa uchumi wa nchi yetu. Mavuno yanayopatikana kwenye uvuvi huu ni makubwa kuliko kiasi kinachoripotiwa. Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati madhubuti ili Mavuno yanayopatikana yadhibitiwe na faida iweze kuonekana badala ya wachache kunufaika.

(v) Wawekezaji katika sekta ya uvuvi

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa ili sekta ya uvuvi ikue kwa kiwango cha kuridhisha na kuchangia kukua kwa pato la taifa ni lazima kuwepo na uwekezaji wa kutosha. Kamati inaishauri Serikali iweke programu na mipango mizuri ya kuwavutia wawekezaji wakubwa watakaofanya uvuvi wa kibiashara *(Large Scale Fishing)* na kujenga viwanda vya kusindika samaki.

7.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa nafasi hii ili kuwasilisha Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Napenda kuwatambua wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Prof. Peter Mahamudu Msolla, Mb- Mwenyekiti
2. Mhe. Said J. Nkumba, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe Prof. David Homeli Mwakyusa, Mb - Mjumbe

4. Mhe. Subira Mgalu, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Asaa Othman Hamad, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Abdusalaam S. Ameir, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Abdalla Haji Ali, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Namelok E. M. Sokoine, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Dr. Christine G. Ishengoma, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Sylvestry Francis Koka, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Moshi S. Kakoso, Mb - Mjumbe
12. Mhe.Kheri Khatib Ameir, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Meshack jeremia opulukwa, Mb- Mjumbe
14. Mhe. Philemon Kiwelu Ndesamburo, Mb- Mjumbe
15. Mhe. Sadifa Juma Khamis, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Amina Nassoro Makilagi, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Donald Kelvin Max, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Magdalena Hamisi Sakaya, Mb- Mjumbe
20. Mhe. Haji Juma Sereweji, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Jitu VRAJLAL Soni, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Dkt Lucy Sawere Nkya, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati napenda kuwapongeza Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mhe. Dkt. Titus Mlengeya Kamani (Mb), na Naibu Waziri, Mhe. Kaika Saning'o Telele (Mb), kwa ushirikiano wao mzuri waliyoipa Kamati katika kipindi chote hiki. Aidha, nampongeza Katibu Mkuu Dkt. Charles Nyamrunda na Naibu Katibu mkuu Dkt. Yohana Budeba pamoja na wataalam wote wa Wizara kwa ushirikiano wao wakati wa kujadili na kuchambua bajeti ya Wizara kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah na Makatibu wa Kamati Ndugu Elieka Saanya na Ndugu Angelina Sanga kwa kuiwezesha Kamati kufanikisha shughuli zake na kuratibu taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge lako Tukufu likubali na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, **Fungu 99** jumla ya **shilingi 66,142,627,000/=** kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha.

KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI
22 Mei, 2014

SPIKA: Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Rose Kamili!

Taarifa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya 2014/2015 ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kama ilivyosomwa Bungeni

HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI MHESHIMIWA ROSE KAMILI SUKUM (MB), WIZARA YA MIFUGO NA MAENDELEO YA UVUVI, KUHUSU MAPITIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

(Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9), ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2013)

MHE. ROSE K. SUKUM - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa hii kuja kuiwasilisha hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu kwa kunipa uzima na nguvu kuweza kusimama mbele ya Bunge hili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Aidha, namshukuru Kiongozi wa Upinzani Bungeni kwa kuniteua mimi na Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwaga kuwa Wasemaji Wakuu wa Wizara hii. Kwa umuhimu wa pekee nimshukuru Mheshimiwa Mkiwa kwa ushirikiano wake mkubwa katika maandalizi ya hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, naomba hotuba hii iingizwe kwenye *hansard* kama ilivyowasilishwa mezani kwani ni kubwa sana nami nitasoma kwa ufupi.

Mheshimiwa Spika, utangulizi; Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 494 (a) la tarehe 17 Desemba, 2010 imepewa majukumu yafuatayo:-

(i) Kutayarisha, kufanya mapitio na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, mipango na mikakati ya kuendeleza sekta ya mifugo na uvuvi;
(ii) Kupanga na kusimamia matumizi ya ardhi kwa ajili ya mifugo;

(iii) Kuendeleza na kusimamia uendelezaji wa miundombinu ya mifugo na uvuvi;

(iv) Kusimamia uendelezaji wa mazao yatokanayo na mifugo na uvuvi;

(v) Kuendeleza ufugaji wa samaki; na

(vi) Kudhibiti magonjwa ya mifugo pamoja na wadudu wanaoeneza magonjwa hayo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, aidha, dira kuu ni kuhakikisha kuwa rasilimali za mifugo na uvuvi zinaendelezwa na kutunzwa katika mazingira endelevu kwa ajili ya ukuaji wa uchumi na kuboresha maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kabla sijafanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015, sekta kwa sekta; Idara za Wizara na Taasisi zake, nikumbushe kwamba mwaka 2013 ulikuwa mwaka wa msiba kwa wafugaji na leo tunatoa tanga.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013 ni mwaka ambao Taifa lilishuhudia mauaji ya wafugaji na wakulima kwa kile kilichoelezwa kwamba ni migogoro ya ardhi. Aidha, nchi ilishuhudia mauaji ya wafugaji na mifugo yao kwa kile kilichoelezwa kwamba ni migogoro baina ya wafugaji na hifadhi.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya hali hizo ni Bunge kukabidhi majukumu kwa Kamati zake za Kudumu kushughulikia masuala yenye kugusa mustakabali wa sekta ya mifugo nchini. Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ilifanya uchunguzi kuhusu "Operesheni Tokomeza" na ripoti yake ilisomwa Bungeni na kusababisha Mawaziri wanne kuwajibishwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kuondolewa kwa Mawaziri pekee bila utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati yenye kugusa moja kwa moja wafugaji na hatma ya mifugo, ni udhaifu mkubwa kwa upande wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, hatua ya Rais kuunda Tume haipaswi kutumika kama kisingizio kwa Serikali kuacha kutoa taarifa Bungeni juu ya mapendekezo yote ambayo hayahitaji kusubiri mpaka Tume kukamilisha kazi yake. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali katika majumuisho itoe majibu juu ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati na Maazimio ya Bunge yaliyohusu mifugo na wafugaji.

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawahimiza Wabunge katika kufanya mapitio ya utekelezaji na kujadili makadirio ya Wizara hii wafanye rejea katika taarifa ya "Operesheni Tokomeza" iliyowasilishwa Bungeni na Maazimio kupitishwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inalikumbusha Bunge hili kuwa mwaka 2013 iliundwa Kamati iliyohusisha Wajumbe kutoka Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji na Wajumbe kutoka Kamati zingine, ilipewa kazi ya kwenda kuchunguza migogoro ya ardhi baina ya wakulima, wafugaji, hifadhi na wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mpaka sasa Kamati tajwa ya Bunge haijawasilisha Bungeni matokeo ya uchunguzi huo hali ambayo inafanya Bunge kujadili mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo, bila kuwa na taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka maelezo yatolewe Bungeni ni kwa nini taarifa ya Kamati hiyo haijawasilishwa mpaka hivi sasa?

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kabla ya kuendelea na mjadala juu ya Wizara hii ya Mifugo, taarifa ya Kamati husika iwasilishwe mezani ili Wabunge waweze kuitumia kama rejea katika kuchukua hatua za kuboresha sekta ya mifugo nchini ili kuepusha migogoro baina ya Wafugaji na Wakulima, Hifadhi na Wawekezaji inayoendelea nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi yangu ya Uwaziri Kivuli wa Wizara hii, nilitaka kushiriki kuihoji Serikali juu ya masuala ya kuanzia kwenye Kamati. Hata hivyo nilizuiwa na Mwenyekiti wa Kamati husika kushiriki vikao vya Kamati hali ambayo inaacha maswali kuhusu ushirika wa siri baina ya Mwenyekiti wa Kamati na Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, nitumie fursa hii kueleza kilio cha wafugaji kuhusiana na ushuru wa mifugo. Ushuru wa mifugo kwa muda mrefu umekuwa kero kwa wafugaji, wafanyabiashara na Halmashauri kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ushuru umekuwa ukitozwa bila utaratibu maalum ambapo baadhi yao hutumia Watendaji wa Vijiji, Kata na Mawakala, hali inayosababisha kero kwa wafugaji na wanunuzi wa mifugo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufuta ushuru huo kwani haimnufaishi mfugaji. Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa imeeleza wazi kuwa asilimia 10 ya makusanyo ya ushuru utumike kuhudumia mifugo ikiwa ni pamoja na kununulia madawa ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Bajeti; kwa mwaka wa fedha, 2012/2013, Wizara ilikuwa imetengewa jumla ya shilingi bilioni 54 na kwa mwaka wa fedha 2013/2014 zilitengwa jumla ya shilingi bilioni 67.18.

Mheshimiwa Spika, Randama ya Wizara inaonesha kuwa hadi mwezi Aprili, 2014, fedha za ndani kwa ajili ya maendeleo zilipokelewa jumla ya shilingi bilioni 2.3 tu, kati ya shilingi bilioni 23.5, sawa na asilimia 9.7 tu ya fedha za ndani. Hoja ni kwa vipi tunaweza kutekeleza mipango kwa fedha hizo wakati ilikadiriwa kutumia shilingi bilioni 23.5. Kambi Rasmi inaomba maelezo ya hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara inaomba Bunge liidhinishe jumla ya shilingi bilioni 66.14 ili iweze kutekeleza majukumu yake kama yalivyopitishwa na Tume ya Mipango. Kati ya fedha hizo, fedha za maendeleo ni shilingi bilioni 25.190. Aidha, fedha za ndani kwa ajili ya maendeleo ni shilingi bilioni 23 na fedha za nje ni shilingi bilioni 2.19. Pia kila Idara imetengewa kasma yake kwa matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeomba jumla ya shilingi bilioni 40.95 kama fedha za matumizi ya kawaida, kati ya fedha hizo mishahara ni shilingi bilioni 22.97 na matumizi mengine ni shilingi bilioni 17.98. Aidha, katika matumizi mengineyo *(OC)* kila idara imetengewa kasma yake.

Mheshimiwa Spika, jambo la kushangaza, katika kupitia Randama inaonesha kuwa, kwa fedha za maendeleo Kifungu 1003 - Idara ya Sera na mipango, kasma zifuatazo zitatekelezwa kwa fedha za maendeleo:-

Kasma 220100- Ununuzi wa shajala, kulipia gharama za kurudufu *program* za kompyuta, jumla ni shilingi milioni 59. Naomba Wabunge muangalie matumizi ya Kawaida ukurasa wa 122, kasma hiyo hiyo inaonesha zinaombwa shilingi milioni 85.3. Kambi Rasmi inaitaka Serikali kutoa maelezo kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kasma: 220300 ununuzi wa *Fuel, Oils, Lubricants,* jumla shilingi milioni 176. Kasma: 220700 – Gharama za kukodi kumbi za kufanyia mikutano na semina, jumla shilingi milioni 12. Kasma: 221000, Gharama za usafiri ndani ya nchi na posho ya kujikimu kwa Watumishi wa Idara, jumla shilingi milioni 212. Aidha, katika matumizi ya kawaida idara hiyo na kasma hiyo hiyo imetenga jumla ya shilingi milioni 104.6. Hapa maana yake ni kwamba idara hiyo na kasma hiyo imetengewa jumla ya shilingi milioni 316.6 za *OC* kwa kutumia hela za maendeleo shilingi milioni 212. Huu ni wizi.

Mheshimiwa Spika, ukifanya ulinganisho wa bajeti inayotengwa kwa ajili ya kuimarisha huduma za mifugo au uvuvi, utaona ni kwa kiwango gani Serikali isivyokuwa na nia ya kweli ya kuinua sekta hii.

Mheshimiwa Spika, hapa tunatoa hela na hivyo tarakimu ni muhimu kuliko maneno ambayo miaka yote ndiyo yanairudisha nyuma sekta. Kama ni tarakimu ndio hizo tulizoletewa na kupitishwa na Kamati ya Bunge lako, je, si tutachekwa kama watu watapitia randama hii? Hii ni aibu kubwa kama Bunge lako Tukufu litapitisha bajeti hii ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa kutumia hela za maendeleo kama *OC*.

Mheshimiwa Spika, aidha, jumla ya shilingi milioni 58.45 katika kasma 410700 zilitumika kama *OC* kwa kugharamia utayarishaji wa ripoti na nyaraka wakati fedha hizo zilikuwa ni za maendeleo. Kambi Rasmi ya Upinzani imeona jumla ya shilingi milioni 517.45 za Maendeleo zinatumika kama *OC*, wakati huo huo Idara hii kwa matumizi mengine imetengewa jumla ya shilingi milioni 736.73. Angalieni kwenye Randama ukurasa wa 90.

Mheshimiwa Spika, kwa maana nyingine ni kwamba kwa idara hii Sera na Mipango fedha za matumizi mengineyo ni bilioni 1.3 kwa kuwa shilingi (milioni 517.45 ilitumika kama *OC* badala ya maendeleo. Jambo hilo linasababisha kupungua kwa fedha za maendeleo kutoka shilingi bilioni 1.3 hadi shilingi milioni 834.5 tu jambo ambalo litaathiri sana maendeleo katika Idara hii. Tazama mchanganuo kwenye Randama ukurasa wa 156 mpaka ukurasa wa 166.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika Idara ya utafiti, mafunzo na ugani, Kifungu 1004, fedha za maendeleo zimetengwa kutumika kama matumizi mengineyo ya *OC* wakati kifungu hiki kimeshatengewa fedha za matumizi mengineyo *OC*.

Mheshimiwa Spika, Kasma zifuatazo zinaonyesha jinsi ambavyo fedha za maendeleo zinavyotumika vibaya:-

(1) Kasma: 270600, kwa ajili ya vitabu, shajala, majarida, vifaa vya kompyuta, kurudufu na kulipia gharama za kurudufia. Jumla shilingi milioni 37.5.

(2) Kasma: 220200 - Kulipia umeme na maji, jumla shilingi milioni 74.23. Kasma hiyo hiyo matumizi ya kawaida imetengewa jumla ya shilingi milioni sita.

(3) Kasma: 220300, manunuzi ya mafuta ya magari ya idara, jumla shilingi milioni 60.7. Pia kasma kwa upande wa matumizi ya kawaida imetengewa jumla ya shilingi milioni 49.93.

(4) Kasma: 220600, kununua vifaa, mavazi na viatu vya kinga kwa watumishi wa idara, jumla shilingi milioni 5.15.

(5) Kasma: 221000, Gharama za usafiri, fedha za kujikimu kwa viongozi na watumishi wa idara wanaposafiri kikazi ndani ya nchi, jumla shilingi milioni 113.95.

(6) Kasma: 221200, Gharama za matangazo na machapisho ya idara, jumla shilingi milioni 12.

(7) Kasma: 221400: Chai na viburudisho wakati wa mafunzo na mikutano ya Idara, jumla shilingi milioni tatu.

(8) Kasma: 410600, ununuzi wa samani, jumla shilingi milioni 39.

(9) Kasma: 410600, ununuzi wa kompyuta, mashine za kurudufu, printa na skana, jumla shilingi milioni 35.

Mheshimiwa Spika, matumizi hayo ambayo jumla yake ni shilingi milioni 380.23. Si matumizi mengine, bali ni ya maendeleo kwani Idara hii imetengewa jumla ya shilingi bilioni 4.65 kwa matumizi mengine. Hii inaonesha kwamba kuna *double allocation* kwa matumizi yale yale.

Mheshimiwa Spika, hizi idara mbili ambazo Kambi Rasmi imezipitia ni kwamba, vifungu hivyo hivyo kwa matumizi ya kawaida vimetengewa fedha na kwa upande wa fedha za maendeleo vimetengewa fedha pia kwa matumizi yale yale.

Mheshimiwa Spika, hoja hapa ni kwamba, ina maana kwamba Watendaji wa Idara hawawezi kutenganisha kati ya fedha za maendeleo na matumizi mengineyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inashindwa kuamini kama kweli Kamati ya Bunge inayoongozwa na Mhe Profesa, pia imeshindwa kuona fedha hizi ambazo zimewekwa maeneo yasiyostahili kwa matumizi hayo, kwani tayari yalikwisha kuwekwa katika bajeti ya matumizi mengineyo *(OC)* ya bilioni 17.

Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji ni kwa nini fedha za maendeleo zitumike kwa posho za Watendaji na matumizi mengineyo badala ya kutenga ardhi ya kutosha, kununua vifaa vya uvuvi, majosho, malambo na mambo mengine kwa ajili ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inaanza kuamini kwamba upungufu mkubwa wa Wizara hii sio fedha, bali ni fedha kufichwa katika vifungu ambavyo havina tija kwa maendeleo ya Wizara. Hivyo basi, tunaomba Serikali ilieleze Bunge hii ilikuwa na bahati mbaya au ni hila ya makusudi ya Serikali ya CCM kuficha fedha katika vifungu vya bajeti kwa ajili ya kugharamia Uchaguzi Mkuu ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia, upya mkakati wake wa utoaji wa fedha za maendeleo ni wapi tunatakiwa tuweke fedha na hapo patazalisha nini na kwa muda gani.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba sekta ya chakula ni sekta inayokua kwa haraka na mzunguko wake ni mkubwa sana, hivyo kuwekeza kwenye viwanda vinavyojihusisha na mazao ya mifugo na samaki maana yake ni kuongeza mzunguko wa uchumi sambamba na kuzidisha ajira na vivyo hivyo kuondoa na kupunguza tatizo la ajira hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, sekta ya mifugo, sote tunafahamu kuwa asilimia 80 ya Watanzania wanaishi vijijini kwa kutegemea kilimo, ufugaji na uvuvi lakini wengi wao bado ni maskini. Kwa kutambua hali duni ya ufugaji na wavuvi nchini, Serikali ilichukua hatua kuhakikisha kuwa Sekta ya Mifugo inakua kwa kiwango kinachotakiwa ili kukidhi mahitaji ya jamii, kuboresha maisha ya wafugaji na kuhakikisha kuwa ufugaji wa kisasa na wa kibiashara. Hayo yalijadiliwa mwezi Aprili mwaka 2001 katika mkutano mkuu wa wadau wa mifugo ambao pia uliainisha Dira ya Maendeleo ya Sekta ya Mifugo hadi mwaka 2025 inayotamka na nanukuu:

"Kuwe na Sekta ya Mifugo ambapo ifikapo mwaka 2025 kwa sehemu kubwa, itakuwa na ufugaji wa kisasa na endelevu, yenye mifugo bora, yenye uzalishaji mzuri, inayoendeshwa kibiashara na yenye kuboresha lishe ya Mtanzania. Kuinua kipato cha mfugaji na Taifa na kuhifadhi mazingira".

Mheshimiwa Spika, Kikao hicho cha wadau cha mwaka 2001 na kingine cha mwaka 2006, vyote vilionesha matatizo na kuonesha jinsi gani ya kuyamaliza au kuyapunguza, lakini hadi sasa ni miaka takriban kumi na tatu toka kikao cha kwanza cha wadau kikae huko Arusha, matatizo ya wafugaji yanazidi kuwa makubwa zaidi kuliko yalivyokuwa hapo nyuma. Je, Serikali

inasema nini kuhusu kufanyia kazi maoni na ushauri wa wadau wa sekta hii waliyoyatoa katika mikutano yake na wadau hao?

Mheshimiwa Spika, huduma za mifugo, tumeua tukiambiwa na Serikali ya CCM kuwa kuna Benki ya Ardhi ambayo ni kwa ajili ya uwekezaji. Swali ni je, hiyo ardhi iliyo kwenye Benki ni kwa nini wafugaji wasipewe ili kuondokana na adha wanayokabiliana nayo ya kuporwa mifugo kila kukicha na vyombo vya dola.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ya CCM imeshindwa kuwapatia maeneo maalum kwa ajili ya malisho kwa maendeleo ya mifugo yao. Wafugaji wamekuwa wakihamishwa na wakifukuzwa kutoka eneo moja la nchi hadi eneo lingine kama vile hawana haki ya kufanya shughuli za kiuchumi na ufugaji katika nchi yao. Ni aibu kwa Serikali kushindwa kuwapatia wafugaji mahitaji muhimu ambayo yangepelekea ufugaji wao kuwa wa kisasa, kibiashara na endelevu kama ilivyobainisha katika Dira ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoeleza hapo awali mojawapo ya jukumu la Wizara hii ni kupanga na kusimamia matumizi ya ardhi kwa ajili ya mifugo. Kwa mujibu wa Randama inaonesha kuwa Wizara imetenga maeneo ya ufugaji hekta milioni 1.3. Aidha, utafiti unasema kuwa ng'ombe mmoja anatakiwa kuchungiwa kwenye eneo la ekari sita mpaka nane kwa mwaka. Hivyo basi, kwa hekta milioni 1.3 maana yake ni malisho ya ng'ombe 541,667 tu. Tukumbuke kwamba kwa mujibu wa takwimu za mifugo tuliyonayo ni ng'ombe milioni 21 na mbuzi na kondoo milioni 21.

Mheshimiwa Spika, idadi hiyo ya ng'ombe tuliyonayo tunahitaji malisho ya ekari milioni 126 ambazo ni sawa na hekta milioni 50.4. Wizara ambayo ina jukumu la kupanga ardhi ya matumizi ya mifugo imetenga milioni 2.6 tu ya mahitaji halisi ya ardhi ya ng'ombe na hapo bado eneo la malisho kwa ajili ya mbuzi na kondoo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji, kwa takwimu hizo za mahitaji ya malisho ni kwa vipi ufugaji wetu utakuwa na tija kwa nchi na wafugaji wenyewe na je, migogoro ya wafugaji na wakulima itamalizika kama Wizara inatenga eneo ambalo halitoshelezi kwa mahitaji?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa takwimu za Serikali zinasema kuwa, Tanzania ina jumla ya hekta milioni 60 zinazofaa kwa ajili ya malisho. Hivyo basi, Kambi ya Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa *spirit* ile ile inayotumika kutenga maeneo kwa ajili ya wanyamapori, itumike pia kutenga eneo la kutosha kwa ajili ya ufugaji. Kwani ni dhahiri Wizara imeweka lengo la kugawana, kusimamia matumizi ya ardhi ya mifugo ambalo kiuhalisia haina uwezo nalo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji ni hatua gani zinazochukuliwa kukabiliana na changamoto hiyo kwa kuwa tunashuhudia migogoro na mauaji mengi yanayoendelea kati ya wakulima na wafugaji hususani katika Wilaya ya Kiteto na Mvomero na sehemu nyingine mbalimbali za nchi hii.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizopo ni kwamba, Baraza la Ardhi la Nyumba na Wilaya ya Morogoro ilitoa amri *Stop Order* kuwa wafugaji waishio Vijiji vya Kongwa na Kisaki Kituoni wasifukuzwe hadi kesi itakaposikilizwa. Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Saidi Amanzi alipuuza amri halali ya Baraza na kuamuru Polisi kusimamia zoezi hilo la kuondoa watu. Aidha, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro pamoja na Mkuu wa Wilaya walivunja amri ya Baraza iliyotaka wafugaji katika Tarafa ya Ngerengere wasiondolewe hadi kesi iliyofunguliwa Mahakama Kuu iweze kusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, hoja ya msingi ni kwa nini Watendaji hao wa Serikali wanashindwa kuheshimu utendaji wa mhimili wa Mahakama. Kwa kuwa wao ndiyo wanatakiwa wawe mfano kwa wengine katika kutekeleza Utawala wa Sheria. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali au Ofisi ya Waziri Mkuu kuwachukulia hatua za kinidhamu Watendaji hao wanaonyanyasa wafugaji katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Ranchi za Taifa. Kwa sasa wafugaji wana chama chao. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, ni muda muafaka wafugaji kwa ushirikiano na *NARCO* kumiliki Ranchi ya Ruvu na Ranchi zingine kwani wafugaji kupitia Chama chao wana uwezo wa kuweka mtaji na *NARCO* wakawekeza taaluma yao. Kinyume na hapo Ranchi hiyo itatolewa bure kwa wageni wanaokuja bila fedha na kuondoka na fedha zetu nyingi kwenda kwao. Kwa hiyo, hili lionwe kwa undani zaidi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuongeza ubora wa bidhaa za mifugo. Sera ya Mifugo ya mwaka 2006 inasisitiza umuhimu wa kuongeza thamani ya mazao yatokanayo na mifugo ili yaweze kuingia katika soko la ushindani na pia kuyaongezea muda wa hifadhi. Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji Serikali imefanya nini kuhamasisha na kuhimiza Vyama vya Wafugaji na wafanyabiashara wa ng'ombe wa nyama na maziwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, vile vile Serikali inawaandaaje wafugaji kupata mitaji na mikopo kuboresha miundombinu ya kukusanya na kusambaza maziwa, uwepo wa viwanda vya kusindika, uhamasishaji unywaji wa maziwa na kudhibiti magonjwa ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa shughuli za uvuvi katika bahari kuu. Kambi Rasmi ya Upinzani toka mwaka 2008 imekuwa ikitoa ushauri kwa Serikali kuhusu jinsi ya kunufaika na uvuvi katika bahari kuu. Kambi Rasmi ya Upinzani inarudia tena ambacho tulikisema katika bajeti ya mwaka 2008/2009 na 2009/2010 kuhusu uvuvi katika bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ya CCM haisikilizi ushauri, lakini kutokusikiliza huko ni kutokana na ukweli kwamba meli nyingi zinazovua bahari kuu zina ubia na viongozi waandamizi wa CCM na Serikali yake. Hoja ni je, nchi itaendelea kufilisiwa na Kada hiyo ya viongozi hadi lini.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa zilizopo ni kwamba, watuhumiwa hao wameshinda kesi na sasa Serikali inatakiwa kulipa fidia. Je, kama tulivyohoji hapo mwaka 2012 kuwa tumefaidika na nini hasa na hiyo meli ambayo ilikamatwa? Kwani meli imezama na hakuna faida zaidi ya watuhumiwa kukaa jela na kula chakula cha wafungwa. Nazungumzia ile meli ya Magufuli.

Mheshimiwa Spika, changamoto za wavuvi Ziwa Victoria. Kwa upande wa wavuvi wafanyao kazi zao katika ziwa hili wanakabiliwa na matatizo yafuatayo:-

(1) Ukosefu wa vitendea kazi, mfano, Ilemela tangu imeanzishwa mwaka 2012 haina *speed boat* ya kuwawezesha Maafisa Uvuvi kufanya doria dhidi ya uvuvi haramu, lakini pia kutoa huduma ya ugani katika maeneo ya uvuvi.

(2) Ukosefu wa fedha kwa ajili ya kuwezesha vikundi ambavyo huhamasishwa na Maafisa Uvuvi juu ya ufugaji wa samaki.

(3) Kuna upotevu mkubwa sana wa mazao ya samaki hasa dagaa na hivyo kusababisha upotevu wa rasilimali muda, fedha, wa rasilimali na hivyo kupelekea wavuvi kubakia duni. Serikali itenge bajeti ya kutosha kwa Maafisa Uvuvi kuwafikia wavuvi na kutoa elimu ya kuchakata mazao ya uvuvi, lakini pia itenge bajeti ya kusaidia vikundi vya

wavuvi kuondokana na ukaushaji wa dagaa na mazao mengine ya uvuvi kwenye mchanga.

Mheshimiwa Spika, wavuvi wadogo wanakutana na adha ya kulipa ushuru kwa kila Halmashauri. Mfano, ni wavuvi wa Ilemela wakivuka kwenda Halmashauri ya Nyamagana, Sengerema, Ukerewe na Geita kote wanatakiwa kulipia leseni za Halmashauri husika na pengine na faini juu.

Mheshimiwa Spika, mbona magari tunakata leseni moja na tunatembea Mikoa yote ya Tanzania. Je, kwa nini wavuvi wasikate hiyo leseni moja nao wakazunguka nchi nzima. Ni kwa nini kuna tatizo hilo kwa upande wa wavuvi? Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka mpango madhubuti wa kuondoa matatizo haya kama yanavyoainishwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, ufugaji wa samaki. Wizara katika majukumu yake, jukumu mojawapo ni kuendeleza ufugaji wa samaki. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuiambia, kusema sekta hii kuwa bado haijapewa umuhimu unaostahili kiuhalisia, bali ni maneno kwenye vitabu.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wadogo wenye moyo wa kufuga samaki ni ukweli ulio wazi kwamba, bado mazingira ni magumu kwa wafugaji wenye mitaji midogo. Nasema hayo kwa kuangalia bei ya kifaranga kimoja ambacho hakijatenganishwa jinsia ni sh. 100/= na kifaranga ambacho kimetanganishwa jinsia ni sh. 250/=. Chakula kwa ajili ya kuwalisha samaki hao ni sh. 3,500/= na kwa hali ya kawaida hadi samaki wafikie muda wa kuvunwa wakiwa na uzito wa gramu 500 hadi 700 inachukua miezi saba hadi tisa kama ulishaji utakuwa kwa kiwango kinachotakiwa. Je, huoni kwamba hao watu wanapata shida sana na hawatakuwa na mtaji huo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja hapa ni je, kwa wafugaji wenye kipato kidogo wanasaidiwa vipi katika hili? Aidha, kwa mujibu wa wananchi walio Mikoa ya Kanda ya Ziwa hasa Kagera kifanga kimoja cha sato kinauzwa kwa sh. 300/= hadi 500/=. Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kujua chakula cha kulisha samaki kwa Tanzania kinatengenezwa na kiwanda kipi na kipo Mkoa gani? Kama hakipo Wizara hii ina mpango gani wa kuingia ubia na wadau katika kuanzisha Kiwanda cha Kutengeneza Chakula cha Samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, kutokana na ukweli kwamba Sekta hii ya Mifugo na Uvuvi imekuwa haitengewi fedha wakati ina fursa kubwa ya kubadilisha maisha ya wananchi wengi wa Tanzania na pia kutokana na ukweli kwamba kuna matumizi ambaye yenye mashaka kwenye upande wa fedha za maendeleo. Hivyo basi, ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani, bajeti ya Wizara hii ifumuliwe upya na Kamati yetu ya Bajeti ipangwe ili kuondoa fedha zilizowekwa kwenye dhamira ovu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru wananchi wa Hanang na wadau wote wa mifugo na uvuvi nchini kwa ushirikiano wanaonipa katika kazi yangu ya kushughulikia ustawi wa Sekta hii ya Mifugo na Uvuvi katika nchi yetu. Aidha, nawashukuru Wabunge wote kwa taarifa wanazonipa kuhusu Sekta husika katika majimbo yao. Naishukuru pia familia yangu kwa kunipa moyo katika majukumu yangu ya Kibunge. Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Spika naomba sasa, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana.

Taarifa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya 2014/2015 ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kama ilivyowasilishwa Mezani

HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI MHE. ROSE KAMILI SUKUM (MB), WIZARA YA MIFUGO NA MAENDELEO YA UVUVI, KUHUSU MAPITIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

(Inatolewa chini ya Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2013)

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 494A la tarehe 17 Desemba 2010 imepewa majukumu yafuatayo:

(i) Kutayarisha, kufanya mapitio na kusimamia utekelezaji wa sera,sheria,mipango na mikakati ya kuendeleza sekta ya mifugo na uvuvi;

(ii) Kupanga na kusimamia matumizi ya ardhi kwa ajili ya mifugo;
(iii) Kuendeleza na kusimamia uendelezaji wa miundombinu ya mifugo na uvuvi;

(iv) Kusimamia uendelezaji wa mazao yatokanayo na mifugo na uvuvi;

(v) Kuendeleza ufugaji wa samaki;

(vi) Kudhibiti magonjwa ya mifugo pamoja na wadudu wanaoeneza magonjwa hayo; nakadhalika.

Mheshimiwa Spika, Aidha, Dira kuu ni kuhakikisha kuwa rasilimali za mifugo na uvuvi zinaendelezwa na kutunzwa katika mazingira endelevu kwa ajili ya ukuaji wa uchumi na kuboresha maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika; Kabla sijafanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 sekta kwa sekta; idara za Wizara na Taasisi zake nikumbushe kwamba mwaka 2013 ulikuwa mwaka wa pekee kwa wafugaji.

Mwaka 2013 ni mwaka ambao taifa lilishuhudia mauaji ya wafugaji na wakulima kwa kile kilichoelezwa kwamba ni migogoro ya ardhi. Aidha, Nchi ilishuhudia mauaji ya wafugaji na mifugo yao kwa kile kilichoelezwa kwamba ni migogoro baina ya wafugaji na hifadhi.

Mheshimiwa Spika; Matokeo ya hali hizo ni Bunge kukabidhi majukumu kwa kamati zake za kudumu kushughulikia masuala yenye kugusa mustakabali wa sekta ya mifugo nchini. Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ilifanya uchunguzi kuhusu "Operesheni Tokomeza" na ripoti yake ilisomwa bungeni na kusababisha mawaziri wanne kuwajibishwa. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kuondolewa kwa mawaziri pekee bila utekelezaji wa mapendekezo

ya kamati yenye kugusa moja kwa moja wafugaji na hatma ya mifugo ni udhaifu mkubwa kwa upande wa Serikali.

Mheshimiwa Spika; Hatua ya Rais kuunda Tume haipaswi kutumika kama kisingizio kwa Serikali kuacha kutoa taarifa bungeni juu ya mapendekezo yote ambayo hayahitaji kusubiri mpaka Tume kukamilisha kazi yake. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali katika majumuisho itoe majibu juu ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati na maazimio ya Bunge yaliyohusu mifugo na wafugaji. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawahimiza wabunge katika kufanya mapitio ya utekelezaji na kujadili makadirio ya Wizara hii wafanye rejea katika Taarifa ya "Operesheni Tokomeza" iliyowasilishwa Bungeni na maazimio kupitishwa.

Mheshimiwa Spika; Kambi Rasmi ya Upinzani inalikumbusha Bunge hili kuwa mwaka 2013 Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ilipewa kazi ya kwenda kuchunguza migogoro ya ardhi baina ya wakulima, wafugaji, hifadhi na wawekezaji. Hata hivyo, mpaka sasa Kamati tajwa ya Bunge haijawasilisha bungeni matokeo ya uchunguzi huo hali ambayo inafanya Bunge kujadili mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo bila kuwa na taarifa ya kamati.

Mheshimiwa Spika; Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka maelezo yatolewe Bungeni ni kwanini taarifa ya Kamati hiyo haijawasilishwa mpaka hivi sasa? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kabla ya kuendelea na mjadala juu ya Wizara hii ya mifugo, taarifa ya Kamati husika iwasilishwe mezani ili wabunge waweze kuitumia kama rejea katika kuchukua hatua za kuboresha sekta ya mifugo nchini ili kuepusha migogoro baina ya wafugaji na wakulima, hifadhi na wawekezaji inayoendelea nchini. Kwa nafasi yangu ya Waziri Kivuli wa Wizara hii nilitaka kushiriki kuihoji Serikali juu ya masuala haya kuanzia kwenye Kamati hata hivyo nilizuiwa na Mwenyekiti wa Kamati husika kushiriki vikao vya Kamati hali ambayo inaacha maswali kuhusu ushirika wa usiri baina ya Mwenyekiti wa Kamati na Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, nitumie fursa hii kueleza kilio cha wafugaji kuhusiana na ushuru wa mifugo. Ushuru wa mifugo kwa muda mrefu umekuwa kero kwa wafugaji, wafanyabiashara na halmashauri kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Ushuru umekuwa ukitozwa bila utaratibu maalum ambapo baadhi yao hutumia Watendaji wa Vijiji na mawakala hali inayosababisha kero kwa wafugaji na wanunuzi wa mifugo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufuta ushuru huo kwani haimnufaishi mfugaji. Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa imeeleza wazi kuwa asilimia 10% ya makusanyo ya ushuru utumike kuhudimia mifugo ikiwa ni pamoja na kununulia madawa ya mifugo;

2. MAPITIO YA BAJETI

Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha, 2012/13 Wizara ilikuwa imetengewa jumla ya shilingi bilioni 54 na kwa mwaka wa fedha 2013/14 zilitengwa jumla ya shilingi bilioni 67.18.

Mheshimiwa Spika, Randama ya Wizara inaonyesha kuwa hadi mwezi April, 2014, fedha za ndani kwa ajili ya maendeleo zilipokelewa jumla ya shilingi bilioni 2.3 tu kati ya shilingi bilioni 23.5. sawa na asilimia 9.7 tu ya fedha za ndani. Hoja ni kwa vipi tunaweza kutekeleza mipango kwa fedha hizo wakati ilikadiriwa kutumia shilingi bilioni 23.5. Kambi Rasmi inaomba maelezo ya hilo.

Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2014/15 wizara inaomba Bunge liidhinishe jumla ya shilingi bilioni 66.143 ili iweze kutekeleza majukumu yake kama yalivyopitishwa na tume ya mipango. Kati ya fedha hizo, fedha za maendeleo ni shilingi bilioni 25.190. Aidha, fedha za ndani kwa ajili ya maendeleo ni shilingi bilioni 23 na fedha za nje ni shilingi bilioni 2.190. Pia kila Idara imetengewa kasma yake kwa matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeomba jumla ya shilingi bilioni 40.95 kama fedha za matumizi ya kawaida, kati ya fedha hizo mishahara ni shilingi bilioni 22.97 na matumizi mengine ni shilingi bilioni 17.98. Aidha, katika matumizi mengineyo (OC) kila idara imetengewa kasma yake.
Mheshimiwa Spika, Katika kupitia Randama inaonesha kuwa Kwa fedha za Maendeleo Kifungu 1003- Idara ya Sera na mipango, **Kasma** zifuatazo zitatekelezwa:

Kasma: 220100- Ununuzi wa shajala,kulipia gharama za kurudufu program za kompyuta, jumla shilingi milioni 59. Naomba Wabunge muangalie matumizi ya Kawaida Uk. 122 Kasma hiyo hiyo inaonyesha zinaombwa shilingi milioni 85.3. Kambi Rasmi inaitaka Serikali kutoa maelezo kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Spika, **Kasma: 220300** Fuel,Oils, Lubricants (kimeandikwa- kununua mafuta ya magari na ujenzi wa malambo)- Jumla shilingi milioni 176. **Kasma: 220700** –Gharama za kukodi kumbi za kufanyia mikutano na semina, jumla shilingi milioni 12. **Kasma: 221000,** Gharama za usafiri ndani ya nchi na posho ya kujikimu kwa watumishi wa Idara, jumla shilingi milioni 212, aidha, katika matumizi ya kawaida idara hiyo na kasma hiyo hiyo imetenga jumla ya shilingi milioni 104.6. Hapa maana yake ni kwamba idara hiyo na kasma hiyo imetengewa jumla ya **shilingi milioni 316.6.**

Mheshimiwa Spika, ukifanya ulinganisho wa bajeti inayotengwa kwa ajili ya kuimarisha huduma za mifugo au uvuvi utaona ni kwa kiwango gani Serikali isivyokuwa na nia ya kweli ya kuinua sekta hii. Mheshimiwa Spika, hapa tunatoa hela na hivyo tarakimu ni muhimu kuliko maneno ambayo miaka yote ndiyo yanairudisha nyuma sekta. Kama ni tarakimu ndio hizo tulizoletewa na kupitishwa na Kamati ya Bunge lako. Je si tutachekwa kama watu watapitia randama hii? Hii ni aibu kubwa kama Bunge lako tukufu litapitisha bajeti hii ya Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Kasma: 410700, Gharama za utayarishaji wa ripoti na nyaraka, jumla shilingi milioni 58.45

Mheshimiwa Spika, matumizi hayo, Kambi Rasmi ya Upinzani inayaona ni matumizi mengineyo na sio ya Maendeleo, na jumla yake ni shilingi **milioni 517.45.** Wakati huo huo idara hii kwa matumizi mengine imetengewa jumla ya shilingi **milioni 736.73**(Randama Uk.90)

Mheshimiwa Spika, kwa maana nyingine ni kwamba kwa idara hii fedha za matumizi mengineyo ni **shilingi (milioni 517.45 + 736.73 = bilioni1.2543) na za maendeleo ni shilingi milioni 834.5 tu kati ya shilingi bilioni 1.35 kama Randama inavyoonyesha.**

Mheshimiwa Spika, Kwa Idara ya utafit, mafunzo na ugani, **Kifungu 1004. Kasma:270600,** kununua vitabu,shajala, majarida, vifaa vya kompyuta, kurudufia na kulipia gharama za kurudufia. Jumla shilingi milioni 37.5 **Kasma: 220200**. Kulipia umeme na maji, jumla shilingi milioni 74.23. Kasma hiyo hiyo matumizi ya kawaida imetengewa jumla ya shilingi milioni 6. **Kasma: 220300,** manunuzi ya mafuta ya magari ya idara, Jumla shilingi milioni 60.7 Pia kasma hiyo kwa upande wa matumizi ya kawaida imetengewa jumla ya shilingi **milioni 49.93**. **Kasma: 220600,** kununua vifaa, mavazi na viatu vya kinga kwa watumishi wa idara, Jumla shilingi milioni 5.15. **Kasma: 221000,** Gharama za usafiri, fedha za kujikimu kwa viongozi na watumishi wa idara wanaposafiri kikazi ndani ya nchi. Jumla shilingi milioni 113.95 **Kasma: 221200**, Gharama za matanagazo na machapisho ya idara, jumla shilingi milioni 12. **Kasma: 221400:** Chain a viburudisho wakati wa mafunzo na mikutano ya Idara, jumla shilingi milioni 3. **Kasma: 410600,**

ununuzi wa samani, jumla shilingi milioni 39. **Kasma: 410600,** ununuzi wa kompyuta, mashine za kurudufu, printa na skana, jumla shilingi milioni 35.

Mheshimiwa Spika, kwa matumizi hayo ambayo kwa mtazamo wetu sio ya maendeleo, jumla ni **shilingi milioni 380.23.** Wakati matumizi mengineyo kwa idara hii zimetengwa jumla ya **shilingi bilioni 4.65**

Mheshimiwa Spika, hizi idara mbili ambazo Kambi Rasmi imezipitia ni kwamba vifungu hivyo hivyo kwa matumizi ya kawaida vimetengewa fedha, na kwa upande wa fedha za maendeleo vimetengewa fedha lakini kwa matumizi kama ambavyo tumeainisha hapo awali. Hoja hapa ni, kweli watendaji wa idara hawawezi kutenganisha kati ya fedha za maendeleo na matumizi mengineyo (OC)?

Aidha, **Kambi Rasmi ya Upinzani** inashindwa kuamini kama kweli Kamati ya Bunge inayoongozwa na Mhe Profesa, pia imeshindwa kuona fedha hizi ambazo zimewekwa maeneo yasiyostahili kwa matumizi hayo, kwani tayari yalikwisha wekwa katika bajeti ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inaanza kuamini kwamba mapungufu makubwa ya wizara hii sio fedha bali ni fedha kufichwa katika vifungu ambavyo havina tija kwa maendeleo ya wizara. Hivyo basi tunaomba Serikali ilieleze Bunge hii ilikuwa na bahati mbaya au ni makusudi CCM inatafuta hela za Uchaguzi wa Serikali za mitaa?

Mheshimiwa Spika, Kwa kuangalia takwimu hizo, Kambi Rasmi inajiuliza, kama mwaka 2013/14 fedha za ndani zilizoombwa ni shilingi bilioni 23.5 na zikatolewa shilingi bilioni 2.23 tu. Hivyo basi, kuna mantiki gani kuomba kiasi kikubwa tena wakati mazoea ya Serikali ni kutoa asilimia 5 hadi 10 ya fedha ndani tu kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia, upya mkakati wake wa utoaji wa fedha za maendeleo ni wapi tunatakiwa tuweke fedha na hapo patazalisha nini na kwa muda gani. Ukweli ni kwamba sekta ya chakula ni sekta inayokuwa kwa haraka na mzunguko wake ni mkubwa sana, hivyo kuwekeza kwenye viwanda vinavyojihusisha na mazao ya mifugo na samaki maana yake ni kuongeza mzunguko wa uchumi sambamba na kuzidisha ajira na hivyo kuondoa/ kupunguza tatizo la ajira hapa nchini.

3. SEKTA YA MIFUGO

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kuwa asilimia 80 ya watanzania wanaishi vijijini kwa kutegemea kilimo, ufugaji na uvuvi lakini wengi wao bado ni maskini. Kwa kutambua hali duni ya ufugaji na wavuvi nchini, Serikali ilichukua hatua kuhakikisha kuwa Sekta ya Mifugo inakua kwa kiwango kinachotakiwa ili kukidhi mahitaji ya jamii, kuboresha maisha ya wafugaji na kuhakikisha kuwa ufugaji ni wa kisasa na wa kibiashara. Hayo yalijadiliwa mwezi April mwaka 2001 katika mkutano mkuu wa wadau wa mifugo ambao pia uliainisha mwelekeo wa Sekta pia uliainisha Dira ya Maendeleo ya Sekta ya Mifugo hadi mwaka 2025 inayotamka, na nanukuu:

> *"Kuwe na Sekta ya Mifugo ambapo ifikapo mwaka 2025 kwa sehemu kubwa, itakuwa na ufugaji wa kisasa na endelevu, yenye mifugo bora, yenye uzalishaji mzuri, inayoendeshwa kibiashara na yenye kuboresha lishe ya Mtanzania. Kuinua kipato cha mfugaji na Taifa na kuhifadhi mazingira".*

Mheshimiwa Spika, Kikao hicho cha wadau cha mwaka 2001 na kingine cha mwaka 2006, vyote vilionyesha matatizo na kuonyesha jinsi gani ya kuyamaliza au kuyapunguza lakini hadi sasa ni miaka takriban kumi na tatu toka kikao cha kwanza cha wadau kikae huko Arusha, matatizo ya wafugaji yanazidi kuwa makubwa zaidi kuliko yalivyokuwa hapo nyuma. Je, Serikali inasema kuhusu kufanyia kazi maoni na ushauri wa wadau wa sekta hii waliyoyatoa katika mikutano yake na wadau hao?

Mheshimiwa Spika, Takwimu za Serikali zinaonyesha kuwa sekta ndogo ya **mifugo na uwindaji** ilikua kutoka asilimia 3.1 hadi asilimia 3.8 kwa kipindi cha mwaka 2013.Katika kipindi cha mwaka 2005/06 Sekta ya Mifugo ilikua kwa asilimia 5.2. Ukuaji huo bado ulikuwa ni mdogo kuliko kiwango kilichoainishwa kwenye MKUKUTA, unaotaka Sekta ya Mifugo kukua hadi asilimia 9 ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa Serikali inatumia takwimu kwa makusudi kwa kuonyesha kuwa sekta imekuwa wakati mifugo imechanganywa na uwindaji. Kwa mtazamo wetu tunaona sekta iliyokuwa ni ya uwindaji na si mifugo.
Mheshimiwa Spika, Bajeti ya matokeo mara zote uanzia kwa kile ambacho wananchi wanataka na wananchi wako radhi kulipia matokeo ya huduma hizo. Hivyo basi bajeti hii inapitia hatua zifuatazo:

1. Serikali kuweka kiwango cha bei ambacho wananchi wako radhi kutumia katika kupata huduma.

2. Kuweka vipaumbele na kueleza matokeo ya vipaumbele ambavyo ni vya wananchi sambamba na jinsi ya kupima matokeo ya vipaumbele hivyo.

3. Kuweka gharama kwa kila kipaumbele, na kugawa raslimali kulingana na vipaumbele vya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Nimeweka utangulizi huo wa bajeti ya matokeo au bajeti ya wananchi ili kuiuliza Serikali bajeti hii ya mifugo, vipaumbele vya wafugaji nini na wafugaji wako radhi kutumia au kulipa kiasi gani katika kupata huduma za maendeleo kwa mifugo yao?

Mheshimiwa Spika, Naomba kunukuu kauli ya aliyekuwa waziri wa Mifugo mwaka 2006 Mhe Dr.Shukuru Kawamba aliyoitoa katika mkutano wa wadau wa mifuko katika ukumbi wa Msekwa wakati akiongea na wadau wa sekta ya Mifugo nchini, ambapo mgeni rasmi alikuwa ni Rais Jakaya Kikwete**.**

"Mheshimiwa Rais, mkutano huu wa Wadau wa Sekta ya Mifugo unafuatia Mkutano uliyofanyika Arusha mwaka 2001 na kufunguliwa na Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. Mkutano huo ulianisha matatizo yanayofanya ufugaji wetu usiweze kutoa mchango unaostahili kwa pato la Taifa na kuwaondolea wafugaji umaskini. Aidha, mkutano huo uliweka Dira ya Sekta ya Mifugo ambayo inatekeleza Dira ya Taifa ya mwaka 2025 na Malengo ya Kitaifa ya Millenia (Millenium Development Goals - MDGs). Mheshimiwa Rais Mstaafu wakati akihutubia mkutano huo alitoa changamoto zifuatazo kwa wadau.

1. ***Maisha ya Wafugaji****: Ni kwa nini mifugo ambayo ni mali, haijaweza kuboresha maisha ya wafugaji walio wengi?*

2. ***Mchango wa Sekta ya Mifugo kwenye uchumi*** *: Kwa nini mchango wa Sekta ya Mifugo kwenye uchumi wa maeneo ya wafugaji na hatimaye kwenye uchumi wa taifa, bado ni mdogo?*

3. ***Ufugaji kibiashara na viwanda:*** *Ni kwa nini ufugaji wa kisasa, wa kibiashara pamoja na viwanda vya kusindika mazao ya mifugo bado umedumaa?*

Vilevile, Mheshimiwa Rais Mstaafu alitoa rai ambayo napenda kunukuu

"***Natoa rai tufanye mambo ya uhakika, ubabaishaji uwe mwiko. Sera za jumla za uchumi sasa ziko tayari kuhimili ukuaji wa uchumi ikiwemo sekta ndogo ya mifugo. Wakati wa kubadili gia ya maendeleo ya ufugaji na taifa letu ni sasa. Tusiogope kufanya maamuzi. Tusiogope kuthubutu. Tusiogope kubadili maisha na mienendo tuliyoizoea. Nina hakika tukishirikiana na kusaidiana tutafanikiwa."*** Mwisho wa kunukuu.

Kambi Rasmi ya Upinzani ina maswali mawili kwa nukuu hiyo ya Mhe Mkapa;

4. Ubabaishaji aliouona Mhe Mkapa katika sekta hii ya mifugo umekwisha?

5. Je, uthubutu katika kufanya maamuzi hasa katika kutoa mikopo na kuweka bima kwenye sekta ndogo ya mifugo itawezekana lini?

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa andiko la Dkt. Joseph Hella wa SUA[1] "**Inasadikiwa kuwa theluthi moja (1/3) ya watu maskini sana duniani, kati ya watu bilioni 2.8 wanaoishi kwa kutegemea chini ya dola 2 za kimarekani kwa siku ni wafugaji.**

[1]Nafasi ya sekta ya Mifugo katika uchumi wa Dunia na katika kuinua pato la taifa na kuondoa umaskini nchini
Taarifa zaidi inabainisha kuwa katika nchi nyingi zinazoendelea, mifugo na ufugaji ni moja ya njia chache zilizopo au zilizobakia kwa watu maskini kujipatia mali. Aidha, kundi hilo la wakulima wafugaji ndio linamiliki 95% ya mifugo yote hapa nchini. Bahati mbaya wengi wao ndio maskini sana"

Mheshimiwa Spika, Andiko hilo liliwasilishwa kwenye mkutano wa wadau mwaka 2006 mgeni rasmi akiwa Rais wa nchi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali iwaeleze watanzania hasa wafugaji ni kwa vipi inaweza kuondokana na umasikini wa kipato wakati huo huo mali za kundi maskini zinaporwa na Serikali hiyo hiyo, rejea operation mbalimbali za kuhamisha wafugaji kutoka baadhi ya mikoa kwa nguvu na kuua mifugo kwa maksudi kwa kisingizio cha mifugo kuvamia maeneo ya hifadhi za wanyamapori.

6. HUDUMA ZA MIFUGO

Mheshimiwa Spika, Ukisoma ilani ya uchaguzi wa CCM ya mwaka 2005-2010 uk.16 aya ya 32 inasema kuwa; **"***Pamoja na kwamba Tanzania ina mifugo mingi sana; mchango wa mifugo kwenye uchumi wa Taifa ni mdogo. Kwa lengo la kuendeleza Sekta ya Mifugo ili ichangie zaidi ukuaji wa uchumi wa Taifa na kuwaongezea kipato wafugaji, Serikali za CCM zitaendeleza kwa msisitizo zaidi lengo la kuzingatia zaidi ubora kuliko wingi pekee katika ufugaji."*

Aidha **"***Katika kipindi cha Ilani 2010-2015 mkazo utaelekezwa katika matumizi ya maarifa katika sekta ya mifugo. Jukumu kuu la msingi katika ufugaji litakuwa ni kuleta mabadiliko yatakayoiondoa sekta hii kutoa uduni wa ufugaji na kuwabadili wafugaji wetu kutoka wafugaji wahamaji. Mkazo utaelekezwa katika kutatua matatizo ya malisho na maji na kuwafikisha wafugaji katika ukulima mchanganyiko na ufugaji wa mabandani wenye tija kubwa, utakaotoa nyama na maziwa bora*[2]*."*

[2] Ilani ya CCM ya 2010-2015 uk. 15, aya ya 25

Mheshimiwa Spika, Njia mojawapo inayotumika na wafugaji katika kukabiliana na upungufu wa malisho na maji ni kuhamisha mifugo wakati wa msimu wa kilimo na kurudi wakati wa kiangazi; kwa mfano katika wilaya ya Meatu, mifugo huhamia Makao; Maswa, huhamia Hifadhi ya Taifa ya Maswa; na Bariadi huhamia kwenye nyanda za malisho Musoma. Kadhalika katika kipindi cha kiangazi, mifugo kutoka Meatu, Maswa, Bariadi na Kishapu huhamia Nzega, Igunga na Manyoni (Itigi). Hanang' kuhamia Mbugwe-Manyoni, Handeni-Tanga, Pwani na Morogoro.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na uhamaji wa msimu, baadhi ya wafugaji wamekuwa wakihamia mikoa mingine na kuweka makazi ya kudumu. Kwa mfano wafugaji kutoka Shinyanga, Tabora, Mwanza walihamia Rukwa, Mbeya na hivyo hivyo kwa wafugaji kutoka mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro walielekea Pwani, Morogoro, Mbeya, Iringa.

Mheshimiwa Spika, Ni ukweli kwamba wafugaji wamekuwa wakitumia utaratibu huu wa kuhamahama miaka yote na si Tanzania tu bali ni mfumo unaotumika kwa ufugaji wa aina hii kwa nchi zilizo na wafugaji wa aina hii.

Mheshimiwa Spika, Tatizo hili limeoneka kuwa ni kubwa kutokana na ukweli kwamba maeneo waliyokuwa wakitumia wafugaji hao yametwaliwa na Serikali kwa matumizi mengine ambayo hayana uhusiano na ufugaji.

Mheshimiwa Spika, Uhaba wa ardhi, maji na malisho ni kati ya matatizo sugu yanayoikabili Sekta ya Mifugo Sababu za upungufu huu ni kama zilivyoelezwa. Pamoja na kuwepo na upungufu huu wa uhaba wa ardhi hakuna mpango maalum wa kugawa maeneo ya malisho na kuyamilikisha kwa wafugaji kwa kuzingatia haki za kimila na sheria ya vijiji ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, Tumekuwa tukiambiwa mara zote na Serikali ya CCM kuwa kuna benki ya ardhí ambayo ni kwa ajili ya uwekezaji, swali ni je hiyo ardí iliyo kwenye benki ni kwanini wafugaji wasipewe ili kuondokana na adha wanayokabiliana nayo ya kuporwa mifugo kila kukicha na vyombo vya dola?

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ya CCM imeshindwa kuwapatia maeneo maalum kwa ajili ya malisho kwa maendeleo ya mifugo yao. Wafugaji wamekuwa wakihamishwa na au wakifukuzwa kutoka eneo moja la nchi hadi eneo lingine kama vile hawana haki ya kufanya shughuli za kiuchumi kama ufugaji katika nchi yao. Ni aibu kwa Serikali kushindwa kuwapatia wafugaji mahitaji muhimu ambayo yangepelekea ufugaji wao kuwa wa kisasa, kibiashara na endelevu kama ilivyobainisha katika dira ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Ni ukweli kwamba Tanzania ina mifugo mingi, lakini kwa muktadha wa CCM ni kwamba njia pekee ya kupunguza mifugo hiyo ili iendane na malisho yaliyopo ni kuiteketeza **(operation tokomeza na operation zingine za kuhamisha mifugo toka mkoa mmoja kwenda mwingine)** njia itakayo wabadili wafugaji kutoka kuwa wahamaji wachungaji na kuwa wafugaji wa mabandani wenye tija kubwa kama ilani yao inavyosema.

7. MIGOGORO YA ARDHI INAYOHUSU WAFUGAJI

Mheshimiwa Spika, Ni ukweli uliowazi kuwa ardhi ambayo ipo inatosha kabisa kwa makundi mbalimbali ya kijamii kufanya shughuli zake za kiuchumi bila mifarakano miongoni mwake.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na ongezeko kubwa la watu (kutoka 11,960,000 mwaka 1967 hadi 45,670,000 mwaka 2012) kumekuwepo na ongezeko la mahitaji ya chakula. Katika kipindi hiki kilimo kimepanuka na kuingia katika maeneo ambayo zamani hayakutumika kwa kilimo, kwa mfano, kilimo cha ngano (Basuto Hanang), shayiri (Loliondo na West Kilimanjaro), maharage (Lolkisale/Simanjiro), mpunga na pamba Kanda ya Ziwa. Kupanuka kwa kilimo kumepunguza maeneo ya malisho. Sio shughuli za kilimo tu bali pia utwaaji wa maeneo makubwa kwa ajili ya shughuli za uchimbaji madini katika mikoa ya kati na kanda ya ziwa na kuongezeka kwa maeneo ya hifadhi za taifa kutoka kilomita za mraba 85,430 (mwaka 1920) hadi 163,479 hivi sasa, na hivyo kuwalazimu wafugaji kuhamia maeneo mengine ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza ni kwa vipi Serikali makini inaweza kupanga bila ya kuona athari zinazojitokeza kwa kundi hili muhimu kwa uhai wa nchi yetu? Huu ni ukosefu wa ubunifu na kupanga mipango kwa kufikiria matakwa ya kundi dogo la watu walio madarakani. Hoja hii inatiliwa nguvu na nini akina nani wamemilikishwa mashamba makubwa na yaliyokuwa mashamba ya mifugo ya taifa?

Mheshimiwa Spika, Naomba ninukuu kile tulichokisema mwaka jana katika mawasilisho yetu ***"Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina rasilimali kubwa ya maliasili ikiwemo ardhi, malisho na idadi kubwa ya mifugo. Kati ya jumla ya hekta milioni 94 za rasilimali ya ardhi, hekta milioni 60 ni nyanda za malisho zinazofaa kwa ufugaji. Kwa sasa kuna ng'ombe milioni 21.3, mbuzi milioni 15.2 na kondoo milioni 6.4. Mifugo mingine ni pamoja na nguruwe milioni 1.9 na kuku wa asili milioni 58. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2012/2013 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2013/2014, Kiambatanisho Na. 3 kinaonesha kuwa, kwa mikoa 21, wilaya 69 na vijiji vilivyopimwa 479, eneo la malisho ambalo linasadikiwa kuwa limetengwa kwa ajili ya wafugaji kuwa ni hekta milioni 1.28. Hii ni sawa na asilimia 2.13 ya hekta milioni 60 za nyanda za malisho katika nchi hii. Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri awaeleze wafugaji kwa ng'ombe milioni 21.3 na mbuzi na kondoo milioni 21.5 wanatakiwa wachungwe kwenye eneo la ukubwa gani?"***

Mheshimiwa Spika, Migogoro mingi ambayo wananchi hasa wafugaji wameteswa na kuporwa mifugo yao kwa kiasi kikubwa imetokana na Serikali kufikia maamuzi yake kwa kuangalia sheria zinazohusu Wanyapori na Mazingira pekee bila ya kuangalia sheria ya Ardhi za Vijiji, ambayo kwayo imeruhusu uwepo wa wafugaji hao kwenye maeneo husika.
Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kuelewa ni eneo la malisho kiasi gani linaweza kuhimili idadi ya ng'ombe milioni 21.3 kwa pamoja na mbuzi na kondoo milioni 21.5 bado lipo kama tulivyouliza mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyo eleza hapo awali mojawapo ya jukumu la Wizara hii ni kupanga na kusimamia matumizi ya ardhi kwa ajili ya mifugo.

Kwa mujibu wa randama inaonyesha kuwa Wizara imetenga maeneo ya ufugaji hekta milioni 1.3, aidha utafiti unasema kuwa ng'ombe mmoja anatakiwa kuchungiwa kwenye eneo la ekari 6, hivyo basi kwa hekta milioni 1.3 maana yake ni malisho ya ng'ombe 541667 tu. Tukumbuke kwamba, kwa mujibu wa takwimu za mifugo tuliyonayo ni ng'ombe miliooni 21 na mbuzi na kondoo milioni 21.

Mheshimiwa Spika, idadi hiyo ya ngo'ombe tuliyonayo tunahitaji malisho ya ekari milioni 126 ambazo ni sawa na hekta milioni 50.4. Wizara ambayo inajukumu la kupanga ardhi ya matumizi

ya mifugo imetenga asilimia 2.6 tu ya mahitaji halisi ya ardhi kwa ajili ya n'gombe, na hapo bado eneo la malisho kwa ajili ya mbuzi na kondoo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji kwa takwimu hizo za mahitaji ya malisho ni kwa vipi ufugaji wetu utakuwa na tija kwa nchi na wafugaji wenyewe? Na je migogoro ya wafugaji na wakulima itamalizika kama wizara inatenga eneo ambalo halitoshelezi mahitaji?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Takwimu za Serikali zinasema kuwa Tanzania ina jula ya hekta milioni 60 zinazofaa kwa ajili ya malisho, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa "spirit" ile ile inayotumika kutenga maeneo kwa ajili ya wanyamapori itumike pia kutenga eneo la kutosha kwa ajili ya ufugaji, kwani ni dhahiri wizara imeweka lengo la kugawana kusimamia matumizi ya ardhi ya mifugo ambalo kiuhalisia haina uwezo nalo.
Mheshimiwa Spika, Ardhi kwa ajili ya uendelezaji wa ufugaji hapa nchini kwa kiwango kikubwa hutumika kijumuia bila uhakika wa umiliki na kusababisha migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, uharibifu wa ardhi na kuenea kwa magonjwa ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji ni hatua gani zilizochukuliwa kukabiliana na changamoto hiyo kwa kuwa tunashuhudia migorogoro na mauaji mengi inayoendelea kati ya wakulima na wafugaji hususan katika wilaya Kiteto na Mvomero na sehemu mbalimbali ya nchi.

Mheshimiwa Spika,Taarifa zilizopo ni kwamba Baraza la Ardhi na Nyumba-Wilaya ya Morogoro lilitoa amri (Stop Order) kuwa wafugaji waishio vijiji vya Kongwa na Kisaki kituoni wasifukuzwe hadi kesi itakaposikilizwa. Mkuu wa Wilaya ya Morogoro (Said Amanzi) alipuuza amri halali ya Baraza kwa kuamuru polisi kusimamia zoiezi hilo. Aidha, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro pamoja na Mkuu wa Wilaya walivunja amri ya Baraza iliyotaka wafugaji katika tarafa ya Ngerengere wasiondolewe hadi kesi iliyofunguliwa Mahakama Kuu (Kitengo cha Ardhi) isikilizwe.

Mheshimiwa Spika, Hoja ya msingi ni kwanini watendaji hao wa Serikali wanashindwa kuheshimu utendaji wa mhimili wa Mahakama? Kwa kuwa wao ndio wanatakiwa wawe mfano kwa wengine katika kutekeleza utawala wa sheria. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali (Ofisi ya Waziri Mkuu) kuwachukulia hatua za kinidhamu watendaji hao.

Mheshimiwa Spika, Ni ukweli kuwa wafugaji wanauwezo mkubwa kiuchumi, wanachohitaji ni ARDHI na WATAALAMU kwani huduma zingine wanauwezo wa kufanya wenyewe, na hili Watendaji wa Serikali wanalitambua ndio sababu bajeti ndogo inayotolewa kwa ajili ya huduma za mifugo kama vile majosho, malambo na dawa za chanjo haziwafikii walengwa. Sehemu kubwa zinaishia kwenye mifuko binafsi ya watendaji. Hivyo basi ni vyema sasa wafugaji wapimiwe maeneo na kupewa umiliki wa ardhi kuanzia ekari 500 kwenye mikoa yenye maeno makubwa ambayo hayana migogoro ili wayaendeleze na hiyo ndiyo itakuwa dawa ya kuacha kuhamahama.

Aidha Mheshimiwa Spika, Kambi inashauri kutungwa sheria itakayotambua maeneo ya wafuagaji dhidi ya watumiaji wengine wa ardhi hususan wakulima, hifadhi na makazi ili kupunguza migogoro iliyopo kati watumiaji hao wa ardhi;

8. RANCHI ZA TAIFA

Mheshimiwa Spika, Tarehe 30 January 2013 katika mkutano wa kumi wa Bunge Serikali ilijibu swali na 26, lililohusu ranchi zilizo mkoa wa Kagera za Kitengule, Missenyi, Mabale, Kagoma - Muleba na Kikulula - Karagwe ambapo baadhi ya maeneo yake yalikuwa yanamilikiwa kihalali

na vijiji vinavyozunguka maeneo hayo wakiyatumia kwa shughuli za ufugaji lakini kutokana na ukiritimba wa kiutendaji wa kufanya maamuzi bila kufikia maeneo husika, baadhi ya vijiji na wananchi wake wamebinafsishwa:- (a) Je, kwa nini wananchi waliokuwa wakiishi maeneo hayo wasiruhusiwe kuendelea na maisha yao kama walivyokuwa awali? (b) Je, kwa nini Serikali isiyarudishe maeneo hayo kwani waliopewa wanayakodisha kwa wafugaji toka nchi jirani? (c) Je, ni Watanzania gani kwa majina waliogawiwa maeneo kwenye ranchi hizo?

Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kutoa orodha ya majina ya Wawekezaji Watanzania waliogawiwa maeneo hayo ya ranchi

Mheshimiwa Spika, Kwa masikitiko makubwa hadi sasa ni mwaka mzima toka swali hilo liulizwe orodha hiyo bado Serikali haijanipatia. Je, huu sio udhalilishaji wa bunge na wabunge? Ni ugumu gani wa kutoa orodha hiyo? Huu ni uthibitisho tosha kuwa wengi wa wamiliki wa ranchi hizo si watanzania au si watu wenye nia ya dhati ya kuziendeleza badala yake wanazikodisha kwa wafugaji toka nchi jirani.
Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba Ranchi ziligawiwa na kupewa watu ambao hawaziendelezi, jambo la msingi ni zigawanywe upya na wapewe wafugaji ambao wana mifugo mingi ambao wanafukuzwa kila waendapo. Aidha maeneo yaliyokuwa ni kwa ajili ya mifugo kwa sasa yamebadilishwa matumizi na hivyo wafugaji wamebaki kuwa wahamaji tu. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema ni muda mwafaka sasa kurudishwa kwa wafugaji kama ilivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa taarifa ya Mtendaji Mkuu wa Ranchi za Taifa kwamba: kutokuwepo kwa uwekezaji wa maana katika ranchi kuwa kumechangia kushuka kwa idadi ya ng'ombe kwenye mashamba kutoka ng'ombe 38,736 mwaka 2000 mpaka 29,939 mwaka 2009/10 na hadi kufikia mwezi Novemba 2010 idadi imefikia 27,000. Hata hivyo ana wahimiza watanzania wenye uwezo kujitokeza kuwekeza katika mashamba ya kampuni yake. Aidha, Serikali bado anasema inatafuta na kushawishi wawekeaji kwa ajili ya mashamba ya Ruvu, Mzeri Hill, West Kilimanjaro, Kongwa na kalambo ili kuongeza uzalishaji kutoka asilimia 30 kwa mwaka kiasi ambacho ni kidogo ukilinganisha na eneo ambalo ranchi zimo.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa takwimu hizo ni aibu kwa Serikali kuwa na maeneo makubwa lakini tija yake ni ndogo sana na watendaji wanalipwa mishahara kila mwezi wakati uzalishaji unashuka kila kukicha.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kwamba itachukua miaka hata hamsini ijayo na watakao kuja kuwekeza katika sekta hii ya mifugo watakuwa wao ndio wameshika mpini huu ni udhaifu kwa upande wetu. Kambi ya Upinzani inaamini kuwa wafugaji wenyewe, hao wanaoitwa wachungaji wanauwezo wa kuwekeza kama wataeleweshwa vyema.

Mheshimiwa Spika, Ng'ombe wao wanaweza kubadilishwa kuwa fedha na wataalam wa waliopo katika Ranchi za Taifa na sehemu zingine wakashirikiana nao na matunda ya uwekezaji yakaonekana. Hivyo sera ya PPP inaweza kuwa na maana zaidi kuliko ilivyo sasa na sio lazima wawekezaji waje na mabegi ya fedha kama inavyoelezwa hapa kuwa bado wanatafutwa.

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi maalum uliofanywa na CAG kwa Ranchi za Taifa (NARCO) kuhusu mkopo TIB na CRDB wa jumla ya shilingi bilioni 3.280. Mapungufu yalionekana katika matumizi ya mikopo hiyo. Mkopo wa TIB ulikuwa na riba ya asilimia 16 kwa mwaka na mkopo wa benki ya CRDB ulikuwa na riba ya asilimia 17 kwa mwaka. Riba hizo zilikuwa juu sana ukilinganisha na faida. Kampuni ya Ranchi za Taifa imeshapata hasara ya jumla ya shilingi milioni 325.901 kutoka mwaka 2011 hadi Aprili, 2013 kutokana na riba kubwa inayotozwa kwenye mikopo hiyo. NARCO

haikuwa na udhibiti wa ndani ulio madhubuti kwenye kuangalia fedha za mauzo ya ng'ombe. Aidha, ukaguzi maalum ulibaini upotevu wa ng'ombe 376 kutoka katika Ranchi ya Ruvu katika kipindi cha kuanzia Julai, 2012 hadi Aprili, 2013. Upotevu huo ulisababisha hasara kubwa kwa shirika hilo[3].

Mheshimiwa Spika, Kwa sasa wafugaji wana CHAMA CHAO hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani inasema ni muda mwafaka Wafugaji kwa ushirikiano na NARCO kumiliki RANCHI ya RUVU. Kwani Wafugaji kupitia CHAMA CHAO wanauwezo wa kuweka mtaji na NARCO kuwekeza TAALUMA YAO. Kinyume na hapo RANCHI hiyo itatolewa bure kwa wageni wanaokuja bila fedha na kuondoka na fedha tele.

9. KUONGEZA UBORA WA BIDHAA ZA MIFUGO

Mheshimiwa Spika, Sera ya Mifugo 2006 inasisitiza umuhimu wa kuongeza thamani kwa mazao yatokanayo na mifugo ili yaweze kuingia katika soko la ushindani na pia kuyaongezea muda wa hifadhi. Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji serikali imefanya nini kuhamasisha na kuhimiza uanzishwaji wa vyama vya wafugaji na wafanyabiashara wa ng'ombe wa

[3] Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali - *Ripoti ya Mashirika ya Umma 2012/2013*

nyama na maziwa hapa nchini. Vile vile, seriakali inawandaaje wafugaji kupata mitaji na mikopo, kuboresha miundombinu ya kukusanya na kusambaza maziwa, uwepo wa viwanda vya kusindika, uhamasishaji unywaji wa maziwa na udhibiti wa magonjwa ya mifugo;

10. SEKTA YA UVUVI:

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2000, sekta ya uvuvi iliendelea kukua kwa wastani wa asilimia tano mwaka 2008 kabla ya kushuka kwa kiwango kufikia asilimia 2.7katika mwaka 2009.Tanzania ina maliasili za kutosha za uvuvi, ikiwa pamoja na maji baridi na maji chumvi, ambazo kama zingetumika vizuri zingesaidia kuboresha maisha ya watu, ikiwa ni pamoja na lishe.

Mheshimiwa Spika, Changamoto kubwa zinazoikabili sekta ya uvuvi ni pamoja na uvuvi haramu na biashara za magendo za samaki na mazao ya samaki mipakani ambazo hupunguza mchango wa sekta katika Pato la Taifa na juhudi za kupunguza umaskini. Changamoto nyingine ni pamoja na kutumia nyenzo na teknolojia duni za uvuvi, ukosefu wa mikopo, na uharibifu wa mazingira.

a. USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA UVUVI KATIKA BAHARI KUU

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani tokea mwaka 2008[4] imekuwa ikitoa ushauri kwa Serikali kuhusu jinsi ya kunufaika na uvuvi katika bahari kuu. Kambi Rasmi inarudia tena ambacho tulikisema katika bajeti ya mwaka 2008/9 na 2009/10 kuhusu uvuvi katika bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya uvuvi na hasa ile ya uvuvi wa bahari kuu (deep sea fishing) ni sekta ambayo kwa miaka mingi tumekuwa tukiipigia kelele nyingi sana kuwa Tanzania haijaitumia vizuri katika kukusanya mapato. Haya ni baadhi ya yale tuliyoshauri, Katika kuhakikisha kuwa Sekta Uvuvi

[4] Taarifa rasmi za Bunge- tarehe 16 Juni,2008

inaleta mabadiliko ya kiuchumi kwa nchi na wananchi kwa ujumla, inashauriwa bandari za Mtwara, Dar es Salaam,Tanga na Zanzibar zitenge maeneo ya bandari za samaki (Fish Ports and Fish Processing plants) ili meli zote za uvuvi wa bahari kuu zilazimike kununua mahitaji yao yote ya mafuta, maji, chumvi na vyakula wanapo kuja kukaguliwa kwa ajili ya kukusanya mapato. Aidha njia hii itakuza uchumi wa mtu mmoja mmoja kwa maana ya kuwepo kwa kile

kinachoitwa "forward and backward linkage" Kwa uamuzi huu mapato yanakisiwa kuwa Tshs.3bn ambayo Serikali ingelikusanya.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa Serikali ya CCM haisikilizi ushauri, lakini kutokusikiliza huko ni kutokana na ukweli kwamba, meli nyingi zinazovua bahari kuu zina ubia na viongozi waandamizi wa CCM na Serikali yake. Hoja ni je, nchi itaendelea kufilisiwa na kada hiyo ya viongozi hadi lini?

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa taarifa rasmi za Bunge tarehe **09.08.2012** zinaonyesha kuwa Kambi Rasmi ya Upinzani ilisema yafuatayo, kuhusu meli ya Uvuvi maarufu kama meli ya Magufuli "***Mheshimiwa Spika,*** *Mwezi Februari mwaka huu, habari zilichapishwa kuhusu "ushindi" wa Serikali katika kesi maarufu kama* ***'Kesi ya Samaki wa Magufuli'*** *iliyokuwa ikiwakabili wavuvi raia wa China wamiliki wa meli ya uvuvi ya* ***Tawariq 1*** *waliofanya uvuvi haramu katika pwani ya Bahari ya Hindi, kwenye maji yaliyo katika eneo la Tanzania. Mwezi huo huo wa Februari, gazeti la Nipashe likachapisha habari kutahadharisha kuwa meli hiyo inazama kutokana na kuwepo kwa hujuma kwa mali na vifaa vya meli hiyo kunakofanywa na baadhi ya watu ambao ni maafisa wa bandari.*

Mheshimiwa Spika, *Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya wale wote ambao meli hiyo ilikuwa chini ya uangalizi wao na ni kwa nini meli hiyo sasa haifanyi kazi wakati meli ilikuwa ni nzima kabisa na ilikuwa inafanyakazi kwa ushahidi dhahiri kuwa ilikamatwa ikiwa kazini. Ikiwa meli hii ni mali ya Serikali baada ya kushinda kesi, hujuma iliyofanyiwa na hasara inayopatikana kwa kuzama au kuja kuikarabati, tutakuwa tumetia adabu au tumetiwa adabu?*
Mheshimiwa Spika*, Aidha, Kambi Rasmi Upinzani inauliza, je, hasara ya meli hiyo ya uvuvi ikiwa ni mali ya Wachina, ikizaa kesi nyingine, tunao uhakika kweli wa kushinda tena kesi? au ndiyo tutaingia kwenye deni la gharama kubwa zaidi? Serikali yenyewe kila leo inalia na ukata, bajeti za Wizara kila mwaka wa fedha ni kuhemea kwa wafadhili na mikopo ya riba za kupaa, itazikamua wapi fedha kwa ajili ya kulipia gharama za kesi nyingine mahakamani?"*

Mheshimiwa Spika,Kwa mujibu wa taarifa zilizopo ni kwamba watuhumiwa hao wameshinda kesi na sasa Serikali inatakiwa kulipa fidia. Je kama tulivyohoji hapo mwaka 2012, kuwa je tumefaidika na nini hasa? Kwani meli imezama na hakuna faida zaidi ya watuhumiwa kukaa jela na kula chakula cha wafungwa wetu tu.

b. USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA UVUVI KATIKA ZIWA VICTORIA

7.2.1 Uchunguzi uliofanyika

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi uliofanywa na CAG ulichunguza kama Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi imefuatilia na kutathmini ipasavyo shughuli za uvuvi katika Ziwa Victoria ili kukabiliana na tatizo la uvuvi wa sangara uliopita viwango (Overfishing). Ukaguzi ulitumia taarifa za kipindi cha miaka mitatu kuanzia Juni, 2008 hadi Desemba, 2011. Pia taarifa zilikusanywa kutoka wilaya 15 zenye shughuli za uvuvi katika mikoa ya Mwanza, Kagera na Mara. Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Ofisi ya Waziri Mkuu zina wajibu wa kuandaa, kutekeleza, kufuatilia na kupitia marekebisho ya muundo wa sera na kanuni za uvuvi nchini Tanzania.

7.2.2 Mapungufu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi:

Mheshimiwa Spika, mapungufu yafuatayo, yalibainishwa na CAG**:**

(i) Kiasi cha samaki kinachokadiriwa kubaki ziwani kipo chini kupita kiasi kilichopendekezwa. Kiwango kinachotakiwa kwa Tanzania ni tani 382,500 lakini kiwango kilichopo kinakadiriwa kuwa tani 165,000.

(ii) Asilimia 50 ya wavuvi na vyombo vya uvuvi katika Ziwa Victoria havijasajiliwa.

(iii) Kuna ufuatiliaji hafifu wa shughuli za uvuvi ziwani.

(iv) Vikundi vya usimamizi wa mialo (Beach Management Units) vina uwezo mdogo katika kuzuia uvuvi haramu.

7.2.3. Changamoto za Wavuvi Ziwa Viktoria

Mheshimiwa Spika,
Kwa upande wa wavuvi wafanyao kazi zao katika ziwa hili wanakabiliwa na matatizo yafuatayo:

1. Ukosefu wa vitendea kazi, mfano ILEMELA tangia imeanzishwa mwaka 2012. Haina **"speed boat"** ya kuwawezesha maafisa Uvuvi kufanya doria dhidi ya uvuvi haramu, lakini pia kutoa huduma ya ughani katika maeneo ya uvuvi.

2. Ukosefu wa fedha kwa ajili ya kuwezesha vikundi ambavyo huhamasishwa na maafisa uvuvi juu ya ufugaji wa samaki.

3. Kuna upotevu mkubwa sana wa mazao ya samaki hasa dagaa(Post harvesting loss) na hivyo kusababisha upotevu wa raslimali muda,fedha na hivyo kupelekea wavuvi kubakia duni. Serikali itenge bajeti ya kutosha kwa maafisa uvuvi kuwafikia wavuvi na kutoa elimu ya uchakataji mazao ya uvuvi, lakini pia itenge bajeti ya kusaidia vikundi vya wavuvi kuondokana na ukaushwaji wa dagaa na mazao mengine ya uvuvi kwenye mchanga.

4. Wavuvi wadogo wanakutana na adha ya kulipa ushuru kwa kila halmashauri, mfano ni wavuvi wa Ilemela, wakivuka kwenda halmashuri ya Nyamagana, Sengerema, Ukerewe na Geita kote wanatakiwa kulipia leseni za halmashsuri husika na pengine na faini juu yake. Mheshimiwa Spika, mbona magari tunakata leseni moja na tunatembea mikoa yote ya Tanzania? Je kwa wavuvi tatizo ni nini?

Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka mpango madhubuti ya kuondoa matatizo hayo, kama yalivyoainishwa hapo awali.

a. UFUGAJI WA SAMAKI

Mheshimiwa Spika, Wizara katika majukumu yake, jukumu mojawapo ni kuendeleza ufugaji wa samaki. Kambi Rasmi kwa miaka ya nyuma tumekuwa tukisemea sekta hii kuwa bado haijapewa umuhimu unaostahili kiuhalisia, bali ni maneno kwenye vitabu tu.

Mheshimiwa Spika, Wafugaji wadogo wenye moyo wa kufuga samaki ni ukweli uliowazi kwamba bado mazingira ni magumu kwa wafugaji wenye mitaji midogo.

Mheshimiwa Spika, Ninasema hayo kwa kuangalia bei ya kifaranga kimoja ambacho hakija tenganishwa jinsia ni shilingi 100 na kifaranga ambacho kimetenganishwa jinsi (Monosex) ni

shilingi 250. Chakula kwa ajili ya kuwalisha samaki hao kilo moja ni shilingi 3500. Na kwa hali ya kawaida hadi samaki wafikie muda wa kuvunwa wakiwa na uzito wa gramu 500 hadi 700 inachukua miezi saba hadi tisa, kama ulishaji utakuwa kwa kiwango kinachotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Hoja ni kwamba, utafiti wa kuona aina ipi ya samaki inayokua hadi kufikia uzito tajwa kwa muda wa miezi saba hadi tisa ulifanyika wapi? Tunaitaka Serikali kutoa taarifa rasmi zihusuzo ufugaji wa samaki hasa kwenye "breed" ambayo imefanyiwa utafiti na kunenekana inafaa kwa mazingira yetu na sio taarifa za ufugaji wa Vietnum ambapo wataalam wanapelekwa kutembea.
Mheshimiwa Spika, Hoja hapa ni je, kwa wafugaji wenye kipato kidogo wanasaiwaje katika hili? Aidha, kwa mujibu wa wananchi walio mikoa ya Kanda ya Ziwa hasa Kagera, kifaranga komoja cha Sato kinauzwa kwa shilingi 300 hadi 500.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kujua, chakula cha kulisha samaki kwa Tanzania kinatengenezwa na kiwanda kipi na kipo mkoa gani? Kama hakipo, Wizara hii ina mpango gani wa kuingia ubia na wadau katika kuanzisha kiwanda cha kutengeneza chakula cha samaki?

11. MWISHO

Mheshimiwa Spika,kutokana na ukweli kwamba sekta hii ya mifugo na Uvuvi imekuwa haitengewi fedha wakati ina fursa kubwa ya kubadilisha maisha ya wananchi wengi wa Tanzania, na pia kutokana na ukweli kwamba kuna matumizi ambayo yenye mashaka kwenye upande wa fedha za maendeleo. Hivyo basi, ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani bajeti ya wizara hii ifumuliwe upya na Kamati yetu ya Bajeti ipangwe ili kuondoa fedha zilizowekwa kwa dhamira ovu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

……..
Rose Kamili Sukum (Mb)
Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani
Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi.
23/5/2013

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge imenibidi niondoke kwa sababu nina dharura. Kwa hiyo, namwomba Mwenyekiti aweze kuendelea na shughuli hii. *(Makofi)*

Mwenyekiti (Mhe. Mussa Azzan Zungu) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Tukae au nikae mie?

Waheshimiwa Wabunge tunaanza mjadala. Kamati imeshamaliza, Mwenyekiti na Kambi ya Upinzani wameshamaliza. Tunaanza na Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro.

MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika bajeti ya Sekta muhimu sana ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wataalam wa Wizara pamoja na Taasisi zilizo chini yao kwa kuandaa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Sekta zilizoko chini ya Wizara hii ni muhimu sana. Mifugo ni muhimu, Uvuvi ni muhimu na zote mbili zina fursa nyingi, lakini hatutanufaika na fursa hizi kama fedha za kutosha zisipowekwa katika Sekta hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imeandaa *program* mbili kuendeleza Sekta ya mifugo na *program* ya kuendeleza Sekta ya Uvuvi na ya mifugo tu yenyewe inahitaji zaidi ya shilingi trilioni moja na bilioni 300, lakini bajeti inayopatikana ni ndogo sana na haitakaa tunufaike kwa mtindo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba Wizara ijipange na Serikali kuunda Wakala wa kuendeleza Sekta ya Mifugo na Wakala wa kuendeleza Sekta ya Uvuvi na zifananefanane na *TANROAD*. Mifugo inapouzwa kiasi cha fedha kiende kutunisha Mfuko utakaoendeleza sekta hizi na katika uvuvi pia ni hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha hotuba ya Waziri, ukurasa wa 33, Mheshimiwa Waziri anaongelea jambo jema sana la kwamba kwa mwaka 2014/2015 watafanya kazi na Halmashauri tisa ili kutenga maeneo na kuhakikisha kwamba rasilimali za mifugo, hasa malisho, zinaendelezwa vizuri. Nadhani mahali pa kuanzia, naunga mkono wazo hili, lakini mahali pa kuanzia ni Serikali kwanza kuanza kuheshimu na kulinda maeneo na mipango iliyofanywa na vijiji vyenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo siri, mfano katika Jimbo langu la Kiteto, vijiji saba vimetenga maeneo yao. Wamefuata utaratibu wa Sera ya Ardhi ya mwaka 1995, Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999, Kanuni zake za Mwaka 2001, Sheria ya Matumizi Bora ya Ardhi, Vijiji vikafanya mipango yao, wakatenga maeneo ya makazi, maeneo ya huduma, maeneo ya kilimo na maeneo ya mifugo na eneo moja maalum linalojulikana kama Murtangos, wametenga kama hifadhi ya mazingira, hifadhi ya wanyamapori, pamoja na malisho ya msimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili lilivamiwa na wakulima wengi kutoka nje ya vijiji hivyo, nje ya Wilaya na nje ya Mkoa na kuanza kulima bila kufuata utaratibu na bila kuomba kibali kutoka katika vijiji hivyo ambavyo ni Kijiji cha Kimana, Namelo, Iltirikish, Emart, Nati, Engusero, Osidan pamoja na Loltepesi. Hawa walitenga jumla ya hekta 133,000 kwa matumizi yao kama sehemu ya mipango yao ya ardhi waliyoitenga. Cha kusikitisha ni kwamba wale waliovamia walienda kushitaki Halmashauri pamoja na vijiji husika. Lakini baada ya mlolongo mrefu na mchakato mrefu, Halmashauri ya Kiteto na Vijiji vyake vikashinda kesi kwenye Mahakama ya Rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi ilipotoka; *execution order* imetoka, Mahakama ikamweka *Court Broker* aliyefanya kazi nzuri ya kuwaondoa watu wote na kuvunja vibanda 8,844 na mwishoni alipohitimisha kazi hii akatoa *Handing Over Certificate* tarehe 17/12/2012 na kuikabidhi Halmashauri ya Kiteto eneo lile la Murtangos bila nyumba, bila mazao, bila watu na bila damu kumwagika. Kwa hiyo, uongozi wa Kiteto chini ya *DC* wao, walifanya kazi nzuri na kukamilisha kazi hii kama Mahakama ilivyoelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa walimao ni watu wenye *influence,* mwishoni mwa Januri 2013, mizunguko ikaanza ya watu kuanza kurudi kwenye eneo waliloondolewa, lakini baada ya *operation* ile, 2012, ni kama mamlaka yakahama kutoka Wilayani na kwenda kwenye mamlaka ya Mkoa.

Mwaka 2013 watu wamelima kinyume na amri ya Mahakama. Lakini mbaya zaidi wengi waliokamatwa watu 75 ni vibarua. Waliohalifu, wakubwa wenye hayo mashamba, hakuna aliyekamatwa, hakuna aliyeshikwa na hakuna aliyeshitakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni kitu cha kusikitisha! Mauaji na kila aina ya uhalifu unaotokea, unatokea kwenye maeneo ya pori kwa pori, kisima Na. 1, Na. 2 na haya yote ni maeneo waliyokaa watu walioondolewa katika eneo hilo, hayapo chini ya mamlaka ya vijiji husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudi kwa kusema kwamba ni muhimu Serikali itazame hili na kusimamia Sheria bila upendeleo na bila kigugumizi. Maana baada ya Desemba, 2012 ni kama shughuli hizi zimehamia kwa Mkuu wa Mkoa. Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea Kiteto tarehe 16 mwezi wa Kwanza mwaka huu, 2013 shughuli hii imetoka Mkoani, ipo kwenye *desk* lake kwa sasa kwenye Ofisi yake.

Namwomba Mwakilishi aliyeko hapo mbele, anayemwakilisha Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba hili walisimamie vizuri, na kuna Amri ya Mahakama. Tukiachia vurugu ziendelee, tukasikia kila aina ya upotoshaji, siyo vizuri, maana hili ni tatizo lililokwisha kisheria. Murtangos ni mfano wa vijiji vyenyewe kufanya kazi ambayo Mheshimiwa Waziri anaiongelea katika hotuba yake katika kitabu hiki ukurasa wa 33. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naombe Ofisi ya Waziri Mkuu isimamie hiyo Sheria ili watu wawe na halali yao. Lakini kubwa, mjadala unaoendelea pembeni na kupotosha, ukishakuwa na makazi yenye maelfu ya watu bila uongozi wa aina yoyote, kila aina ya uhalifu itafanyika. Kinachoendelea ni kujaribu kupotosha kwamba haya yanasababishwa na uchochezi na hakuna uchochezi wowote unaofanywa na Kiongozi yeyote wa kuchaguliwa au wa kuteuliwa katika Halmashauri ya Kiteto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena, Serikali isimamie hili ili haki iweze kutendeka.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Anayechangia wa pili ni Mheshimiwa Martha Umbula. Hayupo! Mheshimiwa Suleiman Masoud Nchambi, hayupo. Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mabruki, naye hayuko. Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa na Mheshimiwa Namelok Sokoine ajiandae.

MHE. ABUU H. JUMAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue fursa hii…

(Hapa Mheshimiwa Selemani Nchambi alisimama kutaka kuchangia Hotuba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi)

MWENYEKITI: Kaa chini bwana! *(Kicheko)*

MHE. ABUU H. JUMAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuweza kunipa fursa hii kusimama katika Bunge lako hili ili niweze kuchangia bajeti hii muhimu.

Pili, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuandaa bajeti yao vizuri ambayo inalenga kusukuma suala zima la uchumi nchini kwetu. Vilevile nimpongeze Naibu Waziri kwa kuteuliwa kwake, Mzee wa Songombingo. Nakufahamu mambo yako wewe mzee! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takribani miaka mitatu au minne iliyopita hivi Mheshimiwa Rais aliweka jiwe la msingi pale Ruvu kwenye kiwanda cha machinjio. Mwaka 2013 nilichangia katika Wizara hii na kubwa nilizungumzia suala zima la ucheleweshwaji wa kumaliza kiwanda kile. Mheshimiwa Rais pale alivyokwenda, kiwanda kile kilizinduliwa kwa mbwembwe kubwa na Mheshimiwa Rais aliweka jiwe la msingi na wananchi wengi walihamasishwa waweze kutenga maeneo kwa ajili ya kufuga ng'ombe wa kisasa.

Wananachi wale walifanya kazi hiyo, wametenga maeneo na wamenunua ng'ombe ili waweze kufanya shughuli zao za ufugaji. Lakini cha kusikitisha, mpaka sasa kwenye kiwanda kile na mwaka 2013 katika mchango wangu Mheshimiwa Waziri alisema mwaka huu wataweka bajeti ili waweze kumaliza kiwanda kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimepitia kitabu hiki kurasa zote sijapata kuona kuna fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kumaliza kiwanda kile. Ni tatizo kubwa. Tuna wafugaji wengi pale wanashindwa kupata huduma hiyo kwa ajili ya machinjio. Pale walihamasishwa wananchi wengi kwamba, kutapatikana ajira ya takribani vijana 1,000.

MBUNGE FULANI: Kabisa! *(Makofi)*

MHE. ABUU H. JUMAA: Vijana wangu wamejaa pale Mlandizi wanauza mahindi, *biscuit,* wakitegemea kiwanda kile kingekwisha tungeweza kupata ajira kubwa tuweze kupunguza tatizo kubwa la ajira nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naishauri Serikali kwamba Wizara ijitahidi kadiri ya uwezo wake kuhakikisha kiwanda kile sasa kinamalizika, kwa sababu pale tunapata hasara kubwa. Huduma zote za ufugaji pale, mfano huduma za machinjio tunakosa, lakini kikubwa hasara ambayo inapatikana pale ni kubwa kwa sababu majengo yale yanazidi kuchakaa na pesa za Serikali zimetumika nyingi sana ambazo sasa tunashindwa kujua ni kitu gani ambacho kitatokea baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo ameifanya ya kuboresha mashamba haya ya malisho. Pale Jimboni kwangu liko shamba moja Vikuge na katika Taarifa yake nimeona kwamba wameweza kuliboresha kwa kiasi kikubwa. Lakini naishauri tu Serikali kwamba iangalie, bahati mbaya shamba lile liko eneo ambalo siyo la wafugaji. Wafugaji wengi wako Kata ya Ruvu, Kata ya Kwala na Kata ya Dutumi. Sasa nashauri tu kwamba kwa kuwa bado maeneo ya kule tuna ardhi kubwa sana, ili kuweza kuboresha na maeneo mengine, wangetafuta sasa maeneo kule ili waweze kuweka mashamba ya malisho ili wananchi wetu waweze kupata majani na waweze kufuga vizuri, kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo moja. Wananchi wetu hawa, wafugaji wetu, maeneo ya vijijini kule elimu yao imekuwa ndogo sana. Sasa nilikuwa naishauri sana Serikali ipate muda wa kutosha ili iweze kuwapa wananchi wetu, kwa maana ya wafugaji wetu, wapate elimu ya mifugo hii waweze kufuga kisasa.

Kwa mfano, yako maeneo ambayo tumetenga kule, lakini kwa bahati mbaya wanafuga kienyeji mno, lakini maeneo yale sasa yakiboreshwa kwa maana ya kuwekewa malambo ya kutosha, majosho, dawa za mifugo hizi na wakipata elimu wanaweza wakafuga ng'ombe wao vizuri na ng'ombe ambao wana tija na wakapata soko zuri ambalo linaweza kusaidia uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo tukiendelea unakuta hata watumishi wetu sasa hivi wengi wanakaa Maofisini tu, lakini wanashindwa kwenda *site*. Sasa wangekwenda kule *site* ili waweze kuwaelimisha wananchi wetu wafuge ng'ombe vizuri zaidi, kisasa; hata katika masoko yao na minada yao kule chini. Sasa wanapata shida jinsi ya kuuza ng'ombe, sasa hivi wanauza ng'ombe mzima mzima. Lakini tukiwawekea kule katika minada yao kwamba, sasa hivi ng'ombe wauzwe kwa kilo, tutaweza kuwasaidia zaidi wafugaji wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado eneo letu katika Jimbo la Kibaha Vijijini tuna wafugaji wengi. Tuna ng'ombe wengi, lakini mwaka 2013 katika mchango wangu nilizungumzia kwamba Serikali ijitahidi kuona kwamba inajenga kiwanda pale cha maziwa ili wananchi wetu wakati wanavuna maziwa, waweze kupata soko la maziwa pale, waweze kufanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuna tatizo kubwa vilevile la maeneo. ranchi ya Ruvu ile imekuwa kubwa; sasa nilikuwa naishauri Serikali, ingeweza kutenga maeneo mengine kupunguza ile ranchi ya Ruvu, wafugaji wetu waweze kupata maeneo ili waweze kufuga kisasa zaidi kwa sababu, sasa hivi wanatanga tanga tu katika maeneo mengine na wakati ranchi ile haina kazi kubwa pale. Kwa hiyo, ikiweza kutenga eneo kama hilo, basi tunaweza tukafanya vizuri zaidi katika kuwasaidia wafugaji wetu.

Mhshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

(Hapa Mbunge fulani alimnong'oneza Mheshimiwa
Abuu H. Jumaa aongelee na Watu wa
Sumbawanga)

MHE. ABUU H. JUMAA: Hawa watu wa Sumbawanga wanafuga nini bwana? Tulia!

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Namelock Edward Sokoine, na Mheshimiwa Nchambi ajiandae.

MHE. NAMELOK E. M. SOKOINE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kupata nafasi ya kuweza kuongoza Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imebahatika kwa kuwa na rasilimali nyingi, kubwa za mifugo na uvuvi, lakini uchangiaji wake katika pato la Taifa ni mdogo mno. Hili linasikitisha sana na linachangiwa na bajeti ndogo ya Wizara. Hata bajeti inapokuwa ndogo, fedha hizo hazipatikani kwa wakati, na hata zisipopatikana kwa wakati, wakati mwingine fedha zinapatikana kidogo mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naiomba Serikali ione ni kwa namna gani Wizara hii itasaidiwa ili iweze kupata fedha zake zote kwa wakati hata kama ni ndogo, lakini ili Wizara iweze kutimiza yale yaliyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo matatizo mengi katika sekta hii. Tulikuwa tunaomba Wizara ituambie, imejipangaje ili iweze kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi? Kwa sababu mifugo mingi tuliyokuwanayo haijaendelezwa.

Mfano, mifugo tu tuliyokuwanayo, hii ya kienyeji, ng'ombe mmoja hutoa kati ya lita moja mpaka lita tatu kwa siku, wakati mifugo iliyoendelezwa hutoa kati ya lita 10 hadi 16 kwa siku. Halikadhalika hata ng'ombe wa nyama tuliokuwanao wengi hawajaendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili ng'ombe mmoja akue na kuwa na mpaka kilo 200 hadi 250 anachukua takribani miaka minne mpaka mitano, lakini mifugo iliyoendelezwa huwa na kilo hizo hizo kwa muda wa miezi 18 tu. Je, Wizara imejipangaje katika kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi ili waweze kufaidika na mifugo wanayokuwanayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyotangulia mchangiaji aliyepita kuelezea, pia lipo tatizo lingine la ukosefu wa miundombinu ya kutosha kwa ajili ya mifugo, majosho, maji, lakini pia maeneo ya kulishia mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunaomba Serikali ifanye jitihada za haraka kuhakikisha kwamba maeneo ya kutosha kwa ajili ya wafugaji yanapatikana. Pia liko tatizo la ukosefu wa Wagani wa kutosha, na pia lipo tatizo sugu ambalo kila mtu analifahamu la ugomvi kati ya wakulima na wafugaji na tatizo hili hata hivi sasa, mfano mdogo tu, hili linaloendelea Kiteto, watu wanapoteza maisha yao, lakini ukiangalia tatizo kubwa ni Serikali kuchelewa kupanga matumizi bora ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hata katika sekta ya uvuvi nilikuwa nashauri Wizara ione ni kwa namna gani sasa wavuvi nao wataanza kupatiwa mikopo midogo midogo na kupatiwa ruzuku ili iweze kuwasidia kama wanavyopata wakulima kwenye pembejeo, lakini pia kama wanavyopata wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri yafuatayo yaweze kufanyika. Kwanza kabisa, ili sekta hii iweze kuweza kuchangia katika pato la Taifa, nilikuwa nafikiria Serikali iwekeze vyakutosha katika sekta hii. Nina uhakika Serikali itakapowekeza katika sekta hii vya kutosha, ni rahisi sana sekta hii ikanyanyua wafanyabiashara, lakini pia kuongeza pato katika Taifa.

Aidha, Serikali ichukue hatua za makusudi kabisa, lakini za haraka, maana imekuwa muda mrefu sana kuna uogomvi mkubwa kati ya wakulima na wafugaji. Hata hivi sasa kuna huo ugomvi Kiteto; juzi juzi tumeona kwenye hifadhi zetu ng'ombe wameuawa, lakini jambo la kusikitisha, mpaka hivi sasa Serikali haijasema imechukua hatua gani kukomesha mambo kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika uvuvi zipo meli nyingi zinakuja kuvua katika Bahari Kuu na meli hizo zapata 200, kwa hiyo, tunapoteza fedha nyingi sana. Nilikuwa nashauri pia, Serikali ifanye jitihada za makusudi kununua vyombo vya kisasa ili waweze kufanya doria katika Bahari Kuu. Iwapo Serikali inaona haina fedha za kutosha, basi waone ni jinsi gani wanaweza waka-*subcontract* hiyo kazi, wakatafuta vyombo vingine, wakawasaidia kufanya ulinzi, yaani kukawa na kitu fulani kuliko kuwaachia kama hivi sasa, watu wanakuja wanaendelea kuvua samaki katika Bahari Kuu na nchi yetu inaendelea tu kuwa kama shamba la bibi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nililokuwa nataka kuzungumzia ni kuona ni jinsi gani sasa Serikali inaweza ikajenga Bandari kwa ajili ya uvuvi ili meli zote zinazokuja kwa ajili ya uvuvi ziweze kupita pale, kukaguliwa na kuona vibali, ili tuweze kujua ni kiasi gani wamevua badala ya ilivyo hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, lakini naomba pia Mheshimiwa Waziri atakaposimama atuambie Wizara yake imejipangaje katika hayo niliyomwomba atueleze? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabheja sana. Awali ya yote naomba nimshukuru Muumba wa Mbingu na nchi; niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dkt. Kamani, kaka yangu na Mheshimiwa Telele, kwa kazi nzuri waliyoianza. Kwa sababu kitu kikubwa walichonifurahisha baada tu ya kuingia katika Wizara, Ofisi zilihamia katika maeneo mbalimbali ya nchi ili kuona maeneo yao wanayoyaongoza yanakwendaje. Nawapongeza sana na mwendelee hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mawaziri wengine waige mfano, wasikae Dar es Salaam kwa ajili ya kula *prawns* na *chips,* watoke waende *site* mkaone matatizo, waisaidie Serikali na wananchi. Igeni mfano wa Mheshimiwa Dkt. Kamani na Mheshimiwa Telele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe pole sana kwa wafugaji wangu wa Kata ya Mwamalasa, Kijiji cha Magalata na wengine wa jirani zetu Igunga kijiji cha Sakamaliwa kwa mapigano yaliyotokea na kusababisha maafa. Nawapa pole sana na ninawaahidi kwamba tupo pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi kwa *DC* wangu, Kondoo Nyeupe, ndugu yetu Nkambako *DC* machachari wa Kishapu kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kuongoza na kuendesha Kamati mbili za Ulinzi na Usalama za Wialaya ya Igunga na Kishapu wakati wa mapigano yalipotokea. *DC* alikesha mbugani, aliongoza Kamati ya Ulinzi na Usalama baada ya *DC* wa Igunga kuwa mbali. Mambo yalikwenda vizuri; na wafugaji na wakulima walipata faraja kubwa.

Vile vile nampongeza Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, ndugu yangu Ali Nassoro Funga kwa kuongoza Kamati ya Ulinzi na Usalama mchana kutwa kuhakikisha mapigano ya wafugaji yaliyotokea katika Wilaya ya Igunga na Kishapu yalikwenda vizuri na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri niliongea naye na Naibu aliagizwa Telele kuja alikwenda katika kijiji cha Magarata aliongea na wafugaji na wakulima na mambo yanaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema na kushauri kwa wenzangu, wamesema hapa waliochangia hasa Kambi Rasmi ya Upinzani walipotoa maoni yao na kusema Serikali ya Chama cha Mapinduzi siyo sikivu na haifanyi kazi. Eneo la utawala na raia walioko nchi hii, asilimia 78.2 takribani ya Watanzaia wote ni wafugaji na wakulima.

Kwa hiyo, kama hawajafikiwa na maeneo, ni bora tukawa tunashauri maeneo kwamba Mawaziri hawa waelekezwe na washauriwe wafike kama walivyofanya katika Wilaya ya Kishapu na Igunga.

Ndugu zangu nataka nitoe idadi ya mifugo tuliyonayo. Mimi ni mfugaji, Mheshimiwa Waziri unafahamu, na-*declare interest* ni mfugaji mkubwa sana wa ng'ombe, mbuzi, kondoo na kuku. Mifugo tuliyonayo iliyoko katika ardhi yetu ya Tanzania mimi huiita ni dhahabu

inayotembea. Sioni sababu ya kuendelea kufukua ardhi na kuchimba dhahabu iliyoko chini wakati tunayo dhahabu inayotembea juu ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhahabu hii inayotembea tunao ng'ombe nchi nzima milioni 22.8, tunao mbuzi milioni 15.6, tunao kondoo milioni saba, tunao kuku wa kienyeji wenye supu safi kutoka Kishapu Shinyanga na maeneo mengine ya Singida milioni 35.5, tunao kuku wa kisasa milioni 24.5 na hawa wengine nisiwataje kwa imani ya dini yangu wako milioni mbili. Jumla ya mifugo tuliyonayo takribani ni milioni 107. *(Makofi)*

Sasa mimi niwaombe Waheshimiwa Wabunge, kama Watanzania tuko milioni 45, mifugo wetu wako milioni 107, najua mifugo hawaendi shule, hawahitaji lami, lakini bajeti tunayowatengea tutaendelea kuwalaumu Mawaziri. Sisi Wabunge tunayo mamlaka ya kutetea bajeti hii iwe pana ili wafugaji wetu waliopo Kiteto, Kishapu, Morogoro, Rukwa, Kigoma na maeneo mengine, watengewe maeneo kwa ajili ya ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila kitu ni gharama! Waheshimiwa Wabunge humu tusiwe tu tunapiga porojo, lazima tuangalie umuhimu wa suala hili. Kama wapiga kura wangu wa Kishapu asilimia 88 ni wafugaji na wakulima, kwa bajeti hizi tutakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwasaidie hawa Mawaziri. Vinginevyo, Dkt. Kamani mimi najua unafanya kazi nzuri sana na Naibu na Katibu Mkuu wako, tunawasiliana kwa karibu sana. Pongezi zetu sisi, lazima sasa tuwawashie mshumaa tuhakikishe tunasukuma bajeti ya kutosha kwa ajili ya wafugaji. Ni nani asiyekula kuku? Ni nani asiyekula ng'ombe? Ni nani asiyekula samaki humu ndani? Ni watu wachache sana, tena baada ya kuzuiwa na Daktari na akizuiwa mtu kula mifugo, basi unamwona anaugua kabisa utafikiri ameambiwa kesho unatakiwa kuingia kaburini. *(Makofi)*

Ndugu zangu, mimi niwaombe sana, suala la mifugo lipewe kipaumbele. Kishapu sisi tunaye Mkuu wa Idara, Dkt. Alphonce. Mheshimiwa Waziri ulifika, tulikupa *yoghurt* ya kutoka Kishapu, yoghurt tamu, Daktari anatengeneza kama zile zilizoko *South Africa.* Anatengeneza *yoghurt* nzuri, mazao ya mifugo ni mazuri.

Naomba nikushauri Mheshimiwa Waziri, Ofisi yako ulihamishia katika Wilaya na Majimbo, endelea kufanya hivyo, tenga maeneo kwa ajili ya wafugaji na wakulima; shirikiana na Wizara; alipokuja Naibu Waziri Telele, aliahidi kuleta Tume ndani ya wiki mbili. Tume itakayotoka TAMISEMI, Baraza la Mazingira, Wizara ya Ardhi na mimi nasema ongezea na Wizara ya Sheria, Naibu pale najua yupo *sharp* sana dada yangu, Mheshimiwa Angela; waje wakae ili likihitajika suala la Kisheria, Wizara ipo; likihitajika suala la ardhi na vipimo, Wizara ipo; yakihitajika masuala ya matumizi bora ya ardhi, Baraza lipo; likihitajika suala la mifugo, Waziri upo na mimi Mbunge wa Kishapu nipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Kishapu ni *sharp*, watu wetu ni sharp, hata mifugo yetu ni *sharp*. Arusha kule ndugu zetu wanakula nyama kutoka Kishapu.

Dar es Salaam wanakula kuku na nyama kutoka Kishapu. Tuko tayari kushirikiana na Wizara. Wakati ukijibu hoja Mheshimiwa Waziri nihakikishie ni lini Tume hiyo utakuja nayo wewe mwenyewe tukiambatana na Mbunge wa Kishapu? Tutakualikia Madiwani wa Kishapu, tutakualikia Viongozi wote wa siasa wa vyama vyote tukae tujadili ni namna gani tutatatua migogoro ya wafugaji na Waziri wa Kilimo tumwongeze ndani na yeye tutenge maeneo. Mkishatutengea maeneo, watu wetu ni wazuri sana Kishapu na Watanzania wote ni wapole. Tukishaainisha wakulima ni hapa, tukishaainisha wafugaji ni hapa kama Kiteto. *(Makofi)*

Kiteto suala linalogombaniwa ni sehemu ambayo ilikuwa hifadhi. Kama ni hifadhi, kwa nini mkulima au mfugaji aingie ndani ya hifadhi? Sheria hairuhusu! Kwa nini atetewe mtu wa upande mmoja?

Mheshimiwa Waziri, Tume hii iunde haraka. Wakati unafanya *wind-up* naomba sana ndugu yangu, kama ulivyo, nipe majibu; lini unaanzia Kishapu, utaenda Kiteto na maeneo mengine? Tuwakomboe Watanzania. Watu wanapigana kwa sababu ya kutokuwa na elimu tu, wakielimishwa mambo yanakuwa ni mazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, obheja sana, obheja kulumba. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Cheyo, na Mheshimiwa Sanya jiandae.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Halafu pia mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema tuna wafugaji wawili kama Mawaziri. Kama hii Wizara sasa itawashinda, sijui tutakimbilia wapi! Mimi nina hakika baada ya kuona hii hotuba, tunaweza kuwa na matumaini kwamba labda tutasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ambalo nataka kuomba kwa niaba ya wafugaji, ni heshima kwa wafugaji. Ni hilo tu! Zaidi, ni heshima kutoka kwa Serikali yao, iwathamini wafugaji. Saababu ya kuwathamini wafugaji, ndugu yangu wa Kishapu ameeleza vizuri. Leo Dar es Salaam ng'ombe 1,000 kila siku zinachinjwa kwa ajili ya watu wa Dar es Salaam tu. Bila wafugaji pale hakuna mchuzi, hakuna sijui nyama choma na vitu kama hivyo.

Kwa hiyo, jicho la Serikali ambalo linawabeza wafugaji, lugha ya kuwaambia nyinyi mnatembea sijui maili ngapi, mmekonda sawasawa na ng'ombe zenu, lugha kama hizo hazifai. Tunachohitaji ni kuwaelimisha hawa wafugaji. Wafugaji sio masikini. Hilo tungeliweka kabisa katika vichwa vyetu. Mtu ana ng'ombe 1,000, huyo mtu sio maskini. Ng'ombe mmoja leo Dar es Salaam ni 700,000/=. Elfu moja mara laki saba ni Shilingi milioni 700. Nani kati yetu hapa ambaye ana akiba ya Shilingi milioni mia saba? Kwa hiyo, tulichokosea tu, hatutajua namna ya kutumia utajiri huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza mimi naona ni elimu. Wafugaji wetu na mimi natoka sehemu ya wafugaji, nataka kuwaambia lazima sasa tuanze pia kugeuza tabia zetu. Utamaduni tu wa kujivunia kwamba nina ng'ombe wengi, nitatumia ng'ombe wangu kuoa wake watano; hayo mambo yamepitwa na wakati. Mfugaji wa leo aone ng'ombe wake ni biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kuna mfugaji mmoja juzi hapa ameonana na Mheshimiwa Kinana, huyu bwana ameuza baadhi ya ng'ombe zake, kajenga nyumba nzuri, ana vitara ambayo anatembelea kuangalia ng'ombe zake na sisi wote ambao tumesoma, tunazungumza juu ya Texan. A Texan ni Mwamerika ambaye anaangalia ng'ombe, na kofia yake inajulikana. Ukimwangalia, kweli ni mtu ambaye anaheshimika na ni tajiri. Tunataka Matexan wengi katika nchi yetu, na wapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ya Serikali kuchukua Helkopta kufuata ng'ombe na kuwapiga, nimefurahi Mheshimiwa Waziri umekemea jambo hili. Hili jambo likome kabisa! Hatuna ugomvi na wafugaji, tunachohitaji ni kuwaelimisha tu. Tayari wengine wameshaelimika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunalia vijana hawana kazi, wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri unatoka Lamadi kwa wafugaji, ukiweza kunenepesha ng'ombe 25, ukawapeleka Dar es Salaam, una mamilioni. Hiyo ndiyo elimu tuwape watu wetu.

Nami nataka waelewe hilo, kwa sababu njia ya kuweza kuwanenepesha ni kutumia mashudu ya pamba, ni kutumia mashudu ya alizeti na vitu kama hivyo. Wakitumia mashudu ya alizeti, mashudu ya pamba, hata bei ya pamba pia itaweza kupanda kwa sababu kuna bei ya humu humu nchini badala ya kutegemea bei kutoka nje. Tuwapatie elimu hiyo, inawezekana.

Kama kuna mikopo kwa ajili ya vijana, tuwakopeshe hawa, wanunue ng'ombe 25, wanenepeshe halafu wapeleke wakapate pesa. Ndiyo namna ya kuondoa umaskini, lakini siyo kuwabeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile *operation* tokomeza ilikuwa mbaya kwa wafugaji. Tufiche tunachotaka kuficha, lakini hii ni utovu wa haki za binadamu. Leo naambiwa kuna watu ambao wana mazizi kule kwenye maeneo tengefu, nenda ukayatafute hayo mazizi, wanashikilia ng'ombe za watu; hizo ng'ombe zirudi kwa wenyewe. Halafu zungumza na huyu ndugu yangu Nyalandu, lazima tukae pamoja. Tunachogombea kati ya wanyamapori na ng'ombe, ni malisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusijidanganye, kama tunajua kuna malisho pale kwenye haya maeneo tengefu, kuna Sheria au vipi, watu wanapeleka. Nawe Mheshimiwa Waziri unajua watu wanachunga mle. Mimi ninachosema, kama ni mambo sasa yanafanyika, tutafute njia ya kuyahalalisha.

Kama vile Ngorongoro wanaweza kuishi ng'ombe pamoja na wanyamapori, sioni kwa nini Ng'waswale, Longalombogo, Ng'wang'wari na sehemu nyingine ambako tayari wanapeleka ng'ombe, wanachunga na wanawalipa wale Maofisa wa Wanyamapori, kwa nini hiki kitu isifanywe halali, na kama kuna kulipa tulipe Serikalini? Kuliko kwa hivi sasa tunawanyima malisho, baadhi ya wananchi wanatozwa fedha, wengine wanawekwa Magerezani bila sababu. Zungumzeni hiyo *agenda,* inaweza ikatufikisha mbali. Tunacholilia ni malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ranchi zimesemwa. Ranchi zetu hazina ng'ombe lakini yana chakula cha ng'ombe. Kwa hiyo, kama kuna ranchi ambazo tunaweza tukazikata tukawapa watu, tuwape.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Ni zamu ya Mheshimiwa Sanya, na Mheshimiwa Ridhiwani, ajiandae.

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nakumbushia tu kwamba mwaka 2013 niliondoa Shilingi na Wizara hii ikazidishiwa bajeti yake kwa Shilingi bilioni ishirini. Matokeo yake, mwaka huu tunaona katika vitabu vya Mheshimiwa Waziri kwamba kati ya fedha za maendeleo Shilingi bilioni ishirini na tatu wamepata Shilingi bilioni 3.8 ambayo ni asilimia 13.4 tu. Watafanya nini hawa na lawama zetu zitakuwa kwao kama vile wao ndio wanaoishikilia hii Wizara na fedha zinatoka mifukoni kwao?

Mheshimiwa Mwenyeikiti, ninachotaka kusema ni kwamba Bunge letu halina meno. Tunachukua maamuzi ndani ya Bunge tunayapeleka kwenye Kamati ya bajeti, matokeo yake fedha zinaongezwa, bajeti inayofuata unaona kila Wizara haikupata hata asilimia 50 ya fedha hizo. Tunaelekea wapi? Kesho kutwa tuna Serikali za Mitaa, chaguzi; kuna Bunge la Katiba, uandikishaji, uhuru sherehe, Sherehe za Muungano, kuna Uchaguzi Mkuu; hizi fedha ambazo

zimeingizwa katika vitabu vya Wizara mbalimbali, hazitapatikana kutokana na fedha zinazohitajika katika mambo haya na mtakuja kutuambia mwakani mwezi kama huu, hapa hapa!

Mheshimiwa mwenyekiti, tuna ng'ombe, hatuli nyama. Tuna maziwa, hatunywi maziwa; tuna ngozi, hatutengenezi viatu; tuna matunda, hatuyasindiki; tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Waziri, ningekutaka baada ya Bunge hili, toka mara moja, nenda Saudi Arabia, kazungumze na Viongozi wa Saudi Arabia, utafute soko la kondoo na mbuzi. Wanakwenda Mahujaji milioni tatu kila mwaka na ibada yake haikamiliki kama hajachinja mbuzi au kondoo. Utalipata hilo soko! Yuko Waziri maalum kule Saudi Arabia, anakaa pale kushughulikia masuala ya ibada ya hija. Chukua kondoo Arusha, Mbeya, Iringa weka Bagamoyo mwezi wa mfungo mosi. Mfungo wa pili tia ndani ya meli safirisha peleka Saudi Arabia, ndiyo kuinuka kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni Wizara zenye sekta muhimu ambazo zinaweza zikatupa fedha tukatumia kwa Wizara ya Afya, Wizara ya Elimu ambazo hazina uzalishaji. Lakini tuko makini kwa hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mbuzi, kondoo kutoka Saudi Arabia wanaagizia kutoka Brazili. Tazama *distance from* Brazil mpaka Saudi Arabia na tazama *distance* yetu *from* Dar es Salaam *to Saudi Arabia* tena tuna historia na hawa watu. Nenda Mheshimiwa Waziri, kama huna tiketi njoo mimi nitakutolea tiketi na pesa za hoteli nitakulipia mimi. Wewe kazungumze na Balozi akupe *connection* ufanye hiyo kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna *fishing industry,* hatuvuni samaki. Matokeo yake nini? Kazi yetu kubwa ni kukamata nyavu zenye tundu dogo na kupiga moto. Hatuna *fishing port*; hata ile *feasibility study* ya *fishing port* haijafanyika, hatuna fedha hizo? Tutachangisha sisi hapa Wabunge tukupe; kila mmoja atatoa Sh, 100,000/= au Sh. 500,000/= ili ukafanye, potelea pote! Lakini wananchi wawe na mategemeo, wawe na matumaini!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna *college* za *fishing industry* iko Nyegezi, Mbegani, Kigoma, Rorya lakini nenda kaone, wanayo madarasa, wana *computer*, wana maktaba, hawana chochote! Tutavuna lini hao samaki? Kuanzia Tanga, Dar es Salaam, Mtwara mpaka Lindi, samaki wanazaliwa mpaka wanakufa, sisi tumebakia kula dagaa. Meli moja tu iliyokuja ikakamatwa ya Mheshimiwa Magufuli, mpaka leo ndiyo hiyo hiyo meli moja tu. Kuna meli ngapi zinavuna kule sisi tumelala huku? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tusianzishe mfumo wa kwamba fedha inayopitishwa kwenye Bunge, ipitishwe itoke kweli. Mheshimiwa Waziri mimi leo niko na wewe, unihakikishie hizi fedha zilizotengwa mwaka 2013, umepata 13.4% basi upate angalau 50% kabla ya bajeti ya mwakani ambayo bado mwezi mmoja. Hapo ndiyo nitaona kwamba Serikali iko *serious* kuwajengea mazingira hawa wafugaji, kuwajengea mazingira hawa wavuvi.

Leo ukinenepesha ng'ombe mmoja tu ukachukua madume kutoka Kenya, ng'ombe mmoja leo anafika Sh. 1,470,000/=, tuko wapi? Tuna *22.8 million* ya ng'ombe hapa, maziwa tunazalisha kiasi gani ya kusindika? Lita 138,000. Yaani kila ng'ombe mmoja ametoa tone moja la maziwa. Hata ukichukua hilo tone moja kwa kila ng'ombe, basi una zaidi ya lita milioni moja. Tunavuna wapi?

Mheshimiwa Waziri, nakwambia kama utachukua ng'ombe kwa miaka mitatu, ng'ombe milioni moja tu, Mikoa mbalimbali, ukawaweka na kuzifunga kwa njia za kisasa, ng'ombe hao

wataleta tija na watatengeneza fedha za kuendesha bajeti za Serikali za Wizara ambazo hazizalishi. *(Makofi)*

Vunjeni hii Wizara ya Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum, fedha zake ziingizeni kwenye hizi sekta. Ukweli wenyewe, hii Sekta ya Kilimo na Sekta ya Uvuvi ilikuwa itengenezewe Wizara mbili tofauti. Hizi ni Sekta kubwa muhimu kwa wananchi wetu na kwa Watanzania kwa kuongeza fedha za kigeni katika nchi. Tunazungumza nini? *(Makofi)*

Mwaka 2013 ukienda kuchukua vitabu na *Hansard,* tunayozungumza hapa ya mwaka huu, ndiyo hayo hayo! Ya mwakani, ndiyo hayo hayo! Wamasai hawanenepi wao, wala hawanenepi ng'ombe wao; wanazunguka tu Tanzania nzima kwenda kushoto, kulia, Kusini, Magharibi, hawana elimu! Wapewe elimu hawa ndugu zetu, wapewe na vitendea kazi, yajengwe majosho, zipatiane chanjo za kisasa, malisho bora, mwone kama hamtapata soko.

Mheshimiwa Spika, soko lipo! Nenda Saudi Arabia, wana soko, Oman wana soko, Kuwait wana soko, Qatar wana soko, Ras el Hima, Oman na kila mahali liko soko. Lakini Tanzania nzima *abattoir* zipo mbili au tatu. Tunachinja ng'ombe kama vile tuko ugangani. Eeh, ng'ombe wa waganga. *(Kicheko/Makofi)*

Dar es Salaam peke yake, tunajisifu eti ng'ombe 1,000 kila siku. Dar es Salaam wana uwezo wa kula ng'ombe 3,000 kila siku, lakini uwezo; *circulation of money* haipo, hawana uwezo, tuwajengee uwezo, tujenge uchumi imara kwa kuzitumia hizi sekta mbili ya ufugaji na Sekta ya Uvuvi. *(Makofi)*

Nenda Namibia wanavuna samaki, nenda Moritania wanavuna samaki, nenda *South Africa*, wanavuna samaki na wana sheria za kulinda maeneo yao ya bahari wanayoyamiliki. Sisi hata helikopta moja hakuna. Helikopta tuliyokuwa nayo ya Polisi ni moja; mpaka mahali paingie moto, watu wagombane huko *CUF* na CCM ndiyo helikopta hiyo itakwenda, papapapa! *(Makofi/Kicheko)*

CCM mnaonekana mmechoka, mwakani tuwaondoeni tukae sisi mwone ng'ombe tutauza vipi, mbuzi tutawauza wapi, maziwa atakunywa nani na samaki tutawavua vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ningependa sana kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kupata uteuzi, maana ameaminika kwamba sasa migogoro ile ya wakulima na wafugaji kule Chalinze itakwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inafahamika kwamba Jimbo la Chalinze ni moja kati ya Majimbo ambayo wakazi wake ni mchanganyiko baina ya wakulima na wafugaji. Lakini kwa upande mmoja au mwingine, katika maisha waliyoishi wazee wetu mpaka kufika miaka 2005 kuja juu huku, tumekumbwa na tatizo kubwa la migogoro, ambayo imetupelekea watu kuumiza hasa kwa mfano pale katika Kijiji cha Kimange, ndugu yangu Juma Mkombozi alipata balaa hilo akizuia ng'ome wasiingie shambani kwake, akapigwa mpaka akavunjwa na kiuno, na hivi tunapozungumza bado yuko kitandani anaugulia, hatuelewi hatima yake itakuwaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, tumeendelea kupata matatizo katika eneo la hifadhi ya Wami hasa katika chanzo cha maji, ng'ombe wanavamia, maji yanachafuka mpaka hata mitambo yetu ile nayo inapata shida sana kufanya kazi na maji yanakuwa machafu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme hili kwa sababu nina imani na Mheshimiwa Waziri na anaweza kuangalia juu ya *management* ya ng'ombe hawa hasa katika lile linalosemwa na wengi hapa, ufugaji wa kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, napenda nichangia katika jambo kubwa ambalo limeendelea kufanyika ndani ya eneo hili la mifugo hasa katika kuona afya za ng'ombe hawa zinaimarika vipi.

Moja ya tatizo ambalo tumelipata ndani ya Jimbo la Chalinze katika kipindi hiki cha mvua kubwa ni uharibifu mkubwa wa majosho ya kuogeshea ng'ombe hawa. Kwa mfano, katika Kijiji cha Makweza, Magulumatali, Matuli, Msata na Mkenge uharibifu mkubwa sana wa majosho umetokea. *(Makofi)*

Mimi nina imani kwamba Waziri analisikia hili na kwamba tutakapotoka hapa wakati anakwenda Ofisini Dar es Salaam, basi atanichukua mimi tufike Chalinze pale tusimame hapo hata kwa dakika mbili, tatu ili aweze kusikia kilio cha wananchi wale. *(Makofi)*

Pamoja na hayo, imekuwa ni hadithi ya muda mrefu sana juu ya josho la Kijiji cha Lulenge, Kitongoji cha Lulenge, Kijiji cha Miono na Kihangaiko. Sasa nafikiri Mheshimiwa Waziri, nikiangalia katika hotuba yako ya maelezo haitaji vijiji hivi isipokuwa inaonyesha tu kwamba mna mpango mzuri wa kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie nafasi hii pia kukuuliza Mheshimiwa, mna mpango gani katika eneo hili? Lakini kipo kilio pia kwa watu wa Bagamoyo kwa maana ya Wilaya nzima, ukiunganisha Jimbo la Bwana Kawambwa, Jimbo la Bagamoyo na Jimbo langu la Chalinze juu ya upatikanaji wa chanjo za mifugo. *(Makofi)*

Mwaka 2013 katika bajeti ya mwaka 2012/2013, maombi yaliyoombwa, kilichopatikana kwa Bagamoyo ni asilimia 35 ya mahitaji yote. Sasa nataka nimuulize Mheshimiwa Waziri pia, wana mpango gani; maana nimeona wametaja vitu vizuri vizuri humu ndani, lakini nayo pia nachelea kusema kwamba Jimbo la Chalinze sijaliona.

Pamoja na hayo, liko jambo kama lililosemwa na mchangiaji, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kaka yangu Hamoud juu ya ucheleweshwaji wa ukamilikaji wa mradi wa machinjio Ruvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, labda nikuambie tu, katika eneo letu lile mimi naamini utakapofungua mradi huu, moja ya kitu ambacho utakuwa umetusaidia hasa ni kuondoa migogoro isiyo ya lazima. Mimi naamini tatizo kubwa tulilonalo ni ufinyu wa maeneo ya kulishia, ambapo kutokana na hilo, inapelekea watu kutembea eneo lote la Jimbo la Chalinze wakitafuta malisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakapofungua machinjio ina maana watu watabadilisha hata staili ya ufugaji wao. Kwamba sasa siyo tu watakuwa wanafuga katika maana ya kutafuta sifa ya wingi wa ng'ombe lakini pia watakuwa wanafuga katika kutafuta maisha bora, kuishi pazuri na kuwa na familia zilizo bora na pia kupeleka wanafunzi au vijana wetu mashuleni. *(Makofi)*

Pia nikupongeza Mheshimiwa Waziri na Wizara yako kwa kuendelea kuimarisha Bodi ya nyama. Maana nimeona na kwamba sasa afya zetu walaji nazo zitakaa vizuri. Lakini pamoja na hilo pia niendelee kukupa rai, mwendelee kutoa elimu ya ufugaji bora, lakini pia tuangalie mabadiliko ya sheria ili kuweza kuwalazimisha watu waweze kufuga kisasa. Maana tukiachia kila mtu aamue anachokitaka yeye, haitawezekana.

Pamoja na hayo, mpango bora wa matumizi ya ardhi, Mheshimiwa Waziri ningependa hili nalo uliangalie na katika majumuisho yako, ungetuambia watu wa Chalinze pia una mpango gani juu yetu, maana Mvomero kazi nzuri sana imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Namwita Mheshimiwa Ali Khamis Seif, ajiandae Mheshimiwa Peter Serukamba, hayupo; atafuatia Mheshimiwa Michael Lekule Laizer.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na uzima na kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu. Licha ya kuwa Tanzania ina karibu hekta milioni 60 ambazo zinaweza zikafugwa mifugo mbalimbali, lakini bado kuna migogoro baina ya wakulima na wafugaji. Mifano iko hai, Kiteto imezungumzwa vya kutosha pale, Mvomero yako matatizo hayo, Kilosa, Kilombero na kwingineko kwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika kuliona hili mwezi wa Aprili mwaka 2010 walileta Miswada miwili Bungeni, inayohusiana na suala mifugo.

Muswada wa kwanza ulikuwa unahusu sheria inayoitwa, Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo. Hii ilikuwa ni sheria Na. 12 ya mwaka 2010 ambayo ilikuwa inaitwa kwa Kiingereza, *The Livestock Identification, Registration and Traceability Act* ya mwaka 2010. Lakini sheria ya pili ambayo imeletwa ililetwa wakati huo ni sheria Na. 13 ya mwaka 2010, inaitwa Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo, yaani *The Grazing Land and Animal Feed Resources* ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilipoleta Miswada hii katika mwaka huo ilisema kuwa, ili kuondoa matatizo haya ya wafugaji na wakulima basi Wabunge tuhakikishe kuwa sheria mbili hizi zinapitishwa ili baadaye zisainiwe na Mheshimiwa Rais na kuwa sheria. Kwa kadiri ninavyofahamu, sheria hizi au Miswada hii ni sheria ya nchi sasa. Lakini inavyoonekana, labda Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho hapa atatueleza, sheria hizi mbili zimetusaidia kwa kiasi gani katika kuondoa matatizo yaliyopo baina ya wakulima na wafugaji? Au kama sheria hizi zilikuwa na lengo zitungwe, zibaki katika makabati, watueleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtindo huu, kwa kasi hii, hatufiki mahali. Kwa sababu sheria hizi ni toka mwaka 2010 na huu ni mwaka 2014, ni miaka mine. Siyo ajabu ukaja kuambiwa kanuni za sheria hizi hazijatungwa. Siyo ajabu! Maana kuna uzoefu kuwa sheria za nchi hii, kanuni zinaweza kuchukua miaka mitano mpaka saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sheria hizi hazitumiki, au tuseme Serikali hawaoni migogoro? Kwa hiyo, nataka Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atueleze sheria hizi zinazohusiana na kuondoa matatizo au kuiweka mifugo katika maeneo maalum na kuweka katika mazingira mazuri ya ufugaji zimechuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya uvuvi katika nchi yetu kwa kweli ni mbaya mno. Mchango wa uvuvi katika nchi au katika pato la Taifa ni mdogo. Mwaka 2012 na hata kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, na mwaka 2013, uvuvi umechangia asilimia 1.4 katika pato la Taifa, licha ya kuwa na maziwa, bahari ambayo tuna uvuvi wa bahari kuu lakini mchango wake ni asilimia 1.4. Wakati Namibia pato la Taifa linalotokana na uvuvi ni asilimia 10. Hii inaonyesha bado Serikali haijawa makini katika kudhibiti suala zima la uvuvi, hususan uvuvi wa bahari kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna meli nyingi na wengi wameshazungumza suala hilo kuwa zinakuweko nje, zinavua, haijulikani kinachovuliwa, haijulikani nchi inapata nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaaminika kuwa kila mwaka Serikali inapoteza Dola 220 kutokana na uvuvi wa bahari kuu. Hii ni kwa sababu hakuna ufuatiliaji, wanakwenda kuvua, wanavuna wanavyotaka, wanakwenda wanakotaka na nchi ipo, vyombo vipo na Wizara ipo. Matokeo yake utakuta nchi yetu pato lake kubwa litategemea kuwabana wafanyabiashara wakati vyanzo hivi ambao Mwenyezi Mungu katujaalia vingetusaidia sana kwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Kilwa kuna tatizo kubwa la uvuvi wa mabomu. Tatizo hilo linaweza likasababisha lile bomba ambalo linatoka Songosongo kwenda Somanga Fungu likawa mashakani. Huu ni uvuvi haramu wa mabomu, kwa hiyo, nahisi iko haja kupatikana boti wa doria ili uvuvi huu uzuiliwe na bomba letu liwe katika hali ya usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya uvuvi katika Ziwa Victoria ni mbaya mno, uvuvi haramu umetawala. Hivi sasa inakadiliwa kuwa, au katika mwaka 2000 utafiti uliofanywa katika Ziwa Victoria, katika eneo la mraba kilomita 35,088 kitaalam au kikawaida ilitakiwa kuwe na tani 391 ya Sangara, lakini kilichogundulika katika mwaka 2000 ni tani 200 hii ni kuonyesha kuwa uvuvi haramu umetawala katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe hiyo ilikuwa ni mwaka 2000, leo ni mwaka 2014. Kwa hiyo, hali taabani itakuwa ni mbaya zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema ili Wizara hii iweze kufanya shughuli zake kikawaida inabidi bajeti yake kwa kweli iwe ya uhakika. Wengi wameshasema, walioongezewa Shilingi bilioni 20 lakini walichopata ni Shilingi bilioni mbili na nukta.

Kwa hiyo, katika hali hii kwa kweli Wizara hii itakuwa kila siku tunailaumu lakini hakuna kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kuwa uvuvi na mifugo kwa kweli kama tutaitumia ipasavyo, basi nakuhakikishia uchumi wa nchi yetu utaongezeka na badala…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ali Khamis. Sasa namwita Mheshimiwa Laizer na Mheshimiwa Rose Kamili ajiandae na atafuatiwa na Mheshimiwa Lugola.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba hii ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Waziri wa Mifugo pamoja na Naibu Waziri kwa hotuba yao nzuri sana waliyoisoma. Ni hotuba nzuri ambayo ina mwelekeo kama watapewa fedha za kufanya kazi waliyopanga. Kwanza nitangulize kuishukuru Serikali sana kwa kutupa mifugo. wakati mifugo ya Jimbo langu imekufa, Serikali imetupa mifugo kwa wale wananchi waliofiwa na mifugo ambao wamekuwa maskini wa kutupwa; lakini Serikali imewapa mifugo tena na kuna wachache ambao bado hawajapata na nategemea Serikali itawapa kama ilivyowaahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba mgogoro huu ambao wafugaji na wakulima wanapigana kila siku nadhani ni Serikali tu haikuamua kwa muda mrefu kumaliza matatizo ya migogoro. Kwa sababu inawezekana. Kwa sababu ardhi yetu ni kubwa, lakini Serikali imeacha kwa muda mrefu kutenga maeneo ya wafugaji na kila bajeti wanatoa taarifa kwamba watatenga maeneo ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isipotenga maeneo hayo na kuweka hati miliki kwa kila eneo, bado mgogoro utakuwa mkubwa, utaendelea. Siyo tu migogoro ya wakulima na wafugaji, mgogoro utakaokuja tena ni hifadhi pamoja na wafugaji. Hata hizo hifadhi, wafugaji watavamia kama wakulima wanavyovamia maeneo ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, kuna Wilaya ambayo hawana tena maeneo ya ufugaji. Kwa mfano, Kongwa, ukiwaambia watenge maeneo ya wafugaji, watatenga wapi? Eneo lote limelimwa, imebaki *ranch* ya Kongwa na hata hiyo *ranch* imevamiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiteto ni Wilaya ya Wafugaji, wao wametenga maeneo. Asilimia 80 ya Wilaya ya Kiteto ni eneo la wakulima. Pamoja na kwamba Wilaya ya Kiteto ni wafugaji, lakini asilimia 80 ni kilimo. Wamebakiza asilimia 20 tu ambayo ndiyo wametenga kwa ajili ya hifadhi na mifugo Murtangos, ndiyo sasa inavamiwa. Hivi Serikali mkipima hata hayo maeneo yetu halafu yavamiwe tena, mnyamaze kimya! Utaona kwamba hakuna hata sababu ya kupima.

Kwa hiyo, mgogoro uliopo ni Serikali ndiyo wamekaa kimya, hawakutoa maamuzi. Mahakama imetoa maamuzi, lakini Serikali imetekeleza, ikaachia tena. Naomba watu wasiuane tena pale kwa ajili ya Serikali kushindwa kufuata sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la mifugo. Mimi ni mfugaji. Niwaambie, mifugo ya Jimbo langu ndiyo Kenya wanategemea na wanajivunia na wanasema msiwabughudhi Watanzania wakija, kwa sababu Kenya hawana ng'ombe za kutosha, lakini sisi wenye ng'ombe hatufaidiki, Serikali haifaidiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku nikisimama Bungeni nasema; kila siku! Kwamba, Kenya ndiyo ina-*supply* nyama nyingi nchi za nje kuliko Tanzania, na Maziwa na ngozi. Ni ajabu biashara ya Kenya, ni ng'ombe kutoka Tanzania. Lakini Tanzania yenyewe yenye ng'ombe, wanakaa kimya, hawatafuti masoko, hawatafuti viwanda, halafu mnatuambia kila siku tupunguze ng'ombe. Tupunguze tupeleke wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la soko. Umetangaza kwenye kitabu chako kwamba kuna soko la Longido. Bajeti iliyopita kulikuwa na soko la Longido, lakini Serikali haitoi fedha katika Wizara hii, ni fedha za mishahara tu. Wataalam walioko ni wataalam waliobobea, lakini hawapewi fedha za kufanyia kazi. Wataalam wamekaa na elimu yao Maofisini, hawafanyi kazi. Wafanye kazi na nini hawana pesa?

Kamati ya bajeti nitawashangaa sana mkikaa tena kimya na mmetoa wakati ule Shilingi bilioni 20 na haiukupatikana hata senti, nitawashangaa sana. Mimi bado nachelea kusema, hata hiyo Kamati ya Bajeti nahisi nanyi mna upendeleo mkubwa. Kuna baadhi ya Wizara mnayopendelea kuwapa fedha na kuna nyingine ambazo mnakata fedha, hamwoni kwamba ni bajeti inayokwenda kwa wananchi wenu. *(Makofi)*

Naomba Kamati hii ya bajeti, kuna wafugaji ambao siku hizi wametawanyika nchi nzima wa Barabaig kutoka Hanang. Wametenga maeneo lakini hakuna maji. Katika eneo walilotengewa, basi wawekewe mabwawa na majosho. Wabarabaig watatoweka nchi nzima, wako kila mahali, hawajui tena kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba iundwe Bodi ya Mifugo.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Rose Kamili, na Mheshimiwa Lugola ajiandae, atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Kalogeris.

MHE. ROSE K. SAKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia na mimi pamoja na kwamba niliweza kutoa hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Lakini kubwa zaidi, kwenye mchango wangu, kutokana na taarifa iliyosomwa na Mheshimiwa Waziri wa Mifugo, napenda kusema kwamba hakuna kitu kibaya kama kurudia rudia kitu ambacho kimeisha.

Taarifa aliyoisoma kuhusu kulipa au kutoa fidia kwa wafugaji ilishaisha ile ya Ngorongoro na Loliondo siku nyingi. Sasa tulidhani kinachozungumzwa ni wale ambao wamepata maafa hivi karibuni mwaka 2013 kutokana na Tokomeza, wale ambao ng'ombe wao walisukumwa kwenye maji wakafa, wafugaji wenyewe ambao waliuawa, lakini hiyo haija-*appear* hapa ni jinsi gani wanalipwa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumwambia Mheshimiwa Waziri, kama leo hamtazungumza suala la wafugaji na matatizo yao, nitashika Shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ardhi lililopo ambalo limejitokeza sana sana kwa adha ya wafugaji nchi nzima, haionyeshi wazi! Najua kwamba Wizara haina mamlaka, lakini mmefanya kazi gani? Mmepanga nini? Maana ukiniambia hekta milioni 1.3, mimi sielewi. Ninachotaka kuambiwa ni kwamba, mmejipanga vipi katika hekta ambazo zinafaa milioni 60 hawa wafugaji milioni 21 wametengewa katika Wilaya mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kusema kwamba tumewaachia Halmashauri mbalimbali, kule kwenye Halmashauri hilo limeshindikana na linazungumzwa kila wakati, na ndiyo maana wafugaji wanahamahama, wanahangaika nchi nzima ni kwa sababu Halmashauri zimeshindwa. Sasa je, hizo milioni 60 ziko wapi? Mmejipanga vipi kwenye bajeti ya mwaka huu kuongeza ardhi kwa ajili ya kuwatengea wafugaji wote waliopata hiyo adha kubwa sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda pia upande wa Serikali kila wakati kuwaambia wafugaji kupunguza mifugo. Wafugaji ambao tunawaita wachungi kwa lugha mnayotumia kuwaambia wapunguze mifugo haingii kwenye akili yangu kwa sababu sijasikia mkisema wale wenye mashamba makubwa wapungunze ardhi. Bali mtasema wapunguze ardhi wafugaji eti ndio wanaoharibu ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mwingine Dar es salaam anaongeza magari kumi, mpaka mji unasongamana kwa sababu ya utajiri wake; leo unamwambia huyu mfugaji ili aondokane na umaskini anapoongeza mifugo unamwambia punguza mifugo; hii kwa kweli siyo sahihi. Tutafute namna ng'ombe wajipunguze wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jinsi ya kupunguza ng'ombe au namna ya kupunguza ng'ombe ni kuvunwa. Jinsi gani wavunwe? Ni viwanda viwepo ndani ya nchi hii. Niambieni mmeonyesha habari ya kwamba mna viwanda, siyo viwanda, ni machinjio!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tunachozungumza, viwanda viko vingapi nchi nzima? Sehemu yoyote yenye mifugo, kuwe na kiwanda, ili hawa ng'ombe wajipunguze kwamba wanakwenda kiwandani, nyama inajibadilisha inauzwa nje, ngozi inauzwa nje, kila kitu

kinauzwa. Hapo tayari utakuwa umeinua uchumi wa mwananchi ambaye anahangaika na maisha yake. Kila siku tunasema wafugaji ni maskini.

Mimi nasema mfugaji siyo masikini ila mmeshindwa kuwawezesha kwa kufungua viwanda. Badala yake Serikali imekula viwanda. Kwa sababu viwanda ambavyo vilikuwepo awali, Serikali hii imebinafsisha, wameweka hela zao mifukoni, viwanda vimebaki hewa.

Kwa hiyo, ninachozungumzia ni Serikali iangalie suala la viwanda ndipo hapo unaongeza uchumi wa wafugaji na ng'ombe kujipunguza wenyewe au mifugo hiyo kujipunguza yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda pia kusema kwamba hatuna budi kushika Shilingi kwa Mheshimiwa Waziri, ni kwamba nimeona sehemu ya kuwawezesha wataalam kwenye mafunzo, lakini kuwawezesha hawa wafugaji wa Simiyu, Hanang, Morogoro na sehemu mbalimbali ndani ya nchi hii waweze kupata elimu ya kutosha ni jinsi gani watafuga hawa ng'ombe, haikuonyesha na hela itakuwa ni ndogo sana. Mmezungumza suala la chanjo chanjo, kitu kidogo sana, lakini hela kubwa imekwenda kwa safari nyingi.

Mheshimiwa Waziri, hilo naomba kabisa, tunataka sasa fedha za maendeleo ambayo ni kidogo, haitoshi, lakini basi iwaendee wale wahusika wenyewe isibaki kwenu. Maana ninyi mnataka kusafiri safiri sana, lakini mmewaacha wafugaji wahusika waweze kufanikiwa kwa suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwa suala la wavuvi. Inasikitisha sana! Nafahamu kwamba nchi hii tungekuwa matajiri kupita kiasi, kwa sababu uvuvi ambao upo au maziwa tuliyonayo ni mengi na bahari tunayo. Lakini hatuchukui mrabaha hata kidogo, mnakata leseni tu, suala la mrabaha halipo. Je, ni lini tutaendelea kama hatutaweza kukata hiyo mirabaha? Mimi nadhani sasa tozo ya mrabaha kwa wale waliokata leseni kwa kuvua baharini naomba sana…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Namwita Mheshimiwa Lugola na Mheshimiwa Karogeris jiandae na atafuata Mheshimiwa Peter Serukamba.

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa vile wakati wa kujadili taarifa ya Operesheni Tokomeza Ujangili nilizungumzia sana wafugaji, leo nitazungumzia wavuvi wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti. Hotuba yangu sana sana itakuwa ya kumuasa Waziri na Naibu wake pamoja na kuwaonya katika maeneo mbalimbali. Pengine nianze kwa kuwakumbusha kwamba mkiwa *back benchers* kama sisi nyote wawili, wote tuliimba kwaya moja, Mheshimiwa Waziri ukiimba sauti ya kwanza, Naibu wako akiimba sauti ya pili, mimi nikiimba besi; wote tukiwa tunaimba wimbo mmoja kwamba wavuvi wadogo wameonewa vya kutosha; wavuvi wadogo wamenyonywa kiasi cha kutosha; wavuvi wadogo wamenyanyaswa kiasi cha kutosha! Sote tukawa tunasema bajeti hii ya Mifugo na Uvuvi imekuwa ni ya porojo, imekuwa ni ya ngonjera, imekuwa ni ya ubabaishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina masikitiko makubwa sana. Wenzetu wawili hawa baada ya kwenda huko mbele, nao wameungana na kuleta bajeti za porojo na ubabaishaji na ngonjera. Katika Kitabu chake cha hotuba, ukurasa wa 50 Mheshimiwa Waziri anawaambia

wavuvi wadogo wadogo katika nchi yetu; Mwibara kule na visiwa vyake na Fuba, Sozia, Machwera, Namguma, Irugwa kule, Ukerewe, Ukara, Goziba na Kerebe, anawaaminisha katika hotuba yake kwamba wanao mpango sasa wa kuwapa ruzuku ya zana za uvuvi pamoja na pembejeo zikiwemo unununzi wa boti, unununzi wa *engine* na unununzi wa nyavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Waziri kama hizi siyo ngonjera, vitabu vyako vyote; kitabu cha hotuba ya Bajeti chenye kurasa 122, kitabu cha pili chenye kurasa 516, kitabu cha nne chenye kurasa 283 na kitabu cha randama chenye kurasa 166; hakuna mahali popote, kurasa zote hizo kwenye vitabu vyote ambapo umetenga fedha za ruzuku za kununua boti kwa ajili ya wavuvi wadogo wadogo; za kununua nyavu kwa ajili ya wavuvi wadogo wadogo, wala kununua *engine*. Kwa nini mnaendelea na ngonjera za namna hii?

Kama utakuwa tayari kwenye vitabu vyote hivi kunionyesha mahali ambapo mmeweka ruzuku kama siyo porojo na ngonjera, Wanamwibara mnanisikia; naweka rehani Ubunge wangu kufika leo jioni niweze kujiuzulu Ubunge kama Mheshimiwa Waziri atanionyesha mahali ambapo amewatengea fedha za ruzuku. Jioni ikifika, nitakuandikia *cheque* ya Shilingi milioni 50 kama utanionyesha kuna mahali ambapo umeweka ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti yake sana sana ametenga fedha kuwawezesha watumishi 50 waende kwenye michezo ya SHIMIWI, Shilingi milioni 64; amewawezesha watumishi 300 wakapime afya zao kwa hiari, Shilingi milioni 28; amebaki kuwawezesha watumishi wanaoishi na Virusi vya Ukimwi Shilingi milioni kumi kwa ajili ya chakula. Tunakwenda wapi Mheshimiwa Kamani? Nakuheshimu sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wetu niliowataja, tulishapiga kelele na wewe hapa kwamba ni wakati sasa wa kutowatoza Dola za Kimarekani kulipia leseni za uvuvi. Lakini mpaka leo wavuvi bado wanaendelea kutozwa Dola za Kimarekani. Wavuvi wangu Mwibara kule tangu wazaliwe hawajawahi kuona wala kushika Dola za Kimarekani. Dola za Kimarekani kumi, wanalipia Mtumbwi, Dola kumi wanasajili Mtumbwi, Dola kumi mwenye Mtumbwi analipia Leseni na bado Dola kumi kwa ajili ya ukusanyaji wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli wavuvi hawa kwa kuendelea kutozwa Dola za Marekani, ndiko kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo katika nchi yetu? na mbaya zaidi, wavuvi hawa bado wanalipa leseni zao katika Wilaya moja kwa Dola zote hizi.

Baada ya wiki moja kwa sababu samaki wanahama, samaki hawana mipaka, wakienda Wilaya nyingine ndani ya Wiki moja wanatozwa tena leseni hizi. Tunakwenda wapi na Wizara ya namna hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na Waziri huyu huyu, tulikuwa tunaimba hapa kwamba utaratibu wa kuwatoza wavuvi wanne walioko kwenye chombo cha kuvulia samaki wakati tayari mwenye chombo amekwishalipa leseni zote hizi, ni uonevu. Nikawa natoa mfano, kwa nini Kondakta kwenye Basi yeye…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lugola ahsante sana kwa hoja zako. Sasa namwita Mheshimiwa Kalogeris, ajiandae Mheshimiwa Serukamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Aeshi.

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Lakini kwanza kabla sijaendelea kuchangia nataka nimpe taarifa Waziri

Kivuli wa Mifugo na Uvuvi kwa taarifa aliyotoa Bungeni kuhusu Mkuu wa Wilaya wa Morogoro Vijijini, ndugu yangu Said Amanzi na Mkuu wetu wa Mkoa wa Morogoro, Mheshimiwa Joel Bendera.

Operesheni ambayo ilikuwa inafanyika katika Wilaya ya Morogoro Vijijini na Mkoa wa Morogoro ilikuwa ni Operesheni halali, Operesheni ambayo ilikuwa inatekeleza matakwa ya Sheria za Vijiji katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini na katika Mkoa wa Morogoro. Ninaamini kwamba uwepo wao pale mpaka leo ni kwamba walikuwa wanafanya kazi na kutekeleza amri halali na ndiyo maana hakuna chochote kilichowatokea mpaka leo.

Nawaomba Viongozi wa Mkoa wa Morogoro chini ya Joel Bendera na ndugu yangu Said Amanzi, endeleeni kutekeleza katika kutetea sheria ambazo zipo zinazotakiwa kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba nitoe pongezi kwa kaka yangu Mheshimiwa Kamani pamoja na kaka yangu Mheshimiwa Telele kwa uteuzi ambao wamepewa na Mheshimiwa Rais. Ninaamini Mheshimiwa Rais katika kuwateua alikuwa na sababu za msingi. Kwanza naamini kwa elimu yenu, lakini vilevile kwa jamii ambayo mnatoka. Katika nchi hii, wafugaji wakubwa ni Wasukuma na Wamasai. Kwa hiyo, uteuzi huu alikuwa anautoa katika dhamana ya kwenu kuhakikisha kwamba sasa migogoro ya wakulima na wafugaji inafika mwisho.

Nawaomba ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, kwa bajeti hii ambayo imetoka, ndugu zetu hawa tutakwenda kuwatosa tena kama yaliyomtokea Dkt. Mathayo pamoja na kaka yangu kule. Nawaomba tu kupitia Kamati ya Bajeti, ikiwezekana tuwaongeze bajeti hawa ili waweze kutekeleza majukumu yao kama walivyojipangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nilikuwa nimuombe na ninataka nijue kutoka kwenye Wizara, sasa hivi ukiangalia migogoro ya wakulima na wafugaji imetulia. Sababu za msingi ni kutokana na mvua iliyonyesha, majani ni mengi, lakini vilevile maji ni mengi huko wafugaji waliko. Baada ya kipindi kifupi, cha kiangazi, naamini migogoro italipuka tena, kwa sababu wafugaji watatoka walikokuwa, watarudi kule kwenda kufuata malisho lakini vilevile kufuata maji ambayo mengi yapo kwa watu wanakoishi hasa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali na niiombe Wizara, Mheshimiwa Waziri utakapokuwa unafanya majumuisho, hebu utueleze una mpango gani wa kimkakati katika Wizara yako wa kuchimba mabwawa na majosho sehemu mbalimbali nchini hususan Wilaya ya Morogoro Vijijini. Kwa maana naamini kabisa, tukiweza kupata mabwawa, tukiweza kuwa na majosho tutapunguza migogoro ya wakulima na wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo, nataka nipate taarifa kutoka Serikalini kupitia Wizara. Mheshimiwa Waziri hapa ameonesha na hata Wabunge wengine wamesema, inaonekana ametupia Halmashauri mpango wa kupima ardhi na kutatua migogoro hii. Kupitia Wizara, Mheshimiwa Waziri na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Waziri Mkuu, mna mipango gani mikakati kwa sababu ardhi kwenye Halmashauri sasa hivi imekwisha, hatuna. Vijiji vyetu ambavyo ardhi imepimwa, tayari tulishapanga mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya wakulima, kwa ajili ya wafugaji, lakini ongezeko la mifugo kuna kila sababu ya Wizara kuwa na mipango mikakati ya kutafuta maeneo mengine hasa katika mapori ya akiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijue Waziri ana mikakati gani katika hilo ili migogoro ya wakulima na wafugaji sasa ifike mwisho. Damu za wakulima, damu za wafugaji zimeshamwagika za kutosha katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, wamezungumza wachangiaji hapa, ni ukweli usiofichika mifugo ni mali. Mifugo inaweza ikafanya taifa hili likaenda mbele na hii migogoro ikaondoka kabisa. Nataka nijue, Wizara yake kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na Viwanda mna mipango mikakati gani katika kutafuta masoko ya wafugaji? *(Makofi)*

Ndugu yangu Sanya kaeleza hapa, kondoo tu ukipeleka wakati wa ibada maana yake ni soko. Nadhani wakati umefika sasa pamoja na kuwa na minada ya ndani, pamoja na viwanda ambavyo vinajengwa, kuna kila sababu ya kuendelea kupata viwanda zaidi lakini kuna kila sababu ya hawa ndugu zangu wafugaji kutafutiwa masoko nje ili waweze kuvuna mifugo yao na wakapata fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nataka nipate ufafanuzi kutoka kwa ndugu yangu Waziri, Waheshimiwa Wabunge tumelalamika sana, fedha zimetengwa lakini hazionyeshi tumejipangaje kama Wizara kutoa elimu kwa wafugaji waondokane sasa na kuhodhi makundi makubwa ya ng'ombe, wafuge ng'ombe wachache. Ninategemea wakati ana-*wind* atueleze kifungu gani katika bajeti yake amepanga katika kutoa elimu kwa wafugaji. Hili suala ni muhimu sana, wakati tunatafuta suluhisho la kudumu lakini naamini elimu vilevile ikianza kutolewa, itapunguza migogoro ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante. Sasa ajiandae Mheshimiwa Serukamba na mchangiaji wa mwisho leo ni Mheshimiwa Aeshi.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi nichangie Wizara hii muhimu sana. Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, ni Wizara muhimu sana lakini kwa bahati mbaya tumeamua tuifanye isiwe ya muhimu. Yako maswali mimi najiuliza, hivi leo Tanzania tungekuwa hatuna hata ng'ombe mmoja, hatuna kondoo, hatuna kuku, tungetumia shilingi ngapi kuagiza hizo nyama! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mradi mkubwa lakini kama hatubadili namna yetu ya kufikiri kufanya mifugo iwe na maana kwa Taifa letu kwenye uchumi, tutalalamikiana kila siku. Ukienda leo Ethiopia, Ethiopia katika sekta ambayo inaingiza dola na inachangia uchumi wao kwa ukubwa ni ng'ombe. Sisi tuna ng'ombe, tuna kuku, tuna mbuzi, tuna kila kitu, tuna maziwa, tuna bahari, tatizo letu ni nini? Lazima tatizo letu liko kwenye mipango! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema, hivi kwa nini tusifanye wanavyofanya wengine? Kwenye suala la ng'ombe ili tuache kulalamikiana mifugo imeingia kwenye mashamba yangu tuweke mpango utakaoleta tija. *National Abattoir* iko wapi? Tujenge *National Abattoir.* Kama Serikali haiwezi kujenga itafute *private people* wafanye! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *National Abattoir*, watakuwa na kazi chache sana, kazi yake itakuwa ni kuchinja ng'ombe, kuuza nyama, kutafuta masoko na kuuza *by products* zote, viwanda vyetu vya ngozi vitapata *products*. Hawa kazi yao siyo kufuga, kwenye *National Abattoir*, kazi ya kufuga tuwape watu wa katikati ambao ni wafanyabiashara, mimi na wewe, kila mtu apewe ardhi yake atunze mifugo. Mtu wa katikati kazi yake itakuwa ni kukuza ng'ombe,

kuwanenepesha, kuwapa majani, kuwapa majosho ili ng'ombe wake akishanenepa, anaondoka naye anakwenda kuuza kwenye soko pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu lazima *National Abattoir* awe na uwezo wa kuchinja ng'ombe 10,000 *and above* kwa siku moja, hayuko mtu wa kawaida mfanyabiashara anayeweza kazi hiyo lakini hawa ng'ombe 10,000 atawatoa wapi? Atawatoa kwa sisi wafanyabishara wadogowadogo na sisi ng'ombe wetu tunawatoa wapi, tunakwenda kuwachukua kwa Wasukumu, tunakwenda kuwachukua kwa Wamasai. Maana yake umetengeneza *chain* ya biashara, umetengeneza ajira, umetengeneza kodi, shida ni nini? Kama hatufikiri namna hii, tukadhani tutaendeleza mifugo kwa sababu ya bajeti, tutapiga kelele kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najiuliza sana, tuna-*act* kama mtoto, unajua mtoto mdogo akipata *toy* jipya anasahau *toy* la zamani. Sasa hivi watu wote humu tunaongelea gesi tu, hakuna wimbo mwingine, gesi *as if* gesi ndiyo inakuja kumaliza matatizo yetu. Kama hatujaweza kufanya kwenye ng'ombe, hatujaweza kutumia kilimo kuendelea, hatujaweza kwenye ufugaji, hatujaweza kwenye madini, tunapata *assurance* gani tutafanya vizuri kwenye gesi! *(Makofi)*

Mhehsimiwa Mwenyekiti, maana hili ndilo tatizo letu. Kama Mungu ametupa ng'ombe wote hawa, ametupa maliasili hizi, hazijatuletea maendeleo, hatujipangi tukaleta maendeleo, lakini sasa hivi kila mtu ukimuuliza anaimba gesi, kila mtu sasa gesi imekuja, matatizo sasa yamekwisha, hayawezi kuisha kwa sababu namna tunavyofikiria, hatufikirii vizuri katika kuendeleza maliasili zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Ziwa Tanganyika, Mheshimiwa Kangi amelisema vizuri sana, Ziwa Tanganyika pale Kigoma wavuvi wote, tunaambiwa mtawapa ruzuku lakini kama Mheshimiwa Kangi alivyosema, mbona fedha za ruzuku hazimo kwenye vitabu? Tunazitoa wapi fedha za ruzuku? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawahitaji ruzuku, watu watengenezeeni utaratibu, watengenezeeni masoko. Tukidhani tunaweza tukaendeleza ufugaji, tukaendeleza uvuvi kwa kutoa ruzuku hatuwezi! Maana tunajua, bajeti yetu inataka kwenye elimu, bajeti yetu kwenye maji, bajeti yetu kwenye afya, bajeti yetu kwenda kwenye vikao, bajeti yetu kwenye posho, sasa hizo fedha za ruzuku tunazitoa wapi? Kwa hiyo, wavuvi wanachohitaji, Ziwa Tanganyika leo, kila siku, watu ziwani wananyang'anywa mali zao, Serikali ipo, Jeshi lipo, Polisi wapo, watu wa Kigoma tusemeje sasa? Umefika wakati, moja ya kazi muhimu ya Serikali ni kuwalinda raia na mali zao.

(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachelea kuunga mkono mpaka nipate majibu ya masuala haya niliyozungumza.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimia Aeshi.

MHE. KHALFAN HILALY AESHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, naomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuteuliwa lakini Mheshimiwa Waziri, mimi nataka nikukumbushe kidogo, wakati umeteuliwa, baada ya kuapishwa uliahidi kuzirudisha *ranches* zote zilizochukuliwa na wawekezaji ambao hawajaziendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi naona hapa tunapiga kelele sana, tunalalamika wafugaji hawana maeneo ya kufuga na tunalalamika wakulima hawana maeneo ya kulima. Hii ni *scandal* kubwa, hii ni hatari sana na tusipoliangalia kwa mapema zaidi litakuja kuleta athari kubwa sana siku zijazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri aliahidi na mimi naomba leo nirudie kumkumbusha na baada ya hapo aniahidi tena mimi kwamba *ranches* zote zilizochukuliwa na wawekezaji ambao hawajaziendeleza, naomba tuzirudishe Serikalini, tuwagaie hawa wafugaji tunaohangaika nao siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Rukwa hatujapata bado migogoro mikubwa sana kama hii lakini kinga ni bora kuliko tiba. Tuna *ranches* nyingi kule, zimechukuliwa na wawekezaji ambao hawajaziendeleza. Tumwombe Mheshimiwa Waziri, achukue maamuzi sasa. Yule ambaye ana *ranch* hekta 8,500, ana ng'ombe 1,000, kapimeni maeneo. Ng'ombe 1,000 zinatakiwa hekta 2000 au 3000 mpeni hizo nyingine zilizobaki wapeni wafugaji wengine ili kutatua kero ambazo zinazoweza kutukuta siku zijazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *ranch* ya Kalambo ambayo imesuasua sana na tuna wafugaji wegi. Mheshimiwa Waziri hebu fanya maamuzi, gawa eneo hili. Leo hii mna ng'ombe, ng'ombe wenyewe wala hawanenepi miaka 10, leo hii mnakopesha watu milioni 500 ng'ombe hawajalipa mpaka leo, Mheshimiwa mnafanya biashara gani? Mheshimiwa Waziri, hebu lifuatilie hili, Kalambo *ranch* inadai milioni 500 imemkopesha mwekezaji mpaka leo hazijalipwa, sasa mtaendelea vipi? Tutakuwa tunalalamika tu hapa, mimi nafikiri sasa umefika wakati mchukue maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu aliyekopa alipe na ile ranch kama hamuwezi kuiendeleza, wapeni wafugaji wadogo wadogo, naamini kero hii itakuwa imepungua. Sumbawanga tuna maeneo makubwa lakini wafugaji hawana maeneo, kwa hiyo, tuchukue katika hili, tusimwache mtu anamiliki hekta 8,500, hekta 15,000, hajaendeleza, ana ng'ombe 100, 200, hapana! Si haki, Mheshimiwa Waziri nitaomba majibu kabla sijaunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nitaongelea vavuvi wa *Lake Tanganyika*, namuunga mkono Mheshimiwa Peter Serukamba, kwa kweli wavuvi wetu wameachwa mbali sana. Leo hii inashangaza, mvuvi anatokea Kongo anakuja kuvua *Lake Tanganyika,* anakuja kuvua Kirando, anakuja kuvua Wampembe mpaka Kasanga, hakamatwi, haulizwi, lakini wewe ukitoka kwenda Kongo kwenda kuvua tu lazima ukamatwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tuna wavuvi wadogowadogo wengi wanaohangaika kule *Lake Tanganyika* lakini hata hao, toka tumepata Uhuru nafikiri hata mmoja hajawahi kupata mkopo. Nimwombe Mheshimiwa Waziri alifuatilie suala hili na sisi kule tuna wawekezaji wadogo wadogo, siyo lazima mkulima peke yake, hata mvuvi naye ana haki ya kupata mkopo lakini mmewaacha moja kwa moja na tumewapoteza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekaa kule *Lake Tanganyika,* nimekaa *Lake Rukwa*, kuna vijana wanaopenda uvuvi, wanaopenda kujiajiri wenyewe, tuwasaidie hawa waweze na wenyewe kujipatia ajira. Ajira siyo lazima uajiriwe Serikalini hata uvuvi ni ajira vilevile. Ajira siyo lazima uwe Mbunge hata kilimo ni ajira vilevile. Kwa hiyo, nikuombe tu Mheshimiwa Waziri kwamba safari hii na ninaamini kabisa umekaa Mkoa wa Rukwa, umekaa Katavi, unajua kabisa Mkoa wa Rukwa nini tunahitaji, unajua nini Mkoa wa Katavi tunahitaji. Kwa hiyo, nikuombe sana na uliniahidi kwamba utakuja kutembelea Rukwa mpaka leo toka umeapishwa Mheshimiwa

sijakuona. Kwa hiyo, nitakuomba katika hili utembelee Ziwa Rukwa na Ziwa Tanganyika, uone athari kubwa wanayopata wakulima na wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nisingependa kuchangia mengi, lakini ningeomba tu Mheshimiwa Waziri aniahidi utendaji wake kwamba atakwenda kutembelea *Lake Tanganyika* hususan Kasanga, Kirando…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Wasira kwa nafasi maalum.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi fupi ili niweze kutoa mawazo machache kuhusu sekta hii muhimu sana kwa uchumi wetu. Sekta ya mifugo na sekta ya kilimo, zinakwenda pamoja, wafugaji ndiyo wakulima na wote ndiyo wazalishaji wakubwa wa chakula katika nchi yetu. Nilitaka kutoa mawazo tu kwamba kwa upande wa mifugo kama ilivyo kwa kilimo, tukitegemea kutumia bajeti ya Serikali kuleta mabadiliko makubwa katika uchumi wa mifugo, itatuchukua muda mrefu sana kufanikiwa kwa sababu bajeti ya Serikali ndiyo hiihii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini tulipiga kelele huko nyuma na tumefanikiwa kuanzisha benki ya kilimo na nina imani kwamba benki ya kilimo itafungua milango yake wakati wowote kuanzia sasa. Naamini kwamba tukitumia benki hiyo, tukawekeza katika hizi sekta mbili, sekta ya kilimo na ya mifugo, tunaweza kuleta mabadililo makubwa sana katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitaka kutoa ushauri na hasa kwa Halmashauri za Wilaya, kwa sababu nchi yetu ardhi yake imegawanywa katika vijiji na katika Halmashauri zote nchini. Ardhi ambayo iko nje ya vijiji na ambayo iko nje ya Halmashauri, kama ipo ni kidogo sana, sehemu kubwa ya ardhi yetu iko vijijini. Tunacho chombo katika ofisi ninayoisimamia kinaitwa MKURABITA, nilitaka kuwaomba Halmashauri, watumie kile chombo, tufundishe vijana kulekule vijijini, tuwape *GPS*, tuwape komputa na tuwape vifaa vya upimaji. Hawa vijana peke yao wakifundishwa wanaweza wakapima nchi yetu kwa urahisi sana kuliko kutegemea chombo kimoja ambacho kiko *centrally*. Hata Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, haitaweza kwa muda mfupi kupima kila kijiji cha Tanzania na tukaweza kukipa mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, IKiwa ardhi yetu itapimwa katika ngazi ya kijiji, wanakijiji wenyewe wakapewa *extension services*, huduma ya ugani na Wizara hii, wakafundishwa namna ya kutumia ardhi hiyo, wakafuga kisasa, wakanenepesha mifugo yao, mimi nina imani tatizo letu litapungua, halitaisha lakini litapungua. Ni vizuri tujue ni matatizo gani ambayo yanafanya watu hawa wanahama, ni maji na malisho. Kwa hiyo, tutoe elimu, *extension* palepale, namna ambavyo wanaweza kupata malisho, namna ambavyo wanaweza kukopa, namna wanavyoweza kuanzisha *ranch*, namna wanavyoweza kufuga kisasa katika mazingira yao katika ardhi iliyopimwa, tukifanya hivyo tutaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia watu wengine wanasema, tunasema tupunguze mifugo, hakuna mtu anayewaambia watu punguza mifugo bila sababu wala hutaweza kupunguza, hiyo ni *irrelevant*. Kwa hiyo, mimi nafikiri kupima, kupanga, kukopa na kuwezesha hii sekta, ni jambo la msingi zaidi. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, orodha yetu ya mchana imekamilika. Jioni hii tutaanza na Mheshimiwa Dokta Nkya, Mheshimiwa Maria Hewa na Mheshimiwa Opulukwa.

Sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

(Saa 6.58 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, mchangiaji wetu wa wa kwanza jioni hii ni Mheshimiwa Dkt. Nkya.

MHE. DKT. LUCY S. NKYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba niunge mkono hoja asilimia mia moja, pamoja na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake wote kwa hotuba nzuri ya bajeti ambayo wametuletea leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono, inashangaza kuona kwamba hii sekta ya mifugo na uvuvi ni sekta muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi hii lakini Serikali ni kama inapuuza sekta hii ambayo nasema kwamba ni pesa ambazo zipo, ni sisi kuchangamka tu. Bajeti ya mwaka wa jana fedha za maendeleo wala haikutolewa nyingi; lakini mpaka sasa hivi wametoa asilimia 13 tu na karibu mwaka unakwisha, sasa hiyo asilimia 86.4 itatolewa lini? Tunaomba Serikali ituhakikishie leo katika Bunge lako Tukufu wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*windup* hii bajeti *speech* yake, atuambie hii asilimia 86 italipwa lini ili hiyo miradi ambayo tunajua kwamba ni muhimu, hususan dawa za wanyama pamoja na chanjo ziweze kupatikana kwa sababu ni muhimu sana katika kukuza uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza kwamba vijana hawana ajira, tuliona mfano kwamba Wizara ya Kilimo imeanzisha kambi kwa ajili ya vijana, kuwafundisha na kuwaanzishia miradi ya kilimo ili waweze kujiajiri. Vilevile katika sekta ya mifugo, ufugaji wa kuku, ufugaji wa ng'ombe, kunenepesha mbuzi, ni miradi ambayo kama Wizara ingetuonesha kwenye bajeti yake kwamba itaanzisha angalau vituo vya kufundisha vijana waweze kujitegemea, kuna *veterinary doctors* wengi tu, kuna waliosoma cheti, kuna waliosoma stashahada, shahada hawana kazi, wanahitaji mtu wa kuwakusanya, kuwasaidia, kuwatia moyo na kuwapa *entrepreneurship skills* ili waweze kufuga wanyama wadogo kama kuku, sungura na mbuzi itatusaidia kupunguza hili tatizo la ajira kwa vijana na kuwaondoa vijana ambao wanazurura mijini ambao hawana kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumze kuhusu mgogoro wa wakulima na wafugaji hususan katika Wilaya ya Morogoro Vijijini. Mheshimiwa *DC* pamoja na Mkuu wa Mkoa walipowaondoa wale wafugaji ambao walivamia ilikuwa ni haki kwa sababu walikuwa wanatekeleza sheria na kanuni ambazo tumepitisha katika Halmashauri yetu. Hawajafanya makosa kwa sababu wafugaji waliokuwepo tangu zamani wapo. Baadhi yao ni viongozi wa vijiji, ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi pamoja na Makatibu Kata, wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba, Kiongozi wa Upinzani aridhike kwamba hawa viongozi wawili walikuwa wanatekeleza wajibu wao wa kuhakikisha kwamba kunakuwepo na amani na maelewano katika eneo lao la kazi. Naomba nimhakikishie kwamba, sisi viongozi wa Morogoro Vijijini, tukishirikiana na *DC* na Mkuu wa Mkoa tutaendelea kuhakikisha kwamba wafugaji waliokuwepo hawatabughudhiwa kwa sababu eneo lililopo ni la kuwatosha wao na mifugo yao tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nimkaribishe Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri wake afanye ziara katika Tarafa ya Ngerengere. Ni Tarafa ambayo imekuwa na mitafaruku mikubwa kati ya wafugaji na wakulima. Sio kwamba hawapendani mtafaruku unatokana na tatizo la kutokuwepo na malisho. Kwa hiyo, naomba Wizara iangalie namna ambavyo itaanzisha mashamba ya malisho na mafunzo pamoja na kuwapa wafugaji wetu mbegu za malisho, wapo tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba inabidi wafugaji watembee na ng'ombe kwenda kutafuta maji, naomba Wizara iangalie uwezekano wa kutuongezea malambo hasa katika kijiji cha Magera, Visaraka, Kiwege pamoja na Tununguo, ndiko ambako mitafaruku inatokea mpaka watu wanaumizana. Wafugaji na wakulima wanapendana lakini inapokuja kwamba kila mmoja anagusa *interest* ya kiuchumi ya mwenzake ndipo mitafaruku inatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo naiomba Wizara, ni kwamba sasa hivi kuna wafugaji ambao wameanza kuleta mageuzi ya ufugaji. Wameanza kunenepesha ng'ombe, naomba wapate msaada, wapelekewe na Maafisa Ugani wa kutosha. Kuna vijana wa Kimasai ambao wameanza kusindika maziwa, mmojawapo anaitwa Lucas Lemomo, yuko kijiji cha Diguzi. Ameanza kununua maziwa amefikia mpaka kiwango cha lita karibu 3000 kwa mwaka, anasindika, anatengeneza *cheese* anapeleka Dar es Salaam. Naomba Wizara imuangalie, imsaidie ili aweze kuajiri vijana wengine wengi, wawe mfano wa kuigwa kwa sababu huo mradi wake umeanza kuleta mabadiliko ya fikra kwa wafugaji wa eneo lile la Ngerengere kwamba sasa imefika wakati wa wabadilishe ng'ombe wa kienyeji wanunue ng'ombe wa maziwa, kwa hiyo, wameanza kuuza ng'ombe wao. Kwa hiyo, yeye ameonesha njia lakini naomba Wizara sasa iangalie namna ya kumsaidia kwa sababu lile ni eneo lenye wafugaji wengi, wana ng'ombe wengi lakini kama watabadilika mitafaruku itakuwa imepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda kuzungumzia ni kwamba wafugaji wanapata shida sana kutafuta dawa za ng'ombe wao. Naomba Wizara iangalie namna ambavyo itaongeza upatikanaji wa dawa pamoja na chanjo kwa ajili ya wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule milimani Morogoro kuna maji mengi pamoja na majani ya ng'ombe. Naomba Wizara itusaidie, wale wananchi sasa waanze kuwa na utamaduni wa kufuga ng'ombe wa maziwa kwa sababu tuna uwezo wa kuzalisha maziwa mengi, kuna majani mwaka mzima, kwenye Kata ya Kinole, Kata ya Tegetero, Matombo pamoja na Mkuyuni, kuna majani mengi na majani ya kutosha kwa mwaka mzima. Naomba Wizara iangalie namna ambavyo wataanzisha mradi wa kufuga ng'ombe wa maziwa kwa akina mama na vijana ili waweze kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba kuna kuku wa kienyeji wengi tu lakini bado hatujawa *serious* kwenye ufugaji wa kuku wa kienyeji. Kuku wa kienyeji wanasaidia sana familia maskini kuweza kusomesha watoto. Mama akiuza kuku watatu anampeleka mtoto sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naomba kuunga mkono hoja asilimia mia moja, naomba Waziri anitembelee Morogoro kwenye Tarafa ya Ngerengere. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Maria Hewa.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote na mimi naunga mkono hoja hii. Pili, nimpongeze tu Mheshimiwa Kamani na Naibu wake kwa kupata heshima hiyo ambayo wamepewa na Mheshimiwa Rais kuliongoza jahazi hili la Wizara hii. Wizara hii si lele mama, ni ngumu na hivi ndiyo mnapewa bilioni hizo chache, kazi kwenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na siku zote huwa naanza kuzungumzia mifugo lakini leo nianze kuzungumzia uvuvi maana natoka Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wanasema hivi, laiti kama Serikali ingetutambua wavuvi, wakatuundia chombo tukaweza kujidhibiti sisi wenyewe kama wavuvi; maana tunaelewana nani mvuvi halali na nani mvuvi haramu, Serikail tungeisadia haraka sana. Ombi hilo linakuja kwako chini ya sheria ambayo kama huna basi na itungwe ili waweze kuwa na uvuvi ulio halali. Sasa unalipokeaje, utasimama hapo utatujibu Mheshimiwa Waziri. Ni ombi la wavuvi, wamechoka kuona uvuvi haramu maana mvuvi haramu anayevua anamwelewa anayevua halali. Yeye hali hao aliowavua yeye, anakwenda kula wa mwenzake aliiyevua halali. Sasa iweje? Wanaelewana, uwapokee kwa ombi lao, sijui utawaelezaje, tena wako hapahapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye ufugaji wa samaki wa kwenye mabwawa. Hao samaki wanaitwa vifaranga, wanalalamika wanasema mnawauzia ghali mno, mia tatu mpaka mia tano, mtu anataka kujikwamua awe na ufugaji huo kweli ana mtaji huo? Mmoja huyo mdogo Sh.500, mpaka wakajae bwawa ana mtaji gani? Hilo kabisa namuunga mkono, tena wote hili nadhani tungeliweza kuungana mkono tu pande zote bila kujali itikadi ya siasa zetu humu ili tuweze kuwakomboa wafugaji hawa walio na nia ya kujikomboa kupitia ufugaji kwa njia hiyo. Niombe kabisa, vinginevyo inawezekana labda hatuelewi, basi kama unaweza ukajua kwamba hatuelewi hebu utafute muda, kwa njia yoyote ile utuelimishe, hata kupitia semina sisi Wabunge humu, tukielewa labda ndio tunaweza tukaenda tukatoa elimu iliyo nzuri zaidi huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kabisa Mheshimiwa Waziri atuelewe hili, hebu ibuka na mambo mapya haya tukuone ukali wako na wewe na vitu vipya, si *business as usual*, *no!* Leo na wewe tuletee haya tunayokuambia tuyaone kwa macho mwanangu. Najua, maana wewe hii ni fani yako, umepewa kabisa ili uogelee tuone unaweza ukatufikisha wapi; tupokee katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la tatu sasa, hebu nigusie suala la mifugo. Mimi natoka katika familia ya wafugaji. Mama Nkya hapa amesema, wafugaji na wakulima ni marafiki na ni marafiki wazuri mno lakini nadhani Serikali ndiyo inayotukoroga. Tufike mahali, mmesema kwenye vitabu vyenu kwamba mmepima vijiji 589; hivi vijiji viko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ombi kwa Waziri kupitia kwako, hivi vijiji, kama vitakuwa vingi sana kuvitaja basi atuandikie mahali tuone ni wapi. Maana mimi hofu yangu Serikali unaweza ukakuta wanakwenda kutatua matatizo ya ardhi haya ili wafugaji wawe na eneo lao na wakulima wawe na eneo lao maeneo ambayo wala hayana matatizo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe hilo, kwa sababu kuna wengine hawatembeitembei, kabila la Kisukuma na kabila la Kimasai ndio hao wanaokamatwa kamatwa huko na vituko vituko hivi, je, hao ndio mko *seriously* kuwapimia ili nao watulie? Wanataka mabwawa, wanataka majosho, mkiwapa maji ya kutosha na kuwatengea maeneo ya ufugaji, jamani nani anapenda kuacha familia yake, watatulia hawa, watasomesha watoto, mbona huko Mbeya wanajenga na shule? Baada ya kufika huko wameji-*mobilize* wao wenyewe tu, tuko huku, wanajenga na shule zao kutokana na mifugo yao badala ya kujenga huko wanakotoka, wanapaacha panakuwa maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri wachimbe mabwawa haya huko ambako kuna matatizo kwa makabila hayo ninayoyasema, si kwamba kwa sababu mimi natoka huko, lakini ndio wanaokamatwa kamatwa huko, warudi waje watulie katika maeneo yao. Mimi nina fani

hiyo, ng'ombe ukimuosha, ng'ombe ukimpa malisho yaliyo sahihi, ng'ombe ukimchanja, kinachobaki ni kukaa na dawa tu ambayo ni kwa nadra ataugua. Hata hivyo ukimtimizia yale *seriously* matatu niliyoyataja mwanzo mambo yanajipa, ng'ombe ananenepa tu. Ng'ombe akila akishiba kila kitu kitajipa tu. Matibabu ni kitu cha mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara hii iwe *serious*, ipime maeneo hayo niliyoyataja na watuletee orodha hiyo, mtakuja kugundua kusiko na wafugaji…

(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Opulukwa ajiandae Mheshimiwa Blandes kama hayupo Mheshimiwa Mashishanga.

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia kwenye bajeti ya Wizara hii muhimu, Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla kabisa ya kusema ninachotaka kusema, nichukue nafasi hii fupi sana kuwapongeza Chama cha Wafugaji Tanzania na hususan pale Wilaya ya Meatu kuweza kupata viongozi wapya ambapo waliweza kumchagua Mwenyekiti wao Ndugu Maganga na Makamu wao Ndugu Makula Sumaku pamoja na Katibu wao Ndugu Mashauri Samwel. Napenda kuwasisitiza na kuwaomba waendelee kuwatumikia wafugaji kwa sababu wafugaji ndio nguzo ya Wilaya ya Meatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda nianze na takwimu. Mkoa wa Simiyu una idadi ya watu ambao ni milioni moja nukta tano na ukiangalia kwenye suala la mifugo kuna mifugo milioni mbili nukta sita. Sasa ukichukua ule mchanganuo wa milioni mbili nukta sita ya mifugo, kati ya hiyo ng'ombe ni milioni moja nukta tano ambayo ni sawa na idadi ya watu, ukichukua mbuzi wako laki saba nukta nne, kondoo wako laki mbili na nukta nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake nini? Kwa sa babu idadi ya watu wa Mkoa wa Simiyu ni milioni moja nukta tano na ng'ombe peke yake ukiacha mifugo mingine, nao ni milioni moja nukta tano, kwa hiyo, kila mtu mmoja wa Simiyu anamiliki ng'ombe mmoja. Hii nataka kuonesha jinsi ambavyo ng'ombe tukiwatumia kama fursa, tusiwatumie kama changamoto wanaweza wakatuletea maendeleo makubwa katika Mkoa wetu lakini hususan pia katika wilaya yetu ya Meatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya bajeti ya Waziri amejaribu kuongea kwenye ule ukurasa wa 35 na 36, kwamba kuna utoaji wa kifuta machozi kwa wafugaji ambao walikuwa kwenye yale maeneo ya Kaskazini mwa Tanzania ikiwemo Longido pamoja na Loliondo. Mimi napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri ni kwa nini Serikali iliamua kutoa fidia kwa Mikoa ya Kaskazini tu na wakati ukame, mauaji ya hawa ng'ombe yaliyotokea kutokana na Operesheni Tokomeza pamoja na mambo mengine yametokea nchi nzima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Operesheni Tokomeza iliyofanyika hivi karibuni iliweza kuleta madhara makubwa sana. Zaidi ya ng'ombe 570 waliripotiwa kufa, ikiwa ni pamoja na watu 12 na ng'ombe zaidi ya 150 kule Gurumeti walisukumiwa kwenye mto wakafa mle ndani, waliopona walikuwa ni ng'ombe kumi tu. Sasa kwa nini Wizara isiweze kuwafidia wananchi hawa ambao ng'ombe wao walikufa kutokana na majanga haya ambayo

yalisababishwa na Serikali yenyewe na wala si watu wenyewe waliosababisha mambo haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri inasema kuna maeneo katika Mkoa wa Simiyu ambayo yametengwa ni zaidi ya hekta elfu kumi na moja. Mimi napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri, hizi hekta elfu kumi na moja ziko wapi? Wanasema wametenga hekta elfu nane na mia saba kwenye Wilaya ya Meatu peke yake katika kijiji kimoja. Napenda Mheshimiwa Waziri anijulishe, hiki ni kijiji gani kilichotenga hekta elfu nane, ukijumlisha na zile hekta elfu mbili za Bariadi, kwa sababu mimi naamini maeneo yote ambayo yalikuwa wazi ndiyo yaliyokuwa *converted* yakawa ni *WMA* na maeneo mengine yamekuwa ni *buffer zone* kwenye hifadhi zetu kama Maswa *Game Reserve* pamoja na Ngorongoro *Conservation* na ndiyo maana wafugaji wetu sasa wanahama kutoka maeneo walipo wanaanza kwenda maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wafugaji wengi sana sasa hivi wako Singida, kuna wafugaji wengi sana wako Mbeya, wafugaji wengi wako Rukwa na wameshaanza kuvuka kuingia nchi ya Msumbiji, hii ni kwa sababu hakuna maeneo ambayo yamepimwa au yametengwa kwa ajili ya mifugo hii ambapo Mheshimiwa Waziri anasema maeneo yametengwa kwa ajili ya wafugaji ambayo ni zaidi ya hekta elfu kumi na moja kwa Mkoa wa Simiyu peke yake. Mimi napenda katika majumuisho yake basi atuambie ni vijiji vipi ambavyo vimetenga maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine hapa la mwendelezo wa maeneo ambayo yamechukuliwa kama hifadhi kwa maana ya *WMA*. Haya maeneo anayoyasema Mheshimiwa Waziri leo hii ukifika pale, yanajumuisha vijiji vya Jinamo, Mbushi, Iramba Ndogo, Sungu, kuna Mwabagimu, Rukale, Witamila, Mwagwila, Mwajidalala na Buganza. Maeneo yote haya yamechukuliwa kama Hifadhi za Jamii na hakuna maeneo ambayo wananchi hawa wanaweza wakapeleka mifugo yao na kwenda kuchunga pale. Napenda kuishauri Serikali, tusichukulie mifugo ni kama adhabu, tusichukulie mifugo ni kama changamoto, tuchukulie mifugo hii ni kama fursa kwa watu wetu kwa ajili ya kujiongezea ili waweze kuendesha maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo hii imeleta kipato kikubwa sana katika Mkoa wetu. Ukianzia kwa mfano mwaka 2006 mpaka 2012, mazao yanayotokana na ng'ombe peke yake yaliingiza Sh.90,000,000/=, mbuzi waliingiza Sh.5,600,000/=, ukichukua kondoo peke yake ilikuwa ni Sh.1,000,000/=/. Ukichukua mazao ya maziwa kwa kipindi hichohicho ambapo waliweza kuuza lita zaidi ya 21,000,000/= iliweza kuuingizia Mkoa zaidi ya Sh.17,000,000,000/= kwa kipindi hicho ambacho nilichokwishakitaja hapo. Sasa leo tunaanza kuwachukia wafugaji, tunawaambia wapunguze mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda kuwaambia Waheshimiwa Wabunge, kwetu sisi wafugaji tunaposema ng'ombe ndiyo benki yetu, ng'ombe ndiyo *ATM*, ng'ombe ndiyo *CRDB* na tunasema pia ng'ombe *is the symbol of wealth*. Mtu anapokuwa ana ng'ombe wengi ndio anaheshimika katika jamii yetu sisi ambao ni wafugaji. Mimi napenda kuishauri Serikali tusiowaone wafugaji kama ni watu ambao hawana maana katika jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa kunipa nafasi lakini napenda Mheshimiwa aweze kuyabaini na kuyaelezea haya yote ambayo nimeweza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Blandes, kama hayupo Mheshimiwa Mashishanga, ajiandae Mheshimiwa Shibuda.

MHE. RACHEL M. ROBERT: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kabisa kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hotuba hii ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka asubuhi tumekuwa tuwasikia wachangiaji wengi wakilalamika kuhusu wafugaji na wavuvi. Mimi nimesimama makusudi nikiwa na mambo mawili au matatu mahsusi kabisa.

Mhehimiwa Mwenyekiti, nataka kuikumbusha Serikali mwaka 2005 kulitokea kuhamishwa kwa wafugaji kutoka katika Bonde la Ihefu. Wafugaji hao walinyanyasika sana, haki za binadamu zilikiukwa, walidhalilishwa sana, mali zao zilipoteza sana na mifugo yao ilipotea sana. Tume ya Jaji Chande iliundwa na Mheshimiwa Rais lakini taarifa wala matokeo ya Tume hiyo mpaka leo hii hatujayapata. Inasikitisha sana na bahati mbaya au nzuri wafugaji hao zaidi ya asilimia 80 ni watu kutoka Usukumani, kwa hiyo ni ndugu zangu kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nasikitika kwa sababu Serikali imekaa kimya. Ni kwa nini imekaa kimya kwa sababu hawa wananchi ni Watanzania! Hivi kwani wafugaji katika nchi hii ni wahamiaji? Napenda kupata majibu kutoka kwa Serikali, iko wapi ile Ripoti ya Jaji Chande na ni kwa nini mpaka leo hii haijaja Bungeni toka imepokelewa na Rais ili tuweze kujua kuna tatizo gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Mheshimiwa Waziri Mkuu alisimama hapa akasema kuwa wale waliopatwa na maswahibu hayo watalipwa pesa lakini mpaka sasa hawawezi kulipwa, kwa sababu ndani ya ile Tume hatujui wako akina nani na wanaopaswa kulipwa ni kina nani na nani ambaye hapaswi kulipwa. Naiomba Serikali ile Taarifa Tume ya Jaji Chande iletwe Bungeni, naomba sana kwa sababu wafugaji sasa hivi wamekata tamaa na Serikali yao, wamekata tamaa na maisha kwa sababu wamekuwa wanatembea kutafuta chakula na malisho. Kikubwa ni lini watafidiwa na Serikali lakini Serikali haija-*take* hata *trouble* kuwaomba samahani kwa sababu hili zoezi lilifanywa kinyume kabisa na haki za binadamu, hakuna asiyelijua hili. Serikali imekaa kimya mpaka sasa hivi, hakuna kitu kinachozunguzwa. Hii Tume ya Jaji Chande Taarifa yake iko wapi, tunaiomba. Kamati ya Bunge ambayo imeteuliwa na Mheshimiwa Spika mwaka jana, imejitahidi sana kuomba ripoti hii lakini haikupewa, kuna nini kwenye hiyo ripoti kwa nini haitoki? Pamoja na kuwa Waziri ni mgeni katika hili nafikiri amekuta vitu kwenye dawati lake, nadhamiria sasa kwa mara ya kwanza toka nianze Bunge hili nitashika shilingi nisipopata majibu kutoka kwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii mbona ina maeneo makubwa sana, kwa nini bado kuna migogoro ya wafugaji na wakulima? Serikali inapata kigugumizi gani kuhakikisha wakulima wanapata maeneo yao na wafugaji wanapata maeneo yao? Hii migogoro ya kila siku itaisha lini na wakati tunayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maeneo aliyoyasema Mheshimiwa Waziri kaka yangu, nafikiri yaanishwe ni vijiji gani, ni wapi, ili wafugaji wajue! Kama wachangiaji wengi walivyosema, mkulima na mfugaji ni watu ambao wanaingiliana, jamani tumejaza nyama kwenye mafriji yetu lakini kwa nini leo hawa wafugaji tunawadharau? Ilifikia kipindi kwa sababu ya wafugaji kuhangaikahangaika wakadhalilishwa kwa kuambiwa kuwa wamekonda kama mifugo yao, hii si haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mimi ya kwangu ni hayo na sitataka kuzungumza sana kwa sababu nina hasira, naomba wafugaji waliotolewa Ihefu warudishiwe mali zao na

wathaminishiwe ng'ombe zao. Kama siyo kurudishiwa ng'ombe zao na mali walizopoteza naomba zirudishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, pole na hasira. Sasa ni Mheshimiwa Shibuda, Mheshimiwa Yussuf Hussein, Mheshimiwa Saleh Pamba na Mheshimiwa Martha Umbulla. Mheshimiwa Pamba.

MHE. SALEH A. PAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nakushukuru kunipa nafasi ya kuchangia katika sekta hii na katika mada ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii niwapongeze Mawaziri hawa kwa kuteuliwa, najua ni wachapa kazi, kwa hiyo watai-*turn around* Wizara hii haraka sana iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupata hotuba ya Mheshimiwa Waziri jana nikaenda kuangalia mipango ambayo imeandaliwa katika Wizara hii hasa kwa upande wa sekta ya uvuvi. Wizara hii inao Mpango wa Maendeleo ya Uvuvi wa miaka mitano kuanzia mwaka 2011 – 2016. Pia inayo malengo, wanasema ukuaji wa sekta wanataka itoke kwenye asilimia 4.5 hadi asilimia 7 kwa mwaka, wanataka mchango wa sekta hii utoke kwenye asilimia 1.2 hadi asilimia 5,kwa mwaka, wanataka kukua mapato kutoka 6.5 bilioni hadi bilioni 12, wanataka kuongeza uzalishaji, wanataka kukuza ajira na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni malengo mazuri sana ambayo yametajwa katika mpango wa Wizara hii na mpango wa Serikali wa kuweza kuikuza Sekta hii. Kama walivyosema katika hotuba yao kwamba sekta hii inayo nafasi kubwa ya kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimoja ambacho nimekiona hakiendi sambaamba na mipango mizuri ya Wizara hii, ni jinsi ambavyo Serikali inatenga rasilimali fedha katika Wizara hii. Fedha zinazotengwa hasa katika sekta yote, sekta ya mifugo na uvuvi ni kidogo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, wamesema kwamba katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2011 mpaka 2015, sasa tuko mwaka wanne wa utekelezaji wa Mpango wa Uvuvi, walipendekeza wangetumia shiliingi bilioni 302. Mwaka juzi, mwaka jana na mwaka huu zilitakiwa zitengwe shiingi bilioni sitini, sitini lakini nimeangalia Vitabu vya Bajeti ya Maendeleo ya Wizara hii katika sekta ya uvuvi ni sifuri. Sasa inashangaza kwamba unao mpango mzuri lakini hutengi rasilimali fedha za kuweza kuutekeleza, je, utatekelezaje mipango hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali na hili nadhani ni muhimu sana, tunapohitimisha tuweze kupata kauli ya Wizara na Serikali kwamba kwa kiasi gani watatengea fedha hasa katika sekta hii ya uvuvi. Kwa mwaka huu walitakiwa watenge shilingi bilioni 60 lakini bajeti iliyopo ni shilingi bilioni 25 tu. Sasa wavuvi na sekta ya uvuvi itaendeshwa vipi. Kwa hiyo, nitataka nipate majibu ya Serikali na kama ipo haja ya kuifumua Bajeti ya Serikali, lazima ifumuliwe ili fedha za uvuvi zipatikane ili tuweze kuhakisha kwamba *potential* hii inafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni uwezo wa Serikali. Tunajua kwamba uwezo wa Serikali bado ni mgumu lakini bado tuna jukumu la kuhakikisha kwamba tunaisaidia Serikali na sekta hii inaimarika. Kulikuwepo na mradi wa MACEMP ambapo malengo yake yalikuwa mazuri tu. Lengo lake moja ilikuwa ni kuwasaidia wavuvi wadogowadogo, kuongeza thamani na suala la mazingira. Nataka kujua Serikali kwamba

bajeti ya mwaka jana walisema kwamba wanaandaa *MACEMP II,* nimeitafuta katika vitabu vya Serikali sijaiona. Huu ni mradi mzuri wa kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo lakini hakuna fedha iliyotengwa, hakuna taarifa yoyote inayosema kwamba tumewasiliana na Benki ya Dunia au tumewasiliana na Taasisi yoyote nyingine ili kuweza kutusaidia katika mradi huu, nataka nipate maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uvuvi katika bahari kuu, tunalichezea, tunaibiwa sana kama Serikali. Kwa hiyo, inabidi nayo Serikali ijipange vizuri katika eneo hili. Kwa mfano, kwa taarifa ambazo tunazo ni kwamba Serikali inapoteza siyo chini ya dola milioni 20 kila mwaka kutokana na samaki wanaoibiwa katika bahari kuu. Hilo ni eneo ambalo tunaweza tukapata fedha za kutosha na ufugaji wa samaki pia ni eneo lingine ambalo tunaweza tukapata fedha za kutosha.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante. Mheshimiwa Martha Umbulla ajiandae Mheshimiwa Shibuda, naona amerudi.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kidogo kwenye Wizara hii ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niende moja kwa kwenye migogoro inayowakabili wafugaji na wakulima na hasa kwenye Wilaya ya Kiteto. Wafugaji wanategemea rasilimali ya asili hasa nyasi na miti ambayo Mwenyezi Mungu amewatengenezea lakini wakulima wanafyeka hizo nyasi, miti na kila kitu wanaleta mazao yao wanapanda na ndiyo tegemeo la maisha yao la kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu jamii hizi mbili zinatofautiana sana katika shughuli zao za kibinadamu. Kwa utofauti huo, kwa vyovyote vile tungetegemea kwamba wanapoingiliana lazima kutokee migogoro. Hivyo ndivyo inavyotokea, mahali ambapo kuna wafugaji na wakulima, wakitofautiana sana kwenye masuala ya mambo yao ya maisha, ndipo tofauti zinapotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwa nafasi hii Serikali sasa ilione hili na hasa kwa migogoro mingi inayotokea katika nchi yetu iweze kuhakikisha kwamba Halmashauri zetu zote nchini ziweze kutenga maeneo…

MWENYEKITI: Mheshimiwa Martha, wewe ni mdau wa mambo haya ulitakiwa ku-*declare interest* kabla hujaanza kusema. *(Makofi)*

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivyo na mimi nikiwa sehemu ya Serikali kwamba ndiyo juhudi tunayoifanya lakini nilitaka kusema kwamba sote tuweze kuona na tusaidiane na Serikali kuhakikisha kwamba migogoro hii tunaipunguza kwa ajili ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kidogo kuhusu mgogoro huu wa Hifadhi ya Jamii ambao umekuwa gumzo kidogo wiki iliyopita pengine kwa kuweka picha kidogo kwa wananchi ambao waliweza kupotoshwa hapa na pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji saba katika Wilaya ya Kiteto viliunda Hifadhi ya Jamii inayoitwa Emboley Mortangosi. Hifadhi hiyo iliundwa na wakulima na wafugaji lakini baadaye

ikavamiwa na wakulima wakasahau kwamba waliunda pamoja na wenzao wafugaji. Kutokana na hali hiyo ikapelekea kwenda kwenye vyombo vya sheria na hatimaye kwenye Mahakama ya Rufaa. Baada ya *ruling* ya Mahakama ya Rufaa, ikatuhitaji Serikali tuweze kuingilia kati turudishe amani ya wananchi wetu katika Wilaya ya Kiteto. Tulichofanya tuliweka utaratibu kwamba wale waliovamia, awe ni mkulima au mfugaji, aweze kuondoka katika eneo lile ili tuweke utaratibu vizuri, tupime upya na tusikilize mapendekezo ya wananchi. Kwa hiyo, kazi kubwa ikapewa Serikali nikiwepo mimi na Mkuu wa Mkoa na ndicho tulichofanya na hata hivi ninavyozungumza wakulima wote, wafugaji wote, wote waliovamia eneo hilo wamekwishatoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachoomba ni kwamba sisi viongozi tuendelee kuelimisha wananchi wetu. Viongozi wote tushirikiane badala ya kupotosha wananchi ili tuweze kwa pamoja kupunguza migogoro inayotokea katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu na pale tutakaposhirikiana ndiyo muafaka wenyewe kuhakikisha kwamba wakulima na wafugaji wanaendelea kuishi pamoja na wanaendelea kusaidiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kidogo kuona kwamba unapotenda kazi kwa niaba ya Serikaili na kwa niaba ya wananchi, baadhi ya viongozi wenzako wanakuona kwamba wewe ndio unachochea migogoro. Mimi naomba kwa nafasi hii, mimi ninayehakikisha naleta amani na labda wengine wanaowaambia wavamizi wasitoke, naomba wananchi wapambanue ni nani mchochezi katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona nilisemee hili kwamba sisi viongozi katika nchi hii tushirikiane kwa pamoja, tujenge Halmashauri zetu ili ziweze kuweka matumizi bora ya ardhi na hatimaye migogoro hii kwa vyovyote itapungua na hivyo wakulima na wafugaji waendelee kukaa pamoja kwa sababu sisi wote tunahitajiana na hasa walaji wanahitaji wakulima na wafugaji kwa pamoja. Naomba niishie hapo, niliona nizungumzie hilo, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Shibuda ajiandae Mheshimiwa Murtaza Mangungu.

MHE. JOHN S. MAGALLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa hii ili niweze kuchangia Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo pamoja na Uvuvi. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kuteuliwa kuwa viongozi wa Wizara hii ikizingatiwa kwamba asili yao ni wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekti, naomba Wizara hii sasa itekeleze deni la kuhakikisha kwamba inaratibu mtoko wa dhuluma zinazoleta hitilafu kwa wafugaji. Wanaochukia wafugaji ndiyo haohao wanapenda mishkaki, maziwa, wanapenda nyama chomba lakini nasikitika kusikia kwamba watu wanawachukia wafugaji. Je, ni wapi pana supu ya nyuki, ni wapi pana mishkaki ya nyuki mpaka kuwepo na Wilaya isiyopenda mifugo? Mimi nasikitika sana kuona hizi dhuluma za kuwachukia wafugaji na baadhi ya Wabunge wanasema maneno ya ajabu dhidi ya wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyeiti, katika kuchangia hoja ya Wizara hii, sasa najikita katika hoja ya dhuluma zinazotekelezwa na Wizara Mtambuka na naomba Wizara hizo sasa zihakikishe zinaleta utumishi adhimu kwa wafugaji. Wizara ya Maliasili kupitia Wanyamapori ni laana kwa wafugaji. Vilevile pana ukosefu wa sikio sikivu la viongozi mfano Ma-*DC* na Wakuu wa Mikoa wanapopelekewa malalamiko ya wafugaji. Naomba Serikali ihakikishe inaondoa ombwe hilo. Vilevile pana ombwe la masikio sikivu la kugawia ardhi wafugaji, je, ni lini hili litakamilika? Naishauri Serikali itekeleze siasa na sera ya program okovu kwa vitendo dhulumati vinavyofanywa kwa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitaka Wizara hii itamke ni lini itakuwa na ushirikiano na Wizara ya Ardhi na Wizara ya Maliasili na Utalii na watakuja lini kutoa matamko kwamba wanaandaa huduma endelevu. Vilevile, Wizara ya Viwanda ni lini itakuwa na viwanda vya nyama, viwanda vya ngozi na viwanda vya maziwa? Ni lini ardhi itapatikana hasa kwa wafugaji? Naomba vilevile Serikali iungane na Wizara hii ili kuhakikisha panakuwa na masikio sikivu. Kupitia Wizara ya Maliasili, Ardhi, Viwanda, je, ni lini watatoa tamko la kuhakikisha kwamba maeneo ya malisho ambayo yanapakana na hifadhi yanagawiwa kwa uwiano uleule ambao wamepanua wanyamapori na wanyamakaya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhakikisha Serikali inatekeleza haki zake kwa wafugaji, naiomba iache mila potofu za mitazamo hasi ya kwamba wafugaji hawapendi kupunguza mifugo. Je, pana huduma gani ambayo leo Serikali katika miaka 50 wanaweza kusema wametoa kwa ajili ya kupunguza mifugo? Wafugaji wanataka maisha bora na hawapendi kuwa ni watu wa kutangatanga lakini Serikali ina kigugumizi gani? Kwa nini ina dhuluma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kuna siri gani dhidi ya wafugaji? Naomba nielewe baada ya utumishi mbovu wa Serikali dhidi ya wafugaji kwa nini CCM isinyimwe kura? Je, wafugaji kwa nini wasiwaadhibu? Napenda kuwaambia wana CCM muelewe kwamba Serikali imeitia hatiani CCM kwa kutoa huduma badhilifu na uonevu kwa wafugaji. Kwa nini wafugaji wasiwe na zinduko la fikra mbadala la kutafuta ukombozi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeitia hatiani CCM ikose imani kwa wafugaji, Serikali imekuwa na makosa ya kutolipa fidia kwa wafugaji walioathirika na *operation* mbalimbali, Serikali kupitia TAMISEMI, Wakurugenzi wanawaita wafugaji wahamiaji haramu na wavamizi, wanatoza kodi ambazo ni za rushwa na dhuluma, ng'ombe ya Sh.300,000/= inauzwa kwa Sh.20,000/= au Sh.30,000/=, kwa nini hii isiwe ni hatia ya kuinyima CCM kura kutoka kwa wafugaji? Kama CCM haitaki adhabu ya kifungo dhidi ya kura za wafugaji, namwomba sasa Mwenyekiti wa Taifa ambaye pia ni Rais amuulize Mheshimiwa Kinana utumishi wa Serikali badhilifu huu unastahili adhabu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ina siri gani dhidi ya kubaguliwa wafugaji Wasukuma wakati wenzao wafugaji wa Kimasai wamepewa liwazo. Wafugaji wa Kisukuma wako Mkoa wa Rukwa, Katavi, Tabora, Mwanza, Shinyanga na Morogoro, Mikoa 14 wafugaji wamedhulumika, kwa nini hawajapewa liwazo? Mheshimiwa Rais Kikwete huruma yako uliyowapa wafugaji wa Kimasai tunaomba itekelezwe kwa wafugaji wa makabila mengie, wafugaji wa Kisukuma 90% wanateseka. Kwa nini hivi sasa Wasukuma wasibadilike na kusema baibai CCM kutokana na hizi dhulumati kwa wafugaji? Kupitia Operesheni Tokomeza, kwa nini wafugaji wasiseme kwamba waiadhibu CCM na wenyewe wafanye Operation Tokomeza CCM? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana, leo nimeamua niwaambie kwa sababu ukiona rafiki yako anafanya makosa halafu humwambii humpendi. Kutokana na madhira haya, je, CCM ina ushujaa gani wa kuwaendeleza wafugaji? Katika miaka 50 kuna viwanda gani vya maziwa, nyama na kadhalika? Napenda kusema kwamba utamu wa chai ni sukari na siyo majani ya chai, je, utamu wa siasa na sera na program za CCM ni kitu gani kama siyo dhuluma? Serikali ifungue uamuzi yakinifu kwa kuondoa mkanganyiko wa kusigana kati ya Wizara zinazohusika. Wafugaji ni wazalendo kwa nini waitwe wahamiaji haramu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii CCM siyo ya TANU asilia, CCM ya Nyerere na Karume haikuwa na kauli hizo, iliileta viwanda vya nyama na vya ngozi lakini leo kuna nini? Ubinafsishaji

huu malengo yake ni nini? Je, bado pana CCM asilia na kama kuna mtu anataka mdahalo niko tayari. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhuluma za tozo na dhuluma za ardhi, dhuluma ya mifugo kwa bei ya viwango vya chini, wafugaji watakuwaje lindo la usalama dhidi ya ujangili? Bila suluhu ya liwazo kwa wafugaji, nasema wafugaji wa Mikoa 14 ambao wamepata utumishi dhulumati, sasa mnahitaji pambazuko jipya, zindukeni amkeni na namwomba Mheshimiwa Kinana atuambie Serikali yake itatoa fidia lini, uchaguzi ni keshokutwa majuto ni mjukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, CCM na Serikali wakunjue, wahakikishe wanatenda haki wasije wakalalamika na bado hatujaanza hii ni bashirafu. Naitaka Serikali ianze kuifanyia mema CCM la sivyo Serikali hii inaifukuza CCM madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali sasa iseme ni lini itatekeleza utoaji wa liwazo kwa wafugaji. Nasikitika wafugaji hivi sasa wamekuwa ni watu wanaoteseka na yatima katika nchi hii. Wafugaji wote mnaonisikiliza sasa nawaomba wote mzinduke TANU iliwatetea, mliunga mkono TANU tukapata uhuru dhidi ya wakoloni, naomba umoja huo kama CCM hawautaki sasa mtafute chama mbadala mpate mapunduzi ya fikra tusonge, mapambano yanaendelea, ahsanteni. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mangungu!

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya jambo ambalo linatupa shida sana sisi wanadamu ni kuweza kuzitumia fikra zetu vizuri na kuziwasilisha kwa wenzetu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Mapinduzi ambacho kimesemwa ndicho ambacho kimeandaa sera ambayo inamruhusu mtu yeyote mwenye asili yoyote kuishi mahali popote bila ukanda. Vipo vyama ambavyo vinahubiri sera ya ukanda kwamba kila mtu akae kwake asiende kokote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama inavyoeleweka ni Mbunge wa Kilwa lakini nina Wasukuma pale na nimewapokea kwa sababu ni watoto wetu na tunaendelea kuwalea. Vilevile tuna Wamasai, sasa je itakapofikia kwamba kila mtu abaki katika eneo lake sijui ng'ombe wale ambao wanazidi 50,000 watakwenda kuwekwa wapi, naamini mtawahamishia jirani kwa Mheshimiwa Shibuda ili aweze kuwahifadhi nyumbani kwake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya bajeti ya Wizara hii mimi nimeisoma na kuisikiliza kwa mashaka sana. Tumezungumzia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kilimo, ilikuwa ni kilio. Tumetoka hapo tumekuja kwenye hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi nayo vilevile ni kilio. Sasa tunapoandaa bajeti hizi na Waziri wa Uwezeshaji pamoja na Waziri wa Mipango wamekuja kutusomea hapa tuna mipango ya kuwawezesha na kuwainua wananchi kiuchumi, hizi ndiyo nyanja kuu za kiuchumi za wananchi kilimo, mifugo na uvuvi. Wizara hizi zote hazina bajeti ya kutosha, hili ni jambo ambalo kwa kweli lazima Wabunge wenzangu tuliangalie kwa umakini na tuhakikishe tunaweka namna ya kuweza kuongezea fedha katika kasma ya bajeti hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nilizungumzie, ni jambo la ajabu sana na la kustaajabisha kwenye kasma ya bajeti ya Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi na kwa bahati nzuri Mawaziri wote ni wafugaji hawajui masuala ya uvuvi na wala ladha ya samaki hawaijui ikoje, hili ni tatizo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoweka Wizara hizi pamoja halafu Idara ya Uvuvi eneo ambalo tutawawezesha wavuvi katika maeneo yetu ya Somanga, Mitega, Kivinje mpaka

Pande, hakuna hata senti moja ambayo imewekwa kwa maendeleo ya uvuvi. Tunaanzishaje mabwawa ya kufuga samaki ili wavuvi wasiweze kwenda mbali? Hili mama Hewa amelisema hapa kwamba vifaranga vya samaki ni Sh.300 hadi Sh.500, mimi hivyo vifaranga vya samaki katika ukanda mzima wa Pwani kuanzia Rufiji, Kilwa mpaka Lindi havijawahi kufika, sasa huu ni mpango gani ambao mnauandaa wenzetu? Tuelezeni!

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa suala la *Deep Sea Fishing*, Idara hii itawezaje kufanya kazi, Makao Makuu tunajua yako Zanzibar lakini inawezaje kufanya kazi kwenda maili zote kufuatilia hawa watu ambao wanafanya uvuvi usiofaa? Muwanunulie japo *helicopter* moja au mbili ili kuwawezesha, wawe na boti za kufanya kazi hii, unategemea waende kufanya kazi na ngalawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo tunalipendekeza na nimelizungumzia katika bajeti za miaka yote, ni lazima tuwe na *fishing port,* tungeweza kuwa na *fishing port* Kilwa, Pangani na hata Bagamoyo, ingeweza kusaidia sana kukusanya mapato ya Serikali kwa wavuvi ambao wanakwenda kuvua katika hizo *deep sea*. Hata leo hii tukiwaambia wavuvi warudi Dar es Salaam kuja kukaguliwa wengine wanakunja kona na kukimbia. Sasa hili ni jambo ambalo Serikali ni lazima iliangalie kwa namna ya pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo ambalo linanistaajabisha kwa nini nchi hii inaendelea kuli-*entertain*, kwamba mpaka leo hii tumekuwa tukiagiza samaki kutoka nje ya nchi wakati samaki tulionao hapa ndani wanatosha na hatuwapi vifaa wavuvi wakaweza kuvua ili watosheleze. Samaki zinakuja hapa zinazaliana, zinakimbia na kwenda katika maeneo mengine kwa sababu hizi ni *immigrative species* ambazo huwa zinahama kila baada ya msimu fulani. Sasa hili naomba liangaliwe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la viwanda vya nyama, ni jambo la kustaajabisha sana mpaka sasa Serikali inakuwa na kigugumizi kwenye kuwekeza kwenye viwanda vya nyama. Vilevile *incentives* za kutosha hazitolewi kwa wawekezaji wa viwanda vya nyama na ngozi. Leo hii hawa Wasukuma ambao wanalalamika wanatembea na ng'ombe, isingekuwa wanalalamika kama wangekuwa na sehemu ya kupeleka ng'ombe wao na wakawauza. Kwa hiyo, lazima tufanye ufugaji wenye tija kwa kuanzisha viwanda vya nyama na ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa ni kwamba Serikali lazima iangalie kwa umakini mkubwa sana suala la uagizwaji wa nyama kutoka nje. Leo hii migodi yote ambayo tunayo hapa nchini bila ya kuwa na nyama ya kutosha wataendelea kuagiza nyama kutoka nje na tumekuwa tukipata hasara kubwa sana kwa kutumia fedha zetu za kigeni kwa ajili ya kuagiza nyama ambazo tunazo hapa nchini. Serikali lazima itumie umakini mkubwa sana kuhakikisha kwamba tunaweka *incentives* za kutosha ili wawekezaji waweze kuwekeza katika viwanda vya nyama, tuzalishe nyama na hawa Wasukuma waache huu msamiati wa kutembea na ng'ombe, mtu kuwa na ng'ombe 200,000 au 50,000 na Mheshimiwa Shibuda ataacha kelele zake kuhusu nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naomba kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge orodha yetu inakamilishwa na Mheshimiwa Mkiwa na ndiye mchangiaji wa mwisho na baada ya hapo Waziri ujiandae.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Wizara hii ya Mifugo na Uvivi kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na afya njema kuweza kuchangia katika Bunge lako hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kaka yangu Kamani pamoja na Naibu Wake na nipende kuwaambia Wizara waliyopewa siyo Wizara ya masikhara bali ni Wizara ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema ni Wizara ngumu? Kwa sabadu wafugaji wana mifugo mingi lakini bado hali zao za kimaisha si nzuri, wavuvi ndiyo kabisa. Wavuvi hawana ruzuku ya uvuvi kama wakulima na wafugaji, wavuvi hawana wagani wa kwenda kuwasimamia na kujua uvuvi wao unakwenda salama au vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Ilemela, Kata sita ndani ya Wilaya hii zote zimeguswa na Ziwa Victoria. Nikisema zimeguswa na Ziwa Victoria shughuli kubwa ya wakazi wa Wilaya ya Ilemela ni uvuvi. Cha kusikitisha ni kwamba Halmashauri hazitengi fedha za kuwawezesha Maafisa Uvuvi kuwafikia wavuvi hawa, hakuna *speed boat* za kuweza kudhibiti uvuvi haramu katika Wilaya hii, hakuna vitendea kazi wanavyopewa wavuvi hawa, hakuna mikopo au kusema darasa wanalopewa wavuvi ili waweze kujiendeleza. Kwa hiyo, kwa kuwa naamini kabisa kwamba Mheshimiwa Kamani katika Wilaya yake kuna uvuvi, kwa maana hiyo naposema wavuvi wa Ilemela afahamu kabisa na wavuvi wa Busega wamo ndani yake, je, amejipanga vipi sasa kuacha hizi propaganda, amejipanga vipi kiuhakika ili kuweza kuwanusuru wavuvi na ujambazi wa ndani ya Ziwa Victoria anaufahamu, amejipanga vipi kuweza kuwainua wavuvi wadogowadogo ili waweze kujiendesha kimaisha na bila msukosuko wanaoupata sasa hivi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mifugo na Uvuvi wanakimbilia zaidi kukamata nyavu haramu lakini tulikwishawaomba basi watoe nyavu za mfano kama pembejeo angalau na wavuvi wajue kwamba hizi ndiyo nyavu halali. Kama wengine wanaweza kupata ruzuku ya pembejeo na bado wafugaji wengine wakapata kifuta machozi cha kuweza kujiendesha kimaisha kwa kupata mifugo ya kuanzia maisha baada ya ukame, hili hatulikatai, lakini je, wavuvi mmewapangia nini? Hili napenda nilielewe na Mheshimiwa Kamani ili wavuvi wa Ramadi na Nyashimo waweze kujua nini wamepangiwa, leo niko tayari kukamata shilingi lakini nijue wavuvi wamepangiwa kitu gani cha msingi na siyo blabla kwa sababu ni miaka mingi imebakia kuwa blabla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa ambalo hili limekuwa ni kero, nafikiri mwaka jana mimi nimeliongea, Mheshimiwa Mwijage aliliongelea nafikiri na Waheshimiwa wengine waliliongelea pia, wavuvi kutozwa leseni zaidi ya mara moja. Mvuvi anapokata leseni Halmashauri moja hata kama ndani ya Mkoa huohuo amekata Nyamagana, akifika Ukerewe anaombwa akate leseni nyingine lakini gari ikishakata *motor vehicle* itazunguka Tanzania nzima hamna anayeombwa kukata *motor vehicle* nyingine. Kwa maana hiyo nakuomba Mheshimiwa Kamani kwa sababu mwaka jana niliomba Wizara ya Mifugo na Wizara ya TAMISEMI mkae mliangalie hili na nashukuru sana juzi moja nilimsikia kiongozi mmoja wa Chama cha Mapinduzi akisema kwamba tusiendelee kuwakamua wauza vitumbua lakini kuna watu wamekalia mamilioni hawataki kulipa kodi. Kwa hiyo, tusiendelee kuwakamua wavuvi wadogowadogo wakati katika bahari ya Hindi kuna wavuvi wakubwa na wanakimbia bila kulipa pesa nyingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Kamani ninauliza, hatujatengeneza gati ambapo meli kubwa zikimaliza kuvua zije kukaguliwa mzigo na kama zikiondoka bila kukaguliwa mzigo wanatakiwa walipe faini. Nataka kujua meli hizi zinaondoka bila kukaguliwa mzigo ni faini kiasi gani wamekwishalipa ili pesa hizi ziweze kuja kuwasaidia wavuvi wadogowadogo. Kwa sababu wanapoondoka na zaidi ya shilingi bilioni 352 kwa meli kubwa ambazo pesa hizi zingeweza kuwasaidia wavuvi wadogo hata kwa kupata pembejeo, sasa wavuvi hawa wadogo mna mpango gani nao?

Kama imeshindikana Wizara hii kuchanganywa na Wizara ya Mifugo basi muirudishe Maliasili na iwe na kitengo chake maalum cha kuisimamia ili wavuvi wajue ni wapi wanaweza wakaenda kutafuta madai yao lakini siyo kila siku ni kufukuzana na wavuvi kwenye Ziwa Victoria. Akija Polisi ana njaa, akamfukuze mvuvi amkamate amtoe pesa, akija Afisa Mifugo naye ana njaa amkamate mvuvi amtoe pesa. Kwa maana hiyo, hicho kitu naomba, kama imeshindikana kuingia kwenye Wizara hii basi wavuvi warudishwe Maliasili na Utalii na watafutiwe kitengo chao ili waweze kujisimamia na kujiendesha wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kidogo nigusie suala la mifugo. Watu wengi wameongea kuhusu mifugo na nafikiri huu ni mwaka wa nane mimi naongea kuhusu mifugo. Wanaposema wafugaji wapunguze mifugo hakuna mtu mwenye pesa benki akaambiwa apunguze pesa bila mpangilio. Watafutieni viwanda, majosho na muwafundishe ni jinsi gani waweze kunenepesha ng'ombe, tumeona *NARCO* wana ng'ombe mpaka wana kilo 800 ili hata kuuza auze kwa faida na huku ndiyo kupunguza mifugo lakini siyo tu umwambie apunguze mifugo halafu humwambii kitu kingine. Punguza mifugo anakuja Afisa Mifugo anachukua ng'ombe wake kuwapiga risasi na wengine akiwachukua anasema walipiwe kodi, akilipa Sh.300,000/= anapewa risiti ya Sh.30,000/= pesa nyingine imeishia mfukoni.

Kwa hiyo, tunaomba hawa wafugaji sasa, muwajengee viwanda vya uhakika na ninaamini kabisa hapo mmejipanga, Waziri ni Mfugaji na Mvuvi na Naibu Waziri ni mfugaji. Kwa maana hiyo, bila shaka mkikaa mkitulia, haya mambo yataenda sawa na Wavuvi na Wafugaji wataepukana na adha yote ambayo wanaipata sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Wizara na viongozi wake kuanzia Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza wafugaji kwa kuendelea na ufugaji pamoja na changamoto nyingi zinazowakabili. Hanang ni moja ya Wilaya iliyo na mifugo mingi na wafugaji wengi, lakini haina miundombinu ya wafugaji. Hanang ni eno hilo ndani ya Bonde la Ufa ambapo maji ni changamoto kubwa isiyohimilika kwa wafugaji.

Ninaomba wakati wa majumuisho Mheshimiwa Waziri aeleze katika mwaka huu wa fedha ni malambo mangapi yatajengwa, vilevile Wilaya ya Hanang ina Ziwa Basotu ambapo lina samaki. Ziwa linafungwa mara nyingi bila mpangilio, bila ya elimu kwa wafugaji na hata bila jitihada za kuboresha mazingira ya Ziwa ili samaki wastawi, je, Waziri yupo tayari kuwatumia wataalam watakaotafiti changamoto zinazozuia samaki kustawi je, ni kwa nini Ziwa limefungwa kwa muda mrefu?

Naomba wakati wa kujumuisha uwaeleze Ziwa litafunguliwa lini ili watu wangu wapate faraja?

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nkasi hakuna maeneo tengefu kwa sababu vijiji havijapimwa na hii inaendeleza migogoro kati ya jamii hizi mbili wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukosefu wa ruzuku kwa wavuvi, mpaka sasa wavuvi hawana ruzuku toka Serikalini kwa nini kama tumeweza kuwapatia wakulima ambao ni wengi je, kwa nini wachache hawa wasipewe ruzuku? Naomba maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ndogo kwa Wizara hii inapelekea kuwepo fedha ndogo kwenye Halmashauri. Nkasi inahitaji kupata shilingi milioni 400 kwa mwaka ili kukidhi mahitaji yao lakini imepewa *ceiling* ya shilingi 73,000,000/= wapi na wapi bajeti kubwa inabaki Wizarani na kwenye Kanda (Z.V.C.) kwa nini kuna mifugo huko juu au mifugo ipo katika Wilaya kwenye Halmashauri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nkasi ina upungufu mkubwa wa watumishi wa mifugo kati ya watumishi wanaohitajika 83, kuna watumishi 19 tu na mwaka huu tumeomba watumishi wengi tumepata watatu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitendea kazi, baada ya kuwatenganisha toka Kilimo, Idara ya Uvuvi na Mifugo Wilayani Nkasi hawana gari wala pikipiki, naomba wapewe usafiri. Vifaa tiba hawana *(extention kits),* kumbe inakuwa shida kuhudumia wakulima/wafugaji wanapopata matatizo ya mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. JOHN P. LWANYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa ujenzi wa Bwawa la Itagata, Tarafa ya Itisi, Wilayani Manyoni. Jibu pekee la matatizo ya maji kwa ajili ya mifugo ni mabwawa na malambo. Naiomba Serikali ijenge mabwawa na malambo zaidi hasa katika Kata za Sanjaranda, Aghundi, Idodyandole, Ipande, Kitaraka, Mgandu, Mitundu na Rungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya wakulima na wafugaji imeendelea kuwa kero kubwa. Wahamiaji kutoka mikoa jirani ya Shinyanga, Tabora na Mwanza wameendelea kuja kwa wingi Wilaya ya Manyoni na Mifugo yao mingi, huku wakiharibu sana mazingira. Nashauri Serikali ichukue hatua za kuwalazimisha wananchi wa Mikoa ya Shinyanga na Mwanza wapande miti na nyasi kukabiliana na tatizo la ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. ALLY M. KEISSY: Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu kubwa ya Jimbo langu linahusika na uvuvi katika Ziwa Tanganyika lakini Wizara ya Mifugo na Uvuvi haina mpango wowote wa kuwasaidia wavuvi wa vijiji karibu vyote.

Ninaishukuru sana Wizara ya Mazingira ambayo ndiyo angalau inasaidia kwa kujenga mwalo katika vijiji vya Kirando na Korongwe, lakini Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambayo ndiyo inahusika haina mpango wowote ule hata kusaidia wavuvi sehemu za kukaushia samaki na dagaa kazi yao kubwa ni kuchukua ushuru kwa wavuvi tu, kuwakopesha nyavu na *engine* wavuvi hao, ni kama hakuna chochote kile wakati kuna wavuvi wengi sana maisha yao hayana maendeleo kabisa maana masoko ya kuuza samaki na dagaa hawana kabisa na mara kwa mara kutupa samaki kwa kukosa soko au kuuza kwa bei ya hasara sana na maisha ya wavuvi kuwa na hali mbaya sana.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ethiopia wameendelea sana katika mazao ya ufugaji wa ng'ombe, je, tumekwenda kujifunza waliyofanya? Tuna taarifa kuwa walikuja kujifunza hapa Tanzania. Lakini wanafanya vizuri kuliko sisi kama hatujaenda kujifunza mikakati yao basi twende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia kila la heri kazini na tuna imani nanyi.

MHE. ASHA MSHIMBA JECHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya ingawa zipo changamoto nyingi zinazoikabili Wizara hii kati ya wakulima na wafugaji zinazochangiwa na ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ina mifugo mingi na samaki wengi, Wizara ina mkakati gani wa kuwaendeleza wafugaji na wavuvi ili waweze kuifuga kisasa na kuvua kwenye kina kirefu cha bahari. Aidha, sambamba na kuanzisha viwanda kuweza kuongeza thamani na ajira ili vijana wetu watulie vijijini na kujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inatoa leseni ya uvuvi kwa wavuvi ndani ya nchi kwa vyombo vidogo vidogo na meli kubwa za uvuvi kutoka nje ya nchi, je, meli hizi kubwa za uvuvi za nje ya nchi nani anazifuatilia kujua wamevua tani ngapi na wanastahiki kulipa kwa utaratibu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvuvi haramu, Wizara ina mkakati gani wa kugundua chanzo cha uvuvi haramu ambacho ni wafanyabiashara wanaoleta nyavu haramu na kuadhibiwa badala wavuvi pekee?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina mikakati gani ya kusaidia ajira kwa vijana kwani ni miongoni mwa Wizara ambayo ina uwezo wa kutoa ajira nyingi kwa muda wa kati na muda mrefu na kuongeza Pato la Taifa. Ahsante.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana kuona hakuna mahali popote katika hotuba hii panapoonyesha namna Serikali itakavyosaidia wavuvi wadogo wadogo na hasa wavuvi wa Ziwa Rukwa ambalo limesahaulika miaka yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo vinginevyo siungi mkono hoja.

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia wale wafugaji ambao ng'ombe wao waliuawa kwa kusababishwa na *Operation Tokomeza* walipwe kama watu wa Loliondo na sehemu nyingine huko Mikoa ya Kaskazini. Ahsante.

MHE. SAID M. MTANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa miaka minne sasa iliahidi kutoa motisha kwa vikundi mbalimbali vya uvuvi vilivyochoma nyavu zao za uvuvi haramu, ahadi hiyo kwa vikundi vya Kijiji cha Ruvu, Mchinga I, Mchinga II, Kijiweni na Mvuleni. Mmewavunja moyo na sasa wamerejea tena kwenye uvuvi haramu.

MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikiwa katika mikakati yake ya kudhibiti majangili yanayoendelea kuwaua wanyamapori tunaowahifadhi katika hifadhi zetu za Taifa. Serikali hii ilishindwa kufanya kazi ya kuwadhibiti majangili na badala yake ikajiingiza katika *Operation Tokomeza* ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ng'ombe wa wafugaji wa Lumbe katika Kata ya Lumbe, Wilayani Kaliua wapatao 34,700 walihujumiwa na *operation* hiyo kwa wafugaji kulazimishwa kumlipia kila ng'ombe shilingi 180,000/= kiasi cha ng'ombe 30,000 walilipiwa kwa kiasi cha shilingi 5,400,000,000/= ambazo pamoja na wafugaji kumlipia kila ng'ombe stakabadhi walizopatiwa wafugaji hao si stakabadhi ya Serikali. Aidha ng'ombe 8,700 walichukuliwa na maofisa walioshiriki katika *Operation Tokomeza* katika hifadhi ya Kaliua eneo la Lumbe katika Kata ya Kaliua. Serikali hii hii ndiyo iliyowapora ng'ombe wa wafugaji hao huku ikijua iliwatia katika umaskini wafugaji hao wasiokuwa na hatia. Wafugaji hao walipopaisha sauti zao kuwa wameonewa Serikali hii ilichofanya ni kusitisha tu kitendo chake cha kuendelea kuwatokomeza ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Serikali kusitisha zoezi lake la kuwatokomeza ng'ombe kitendo hicho Serikali hii inaamini iliwapunguzia umaskini hao wafugaji. Je, ni kwa nini Serikali haikuweka bajeti ya kuwafidia wafugaji waliotokomezewa ng'ombe wao huko Kaliua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali inijulishe hatua inayochukua dhidi ya hii dhuluma iliyowafanyia wafugaji hao.

MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao ya uvuvi tegemeo la wanyonge kwa vile wanaweza kukidhi kununua kutokana na kipato chao. Wananchi wanyonge wanaponea dagaa kwa vile nyama na vitoweo vingine bei zake hawazimudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya uvuvi ni ngumu sana na wavuvi hawana motisha yoyote toka Serikalini. Hawapati pembejeo kama wanavyopata wakulima, hawapunguziwi bei ya vifaa vya uvuvi vile vizito kama wanavyopunguziwa wamiliki wa ndege. Mfano, bei ya nyavu moja ni shilingi 650,000/= hadi 800,000/=; bei ya engine ya 60HP ni shilingi milioni 10 na bei ya mbao sasa imevuka maradufu. Ubao mmoja wa 1x12 ni shilingi 45,000/= je, ili ukamilishe mbao zote za kutengeneza mashua ni mamilioni ya shilingi, msumari mmoja wa jahazi ni shilingi 600/= hadi 1,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, samaki mtamu sahanini ila upatikanaji wake lazima uwe milionea au ukope mpaka utoe kope ndiyo uweze kumudu kutengeneza jahazi/boti ya mbao na kuvulia. Wavuvi wanaoweza kumiliki boti za kuvulia za kisasa na zenye vifaa vyote kamilifu ni wachache na wengi ni wageni waovuna na kusafirisha samaki nje ya nchi. Tunaolisha wananchi ni sisi wavuvi wazawa tunaovua katika mazingira duni yasiyo na motisha yoyote. Wizara sasa tunaiomba itusaidie ifuatavyo:-

(i) Kuondoa kodi kwenye mashine za boti *(board engine)*.

(ii) Kuondoa kodi kwenye nyavu za kuvulia na sio nyuzi tu za kushonea nyavu.

(iii) Vifaa mbalimbali vya kuvulia na vya kutengenezea nyavu ili ikamilike basi visitozwe kodi kwani trekta la mvuvi ni nyavu na *engine*.

(iv) Mafunzo kwa wavuvi wa Dar es Salaam yafikiriwe na kodi mbalimbali zipunguzwe.

(v) Mashine za *fish-finder* na *GPS* zisitozwe kodi.

(vi) Life jackets zipatikane kwa urahisi na *radio incase of emergency*, bei zake ziwe *regulated* kwani tunarushwa sana.

(vii) Wavuvi, wamiliki wa vyombo vya uvuvi tuwezeshwe ili tuweze kuvua bahari kuu.

(viii) Wananchi waelimishwe ufugaji wa samaki nchi nzima ili wananchi wapate *source* ya *protein* na *income*.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata majibu ya Serikali kuhusu ukatili unaofanywa na viongozi wa Serikali ikiwemo Wizara ya Maliasili katika Wilaya ya Kilombero na Mkoa wa Morogoro Wilaya zote kwa kunyang'anywa mifugo, kuchoma nyumba, vyakula, baiskeli na kutoza faini zisizo na risiti na wafugaji hao kuachwa na umaskini na ulemavu wa kudumu.

Je, Wizara ina mkakati gani wa kumaliza vitendo hivyo?
Je, mpo tayari kutembelea vijiji vya Wilaya ya Kilombero kujionea wenyewe na kuchukua hatua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata majibu ya Serikali kuhusu migogoro ya wafugaji na wakulima katika Wilaya za Mkoa wa Morogoro kwa wafugaji kulisha mifugo kwenye mashamba ya wakulima pia kuuawa.

Je, Serikali ipo tayari sasa kuunda *task force* kila Kanda ili kufuatilia masuala haya ya kuleta umaskini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvuvi katika hotuba ya Waziri imezungumzia kutoa ruzuku kwa wavuvi, cha kusikitisha pamoja na Wilaya ya Kilombero upo mto mkubwa unaoitwa Mto Kilombero, kwa miaka yote huvua na una samaki wengi na kuna watu (makabila) mengi yanayoishi huko hutumia uvuvi kama njia kuu ya kipato chao kwa biashara na chakula. Mto huo kuna miezi ya mavuno yaani kuanzia mwezi Mei hadi Julai hupatikana samaki aina ya njuju, ndipi (mlamu kaliandili), benasongo, kamba, na kadhalika, hao hupatikana kwa muda maalum, lakini hivi leo na miaka ya hivi karibuni Serikali inafungia wavuvi kuvua samaki, lakini hawapewi mbinu mbadala ya ufugaji samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo nataka majibu ya Serikali ni lini mtawapa wavuvi hawa ruzuku na mafunzo ili wafuge samaki?

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kukushukuru kwa kuendesha Bunge lako Tukufu kwa haki na uadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 83 wa hotuba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ya Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengenya Kamani (Mb) na rafiki yangu, imezungumzia udhibiti wa uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi haramu katika Wilaya ya Kilwa umekithiri hususani utumiaji wa baruti, kwa kweli Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani ni rafiki yangu leo katika majumuisho yake

kama hakunipa jibu linaloridhisha kuhusu kupatikana boti ya doria Kilwa nitatoa shilingi katika bajeti yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa huo 83 Wizara yako imeainisha vituo vya doria kwa kununua boti nne kwa ajili ya vituo vya doria ya Ikola, Kigoma, Mbambabay na Kasanga na pia katika programu ya maendeleo ya uwiano katika Bonde la Ziwa Tanganyika boti za doria nne zimenunuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika orodha hiyo boti zote nane za doria zimekabidhiwa katika Maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi Wilaya ya Kilwa ipewe boti ya doria kwa ajili ya Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baruti zinazopigwa Wilaya ya Kilwa zinahatarisha hata bomba la gesi litokalo Songosongo - Samanga Fungu na lipo mashakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kama sikupewa jibu muafaka la kupata boti ya doria Kilwa nitatoa shilingi katika bajeti yako.

MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mifugo ina umuhimu sana katika kuinua kipato cha mwananchi, pia uvuvi. Lakini Serikali imeshindwa kusimamia suala zima la kuinua ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukishuhudia mapigano na mauaji ya wafugaji wakinyanyaswa na kuuawa. Naiomba Serikali kuweka sheria mpya za kumlinda mfugaji na mifugo yake kwa kuwatengea maeneo wafugaji ili kuondoa mgongano kati ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufugaji wa kuku, mfugo wa kuku ni mfugo wenye faida kwa wananchi kujikwamua kama utasimamiwa ipasavyo, lakini mfugo wa kuku umekuwa ukiogopwa sasa kutokana na kusakamwa na magonjwa sana kuliko bata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mfugo huu ulete faida ya dhati kwa wafugaji, Serikali iwahimize Mabwana Mifugo wasikae ofisini jamani, bali watembee kwa wafugaji kutoa chanjo kwa mifugo hiyo na elimu kwa wafugaji ili wasikate tamaa kufuga kuku wanaoshambuliwa na ugonjwa wa mdondo, Serikali iangalie sana uzembe huo wa Mabwana Mifugo kutozungukia wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udhibiti wa mbung'o na nagana, udhibiti wa mbung'o na hasa katika Mkoa wa Katavi, niishukuru Serikali kupitia pragamu ya *Pan African Tsetse and Trypanosomiasis Eradication Campaign (PATTEC)* kuona itaendelea kudhibiti mbung'o kwani mpaka sasa mbug'o waliokuwa katika Hifadhi ya Katavi wamepungua sana tofauti na siku za nyuma walivyokuwa wakisumbua wasafiri barabara ya Mpanda - Sumbawanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, Naibu Waziri Mheshimiwa Saning'o Kaila Telele na Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara hii muhimu kwa maendeleo na ustawi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti iliyotengwa ya shilingi bilioni 66.1 kwa ajili ya kuendeleza sekta hizi mbili mifugo na uvuvi kwa hakika haitoshelezi. Mimi ninayo imani kubwa na Waziri na Naibu wake kwani wametokana na mifupa ya wafugaji na wavuvi. Naomba bajeti yote ifumuliwe, waongezewe ili wasimamie kwa karibu maendeleo ya mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Wizara lazima vilevile ifanyiwe *reallocation within* ili fedha zitumike kutatua kero ya wafugaji na wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri fedha nyingi zipelekwe kugharamia miundombinu ya mifugo na uvuvi. Mabwawa ya kutosha yachimbwe, majosho yajengwe, maeneo ya malisho yatengwe, dawa za mifugo na pembejeo nyinginezo muhimu waongezewe na weuziwe kwa bei nafuu. Aidha Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wavuvi wapewe taaluma sahihi na vitendea kazi ili tuwe na sekta ya uvuvi itakayochangia kukuza pato la wavuvi na hatimaye kukuza uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua Serikali kupitia Wizara hii, Wizara ya Ardhi na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika zina mpango gani juu kuwepo kwa mpango wa matumizi bora ya ardhi, maendeleo ya mifugo na uvuvi ili kuepusha migogoro ya mara kwa mara kati ya wafugaji na wakulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hizi mbili bado hazijaleta tija kwa wafugaji, wavuvi na Watanzania wote kwa ujumla. Naomba Serikali iifanye sekta ya mifugo na uvuvi zichangie ipasavyo uchumi wetu. Dira ya 2025, Mkukuta II, Malengo ya Milenia, Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa lazima vitafsiriwe kwa vitendo katika sekta hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali lazima itafute wawekezaji wa ndani na nje ili wawekeze katika sekta hizi. Ni kwa njia hii Serikali itaweza kujenga uchumi imara kupitia sekta hizi, uwepo wa makundi makubwa ya ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe, kuku na kadhalika pia maziwa, mito na bahari ni rasilimali muhimu kwa uchumi wetu. Serikali iache mtindo wa kufanyakazi kwa mazoea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kujua mwaka huu 2014/2015 mabwawa mangapi yatachimbwa hasa kwenye mikoa yenye ufugaji mkubwa Mwanza, Simiyu, Shinyanga, Dodoma, Rukwa, Katavi na kadhalika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naomba kuwasilisha.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kupongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kuteuliwa kwao kuiongoza Wizara hii, naomba sana wazidishe jitihada zao za kuinusuru Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya wakulima na wafugaji ni tishio kubwa sana, lisipodhibitiwa litaleta matatizo makubwa sana kwa jamii hizi mbili ambazo zinaweza kuleta vita vya wenyewe kwa wenyewe ndani ya nchi yetu. Naiomba Serikali ihakikishe inawatengea maeneo ya shughuli za wafugaji ili kuepusha matatizo ya wafugaji ya maisha ya kuhamahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la elimu, elimu ni muhimu sana kwa jamii ya wafugaji waweze kupatiwa elimu ya ufugaji wa kisasa. Pindi Wizara ikisaidia na sekta binafsi wanaweza wakabadili mfumo wa ufugaji. Niombe sana Wizara ijielekeze huko kwa ajili ya kutoa elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la viwanda, tukitaka kutatua tatizo la wafugaji ni vyema Serikali ikajielekeza kuwajengea mazingira ya kujenga viwanda vya kusindika nyama sambamba na viwanda vya kuchakata samaki katika maeneo yanayozalisha mazao ya mifugo na mazao ya kwenye maji ya chumvi na maji ya baridi na mito. Niiombe sana Serikali itafute fedha kwa ajili ya kujenga viwanda vitakavyowasaidia kuuza mazao yao na kuwapatia kipato kizuri na kutuingizia Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo ambalo Serikali kupitia Wizara hii haijaendelezwa kabisa uvuvi ukipewa fedha za kutosha ni eneo pekee ambalo litaleta fedha nyingi sana kwa Pato la Taifa na kuboresha maisha ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tuna Bahari ya Hindi na eneo kubwa sana ambalo tumevifanya shamba la bibi kwa sababu ya kukosa vitendea kazi kama meli ya kufanya doria na kudhibiti uvuvi haramu unaofanywa ndani ya bahari kuu na vyombo mbalimbali vya kutoka nje ya nchi kama vile hakuna mtu anayemiliki eneo hilo. Niombe sana Serikali inunue meli ya kudhibiti uvuvi haramu. Lakini eneo lingine Wizara ipewe fedha za kutosha kwa ajili ya kununua mafuta ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uvuvi haramu katika maziwa, kuna uvuvi haramu ndani ya maziwa ya Tanganyika, Victoria, Nyasa na kadhalika huku samaki na mazao mengine yataendelea kutoweka kwa sababu ya uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muwawezeshe kulinda rasilimali ya maziwa hayo, mfano Ziwa Tanganyika kuna nyavu za sumu ambazo zinatoka Burundi, naomba eneo hili mliangalie kudhibiti.

MHE. RAJABU MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi kuhusu Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikipokea ushauri wa mara kwa mara kuhusu namna ya kuboresha sekta ya uvuvi kwa ajili ya kuongeza mapato ya Serikali. Serikali haitumii vizuri uvuvi wa bahari kuu ambapo raia wa kigeni wanaovua samaki na kwenda kuuza nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa linapoteza fedha nyingi kwa mwaka kwa sababu tu ya kutotumia vizuri fursa za uvuvi tulizonazo nchini. Ninaitaka Wizara kuhakikisha kuwa inakuja na mpango mahususi kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu na namna ambavyo Serikali itanufaika na rasilimali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie sakata la migogoro isiyoisha kati ya wakulima na wafugaji. Karibu kila mwaka tumekuwa tukizungumzia na kuitaka Serikali kuhakikisha kuwa ardhi ya nchi yake inapimwa na maeneo mahususi kutengwa kwa ajili ya kubaini maeneo ya wafugaji na maeneo ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji inagharimu maisha kila wakati kati ya makundi haya mawili. Bado Serikali haionekani kutilia maanani kufanyia kazi mapendekezo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka wa bajeti Serikali inasema itachukua hatua juu ya migogoro kwa kutenga maeneo haya, lakini hakuna juhudi za wazi zinazoonekana. Kama Serikali itaendelea kutoa ardhi kubwa kwa wawekezaji bila kuwa na mpango wa kutenga

maeneo ya ardhi kwa wakulima na wafugaji, tatizo hili litazidi kuwa kubwa mwaka hadi mwaka na maafa yatakuwa jambo la kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la Serikali kubinafsisha kiwanda cha *Tanganyika Packers* - Kawe na mpaka sasa kiwanda hicho kimekufa jambo ambalo linafanya nyama isisindikwe na kuuzwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali haitakuwa na mpango mahususi wa kusindika nyama na kukidhi soko la ndani na Kimataifa basi tutegemee nchi jirani kama Kenya kuendelea kutumia fursa ya ng'ombe kutoka Tanzania kusindika nyama na kuuza nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na Serikali itilie maanani mapendekezo yangu.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Mifugo ya mwaka 2006 inatamka Serikali kuainisha, kupima na kumilikisha maeneo ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *speed ya* utekelezaji wa kuweka *land use plan* ni ndogo na wafugaji wamekuwa hawana maeneo yaliyoainishwa. Tumeshuhudia mauaji ya wakulima na wafugaji Mvomero, Kiteto, Chunya, Rufiji na Morogoro Vijjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngo'mbe wamesambaa nchi nzima, wanaharibu vyanzo vya maji, Hifadhi za Taifa, miundombinu na kadhalika, kwa nini Serikali haiweki *land use plan* ili kila kundi la wafugaji wagawiwe maeneo katika Mikoa yao badala ya kuruhusiwa kusambaa nchi nzima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya *PPP* ya mwaka 2010 inaruhusu Serikali kufanya biashara na sekta binafsi, kwa nini haioni umuhimu wa kutumia sheria hii wafugaji washirikiane na Serikali kuanzisha viwanda vya nyama na hivyo wa-*export* nyama, badala ya kuzunguka nchi nzima na mifugo isiyo na ubora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali haitoi elimu ya unenepeshaji wa mifugo kwa ajili ya nyama na hivyo kupata faida zaidi katika mauzo yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono hoja nikipata majibu ya maswali yangu.

MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja na kuipongeza Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuku nashauri Serikali kupitia Wizara hii iongeze mkazo na msisitizo juu ya miradi inayogusa wananchi moja kwa moja kwa mfumo wa *Research into Use (RIU)*. Mradi huu una manufaa makubwa na pia nampongeza mama Vera Mgitu kwa programu yake kwa vijiji vya Songea, Peramiho na vijiji vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ng'ombe nashauri Serikali kujifunza yenyewe kwa programu nzuri ya kijiji cha Lunyanyu Njombe kwani wataalam wa SUA walifanya mradi wa *Participatory Research* kwa ufugaji wa ng'ombe ambao umeleta matokeo makubwa kwa sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara isipuuze ushauri huu kwani utasaidia sana kupunguza umaskini.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Waziri wa Wizara hii pamoja na wasaidizi wake wote kwa juhudi zao za dhati za kuondoa kero za wananchi ambazo kwa miaka mingi zimelalamikiwa na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero yangu kubwa kwa Wizara hii ni kuhusu kutopata ufumbuzi wa kutosha juu ya kiwanda cha nyama cha Mbalizi Mbeya *(Tanganyika Packers)*. Je, ni lini kiwanda hicho kitaanza kufanya kazi? Waziri Mkuu aliagiza Wizara kwamba ihakikishe kwamba kiwanda hicho kinafanya kazi mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona wengi wakipita katika barabara zetu na hivyo kusababisha uharibifu mkubwa wa barabara. Je, Wizara ina mpango gani wa kulipatia ufumbuzi suala hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Mkoa wa Njombe utakuwa na mradi wa maji kupitia fedha za *DADPs* kwenye Jedwali Na. 6 Mkoa wa Njombe haupo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jedwali Na. 7(a) hali ya uvunaji wa samaki 2013/2014 mbona hakuna takwimu za Mto Ruaha na Mtera?

Nashauri kila Halmashauri itenge maeneo ya wakulima na wafugaji ili kupunguza migogoro ya wakulima na wafugaji. Maeneo ya wafugaji yapimwe na yajulikane.

MHE. NAMELOK E. M. SOKOINE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imebahatika kuwa na rasilimali kubwa ya mifugo na uvuvi, lakini Pato kwa Taifa ni dogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu za msingi za kutokomeza kuchangia katika Pato la Taifa kwanza ni kutokuwa na bajeti ya kutosha katika Wizara na hata hiyo ndogo fedha hazipatikani kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya mifugo, maji, malisho, majosho, pamoja na magonjwa kuendelea kuenea. Pia ukosefu wa wagani wa kutosha ambalo ndilo tatizo sugu la muda mrefu ni ugomvi wa mara kwa mara kati ya wakulima na wafugaji, ugomvi wa mara kwa mara kati ya wafugaji maeneo ya hifadhi nashauri ili sekta hii iweze kutoa mchango wake kikamilifu Serikali iwekeze vya kutosha ili wadau wa sekta na Taifa kwa ujumla waweze kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha Serikali ichukue hatua za makusudi kuhakikisha kwamba migogoro kati ya wakulima na wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi ipatiwe ufumbuzi wa kudumu kwa kupunguza matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya uvuvi Serikali itoe ruzuku kama wanavyofanya kwa dawa za mifugo au pembejeo za kilimo, hali kadhalika lifanyike kwenye uvuvi kuwaendeleza wavuvi wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inunue vifaa vya kisasa ili kudhibiti wavuvi katika bahari kuu, ili kuzuia uvuvi usio rasmi ambapo inakadiriwa zaidi ya meli 200 huvua katika bahari kuu bila vibali na hivyo kupoteza mapato mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo umuhimu wa kujenga bahari ya uvuvi ili meli zote ziwe zinakaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kupata nafasi ya kuongoza Wizara na naunga mkono hoja.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwapongeza Mawaziri na watendaji wote wa Wizara kwa kuleta bajeti yao Bungeni ili tuijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wale wote waliotoa masikitiko makubwa kwa ufinyu wa bajeti katika Wizara hii. Wizara hii imekuwa na changamoto nyingi sana zisizotatuliwa kutokana na hasa kuwa na bajeti ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ambayo ningependa kupatiwa ufafanuzi. Fedha za mradi za ujenzi wa machinjio Serikali imeweka utaratibu mzuri sana wa maendeleo wa ujenzi wa machinjio ya kisasa lakini hatujui utengaji wa fedha hizo huwa unaangalia vigezo gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Iringa katika Halmashauri ya Iringa kuwa mradi wa machinjio. Ngelewala mradi huu umeanza toka mwaka 2008, mradi huo ili ukamilike unahitaji shilingi bilioni 1.3 lakini pamoja na kuwa mradi unaendelea vizuri umeshapatiwa shilingi milioni 685 tu, mradi unasua sua sana na upo katika hatua za mwisho za kumalizia, yaani uwekaji wa vipoza nyama, umeme, uzio na kujenga mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali iangalie miradi ambayo ipo katika hatua ya mwisho ya kumalizia ndiyo itoe vipaumbele, tunaamini kuwa miradi hii ingesaidia kuleta ajira na kuongeza uchumi katika Halmashauri na Mkoa wetu kutokana na mazao yanayotokana na ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu basi atoe ufafanuzi wa mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wetu wengi wamekuwa wanafuga mifugo bila kuwa na utaalam wa kutosha kata nyingi sana na vijiji vimekuwa na uhaba mkubwa sawa na wataalam karibu nchi nzima ukiwepo Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda ni vizuri sasa Waziri angetuambia mkakati gani Serikali imejiwekea na kutoa na huu mradi wa BRN ili kuharakisha kuwa haya Matokeo Makubwa Sasa yanabadili hali ya ufugaji wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji uliopo Tanzania ni ufugaji wa kuharibu mazingira tu, hauna tija kwa Taifa. Hii yote imetokana na kutokuwa na mipango mizuri, mifugo ni mali ikisimamiwa vizuri kitaalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo yenye kuleta tija na siyo ufugaji wa kitumwa wa kutembea nchi nzima, kuharibu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya ufugaji yaainishwe vizuri kwa kupimwa, wataalam wa mifugo wapelekwe kwenye maeneo ya wafugaji, wawe na vyanzo vya kutosha ili wafanye kazi vizuri kama usafiri, dawa, majosho, malambo ya kunyweshea mifugo na chanjo za mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahusiano mabaya kati ya wafugaji na wakulima yanahitaji elimu ya kutosha na kuwawekea mipaka ya kueleweka ili wasigombane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii inapuuzwa sana na Serikali, kazi kubwa inayofanywa na Serikali kuchoma nyavu za wavuvi bila kutoa elimu kwa wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isimamie sekta hii kwa kutoa mikopo nafuu kwa wavuvi, zana za kisiasa kwa wavuvi, kutoa elimu ya uvuvi wa wavuvi na kuwa na maafisa uvuvi wa kutosha katika maeneo yote yanayohusiana na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho Serikali inyang'anye mashamba yote ya Ranchi yaliyotolewa kwa wawekezaji na hayajaendelezwa kulingana na mikataba. Serikali achane kulinda watu kwa kuwaonea aibu watu wachache wakati umma unaumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo na baada ya ufafanuzi mzuri nitaunga mkono hoja.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuwapa pole Waziri na Naibu Waziri kwa kuongoza Wizara hii, ni lazima mkaze buti ili kwenda sawia na uvuvi wa kisasa na wa tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuihoji Wizara na ninaomba majibu ya uhakika, ni kwa nini meli za kigeni zinavunja sheria kwa kutofunga gati zinapomaliza kuvua kabla ya kuondoka kwenda nje?

Je, kuna meli ngapi ambazo hazijarudi gatini na zimetozwa faini ya shilingi ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imekuwa kama shamba la bibi kwani kwa mwaka tunapoeza USD milioni 220 ambazo ni shilingi bilioni 352; kiasi hiki ndicho kinachokisiwa kwa mwaka mmoja, hivyo basi napenda kujua kuna nini nyuma ya pazia ambapo wageni hawa hawajawahi kulipa mrabaha? Pia kuna kigogo gani ambaye anafanya ufisadi huu wa kuchukua fedha hizi ambazo zingeisaidia nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jibu la kina wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijibiwe ni lini wavuvi watakuwa huru kama Watanzania ambao wenye magari ambapo hulipia malipo ya barabara mara moja, kwani wavuvi wananyanyasika sana kwa kulipa leseni mara tu anapotoka eneo moja na kwenda eneo lingine hata kama ni mkoa huo huo mfano, mvuvi amekata leseni Wilaya ya Ilemela lakini akigusa tu Wilaya jirani ya Nyamagana, Ukerewe, Sengerema anatakiwa alipe tena leseni zaidi ya shilingi 100,000/= naomba kujua hali hii itakoma lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kabisa kuwa Serikali haina nia thabiti ya kumuendeleza mvuvi, kwani katika ukurasa wa 36 wa hotuba yako ambapo wafugaji wa Ngorongoro na Longido kwa pamoja kuweza kuwanusuru wafugaji waliopoteza mifugo yao na kifuta machozi kuwa ni shilingi bilioni 7.4. hii ni nia njema sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi naomba muwaangalie wavuvi wadogo wadogo kuwasaidia zana za uvuvi zinazohitajika ili waachane na uvuvi haramu na waweze kupata tija ili kuwaokoa maskini hawa. Pia wapate wataalam wa ufugaji wa samaki ili kuendana na MKUKUTA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ilemela yenye kata tisa, kata sita zote zimeguswa na Ziwa Victoria, hivyo basi shughuli kuu kwa watu ndani ya Ziwa Victoria wanavua kwa shida sana kwani kuna maharamia ndani ya Ziwa ambao wanawapa shida wavuvi, hivyo ni muhimu kabisa tukaweza kuwapatia maafisa uvuvi na askari wa doria boti iendayo kasi kwa ajili ya ulinzi wa wavuvi, kwa ajili ya wageni wa uvuvi kuweza kukabiliana na uvuvi haramu. Hii itasaidia kukomesha maharamia na uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maafisa uvuvi katika Halmashauri hawapati fedha za kutosha katika kutekeleza kazi zao, hawana usafiri na hata fedha za kutekeleza kazi zao hivyo ni muhimu kabisa maafisa hao wapewe bajeti ya kutosha kwani hawa ndiyo walimu wa wavuvi. Pia pawe na fungu la kuviwezesha vikundi kwa kuwa kazi mojawapo ya wagani wa uvuvi ni pamoja na kutoa elimu kwa wafugaji samaki, waanikaji dagaa na wapiga reki pia.

Chanja nazo ni muhimu kwa kuanikia dagaa na samaki pia, hasa Kanda ya Ziwa na pia Mkoa wa Mwanza hasa Kanda ya Ziwa na pia Mkoa wa Mwanza hasa katika Wilaya ya Ilemela. Sababu kata nyingi za Wilaya hii ni wavuvi. Wavuvi wa Ramadi, Nyashimo na maeneo mengi, angalia sana Mheshimiwa Waziri hiki kisije kuwa kitanzi cha uchaguzi kwako. Ahsante.

MHE. ABDULSALAAM S. AMER: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja yote na napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kuteuliwa kushika nafasi hizi. Fursa hii waliyopewa ni nzito na yenye majukumu magumu. Wafugaji na wavuvi wana imani na mategemeo makubwa kwa Mawaziri hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli mbiu ya Watanzania kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa maendeleo ya nchi yetu, nami napenda kuwasisitiza viongozi wa Wizara angalau wafugaji na wavuvi tuwe na kauli mbiu yetu kuwa mifugo na uvuvi iwe uti wa mgongo kwa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi za watendaji wa Wizara hii, bado kuna upungufu mkubwa hasa katika kupata taarifa sahihi na takwimu zote. Nikiwa Mjumbe wa Kudumu wa Kamati ya Bunge kwa Wizara hii takwimu kwa kweli sio za uhakika, mara nyingi wanasema makadirio, hakuna mfugaji au mvuvi atakayetoa takwimu za kweli bila ya watendaji kuwafuata au kufanya kazi hiyo kila siku sio taarifa za kutosha kwa kata na vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na utendaji mzuri Wizara hii na mipango mizuri waliyokuwanayo kuhusu miradi ya malambo, fedha nyingi zinazotumiwa kwenye Halmashauri zetu hazielekezwi katika mradi hiyo. Mfano hai Wilaya yangu ya Kilosa mwaka 2011 Serikali ilitoa milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa lambo la wafugaji, mpaka leo fedha zimetumika kwa maharamia wengine, mpaka leo hakuna cha lambo wala chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliwaahidi wafugaji hao katika mikutano yangu na kwa kuwa nilikuwa na uhakika wa fedha hizo hatimaye fedha zimeyeyuka, naomba sana Waheshimiwa Mawaziri kwa kufuatilia jambo hili kwani litakuwa ni chanzo cha wafugaji hao kuhama hama. Narudia tena chonde chonde kwa wafugaji wangu wa Mfilisi, Mji Mdogo wa Mikumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na utendaji mzuri wa Mawaziri na timu zao, lakini hakutakuwa na ufanisi iwapo hawatapewa fedha zilizoombwa na kwa wakati, kwani

ucheleweshaji na kutopewa fedha ni sawa na kutwanga maji kwenye kinu. Naomba sana Serikali ilione hili kwa macho mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho narudia tena kuwapongeza Mawaziri kwani wao pia ni wafugaji, wanajua matatizo na mafanikio ya mifugo na uzoefu wa uvuvi.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na watendaji wote wa Wizara hii. Pamoja na pongezi napenda kuleta maoni yangu yafutayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ranchi ya Kitengule iligawanywa katika *blocks* za wafugaji wadogo wadogo. Zipo takribani *blocks* 13, wamepewa wazawa na wengine ni wageni. Pia wengine hawana ng'ombe bali wanatumia maeneo hayo kuwakodisha wageni toka nchi jirani. Wenye ng'ombe wengi wamenyimwa *blocks* na mimi nikiwa mmojawapo namiliki ng'ombe zaidi ya 1000 lakini sina eneo la kufugia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Kihanga ilipo Ranchi ya Kitengule ina vijiji sita na wafugaji wengi, lakini vijiji havikupewa eneo la malisho ya mifugo yao. Mwka juzi Serikali ilivipa vijiji hivi hekta 2000 tu na hizo hekta 2,000 bado hazijakabidhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni ya *Kagera Sugar* imepewa karibu nusu ya ranchi yote wakati hawavitumii, wanatumia eneo hilo kukodisha wafugaji kila ng'ombe analipiwa shilingi 50,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba eneo la *Kagera Sugar* walilopewa lipunguzwe wapewe wananchi wa vijiji vya Mushabaiguru, Katanda, Kibwera, Kihanga, Kishoju na Mulamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Waziri naomba ufike Kata ya Kihanga usikilize kero hii na kuitatua na iishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhamilishaji, *artificial insermination* bado haijafanikiwa kwa wafugaji wetu wa vijijini. Serikali isaidie kituo cha *NAIC, Usa River* kwani kituo hiki hakina mitambo mizuri ya kuzalisha mbegu bora. Pia Maafisa Mifugo wa Kata wapewe elimu/mafunzo kazini kuhusu uhamilishaji.

Kuhusu pori la akiba la Kimisi Wilayani Karagwe, pori hili linahifadhi majambazi tu na lina wanyama wachache sana. Tunaomba lirudishwe kwa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe ili wananchi wagawiwe, wafuge kisasa na kwa faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itafute wawekezaji wa uhakika katika viwanda vya nyama na maziwa katika Wilaya ya Karagwe.

MHE. MADGALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote kwa kuandaa hotuba na kuileta kwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya ardhi na mifugo imeeleza wazi kwamba Serikali itatenga maeneo ya malisho ya mifugo na kuyatangaza kwenye Gazeti la Serikali. Serikali ilieleze Bunge ni maeneo mangapi na wapi, kiasi gani yametengwa kwa ajili ya wafugaji hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tunashuhudia wakati wa mvua inanyesha nyasi ni nyingi sana kwa malisho ya mifugo. Hakuna juhudi zozote za kuwa na majani haya na kuyakausha/kutengeneza *hays* kwa ajili ya akiba ya chakula cha mifugo kwa kukosa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ukame mifugo mingi inakufa kwa kukosa chakula, Serikali ileleze Bunge kwa nini hakuna utaratibu wa kuwawezesha wananchi kielimu na ujuzi kutengeneza *hays* na *silage* kwa chakula cha akiba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu unaotumiwa na Wizara kutoa ruzuku ya dawa za mifugo hauwanufaishi kabisa wafugaji wanaotengwa. Kitendo cha kutumia *dealers*/wauzaji wa dawa za vyakula vya mifugo kuwapatia dawa kwa bei nafuu ili wao wawauzie wafugaji kwa bei ya ruzuku wakati hakuna ufuatiliaji wowote unaofanywa na Wizara kuona kama walengwa wananufaika ni makosa makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilieleze Bunge walipoamua kutumia utaratibu huu wafugaji walishirikishwa? Serikali ilieleze Bunge tangu mpango huu umeanza wamefanya tathimini na kuona wafugaji wamefaidikaje na mafanikio yakoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wafugaji wa Wilaya ya Kaliua, Mkoa wa Tabora katika Kata za Kangeme na Zagimlole mifugo yao ilipigwa mnada kinyume na taratibu za nchi, wafugaji wakafilisiwa na mpaka sasa wamebaki maskini. Matatizo yale yalifikishwa Serikalini/Wizarani na Serikali kuahidi kuchunguza masuala hayo na kuchukua hatua za kihistoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ni miaka miwili hakuna jibu lolote, wafugaji wale wanauliza vipi, Serikali imefikia wapi? Nini hatma yao na watoto wao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini ya wafugaji wote na hasa wa Mkoa wa Tabora na kwingineko ambako wameonekana kama wakimbizi ndani ya nchi yao na mifugo yao kuuawa kwa risasi na mapanga sasa watapumua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isitishe operesheni yoyote ya kwenda kuvamia wafugaji maeneo ya jirani na hifadhi kwa madai kwamba wamechungwa hifadhini wakati mipaka ya hifadhi hizo haijaainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tabia ya *game officers* kuvuna mamilioni kutoka kwa wafugaji wanafanya kama mtaji wao ikome kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia ya kuwainua wafugaji na wavuvi ni kuwapa mazingira mazuri ya kufugia na kutafuta masoko mazuri kwa mifugo yao na mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Mwneyekiti, viwanda vya maziwa vya Arusha vilinunuliwa na Wakenya kwa lengo la kusaidia kusindika maziwa, wanachofanya ni kutumia vile viwanda kama *collection point center* ya kukusanya maziwa na wanapeleka Kenya kwao, wanakwenda ku-*process* huko. Matokeo yake wao wana *export* mazao ya mifugo kwa kutoa maziwa kwetu na vijana wao wanapata ajira kwenye viwanda vyao wakati wa kwetu wanazurura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilieleze Bunge ni kwa nini imeruhusu viwanda *(processing plant)* kugeuzwa *collection point,* mkataba umevunjwa na Serikali imekaa kimya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kuelezwa nini hatma ya Chuo cha Iwari pale Mbegani *(FETA)* ambacho kinatoa elimu na mafunzo ya uvuvi na ni *center* ya kuzalisha vifaranga vya samaki kwa bei nafuu na yenye ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepanga kujenga bandari kubwa pale lakini haujasema chochote juu ya chuo hiki?

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kuiuliza Serikali kuhusu utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2013/2014. Kwa nini kati ya shilingi bilioni 23.488 tengeo la bajeti ya maendeleo (fedha za ndani) ni kiasi kidogo tu cha shilingi bilioni 2.229 ambayo ni 9.5% ambacho kilikuwa kimetolewa kufikia Aprili 2014 je, asilimia 90.5 iliyobaki itakuwa imetolewa kufikia mwishoni mwa Juni, 2014?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa najielekeza kwenye Wilaya ya Bukombe ambayo inao wafugaji wengi ambao wanakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Hawana elimu ya kunenepesha mifugo.
(ii) Hawana elimu ya ufugaji wa kisasa.
(iii) Maeneo ya malisho yaliyopo hayatoshelezi idadi ya mifugo iliyopo Bukombe.
(iv) Hawana soko bora la nje.
(v) Hakuna viwanda vidogo vya maziwa vya kutengeneza mazao ya maziwa kama siagi, jibini, yogati na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro isiyoisha baina ya wakulima na wafugaji kutokana na Serikali kutotenga maeneo ya kilimo na ufugaji ni migogoro isiyoisha na eneo la hifadhi ya Kigosi na ukosefu wa majosho, mabwawa na malambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro baina ya wafugaji na wakulima nakubaliana na penedekezo la Kamati ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kuitaka Serikali ipime maeneo ya kilimo na mifugo ili iondokane kabisa na migogoro baina ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miogoro baina ya wafugaji na hifadhi ya Kigosi. Mgogoro huu ni wa siku nyingi, wafugaji wengi wamepoteza ng'ombe wengi na wengi wamepoteza fedha nyingi zinazowanufaisha askari wa hifadhi hizo na Operesheni Tokomeza ya mwaka 2013 ilisababisha upotevu wa mifugo wengi sana na mateso mengi kwa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na pendekezo la Kamati inayopendekeza kuwa Serikali ifanye tathimini ya maeneo ambayo yamepoteza sifa ya kuwa hifadhi yapimwe upya na yatangazwe katika Gazeti la Serikali ili yatumike kwa ufugaji na kilimo (ukurasa 8).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi na mimi tumekuwa tukipendekeza jambo hili lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. Naomba Waziri atujibu, ni lini Serikali itashughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba (ukurasa 51-52) Mheshimiwa Waziri anaeleza juhudi za Serikali kuhamisha wananchi kuhusu ufugaji wa samaki. Kwa bahati mbaya kuhusu juhudi hizo za Serikali sisi Bukombe hatuzioni Bukombe hakuna juhudi zozote kama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka mwaka 2011 nimekuwa nikichangia kuhimiza Serikali iwe na mpango mkakati wa kukuza ufugaji wa samaki kwenye mabwawa vijijini. Vijijini ni mahali penye ardhi kubwa ya kutosha na kama ufugaji wa aina hii utakuzwa na kuendelezwa wananchi wengi watapata ajira, kipato na lishe ya uhakika pamoja na hali ya maisha kuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hatua ya kuanzia Wizara ingepeleka wataalam wa uchimbaji wa mabwawa ya kufugia samaki ili wawape elimu wananchi wenye nia ya kutaka kufuga samaki.

MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi yakinifu, usanifu na uchunguzi wa mazingira *(EIA)* umekamilika kwa jumla ya takribani miaka saba sasa bwawa hili ni kwa ajili ya kunyweshea mifugo, umwagiliaji mashamba, kilimo cha mahindi na mpunga maji yaliyochujwa na kudhibiti mafuriko na uvunwaji maji ili yakiwepo kwa aina mbalimbali, pia kukuza kipato cha wanagoweko na Jimbo zima la Igalula, bwawa hili lini linaanza kujengwa na kukamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji wa kisasa unapunguza idadi ya mifugo ili wawe wachache na walionenepa na hivyo kuongeza tija, ufanisi na faida kwa mifugo na mazao yake. *NAIC* ya Arusha ituletee elimu kwa idadi kubwa ya wafugaji jimboni Igalula tupunguze athari ya uharibifu wa mazingira na upotevu wa sehemu oevu, vyanzo vya maji na misitu muhimu kwa mvua kunyesha na nyasi kustawi kama malisho. Nini mpango wa Wizara kuwezesha hali hii tuwapite Botswana na Ethiopia kwa kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upandaji nyasi kwa mikoa yenye mifugo mwezi Oktoba, 2010 pale Ilolywansimba, Isikizwa, Uyui Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alieleza Wizara ya Mifugo na Uvuvi isimamie sera ya upandaji nyasi katika kila mkoa kwa ajili ya malisho ya mifugo kama shamba la nyasi Kongwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mabwawa, majosho malambo, minada, machinjio na usindikaji wa mazao ya mifugo na uvuvi vitasaidia pato la mfugaji na mvuvi wa matumizi bora ya ardhi na kuepuka migogoro baina ya wakulima na wafugaji wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. DKT. LUCY S. NKYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wao kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusisitiza kwamba sekta ya mifugo na uvuvi itakuwa na mchango mkubwa sana kwa uchumi wetu kama Wizara hii itapewa fedha za kutosha kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumkaribisha Mheshimiwa Waziri Jimboni kwangu hususani katika Tarafa ya Ngerengere ambako kuna mgogoro mkubwa sana dhidi ya wafugaji na wakulima. Mgogoro huu kiini chake ni ukosefu wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo. Naomba Wizara isaidie angalau malambo mawili katika vijiji vya Magera na Visaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malambo haya yatapunguza migogoro kwani ng'ombe hawatapita tena kwenye mashamba ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara isaidie yafuatayo ili kuboresha maisha ya wafugaji wa Tarafa ya Ngerengere, kwanza kuanzishwe mradi wa kunenepesha mifugo ili wafugaji wawekeze kupata tija zaidi kama huu mradi utaanza kwa kufanikiwa wafugaji watakuwa tayari kupunguza mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wasaidie kuanzisha mashamba ya malisho ya mifugo, Wizara iwasaidie vijana ambao wameanzisha usindikaji wa maziwa akiwemo Ndugu Lucas

Lemomo wa Kijiji cha Diguzi, Kata ya Matulo. Kiwanda hiki kinahamasiha kuweka mifugo ya kienyeji na kununua ngo'ombe wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ianze kambi za vijana kwa ajili ya kuwafunza ufugaji wa Kuku, sungura, mbwa na hata mabwawa ya samaki ili waweze kujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iangalie uwezekano wa kuanzisha ufugaji wa ngo'mbe wa maziwa katika Kata za Milimani kwani kuna majani mengi na maji ya kutosha kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo naunga mkono hoja asilimia mia moja. Nawatakia utekelezaji wenye mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usisahau kwamba nimeomba Waziri au Naibu waziri mfanye ziara katika Tarafa ya Ngerengere kuona hali halisi ya migogoro ya wakulima na wafugaji katika Wilaya ya Morogoro.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naona maswali yafuatayo ambayo ningependa kupata ufafanuzi kutoka kwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa tatu wa randama wameeleza majukumu ya Wizara ni kupanga na kusimamia matumizi ya ardhi kwa ajili ya mifugo. Je, sasa ni jukumu la nani kupanga na kusimamia matumizi ya ardhi kwa ajili ya uvuvi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wanafunzi wa Chuo cha Uvuvi Nyegezi – Mwanza kozi ya *Fisheries Management and Technology* mwaka wa tatu na kozi ya *Fisheries Science and Technology* mwaka wa pili wamenyimwa fedha za kwenda *field* tarehe 28/04/2014; fedha hii ya kujikimu imekuwa ikitolewa, kwa nini sasa mwaka huu haitolewi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua kwa nini uvuaji wa samaki wakubwa wamepungua katika bahari na maziwa na jambo hili linasababishwa na vifaa duni kwa mfano Ziwa Tanganyika ni Ziwa lenye kina kirefu kwa aina ya vyombo vinavyotumika. Ni dhahiri hawawezi kuvua samaki wakubwa, je, Wizara ina mkakati gani wa kuwapatia vyombo vya kisasa wavuvi hawa wenye zana duni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema kuangalia idadi ya vyombo vya uvuvi, aina za uvuvi na je, ni endelevu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusitoe leseni na vibali kwa nia ya kukusanya mapato ilihali tunawamaliza samaki sehemu husika. Ni vyema kufanya utafiti kujua chanzo, mazalia ya samaki na uwezo wa kuwavua kwa mwaka, vinginevyo tutamaliza samaki na Taifa kupata hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ni vipi Wizara yako imejipanga katika maziwa madogo madogo kuwe kuna utaratibu wa kufunga na kufungua maziwa kwa mujibu wa sheria ndogo za sehemu husika ili kuwanusuru samaki kuzaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia utunzaji wa mazingira kwa mfano, ulimaji kando kando ya Ziwa na ukuaji wa magugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua kuna mkakati gani wa kutoa elimu kwa wafanyabishara wa samaki wadogo wadogo na wakubwa kwamba ni aina na *size* gani ya

samaki wanapaswa kuuzwa/ili kuwe na *follow up* kwa wakiukaji na kuhamasiha *campaign* ya *undersized* wasinunuliwe pamoja na wale walioulilwa na sumu. Shukrani.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuchangia hotuba ya Wizara hii ambayo kimsingi ikisimamiwa vizuri inaweza kutoa mchango mkubwa katika maendelo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri mwenye dhamana kwa kiasi kikubwa imezungumzia mifugo na hasa ng'ombe. Jambo la kusikitisha ni kuwa hata hiyo sekta ndogo ya ng'ombe haionyeshwi ni kwa vipi itasaidiwa ili iweze kuchochea maendeleo ya wadau na uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuelekeza nguvu zake katika kubadili utamaduni wa kufuga ng'ombe kwa kiasi kikubwa sana kinachoendelea nchini ni uchungaji yaani kuhama toka sehemu moja kwenda nyingine wakitafuta malisho na maji. Maendeleo ya mifugo ni kulenga tija, yaani katika eneo dogo ng'ombe wanalishwa, kunenepa na kuweza kutoa mazao, hii iwe maziwa au nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo madai kuwa baadhi ya hifadhi za Serikali basi zitengwe kwa ajili ya ufugaji. Wazo hili ni zuri sana lakini utekelezaji wa uamuzi ni muhimu ufanyike kwa makini sana. Tuepuke kuendeleza ufugaji wa kuchunga, maeneo hayo mapya yalengwe kuwa mfano wa maendeleo yenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo hayo yaandaliwe kuwa na malisho na maji. Mashamba ya malisho ambapo nyasi zitavunwa na kuhifadhiwa kwa matumizi ya baadaye yaandaliwe. Wanufaika watakaopewa nashauri wapewe masharti ya kuwa na mifugo ile inayokuwa haraka na kunenepa sana kwa nyama au kutoa maziwa mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya sekta ya mifugo hasa ngo'mbe itakuwa ya tija na yenye utengamano katika jamii iwapo kwa nguvu kubwa tutaondokana na ufugaji wa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii haionyeshi hilo hivyo, nishawishike kusema kuwa maendeleo tunayotamani hayapatikani na uhasama kati ya wachungaji na wakulima utaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika lake la NARCO iliamua kugawa maeneo madogo *(sub-lease)* ili kutumia ranchi zake kikamilifu na kuwaendeleza wananchi. Nisikitike kueleza kuwa bajeti ya Wizara haitoi muongozo juu ya utatuzi wa migogoro inayoikabili vitalu hivi hasa mkoani Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na upungufu wa kiutendaji katika kugawa maaeneo hayo ipo hali ya kuhasimiana katika hali/azma ya kufikia malengo kwa wadau wote haitafikiwa. Lakini pia tofauti na hotuba ya Waziri kwenye ukurasa wa 27, NARCO haifanyi kazi yoyote ya usimamizi. Vitalu vingi Mkoani Kagera waliomilikishwa wanavitumia kwa kukodisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, NARCO haifanyi usimamizi na ushauri wowote kwa uendeshaji wa vitalu Mkoani Kagera. Vitalu hivi kwa kiasi kikubwa vinakodishwa kwa wachungaji toka nchi jirani. Laiti vitalu hivi vingesimamiwa kisasa hata hao wanaolalamika wasingekuwa na sababu ya kufanya hivyo, tujitahidi kukubali tatizo na kujenga ujasiri wa kutafuta majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri kwa kiasi kidogo sana hotuba ya Wizara imezungumzia sekta ya uvuvi na ufugaji wa viumbe maji. Bajeti hii inayo upungufu mkubwa wa kutokuelezea maendeleo ya uvuvi. Ipo haja kwa Serikali kupitia upya bajeti hii ili wananchi wanaotegemea sekta hii nao waweze kunufaika zaidi ya manufaa kwa wananchi, uwekezaji na usimamizi wa sekta ya uvuvi utasukuma kwa kasi maendeleo ya uchumi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi katika maji baridi na zaidi Maziwa ya Tanganyika na Victoria unachangaia kwa kiasi kikubwa pato litokanalo na uvuvi. Hata hivyo maeneo haya yanasumbuliwa na tishio la usalama kwani wavuvi wamekuwa wakivamiwa na kunyang'anywa zana za uvuvi chini ya mtutu wa silaha. Serikali iwasaidie wavuvi japo kwa kuhakikilisha kuwa maeneo yao ni salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo pia suala la kimkakati Kitaifa. Tanzania pamoja na kuwa na eneo kubwa la maji ya Ziwa Victoria, manufaa ya uvuvi yanafaidisha nchi za Kenya na Uganda. Hii ni kutokana na kutokuwa na vivutio kwa wenye viwanda ikiwemo kuvutia ndege za mizigo kutua Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nizingumzie ufugaji wa samaki. Hapa kuna tija kubwa sana hasa kwa kando ya ziwa. Moja tunawezesha wananchi walioondolewa katika shughuli na uvuvi wa kisasa waweze kufuga samaki, pili tunawezesha wananchi kupata kitoweo ambacho kutokana na mahitaji kuongezeka wananchi wa kawaida hawamudu.

Mheshimiw Mwenyekiti, suluhisho ni kuondoa kikwazo cha wananchi kufuga samaki. Kikwazo ni chakula na hapa tatizo ni hiyo sehemu ya mtambo iitwayo *palletazer,* narudia kuomba wananchi wawezeshwe.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta za mifugo na uvuvi zikipewa kipaumbele zinaweza kuwa na mchango mkubwa katika uchumi wa nchi na kuboresha maisha ya wananchi tofauti na ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo na uvuvi ni sekta zenye kuweza kulisha wananchi na kuongeza kipato kwa nchi. Mazao ya mifugo na uvuvi na bidhaa zake yana soko la moja kwa moja la Kitaifa na Kimataifa. Hivyo katika majumuisho ya mapitio ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 naomba Waziri atoe majibu kuhusu:-

Kwanza ni kuamini fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa mpaka Aprili 2014 ni shilingi bilioni 3.8 tu sawa na asilimia 13.4 tu? Na lini fedha zilizobaki zitatolewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kufuatia ongezeko la jumla la kiwango cha fedha kilichotengwa kwenye bajeti ya 2013/2014 kwa ajili ya utafiti ni kwa nini bado tafiti za utafiti wa mifugo Tanzania (TALIRI) na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) zimekuwa bado na utegemezi wa tafiti zinazofadhiliwa na wahisani ambazo ni kidogo ukilinganisha na mahitaji? Mchango wa Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) katika utafiti kwenye sekta za mifugo na uvuvi bado ni ndogo. Hali hiyo inapaswa kurekebishwa kwenye makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, pamoja na maelezo ya ujumbe katika hotuba ya Waziri kwamba Serikali ipo tayari kuchukua hatua juu ya viwanda kwenye sekta za mifugo na uvuvi vilivyokiuka masharti ya ubinafsishaji, ni muhimu Wizara ikataja orodha ya viwanda hivyo. Wizara irejee ripoti ya Shirika Hodhi la Mali za Umma (CHC) ya Januari, 2014 na kueleza hatua ilizochukua juu ya makampuni na mali zilizotajwa kwenye ripoti hiyo. Aidha, naomba maelezo ya Wizara ya nini kilitokea katika ubinafsishaji wa Kiwanda cha Ubungo *Diary* (Ubungo Maziwa)

na hatua gani zinakusudiwa kuchukuliwa juu ya udhaifu ulijitokeza katika ubinafsishaji wa kiwanda hicho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 3.3 cha hotuba ya Waziri juu ya ubunifu na utekelezaji wa sera na sheria za sekta, Waziri ametaja nyaraka mbalimbali zilizosambazwa. Naomba kupatiwa nakala za sera, sheria, mikakati na programu tajwa kwa ajili ya kazi za Kibunge za kuishauri na kusimamia Serikali. Aidha kwa miradi inayotekelezwa katika Manispaa ya Kinondoni na Jiji la Dar es Salaam kwa ujumla, Wizara kwa kushirikiana na Maafisa katika Halmashauri watuhusishe kwa karibu zaidi Wabunge tupate taarifa mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikana na Wizara nyingine zinazohusika pamoja na Ofisi ya Rais iharakishe uanzishaji upimaji, umilikishaji na uendelezaji wa maeneo ya ufugaji ili yawe endelevu. Hatua hii itachangia pia kupunguza migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Mkakati huu utekelezwe pia kama mbinu ya kudhibiti uharibifu wa mazingira, katika kipindi hiki ambacho wananchi wanaathirika pia na mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo mahsusi ya utekelezaji wa dhana, dhima na dira hiyo kwa upande wa Mkoa wa Pwani hususan katika maeneo ya Ruvu ambayo yanaathirika kwa wananchi wa Dar es Salaam katika sekta za mifugo na maji. Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) ielezwe ni kwa kiwango gani imetenga maeneo kwa wafugaji wadogo na wazalishaji wadogo wa nyama ili kupanua wigo wa ajira hasa kwa vijana wa kike na wa kiume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa machinjio ya Ruvu ni mradi muhimu ambao utaleta tija kwa soko la nyama la Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na maeneo mengine ya jirani. Hata hivyo kuna udhaifu katika utekelezaji wa mradi huu kwa kuzingatia ahadi za nyuma za Serikali na masuala ambayo Wabunge mbalimbali tulihoji mwaka 2011 na 2012. Hivyo, kazi hiyo inayofanywa na mshauri mwelekezi anayetamkwa ni muhimu ahusishe kwa karibu wadau ikiwemo Wabunge wa mikoa ya Pwani na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tasnia ya kuku, naomba kupewa ripoti ya mkutano ambao Wizara ilifanya na wadau kujadili hali ya tasnia juu ya namna ya kutumia fursa na nipewe pia mkakati ulioandaliwa. Aidha, naomba maelezo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015 inakusudia kutekeleza kazi gani kwa kushirikiana na Manispaa ya Kinondoni katika kuendeleza tasnia ya kuku katika maeneo ya pembezoni ya Kata mbalimbali za Jimbo la Ubungo ambayo kuna wafugaji wa kuku. Aidha, Wizara inaposhirikiana na Kampuni ya *Black Mark* kwenye maonyesho ya tasnia hii kama ilivyofanya katika ukumbi wa Mlimani City, Oktoba 2013. Katika kutekeleza mkakati wa kufufua na kuendeleza sekta ya viwanda vya ngozi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi iwe na mradi maalum kupitia mfuko wa maendeleo ya mifugo *(Livestock Development Fund)* kwenye Manispaa ya Kinondoni katika maeneo ya viwanda ya Ubungo kwa ajili ya wazalishaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uvuvi ina uwezo wa kuchangia kwa kiwango kikubwa kwenye uchumi wa nchi na kuboresha maisha ya wananchi. Kiwango cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya kusaidia wavuvi wadogo kupitia vikundi vyao ni kidogo. Wizara ya Mifugo na Uvuvi izingatie kuwa kuwawezesha wavuvi wadogo, ni vyezo muhimu ya kuboresha ajira zao na kulinda mazingira katika mito, maziwa na bahari na hivyo kuwezesha uvuvi na uvunaji endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha katika mabonde ya Jimbo la Ubungo na ya maeneo ya jirani ya Kibaha na Mkoa wa Pwani kwa ujumla ni muhimu kuweka mkazo kwenye ufugaji wa samaki katika mabwawa *(aqua agriculture)*. Mabonde hayo yanapoachwa bila kutumika mwisho wake hujazwa na wakazi holela na miundombinu mingine yenye kuweka mazingira ya mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uvuvi mkubwa katika kina kirefu *(deep sea fishing),* ahadi ya kujenga bahari ya uvuvi imekuwa ikitolewa mara kwa mara bila utekelezaji. Hivyo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ishauriwe na Ofisi ya Rais na Wizara nyingine zenye dhamana ili mikakati iliyosainiwa ya ujenzi wa bandari mpya ya Bagamoyo, iboreshwe bandari inayojengwa, itenge pia eneo maalum la bandari ya uvuvi ambayo itakuwa ni gati mojawapo kati ya magati yanayokusudiwa kujengwa. Hatua hii itachochea pia uwekezaji wa viwanda vya bidhaa zinazotokana na uvuvi katika maeneo maalum ya uwekezaji (EPZ na SEZ) ya Bagamoyo, Mkoani Pwani na ya Ubungo Jijini Dar es Salaam kuongeza ajira kwa wananchi na mapato kwa nchi.

Katika kuhakikisha kwamba ufumbuzi wa migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi unapatikana, naunga mkono maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba ripoti ya Kamati iliyoundwa na Mwenyekiti iwasilishwe Bungeni. Aidha, Serikali katika majumuisho itoe majibu ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge kupata ripoti ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira juu ya Operesheni Tokomeza yanayohusu wafugaji na sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Maziwa irejee majukumu yake na mamlaka iliyonayo kwa mujibu wa Sheria ya Maziwa sura 262 ishirikiane na Mbunge kutoa elimu kwa wadau kuhusu sheria hiyo na kuhamasisha pia wadau wengine kuunga mkono mpango wa unywaji maziwa mashuleni ulioanza kutekelezwa kwenye Manispaa ya Kinondoni.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inashughulikia mambo mawili uvuvi na mifugo, pia uvuvi una sehemu mbili, uvuvi maziwani na baharini, nini kinafanyika? Ni uvuvi wa maziwa tu na mifugo ndiyo kinachoshughulikiwa na uvuvi baharini hawa shughulikii!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kuna bahari kuu itokayo Msumbiji kupitia Lindi kwenda Dar es Salaam – Tanzania, kwenda Mombasa – Kenya, kwa nini kusiwe na kiwanda cha minofu Lindi? Tunaomba viwanda vya minofu ya samaki Lindi, siku hizi kuna umeme wa gesi. Kwa nini Serikali isishawishi wawekezaji kuleta viwanda hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya operesheni uvuvi haramu wa kutumia mabomu mwaka 1998 Lindi na Mtwara, wavuvi wale waliojisalimisha uvuvi haramu wa kutumia mabomu wavuvi wale wameachwa hivi hivi bila kupewa zana mbadala. Kwa hivyo wanaweza kurudia tena kutumia mabomu. Mabomu wanayotumia ni sumu kwa binadamu yanaweza kuleta madhara. Tunaomba Serikali iwasaidie mikoa ya Lindi na Mtwara kuwapa wavuvi hawa zana mbadala za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama wa maeneo ya bahari, ulinzi wa bahari, baada ya operesheni wa uvuvi haramu mwaka 1998 Lindi na Mtwara Serikali iliahidi kuleta boti kwa ajili ya ulinzi wa bahari kwa kudhibiti uvuvi haramu. Je, Serikali ni lini itatimiza ahadi yake ya kuleta boti katika Mkoa wa Lindi na Mtwara?

MHE. BERNADETA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri Katibu Mkuu na watendaji wote kwa hotuba nzuri. Nampongeza sana Waziri na Naibu Waziri, mmeanza vizuri na sisi Watanzania tuna imani kubwa na ninyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi leo kuna Halmashauri na vijiji vingi ambayo bado hawajaandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi ili kutenga maeneo ya wafugaji na wakulima. Kutokuwepo mipango hii au kushindwa kuhamasisha maeneo ya wafugaji wa wakulisha kumesababisha migogoro mikubwa na hata vifo. Je, Wizara ina mipango gani ya kupunguza migogoro kati ya wakulima na wafugaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, samaki wamepungua sana katika Ziwa Victoria sababu ya uvuvi haramu na wingi wa wavuvi. Ili kuongeza upatikanaji wa samaki na kuwawezesha kukua kwa nini Serikali isifikirie kutoa miezi sita ya kusimamisha shughuli zote za uvuvi kwenye Ziwa Victoria ili samaki waongezeke kukua. Nchi za nje mara nyingi hutumia utaratibu huu, je, ninyi mna mpango gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wananchi wengi mkoani Kagera walioitikia ufugaji wa samaki kwenye mabwawa. Tatizo kubwa wanalolipata ni upatikanaji wa chakula sahihi kwa samaki hawa. Waziri Mkuu akiwa ziarani Mkoa wa Kagera, aliahidi kuwaletea mashine ya kutengeneza chakula sahihi cha samaki *(pellets)*. Ni lini hii mashine italetwa Mkoa wa Kagera?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji kule Bubale, Misenyi, Serikali iliamua kurudisha baadhi ya *blocks* kwa wananchi, ni lini zoezi hili litakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja.

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja hii.

Pamoja na kuunga mkono hoja hii, Wizara bado ina changamoto nyingi ambazo inabidi zitatuliwe ili kurudisha imani ya wananchi kwa Serikali yao. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na:-

(i) Migogoro ya muda mrefu baina ya wakulima na wafugaji. Migogoro hii hasa katika Wilaya ya Rufiji Kata za Mtunda, Mbuchi na Maparoni hali ni tete sana. Eneo hili ni lile lililo kwenye enoe la mafuriko ya Mto Rufiji *(Rufiji flood plain)*. Wananchi wanaoishi katika eneo hili ni wakulima ambao hunufaika zaidi na rutuba iliyopo inayotokana na *silt* na *deposition* ya udongo unaotokana na mafuriko.

Aidha, eneo hili hata Halmashairi ya Wilaya imepiga marufuku kuweka mifugo, jambo la kushangaza ni kuwa eneo lote sasa limevamiwa na wafugaji wanaishi humo na mifugo yao na kusababisha migogoro ya mara kwa mara.

Naiomba Serikali Kuu ikishirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji iingilie kati suala hili na kuwahamisha wafugaji katika eneo hili na kuwapeleka katika maeneo mengine yaliyotengwa katika Wilaya hii.

(ii) Kwa upande wa uvuvi, Jimbo la Kibiti ambalo ndilo linalomiliki eneo la Delta ya Mto Rufiji na maarufu sana kwa uvuvi wa samaki aina zote na hasa Kamba *(prawns)*, naishukuru sana Serikali kwa kujenga mwalo pale Nyamisati ili wavuvi wakileta samaki wahifadhiwe katika majokofu yaliyokuwa kwenye mwalo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni jema na hasa ukizingatia kuwa si muda mrefu kijiji hiki kitapata umeme. Naiomba Serikali ihakikishe kuwa wanakamilisha mwalo huo kwa kuweka vifaa vyote vinavyohitajika vya kuhifadhia. Aidha, katika mwaka huu tuna matarajio makubwa

sana ya kuvua samaki wengi katika eneo hili na hasa kamba *(prawns)* kutokana na mafuriko makubwa yaliyotokea.

Naiomba Serikali kwa mwaka huu wa fedha wasiishie kujenga mwalo tu bali waende Nyamisati na maeneo mengine ya delta kutoa elimu kwa wavuvi ili kuhakikisha kuwa wavuvi hawa wanatumia njia bora na endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha naiomba Serikali iendelee kuangalia eneo hili la delta ambalo wananchi wake wengi ni maskini, kuwapatia *grants* wavuvi hao ili waweze kununua zana bora na za kisasa ili kuinua uchumi wa maeneo na wananchi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro kati ya ardhi za vijiji na mipaka ya mapori ya hifadhi, Serikali inabidi ichukue na ifanye utafiti wa kina kuhusiana na namna ya kuja na mipango madhubuti ya njia za kutatua matatizo, migogoro ya ardhi na migongano kati ya wakulima na wafugaji ili tuwe na jamii inayoishi katika usalama na ulinzi juu ya mali zao na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inajitahidi kutoa elimu ya kutosha kupitia Halmashauri zake kuwaelimisha wafugaji juu ya ufugaji bora kwa mazao bora na mengi zaidi ili kuondoa migogoro ambayo imekuwa ikijitokeza mara kwa mara katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya uvuvi, umefika wakati sasa Serikali iangalie upya mipango yake ya namna ya kuboresha sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika baadhi ya maziwa kama Ziwa Rukwa, Tanganyika samaki wamekuwa wakipungua kila wakati na vina vyake vya maji kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iangalie namna ya kuendeleza uvuvi na ufugaji wa samaki katika maziwa haya hasa Ziwa Rukwa kwa uanzisha ufugaji wa samaki ili wananchi wa eneo hilo waweze pia kujiongezea vipato na kujiletea maendeleo kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili hebu tujifunze kutoka katika nchi kama Namibia na Sychelles wanaofanya vizuri katika shughuli za uvuvi hasa shughuli za ufugaji wa samaki, lakini pia tujifunze pia kutoka katika nchi za Botswana na Ethiopia ambao wamekuwa juu ya Afrika katika sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nchi hizi zimeweza ni kwa nini sisi kama Tanzania tunashindwa? Je, wenzetu hawa ni tofauti sana na Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefika wakati sasa ni lazima tuwajibike katika kuwaletea maendeleo wananchi kwa kutumia rasilimali tulizonazo ili kauli mbiu ya Ilani ya CCM ya Maisha Bora kwa kila Mtanzania iweze kutekelezeka na kuwaletea wananchi matumaini ya maisha na maendeleo kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. KULTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010 Serikali ilileta Miswada miwili ya sheria ili kuondoa migogoro baina ya wakulima na wafugaji. Sheria hizi ni Sheria Na. 12/2010 inayoitwa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo ya mwaka 2010 *(The Livestock Identification Registration and Traceability Act 2010)* na Sheria Na. 13/2010 inayoitwa Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo 2010 *(The Grazing Land and Annual Feed Resources act 2010)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilisema uwepo wa sheria hizi utasaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa ama kupunguza uwepo wa migogoro baina ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni miaka minne tangu sheria hizi ziletwe Bungeni na migogoro ya wakulima na wafugaji inaongezeka kwa kasi na wananchi wengi wanauawa. Je, Serikali inatamka nini juu ya utekelezaui wa sheria hii na je, kanuni za sheria hizi zimeshatungwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uvuvi, Serikali inaonesha wazi kuwa haina nia ya dhati ya kuendeleza sekta hii ambayo ingeweza kutupatia mapato makubwa kwenye uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zinaonesha kuwa nchi yetu inapoteza wastani wa USD milioni 220 kwa mwaka kutokana na Serikali kutokusanya fedha za meli kubwa za kigeni zinazovua katika bahari kuu, maziwa na mito yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaeleza katika taarifa zake kuwa sekta ya uvuvi inachangia asilimia 1.4 katika Pato la Taifa, je, Serikali haioni aibu kutoa taarifa hii wakati ina uwezo wa kukusanya zaidi ya bilioni 352 katika sekta hii kila mwaka?

Mwisho kwa msisitizo tunaitaka Serikali itoe maelezo yenye uhakika, je, Serikali ina mikakati gani ya makusudi ya kuhakikisha migogoro ya wakulima na wafungaji inamalizika Tanzania nzima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri kwanza kwa kuteuliwa kwake, pia nimpongeze kwa hotuba nzuri. Nimpongeze Naibu Waziri, pia Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa utekelezaji mzuri na majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni Wizara muhimu sana katika maeneo ya kiuchumi kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa. Nasema hivyo kutokana na sababu kuwa zaidi ya asilimia 50 ya pato la wananchi katika Kanda ya Ziwa linategemea sana shughuli za uvuvi na shughuli za mifugo.

Pamoja na umuhimu huu mkubwa Serikali bado haijaonyesha mpango kamili wa kuwasaidia wananchi wafugaji na wavuvi kuweza kuongeza kipato chao. Wafugaji wengi wanakabiliwa na changamoto kubwa sana ya kunyanyaswa kwa kutozwa fedha nyingi ili wapate kulisha mifugo yao katika hifadhi mbalimbali zilizopo hapa nchini. Kwa mchango huu ningependa kujua mkakati wa dhati wa Wizara wa kuimarisha sekta hii ya mifugo. Zaidi nashauri wafugaji watengewe maeneo maalum ya malisho ili kuweza kuimarisha sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali wa kuimarisha viwanda vya nyama katika Kanda ya Ziwa itakuwa mkombozi kwa wafugaji kuuza mifugo yao kwa faida. Hivyo napenda kusisitiza Serikali iweke uzito sana katika suala la viwanda vya nyama katika Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvuvi katika ukanda wa Ziwa Victoria ni ukweli usiopingika kwamba sekta ya uvuvi imeachwa sana kiasi kwamba sekta inashindwa kuchangia inavyopaswa katika uchumi wa Taifa. Changamoto hizi ni pamoja na ukosefu wa fedha za kuwezesha vikundi vya uvuvi, vilevile hakuna vitendea kazi kwa wataalam hivyo wanashindwa kutoa huduma ya ugani katika maeneo ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoa mfano katika mikoa ya Geita, Mwanza, Mara na Kagera, changamoto hii ni kubwa sana. Hata Jimboni kwangu Busanda katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita katika maeneo ya Bukondo, Kasanghwa na Kageye wavuvi hawapati huduma za ugani. Hivyo Serikali iongeze ajira za Maafisa Ugani katika sekta za migufo na uvuvi ili wananchi wapate ushauri wa kitaalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo haya machache ninaamini Serikali itafanyia kazi changamoto hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja ya Waziri.

Pili, napenda kumpongeza Waziri kwa kuanza kazi vizuri na kuiwekea mikakati mizuri ili kuiboresha sekta yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kumaliza kabisa migogoro katika sekta ya ufugaji kati ya wakulima na wafugaji, ni lazima maeneo yote yenye mchanganyiko ya wakulima na wafugaji yapimwe na kutenga maeneo kila moja na eneo lake. Nimewahi kutembelea nchi ya Namibia nimeona jinsi wafugaji wanavyotengewa maeneo yao mbali kabisa na wakulima. Wana mashamba ya majani, wana mabwawa, wana huduma zote za majosho na dawa za mifugo. Hakuna migogoro yoyote inayotokea na mifugo inastawi vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uvuvi, wavuvi wadogo wadogo hapa nchini hawajapata msaada wa Serikali kwa kiwango cha kutosha, umaskini unaendelea kuwaandama. Sababu kubwa ni wavuvi kutokuwa na nyezo za kisasa za uvuvi, wala utaalamu wa uvuvi wa kisasa. Mfano ni wavuvi waishio kandokando ya Ziwa Nyasa hasa Kata za Tarafa za Mwambao Wilaya ya Ludewa, Tarafa za Unyakyusa, Wilaya ya Kyela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka 50 sasa ya uhuru wavuvi wale hawajabadilika, wanaishi katika makambi ya wavuvi, hawana uwezeshwaji, wanaambukizana UKIMWI bila elimu yoyote ya kinga. Je, Waziri yupo tayari kuyatembelea maeneo hayo na kujionea adha kubwa wanayopata wavuvi wa mwambao wa Ziwa Nyasa?

Nitaomba Waziri atueleze yupo tayari kufanya ziara hiyo? Hii itamsaidia Waziri kupanga programu za kuwawezesha wavuvi wa Ziwa Nyasa kama wavuvi wa Maziwa ya Victoria, Tanganyika na Bahari wanavyosaidiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba Waziri atakapotoa majumuisho, awaeleze wavuvi wa Ziwa Nyasa atakavyowasaidia. Ikumbukwe kuwa uboreshaji wa wavuvi katika Ziwa Nyasa ni kuwasaidia pia wanawake ambao nao wanapata ajira katika hatua ya ukaushaji wa samaki. Mipango kwa wavuvi wa Ziwa Nyasa itajwe ili nao wafarijike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mafupi ninazidi kumuomba Waziri ajibu hoja zangu wakati atakapojibu hoja za Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuunga mkono hoja hii, mwisho naomba Waziri alieleze Bunge lako Tukufu, ni nini hatua ya Kiwanda cha Nyama cha Mbeya - Mbalizi kilichokamilika na kukaa bila kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 20 sasa. Je, ni lini Serikali itamtafuta mwekezaji katika kiwanda hiki? Katika eneo hili vijana wanaendelea kutangatanga hawana ajira ambapo kiwanda hiki kingeweza kuwaajiri vijana wengi. Naomba Waziri atupe maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo machache, naunga mkono hoja hii. Namtakia Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara utekelezaji mzuri wa bajeti yao ya Wizara.

MHE. GREGORY G. TEU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, wataalamu na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri mnayofanya kwa kutimiza majukumu yenu ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inalo jukumu la kupanga na kusimamia matumizi ya ardhi kwa ajili ya mifugo. Hivi sasa upo mgogoro wa ardhi kati ya *Tanzania Livestock Research Institute (TALIRI)* kilichopo katika Jimbo la Mpwapwa. Mgogoro huu ni baina ya eneo la kijiji cha Kibodyani na chuo unahusu mipaka ya kijiji na chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwepo na amani pamoja na utulivu kati ya chuo na wananchi hao, mgogoro huu uamuzi wake mmefikia wapi? Wizara mama imechukua hatua gani ya kuleta usuluhisho wa kudumu hivi sasa? Kauli ya Wizara mama kuhusu suala hili naamini italeta amani na utulivu chuoni na kijijini kwa kuzingatia yale yaliyokwishatokea nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imebainika kwamba kuna kitengo cha utafiti wa mifugo chini ya TALIRI kilichokuwepo Jimboni Mpwapwa, kitengo hiki kinajihusisha zaidi na uboreshaji wa mifugo kwa maana ya kuku, hususani kuzalisha vifaranga vya kuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitengo hiki kilihamishwa kinyemela bila ya taarifa hata ya uongozi wa Wilaya ya Mpwapwa. Kitengo hiki kimehamishwa na kupelekwa Mkoani Dodoma. Je, Wizara husika inasema nini kuhusu ofisi hii kuhamishwa kinyemela?

Mheshimiwa Mwenyekiti, makao makuu ya Kitengo cha Uhamishaji wa Mifugo *(Artficial insemination)* yalikuwa yahamishiwe TALIRI – Mpwapwa, mpaka sasa uamuzi huu haujatekelezwa kama ilivyokusudiwa hapo awali, je, Kitengo hiki muhimu kitahamishwa lini katika Wilaya ya Mpwapwa?

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara hii kwa ufuatiliaji wa masula ya mifugo hasa ya wanyama wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umefika ni lazima wafugaji waelimishwe ufugaji bora ambao utatoa tija. Hali ilivyo sasa wafugaji bado wanarundika mifugo isiyo na tija na kuzurura nayo nchi nzima ikiwa na ng'ombe wengi waliokonda ambao kila mmoja hafiki hata kilo mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sasa wafugaji hao hawapati mapato mazuri ya ng'ombe wao wanabidi waweke wengi sana, Wizara ina mkakati gani wa kuwasaidia wafuge kisasa kwa tija na wapunguze idadi ya mifugo na pia kulinda mazingira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imegawanyika kwenye wananchi wenye kazi za asili kazi hizo ni wakulima, wafugaji, wavuvi na wanaochanganya wakulima na wafugaji. Ni kwa nini

maeneo ya Watanzania ambao kwa asili ni wakulima wazuri hawafugi wanyama kama ng'ombe? Mikoa hiyo ni mikoa ya Tanga, eneo kubwa la Pwani, Lindi, Mtwara na Dar es salaam ambao hawa ni wavuvi, badala ya wananchi hawa kuambiwa/kushauriwa wafuge samaki kwenye mabwawa badala ya kulazimishwa watenge maeneo kwa ajili ya utunzaji wa ng'ombe ambao ukweli ni kwamba wengi tayari wameharibu mazingira kwa sababu ya kufuga ng'ombe kupita kiasi na ardhi yao sasa haitoi majani na hivyo kutangatanga nchi nzima kutafuta malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wamekuwa wakiwaonea maeneo ambayo yamehifadhi ardhi yao kuwa na uoto mzuri unaowatoa roho wafugaji, ni kwa nini Serikali isiwalazimishe watu ambao wao wenyewe sio wafugaji kutenga maeneo yao yenye rutuba kwa ajili ya mifugo iliyoletwa kwa lazima na Serikali. Kwa sababu hiyo Serikali kwa sehemu nyingine kubwa imekuwa ndiyo chanzo cha ugomvi kati ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe sasa tamko ili kukomesha ugomvi wa ardhi kwa kutolazimisha sehemu yoyote ya nchi kutolewa kwa matumizi ambayo wananchi katika sehemu hiyo hawahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijawasaidia wavuvi, vijana wengi katika maeneo ya ufugaji ikiwa wanaoishi sehemu kubwa ya pwani, maziwa na mito wangeweza kuendelezwa na vijana kuwapatiwa ajira kwa kuanza ufugaji wa samaki. Hata pale ambapo vijana wenyewe wameanza ufugaji, wamelalamika hawapati msaada wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeomba kujua ni kwa nini Wizara haina mpango mkakati wa kuwasaidia vijana hao wasiweze kufuga samaki hao kisasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakinamama wengi sana wanajishughulisha na ufugaji wa kuku wa kienyeji na kisasa kwa ajili ya nyama na mayai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya chakula cha kuku na dawa ni ghali sana kiasi wakinamama hao hawapati faida kabisa, je, ni kwa nini Serikali isiingilie kati ili chakula cha kuku kiwe na tija? Kama wakulima wanapata ruzuku ya mbolea na mbegu, ni kwa nini wafugaji wa kuku nao wasipate ruzuku ya chanjo na dawa ya kuku pamoja na chakula?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la uvuvi haramu limekuwa sugu. Kwa muda mrefu sana Wabunge na wanaharakati wamepiga kelele katika kupambana na tatizo hili la uvuvi haramu lakini hakuna matokeo yanayoridhisha na hata hivyo hakuna bajeti ya kutosha iliyotengwa kwa shughuli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iongeze fedha katika eneo hili ili uvuvi haramu uweze kutokomezwa kwani ni suala linalohusu afya za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha ingawa nchi yetu imepakana na bahari, maziwa makubwa na pia ingawa ina mito mikubwa, lakini bado suala la uvuvi kuendelezwa halijapewa kipaumbele. Hata katika maeneo yenye samaki wengi, bado hawapatikani kwa urahisi kutokana na urasimu wa wafanyabiashara ambao huwauza kwa bei isiyo nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaweza kusimamia vizuri sekta ya uvuvi kwa madhumuni ya kuiendeleza na kuhakikisha kwamba wananchi wanafaidika kwa kupata mlo wa samaki ambao ni wa muhimu sana katika kutunza afya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro ulioendelea kwa muda mrefu kati ya wafugaji na wakulima hauleti picha nzuri katika nchi yetu. Kwa kuwa ni mujibu wa Wizara hii kupanga na kusimamia matumizi ya ardhi kwa ajili ya mifugo, Wizara iingilie kati migogoro hiyo kwa kutenga maeneo kwa ajili ya matumizi ya ufugaji ili kuondoa migogoro hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo wafugaji wa Tanzania wanauza mifugo yao kwa hasara sana. Utaratibu uliopo ni ule wa kununua ng'ombe mnadani kwa kumtazama tu. Wafugaji wetu wangependa sana kuboreshwa hali hiyo ya kupima mifugo yao pale wanapoiuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bwana mifugo wamepungua sana hapa nchini. Wizara iajiri bwana mifugo wa kutosha ili kutoa ushauri kwa wafugaji ambao wanafuga mifugo mingi sana huku wakiishi katika hali ya umaskini uliokithiri. Elimu itatolewa ya kutosha ili wafugaji waendeshe ufugaji wa kibiashara badala ya hivi sasa ambapo wafugaji wanakuwa na mifugo mingi sana kwa ajili ya sifa tu au kujiridhisha. Elimu ikitolewa kwa wakati, wafugaji wengi watafaidika na hivyo kufuga kibiashara na kujikomboa kutokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache naomba kuwasilisha.

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuiomba Wizara kupiga marufuku utozaji wa leseni za uvuvi kwa dola za kimarekani, hadi leo wavuvi bado wanatozwa kwa fedha za dola za kimarekani. Naomba kauli ya Serikali kwa nini imekuwa na kigugumizi ilihali wavuvi wanaendelea kuwa maskini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapata miaka mitatu Wabunge wenye maeneo ya wavuvi tumelalamikia utaratibu wa kinyonyaji na uonevu wa kuwatoza leseni za uvuvi kila Wilaya wanakoenda ndani ya mwaka mmoja wa leseni, nini kauli ya Serikali juu ya kero hii wa wavuvi? Aidha, Wabunge tumelalamika kwa muda mrefu utaratibu usiofaa wa kuwatoza leseni wavuvi wanne kila mmoja walio katika chombo cha uvuvi wakati tayari mwenye chombo (mtumbwi) amekwishalipia leseni ya uvuvi kwa chombo chake na uvuvi kwa dola kumi za kimarekani kila leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri amesema kuna mpango wa kutoa ruzuku kwa wavuvi wadogo kwa ajili ya ununuzi wa zana za uvuvi na pembejeo zingine zikiwemo boti, injini, nyavu na mishipi. Nimesoma vitabu vyote vya bajeti hakuna mahali palipotengwa fedha za ruzuku kwa wavuvi wadogo. Katika majumuisho naomba nielezwe mahali ilipo ruzuku hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa kujitahidi kufanya kazi kwa bidii licha ya kutopata fedha za utendaji na maendeleo kama zinavyopangwa katika bajeti za kila mwaka chini ya asilimia 13.4 kwa fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ushauri na mapendekezo katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uboreshaji wa taasisi ndani ya Wizara (MPRU) kazi kubwa katika sekta ya uvuvi inasimamiwa na Taasisi kuu ya MPRU ikiwa ni usimamizi wa maeneo ya hifadhi za bahari na maeneo tengefu ya Mafia, Mnazibay na Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi thabiti utawezesha kukuza uwezo wa upatikanaji wa samaki kwa kuzuia uvuvi haramu na kukuza hifadhi za uzalishaji wa samaki. Pia itawezesha kuanzisha kukarabati na kukuza maeneo ya mvuto wa utalii na kuingizia Taifa fedha za kigeni. Kwa msingi huu taasisi inahitaji fedha za kutosha kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kupatiwa boti za kisasa na mafuta ya kutosha ili kuwezesha kufanya doria kwa muda mrefu na kwa maeneo makubwa.

(b) Kupatiwa fedha ili kujenga maeneo mapya na kuboresha maeneo yaliyopo ya hifadhi za bahari.

(c) Kupewa kibali cha ajira ya watumishi ili kuwezesha uwezo endelevu baada ya kustaafu kwa viongozi wakuu katika sekta zote.

(d) Kuboresha uwezo wa usafiri kati ya visiwa vya Mafia na maeneo ya nchi kavu kisiwani na nje ya eneo la kisiwa cha Mafia, Kilwa, Bagamoyo, Tanga na Mnazibay.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya ufugaji samaki maeneo ya bahari na mabwawa. Wizara kupitia taasisi zake na vyombo vya elimu visaidie katika uundaji wa vyama vya wavuvi na katika upandikizaji wa samaki katika mabwawa. Hapa naomba tuende katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ambapo imejenga Bwawa kubwa la umwagiliaji la Misozwe. Pamoja na maji ya umwagiliaji bwawa hili ni kubwa sana na linahitaji kuwezeshwa kwa ufugaji wa samaki. Kipo chama cha umwagiliaji hapo Misozwe chombo ambacho kikipata elimu kitaweza kusimamia ufugaji wa samaki na kilimo cha mpunga, nyanya na maharage na mboga mboga katika eneo la zaidi ya ekari 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujenga sera na mpango wa kutenga maeneo ya wafugaji ili kupunguza migogoro kati ya wakulima na wafugaji Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi iandae sera na mpango wa kutenga maeneo ya ardhi kwa wafugaji. Mfano eneo la kutoka Ruvu hadi Chalinze wapo wafugaji wengi, utaratibu mzuri ukipangwa eneo maalum litengwe katika sehemu hiyo kwa pande zote Kaskazini, Mashariki, Kusini na Magharibi ya miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miji hiyo ya Ruvu na Chalinze yenye umbali wa wastani wa kilomita 20 itengwe na kuwekewa mipaka na kutambuliwa rasmi kwa mipaka halisi kuwa eneo la wafugaji. Yapo maeneo mengi ya ardhi ya Tanzania ambayo bado ipo wazi basi yaanzishwe kupimwa na kutengwa kwa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na kutenga viwango vya fedha za bajeti hii ya mwaka 2014/2015 itolewe kwa asilimia kubwa hadi mia moja.

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kupata fursa hii na mimi nichangie hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ya mwaka wa fedha 2014/2015.

Vilevile nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na wataalamu wake kwa kuwezesha kuandaa bajeti nzuri kwa maendeleo ya sekta nzima ya mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi hafifu umechangia katika uharibifu wa rasilimali, kukuza umaskini na ukosefu wa uhakika wa chakula duniani kote ili kudhibiti hali hii, mfumo wa ikolojia, unaotoa kipaumbele kwenye uendelevu na usawa katika usimamizi wa uvuvi umebuniwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu unaoendeleza mfumo wa ikolojia katika mdogo mdogo wa bahari kwenye maeneo ya tropiki utasaidia sana kuendeleza sekta hii ya uvuvi hivyo kuleta tija. Mpango huu unatekelezwa kwa ushirikiano na nchi za Indonesia, Philippines, Visiwa vya Solomon na Tanzania. Lengo la mpango huu ni kutumia mfumo wa ikolojia katika usimamizi wa uvuvi ili kuboresha uendeshaji na utawala wa uvuvi mdogo mdogo na kuinua uwezo wake katika kuchangia kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa ikolojia unalenga kusimamia uvuvi katika ujumla wake. Ulipobuniwa awali mfumo huu wa ikolojia ulilenga kuboresha usimamizi wa aina moja ya samaki mfano, jodari pekee kwa kuzingatia masuala mengine yanayohusiana na uvuvi wake, kwa mfano viumbe wanaovuliwa lakini si walengwa katika uvuvi huu, makazi ya jodari na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa, mfumo wa ikolojia hauangalii tu usimamizi wa aina moja tu ya samaki, bali mfumo huu unaangalia masuala yanahusiana na uvuvi kwa ujumla wake, ikiwa ni pamoja na kuinua juhudi zilizopo katika mifumo ya kijamii kama usimamizi wa uwiano wa maeneo ya Pwani *(Integrated Coastal Management – ICM)* mfumo wa ikolojia katika uvuvi unanuia kuweka uwiano katika malengo mbalimbali ya kijamii kwa kuzingatia masuala ya viumbe hai, vitu visivyo hai na ya binadamu, aidha unanuia kutumia mfumo huu kwenye mipaka muafaka ya kiikolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati unaotumika katika mpango huu unawalenga wadau wote na masuala yote yaliyomo katika mfumo wa ikolojia ambayo yanapaswa kuwa katika usimamizi wa uvuvi. Kwa mfano, mkakati huu unazingatia matumizi yote katika uvuvi, athari zote kwa samaki, makazi na watu, pamoja na masuala ya kijamii yanayohusiana na uvuvi kama nani hushiriki na nani hufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati huu unazingatia pia masuala yasiyokuwa ya uvuvi kwa mfano tukichulia usimamizi wa uvuvi unaoendeshwa na jamii, mfumo huu wa ikolojia unaweza kupanua wigo wa usimamizi kwa kutambua uwepo wa wavuvi wahamiaji, samaki wanaohamahama muingiliano wa uvuvi unaoendeshwa karibu na fukwe na ule wa mbali na fukwe. Muingiliano wa nchi kavu na bahari, pamoja na masuala ya maisha ya jamii zaidi ya yale yanayohusiana moja kwa moja na uvuvi. Kwa hiyo usimamizi huu mara nyingi unawahusisha wadau wa uvuvi na wale wasiokuwa na uvuvi katika ngazi nyingi za kiutawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchini Tanzania uvuvi mdogo mdogo una nafasi muhimu katika kuchangia uhakika wa chakula na kipato, lakini uzalishaji katika uvuvi umepungua na hali ya mazingira ya samaki baharini imeathirika. Hii inatokana na kiwango kikubwa cha uvunaji wa viumbe baharini, uvuvi usio endelevu na unaotumia mbinu haribifu pamoja na mabadiliko ya mazingira ya Pwani unaotokana na ukataji holela wa mikoko. Ni muhimu kutambua kuwa mazingira bora ya uvuvi na maeneo ya bahari yanachangia uendelevu wa maisha, kipato, ajira pamoja na huduma nyingine zinazotokana na mfumo wa ikolojia.

Kwa hiyo, hatuna budi kulinda na kuimarisha vyanzo vya faida hizi zitokanazo na mazingira asilia. Usimamizi wa uvuvi uliopo sasa nchini Tanzania unafuata mfumo shirikishi wa kutumia vikundi vya kijamii (BMU). Hata hivyo inatambulika kwamba mifumo inayosisitiza uwiano wa masuala mbalimbali yanayohusiana katika uvuvi kama mfumo wa ikolojia unaweza ukawa wa manufaa zaidi, Wilaya ya Bagamoyo iliyopo Kaskazini mwa Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani na eneo ambalo utafiti na uendelezaji wa mfumo wa usimamizi wa kiikolojia unafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uvuvi iliendelea kukua kwa wastani asilimia tano miaka ya karibuni na kabla ya kushuka kwa kiwango kufikia asilimia 2.7 katika miaka ya usoni. Tanzania ina maliasili za kutosha za uvuvi ikiwa ni pamoja na maji baridi na maji chumvi ambazo kama zingetumika vizuri zingesaidia kuboresha maisha ya watu, ikiwa ni pamoja na lishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa zinazokabili sekta ya uvuvi ni pamoja na uvuvi haramu na biashara za magendo za samaki na mazao ya samaki mipakani ambazo hupunguza mchango wa sekta katika Pato la Taifa na juhudi za kupunguza umaskini.

Changamoto nyingine ni pamoja na kutumia nyezo na teknolojia duni za uvuvi, ukosefu wa mikopo na uharibifu wa mazingira, haya yote yanapelekea sekta hii kuzidi kushuka kila kukicha, lakini sekta hii inaweza kuliingizia Taifa pato kubwa sana na hivyo Serikali kuifanya kama ni chanzo chake cha mapato. Mikakati inahitajika kwa Wizara kusimamia ipasavyo na kuhakikisha sekta nzima ya uvuvi inasaidia Serikali katika kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mifugo ina nafasi kubwa katika kujenga uchumi imara wa Taifa, kuongeza kipato kwa Watanzania wanaotegemea mifugo na kutoa fursa za ajira sanjari na kuhifadhi rasilimali za Taifa. Sera hii inaeleza nia ya Serikali na wadau wengine katika kukabiliana na changamoto zinazokabili sekta ya mifugo. Licha ya wafugaji wa Tanzania kuwa na idadi kubwa ya mifugo, bado ni maskini ambapo takwimu zinaonesha kuwa Tanzania ina ng'ombe milioni 22.8, mbuzi milioni 15.6, kondoo milioni 7.0 na kuku milioni 58, lakini hali ya wafugaji nchini ni mbaya na wanaishi maisha duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia hali hiyo nawaomba watendaji wa Serikali kuzuia uharibifu wa mazingira na kuondoa migogoro ya ardhi ili kuwezesha ufugaji wa tija hapa nchini kwetu. Ni jambo la kusikitisha kuona Kanda ya Ziwa Victoria nchini Tanzania inaongoza kuwa na idadi kubwa ya mifugo, lakini na ndiyo yenye kiwango kikubwa cha umaskini wa kipato. Ni lazima tukubali kubadilika na kuwawezesha wafugaji na sekta nzima hii. Jukumu kubwa ni kujenga mazingira mazuri yatakayotoa fursa za kuongeza kipato na ajira kwa wafugaji wadogo, kufuga kibiashara na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufikia haya malengo makuu matatu ya kisera yatatekelezwa kama ifuatavyo:-

(i) Kuendeleza sekta ya mifugo itakayokuwa na mwelekeo wa kibiashara, yenye ufanisi na itakayohimili ushindani wa Kimataifa.

(ii) Kuibua mifumo bora ya uzalishaji itakayoongeza tija miongoni mwa wafugaji wadogo; na

(iii) Kuhifadhi rasilimali za mifugo na kuunda sera na taasisi zitakazosimamia maendeleo na matumizi endelevu ya rasilimali hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu ujao, Watanzania walio wengi wataendelea kuisha vijijini. Naiomba Serikali kuzihimiza kaya zilizo maskini zilizopo vijijini kushiriki katika uzalishaji mifugo, hususani kupitia ufugaji wa wanyama kama sungura, simbilisi, ngamia na kanga kwa ajili ya kupunguza umaskini, kuongeza ajira na kuwa na uhakika wa chakula, mpango huu utasaidia sana na kuleta mabadiliko makubwa sana.

Changamoto kubwa inayokabili tasnia ya mifugo ni namna ya kufikia viwango vya ubora wa mifugo na mazao yake vitakavyokidhi mahitaji ya soko la kikanda na kimataifa. Kwa

hiyo tasnia hii itashiriki kikamilifu katika biashara za Kimataifa kwa kuongeza uuzaji wa mazao nje ya nchi na kukabili ushindani wa bidhaa zinazoingizwa nchini ambapo ulinzi pekee uliopo kwa viwanda vya ndani ni kuweka viwango muafaka vya ushuru na ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya kisera ya kuifanya biashara ya mifugo iendane na mfumo wa kisasa wa biashara ya kimataifa yanahitajika ili kuiwezesha Tanzania kujihusisha kikamilifu kuleta mabadiliko zaidi katika mifumo ya biashara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatia moyo kwamba mabadiliko ya haraka yaliyotokea katika sekta ya mifugo katika miaka ya karibuni yamepokelewa na kukubaliwa na wadau wa sekta wakiwemo wazalishaji, wasindikaji, wafanyabiashara, wauzaji wa pembejeo za mifugo na watoa huduma wengine wapya. Hata hivyo bado kuna baadhi ya maeneo ya pembezoni ambayo hayapati huduma za kutosha. Naishauri Serikali kufanya taratibu kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa kuboresha huduma za mifugo katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vikwazo vinavyoikabili sekta nzima ya mifugo, vikwazo hivyo ndiyo vimekuwa vikirudisha nyuma juhudi nzima za kunyanyua hali za wafugaji wetu hapa nchini. Kumekuwa na vikwazo kama ifuatavyo:-

(i) Ardhi, maji na malisho ni tatizo kubwa katika mfumo wa umilikaji wa ardhi, rasilimali za maji na malisho ni kutokuwa na utaratibu wa kutenga na kumilikisha ardhi kulingana na taratibu za kisheria au kimila. Matatizo mengine ni kupanuka kwa shughuli za kilimo katika maeneo yaliyokuwa yanatumika kwa kufuga na kuchungia, kupanuliwa kwa mbuga za wanyamapori na kuhamahama kwa wafugaji kunakozuia kuendelezwa kwa maeneo yao.

(ii) Aina ya mifugo na mifumo ya uzalishaji kuwepo kwa kusaafu duni za mifugo ya asili pamoja na upungufu wa mifugo chotara kumechangia kwa kiwango kikubwa uzalishaji duni na usio na tija.

Hali hii imechochewa kwa kiwango kikubwa na mifumo ya uzalishaji mifugo inayotumiwa na wafugaji. Hata hivyo mifugo ya asili ina uwezo wa kustahimili mazingira magumu.

(iii) Magonjwa ya mifugo ni kati ya matatizo yanayokabili maendeleo ya tasnia ya mifugo. Kumekuwepo na kuenea kwa magonjwa ya mifugo nchini kama vile magonjwa ya mlipuko yasiyokuwa na mipaka, magonjwa yanayoenezwa na wadudu, magonjwa ya mifugo yanayoambukiza binadamu na magonjwa yanayojitokeza ambayo ni changamoto kubwa kwa maendeleo ya tasnia ya mifugo.

(iv) Usindikaji na masoko ya mazao ya mifugo upo upungufu wa miundombinu kwa ajili ya usindikaji na masoko ya mifugo na mazao yake.

Pia kumekuwepo na uingizaji wa mazao ya mifugo yenye ruzuku kubwa kutoka nje ya nchi ambayo hukatisha tamaa wawekezaji pamoja na kuleta ushindani usio sawa kwa mazao ya mifugo yanayozalishwa au kusindikwa hapa nchini.

(v) Kuhusu ukosefu wa elimu na ujuzi wa kutosha kwa wafugaji huathiri maendeleo ya tasnia ya mifugo nchini. Elimu na ujuzi ni muhimu na husaidia katika kupokea teknolojia sahihi zinazobuniwa na kusambazwa kwa wafugaji.

(vi) Uwekezaji na mikopo, uhaba wa taasisi za kutoa mikopo kwa wajasiriamali wakubwa, wa kati na wadogo wa mifugo na uwekezaji mdogo vinakwaza upanuzi na uzalishaji wa mifugo kibiashara. Zipo fursa nyingi zinazoweza kuongeza mchango wa mifugo katika uchumi wa Taifa na uhakika wa chakula katika kaya iwapo fursa hizo zitatumiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa hizo ni pamoja na kuwepo kwa idadi kubwa na aina mbalimbali za mifugo, rasilimali kubwa ya ardhi ya malisho ambayo inakadiriwa kuwa hekta milioni 60, hali nzuri ya hewa inayofaa kwa ufugaji katika kanda mbalimbali, masoko ya uhakika ya ndani na nje ya nchi, upatikanaji wa watu watakaoweza kufunzwa, pamoja na gharama nafuu za utendaji kazi, ujuzi na elimu ya asili kuhusu mifugo na sera nzuri za kiuchumi.

Vilevile kuna umuhimu wa kuwa na sera ya mifugo nchini itakayochochea ufugaji wa kibiashara unaolenga kuhifadhi mazingira. Nia ni kuboresha maisha ya wafugaji kwa kuwaongezea kipato na uhakika wa chakula kutokana na mazao ya mifugo, hivyo kuchangia katika kufikia malengo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kibaha Vijijini kwa asilimia kubwa watu wake ni wafugaji, wakulima na wajasiriamali, kwa upande wa wafugaji tumekuwa na changamoto nyingi sana katika sekta hii, kumekuwepo na migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na wakulima ambayo imekithiri hivi sasa na kuleta uadui mkubwa baina ya wananchi. Migogoro hii imefikia mahali mpaka inaleta kutokuelewana baina ya viongozi na wananchi kwani imekosa usuluhishi na kuwapo kwa muda mrefu. Tunakabiliwa na changamoto ya malalamiko hivyo kusababisha wafugaji kukosa huduma hiyo kwa mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kutuongezea malambo ili yaendane na idadi ya wananchi. Pia maeneo ya wafugaji bado yamekuwa hayajawekwa wazi kimipaka ili kuonyesha wazi na kutambulika baina yao na wakulima hivyo kupelekea wafugaji na wakulima kuingiliana na kuzuka kwa migogoro.

Naiomba Serikali kushughulikia suala hili kwani katika Jimbo langu la Kibaha Vijijini, tatizo hili limekuwa ni kero na la muda mrefu, vilevile naiomba Wizara kutuma wataalam wake kuja Jimboni kwangu na kutoa elimu ya ufugaji wa kisasa na hivyo kusaidia wafugaji kuwa na mifugo michache ambayo wataweza kuimudu kwa malisho kuliko ilivyo hivi sasa mtu mmoja anamiliki mifugo mingi na hivyo kupelekea kushindwa kumudu katika malisho ama sehemu zilizotengwa kuwa ndogo kulingana na mifugo kuwa mingi, wananchi wangu wakipata elimu hii itawasaidia na pia itasaidia kupunguza migogoro iliyopo hivi sasa Jimboni kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo naiomba Serikali maeneo ambayo yamekuwa hayaendelezwi kama la nchi za Taifa basi wazigawe kwa wananchi ili zilete tija na kupunguza hii migogoro ya ardhi baina ya wafugaji na wakulima, ifike mahali sasa tusisikie tena migogoro hii pale ambapo wafugaji watakuwa wamejitosheleza kwa kuwa na maeneo ya kutosha kwa mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa kuku nchini umegawanyika katika mifumo ya ufugaji wa asili na kibiashara. Ufugaji huu kama ungewekewa mkakati mzuri basi ungenufaisha wananchi wetu kwa kiasi kikubwa na hivyo kukuza uchumi wa mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Mfumo wa ufugaji wa asili huchangia zaidi ya asilimia 70 ya kuku wote wanaofugwa na hutoa nyama na mayai yanayoliwa vijijini na hukidhi asilimia 20 ya mahitaji ya mijini. Aina kuu za koo na chotara wa kuku wa asili ni kuchi, kishingo, sukuma, kinyafuzi na kiduchu. Kwa kiwango

kikubwa, uzalishaji wa kuku wa kibiashara hufanywa katika maeneo ya mijini na maeneo yanayozunguka miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, koo za kuku pamoja na chotara wao wanaofugwa kibiashara ni pamoja na *white leghorns, rhode island red, light sussex, plymouth rock, hisex, hybro na shavers.* Ufugaji wa kuku wa asili na wa kibiashara unakabiliwa na vikwazo mbalimbali ikiwa ni pamoja na magonjwa, lishe, uhaba wa huduma za kitaalam, kosaafu duni na vyama dhaifu vya wafugaji.

Vilevile kuna udhibiti hafifu kwenye vituo vya kutotolea vifaranga na mashamba ya kuku wazazi. Serikali itoe elimu ya kutosha ili kuongeza idadi na ubora wa kuku na mazao yake ili kukidhi mahitaji ya ndani, kuongeza mauzo ya nje na kuhamasisha uzalishaji endelevu wa kuku. Vilevile hapa nchini kuna zaidi ya minada 300 ya awali, 13 ya upili na sita ya mipakani. Minada yote ya awali inasimamiwa na Halmashauri za Wilaya ambapo minada ya upili na ya mipakani inasimamiwa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, minada michache ya awali inafanya kazi ila mingi ni mibovu. Aidha, vipo viwanda sita vya kusindika nyama na machinjio za kisasa saba. Kwa sasa ulaji wa nyama kwa mtu kwa mwaka ni kilo 11 kiasi ambacho ni chini ya kiwango cha kilo 50. Serikali haina budi kuhamasisha ili tuendane na viwango vilivyowekwa Kimataifa, ila usindikaji, uuzaji na ulaji wa nyama bora na mazao yatokanayo na nyama unakabiliwa na kutopatikana kwa wanyama bora, uhaba wa taarifa za masoko, upungufu wa utafiti na mafunzo katika teknolojia ya nyama, uelewa mdogo wa walaji kuhusu ubora wa nyama na ukosefu wa mitaji ya kuwekeza katika viwanda vya kusindika nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hii baadhi ya kampuni za biashara huagiza nyama na mazao yake kutoka nje ya nchi. Uzalishaji wa maziwa ni moja ya shughuli za biashara inayokua haraka katika tasnia ya mifugo. Wanyama wanaofugwa kwa ajili ya uzalishaji wa maziwa hapa nchini ni pamoja na ng'ombe, mbuzi, nyatimaji na ngamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maziwa mengi yanauzwa kutokana na wafugaji wadogo ambao huzalisha takribani asilimia 70 na wafugaji wakubwa huzalisha karibu asilimia 30. Uzalishaji wa maziwa unakadiriwa kuwa lita bilioni 1.38, ambayo ng'ombe wa asili walichangia kwa takribani asilimia 70. Wastani wa utoaji wa maziwa kwa mwaka kwa uzao kwa ng'ombe wa asili ni lita 500 ikilinganishwa na lita 2,000 kwa ng'ombe wa kisasa. Wafugaji wadogo wa ng'ombe wa maziwa wanapatikana kwa wingi katika maeneo ya mjini na maeneo ya viunga vya miji na vijijini katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Iringa, Kagera, Dar es Salaam na Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wastani wa unywaji maziwa kwa mtu kwa mwaka nchini ni lita 39 ikilinganishwa na kiasi cha lita 200 kwa mtu kwa mwaka, takwimu hizi muhimu kama nchi kuzifanyia kazi ili kuleta tija kwa wananchi wetu.

Pia ngozi ni zao la ziada linalotokana na mifugo ambalo hutumika kama malighafi muhimu katika viwanda vya ngozi na huingiza fedha nyingi za kigeni. Idadi kubwa ya ngozi hutokana na mifugo ya asili. Uzalishaji wa ngozi kwa mwaka ni takribani vipande milioni 2.6 vya ng'ombe na vipande milioni 2.5 vya kondoo na mbuzi ambapo asilimia 75 ya vipande hivyo hukusanywa. Aidha, inakadiriwa kuwa asilimia 95 ya ngozi zote huuzwa nje zikiwa ghafi hususani baada ya kukaushwa au kuwekewa chumvi, ngozi kama zao muhimu la biashara halijatambuliwa na wafugaji wengi na hivyo kusababisha maendeleo duni ya tasnia ya ngozi. Ubora wa ngozi unakabiliwa na mbinu duni za ufugaji kama vile upigaji chapa hovyo, udhibiti hafifu wa wadudu wanaoshambulia wanyama na kuharibu ngozi pamoja na uchunaji, uhifadhi

na usindikaji usioridhisha. Hivyo basi Serikali haina budi kuzingatia kwa kutoa elimu ya kutosha kwa wafugaji ili kupitia zao la ngozi ili Serikali ipate fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mazao mengine ya ziada yatokanayo na mifugo na yenye umuhimu kiuchumi ni pamoja na sufu, damu, mifupa, pembe, kwato, manyoya na nywele za mifugo mbalimbali. Mazao hayo hutumika kwa madhumuni mbalimbali yakiwemo utengenezaji wa vyakula vya mifugo, dawa na mavazi hivyo basi ni wajibu wa Serikali kuweka mkazo katika mazao haya ili yaonekane umuhimu wake, lakini uzalishaji na matumizi endelevu ya mazao ya ziada yatokanayo na mifugo yanakabiliwa na uelewa mdogo, kutokuwepo kwa miongozo na taratibu kuhusu uzalishaji, ukusanyaji, usindikaji na teknolojia sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bajeti ya Wizara, Wizara hii ni nyeti na inashughulikia mambo makubwa mawili ambayo ni mifugo na uvuvi, lakini Wizara hii itakuwa inashughulikia pia na matatizo yanayojitokeza kati ya wafugaji na wakulima na hivyo kujikuta inashughulika pia na mambo ya ardhi na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza na kusikitisha Serikali imeendelea kutokuona umuhimu wa Wizara hii na kuendelea kuitengea bajeti ndogo isiyokidhi. Pamoja na udogo wa bajeti, hata hivyo hukwamisha shughuli za Wizara. Ni lini Serikali itamalizia kutoa fedha zilizotengwa kwa bajeti ya mwaka 2013/2014 ili Wizara itekeleze kazi zake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu machinjio ya kisasa, nchi yetu imebarikiwa kuwa na maeneo mengi ya wafugaji lakini tatizo lililopo ni machinjio ya kisasa mfano mzuri ni katika Mkoa wa Singida. Mkoa huu unaongoza kuwa na wafugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo na kuku lakini hakuna machinjio ya kisasa ili kuimarisha ubora wa nyama. Ni lini Serikali itaanzisha machinjio ya kisasa katika Mkoa wa Singida?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda vya ngozi na kwato za wanyama hakuna asiyefahamu umuhimu wa zao la ngozi katika kuchangia Pato la Taifa. Ngozi hutumika kutengeneza viatu, mikoba, mikanda na hata mavazi ya kiasili. Kwato za ng'ombe na wanyama wengine hutumika kutengeneza vipuli, vifungo na bidhaa zingine. Kukosekana kwa elimu kwa wafugaji kuhusu utunzaji mzuri wa ngozi za wanyama wao ni tatizo kubwa linalopelekea kupunguza ubora wa ngozi. Wafugaji wengi wamekuwa wakiwapiga chapa za moto wanyama ili kuweka alama kuzuia wezi, lakini hili hufanyika kwa sababu wafugaji wengi hawajaelimishwa vya kutosha. Elimu inayotolewa kwenye TV, redio au magazeti haitoshi kuwafikia wananchi wengi waishio vijijini hasa ukizingatia *nature* ya wafugaji ambao wengi huishi maporini kusiko na vyombo hivyo vya habari. Njia mbadala itumike kuwaelimisha wafugaji hawa ana kwa ana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo la elimu, nchi yetu inakabiliwa na uhaba mkubwa wa viwanda vya ngozi na hivyo kupelekea utoroshaji mkubwa wa ngozi ghafi. Ni muhimu sana Serikali ikaona umuhimu wa kuanzisha viwanda vya kuongeza thamani ya ngozi, na hilo liende sambamba na kusomesha wataalamu zaidi katika fani hii. Bila kuwa na wataalamu wa kutosha, hata tuwe na viwanda vingi itakuwa ni kazi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro kati ya wafugaji na wakulima kwa muda mrefu sasa kunakuwa na migogoro endelevu kati ya wafugaji na wakulima wakingombea maeneo ya malisho na maji. Suala hili limeleta maafa makubwa sana kwa wananchi wanaoishi

katika maeneo yenye uhaba wa ardhi. Migogoro ipo pia kwa wananchi waishio karibu na hifadhi ambapo hawaruhusiwi kulima au kufuga. Ni kwa nini Serikali inachelewa kupima maeneo yake ili kutenganisha maeneo ya wafugaji na wakulima? Kuna maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya hifadhi na hayatumiki kwa hifadhi, ni kwa nini Serikali isiyatoe maeneo haya kwa wananchi kufanya shughuli zao za ufugaji na ukulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvuvi haramu pamoja na bajeti ya Wizara kutokutosha, ni wakati sasa wa Wizara hii kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kutokomeza uvuvi haramu kwanza kwa kuvifungia viwanda vinavyozalisha nyavu zisizokidhi kwa uvuvi kwa kuwatoza faini kubwa na endelevu pindi wavunjapo sheria na pili kwa kutoa elimu endelevu kwa wavuvi wote nchini ili waone kwamba sekta ya uvuvi ikitumiwa vizuri inaweza kuliongezea Taifa pato kubwa na hivyo kuinua vipato vya watu na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Ofisi ya Mbunge wa Chalinze, nimpongeze Bwana Kamani (Mb), kwa kuaminiwa kuwa yeye ndiye mwenye mwarobaini wa matatizo ya kisekta na kwamba sasa ofisi yangu inamuahidi ushirikiano. Ninapenda kuanza kwa kuunga mkono hoja ya Wizara yake ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Chalinze ni moja kati ya majimbo mengi nchini kwetu ambapo makazi yake ni mchanganyiko, yaani wapo wakulima na wafugaji kwa kipindi chote toka enzi za Wakili Mrisho Kikwete Mizega I hadi ngwe ya pili ya miaka ya 2000 jamii imekuwa inaishi kwa umoja na mshikamano, lakini ghafla tu migogoro mikubwa baina ya jamii hizo imeibuka. Ofisi ya Mbunge wa Jimbo la Chalinze imepokea malalamiko makubwa na mengi toka kwa jamii ya wakulima dhidi ya uvamizi mkubwa unaofanywa na wavamizi wenye mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hii imepelekea kuibuka kwa ugomvi na hasara kubwa imesababishwa na matatizo haya. Mfano ndugu Juma Mkombozi wa Kimange, ambaye alipigwa hadi kuvunjwa kiuno akiwazuia ng'ombe kuvamia shamba lake na kuharibu mazao. Pia mkazi wa Kihangaiko, Msata aliyechomwa na mkuki mkononi na kumsababishia ulemavu. Hawa ni wachache kuliko kuwataja wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvamizi huu si tu kwenye mashamba lakini pia hata kwenye mabwawa ya maji kwa matumizi ya binadamu na kwenye chanzo cha mradi wa maji Wami - Chalinze haswa katika vitongoji vilivyo kando ya Mto Wami upande wa Pongwe Nsungwa, Pongwe Kiona na Kilosa, Mvomelo. Tatizo hili limepelekea kuchafuka kwa maji na kujaa tope kulikopelekea *pump* kushindwa kufanya kazi vizuri na hivyo kupelekea kutopatikana kwa maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, upande wa wafugaji Jimbo la Chalinze wameendelea kupata shida hasa katika kuwapatia afya njema ng'ombe wao. Majosho mengi yameharibika baada ya mvua kubwa na ubora wa majosho hayo. Mfano majosho Chamakweza, Magulumatari, Matuli, Msata, Mkenge yameharibika na hayafai kwa matumizi ya mifugo yetu. Pia majosho mengine yamekuwa ni ahadi zisizotekelezeka mfano josho la Lulenge, Miono hakuna na Kihangaiko ni miaka mingi sasa hakuna josho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ilipata chanjo chache sana kinyume na matarajio yaliyokusudiwa. Ni ombi langu, kuepusha magonjwa ya mlipuko ambayo yanaweza pelekea kuathiri afya za wamiliki wa mifugo hiyo wachungaji na walaji wa mifugo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwendo wa taratibu wa utekelezaji wa machinjio Ruvu, nao pia umekuwa ni kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya sekta hii katika eneo la Wilaya ya Bagamoyo hata wengine wanaoishi maeneo yanayozunguka Jimbo la Chalinze. Pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuendelea kuimarisha Bodi ya Nyama na kuwahimiza wadau wa tasnia ya nyama kujisajili, usalama wa afya zetu walaji unahakikishiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kutoa maombi kwa Wizara kuendelea kutoa elimu juu ya ufugaji bora kwa kuwa sasa mifugo imekuwa mingi kuliko maeneo ya kulisha. Pia sasa muda muafaka wa kuanza kufikiria mabadiliko ya sheria Namba 18 inayozungumzia uchambuzi na maendeleo ya mifugo ili kuonyesha utaratibu mzuri na idadi ya mifugo ambayo watu wanapaswa kuwa nao katika eneo fulani la mraba. Mpango wa matumizi ya bora ya ardhi nao una umuhimu sana, kazi nzuri iliyofanyika Mvomelo ikifanyika Chalinze, Serikali hii itakuwa imetusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize kwa swali je, Serikali ina mpango gani na bandari ndogo ya Saadani ambayo sasa ni zaidi ya miaka mitano toka imefungwa hivyo kuleta tatizo kubwa katika shughuli za kiuchumi kwa watu wa Saadani, Matupwili, Mkange na maeneo ya Manda na Miono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. SHAFFIN A. SUMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. nchi yetu ni nchi ya tatu Barani Afrika katika wingi wa mifugo, lakini hadi sasa wafugaji na Watanzania hawanufaiki kwa wingi wa mifugo tuliyonayo. Inawezekana kabisa watoto wetu kupata maziwa ya kunywa wakiwa mashuleni, ni suala la kujipanga na kushirikiana na Wizara ya Elimu ili watoto wetu wakiwa mashuleni kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo maeneo mengi nchini yana mgogoro baina ya wafugaji na wakulima wakati huo huo nchi yetu ina maeneo ambayo hayafai tena kuwa hifadhi, ni faida gani tunapata kama maeneo ya hifadhi yameharibiwa na hayafai kuendelea kuitwa hifadhi wakati wakulima na wafugaji hawana maeneo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umefika sasa wafugaji wapewe maeneo kwa ajili ya ufugaji tu na eneo hilo linaweza kuvutia wawekezaji kwa ajili ya kusindika maziwa, nyama, viwanda vya ngozi. Maeneo tunayo, mifugo tunayo uwezo tunao tunachokwama ni Kuthubutu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa hii ili nami niweze kutoa maoni yangu kuhusu bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro baina ya wafugaji na wakulima inaonekana ni tatizo ambalo Serikali imeshindwa kulitafutia ufumbuzi. Ni lini Serikali itamaliza tatizo hili kwa kutenga maeneo yanayofaa kwa makundi yote mawili kwa vita vya wenyewe kwa wenyewe? Rejea habari za mauaji ya wakulima na wafugaji katika Wilaya ya Kiteto na maeneo mengine katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuipuuza sekta ya mifugo pamoja na umuhimu wake katika uchumi wa nchi. Sekta ya mifugo imeendelea kujitahidi kutosheleza mahitaji ya nyama nchini na hivyo kuokoa fedha ambazo zingetumika kuagiza nyama toka nje ya nchi.

Katika mwaka huu wa fedha 2014/2015 Serikali imeipatia Wizara hii takribani shilingi bilioni mbili tu sawa na 900% ya bajeti yake kwa mwaka. Huu ni utani na upuuzaji wa kupindukia unaofanywa na Serikali kwa Wizara hii. Serikali inatumia fedha nyingi kwa mambo yasiyo na tija na hata yaliyo nje ya bajeti lakini inashindwa kuipatia Wizara ya Mifugo na Uvuvi fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya maendeleo ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo sekta ya mifugo, sekta ya uvuvi pamoja na umuhimu wake nayo imeendelea kupuuzwa. Uvuvi ni sekta ambayo kama ikipewa umuhimu kwa kupatiwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge inaweza kutoa mchango mkubwa katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imejaaliwa kuwa na rasilimali ya bahari, mito na maziwa. Cha kusikitisha ni kwamba Serikali haijaonesha nia yoyote ya kusimamia uvuvi katika bahari kuu na hivyo kuruhusu uvuvi haramu ambapo meli nyingi za kigeni hufika katika bahari yetu na kuvua na kuondoka bila kizuizi na malipo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo Serikali ingekusanya tu mrabaha kutoka kwa meli ingekamata bila kutoza faini meli zinazovua bila kibali ambazo kwa taarifa zilizopo ni nyingi, basi Serikali ingeweza kuongeza uwezo wa mapato yake na kuondokana na aibu kama hii ya mwaka huu unaoisha wa fedha ambapo Serikali haijatoa fedha kwa angalau 50% kwa Wizara zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefika wakati na Serikali haina uchaguzi bali kuangalia kwa makini sekta hizi za mifugo na uvuvi ili kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. RACHEL R. MASHISHANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja hii kwa uchache ikizingatia inagusa Watanzania wengi sana pamoja na hayo imekuwa ikisaidia katika kuinua vipato vya Taifa pamoja na wafugaji wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na *operation* kadha wa kadha nchini na hasa katika Bonde la Ihefu, Kagera na hata Mikoa ya Shinyanga na kwingineko ambapo wafugaji walipoteza mifugo yao mingi sana katika zoezi hilo. Pamoja na kupoteza mifugo yao bado walidhalilishwa sana kwa kuitwa au kuambiwa kuwa "wamekonda kama mifugo yao." Hizi ni kauli za baadhi ya viongozi walizokuwa wakizitoa kwa wafugaji hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na zoezi hilo kutekelezwa kinyume kabisa na utaratibu, watu walikufa sana pamoja na mifugo yao, lakini nasikitika mpaka leo Serikali imekaa kimya, haijaomba radhi wala kulipa fidia wafugaji hao wakati zoezi lilifanyika kiunyanyasaji na fedheha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujua kauli ya Serikali ikoje kuhusu aidha kuwaomba radhi wafugaji hawa au kuwalipa fidia ya mali zao kutokana na zoezi hilo lililofanyika kinyume na utaratibu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kuunda Tume za kutosha yaani Tume kibao na nyingi kufuatilia suala hili, sijaona hoja siku moja ripoti ya Tume hizi Bungeni wala hadharani. Hii inaonyesha kuwa ripoti hizi zipo kabatini na hazijashughulikiwa kwa sababu tu wafugaji wanaonekana ni watu wasiokuwa na faida katika nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitaka Serikali itamke kuwa ni lini sasa ripoti za Tume zilizoundwa tena zimetumia fedha nyingi sana ikiwemo Tume ya Jaji Chande ripoti hizo zipo wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wamekuwa wakidhalilika sana pamoja na kuwa hakuna sherehe utakayoikuta haina nyama, wala hakuna kaya ambayo haitumii nyama labda wenzetu kutoka Asia (India) tu. Naomba Serikali ione sasa umuhimu kuhakikisha wafugaji haki zao zinalindwa ikiwemo kuwapatia maeneo rasmi kwa ajili ya malisho ili kuepuka migogoro ambayo imekuwa ikitokea baina ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE.GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wa Wizara kwa maandalizi mazuri ya bajeti. Ni dhana ya zamani kwamba Mkoa wa Ruvuma si rafiki kwa wafugaji dhana hiyo si ya kweli kwani Wamisionari pale Peramiho na sehemu nyingine wamekuwa wakifuga ng'ombe wa nyama na maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho tumekuwa hatufanyi Ruvuma na tutabaki hivyo ni kuchunga mifugo, tutaendelea kufuga tu na hapa naomba msaada wa Wizara hii. Mbuga ina mazingira mazuri sana ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, nimetamani sana na wananchi wanapenda hivyo kuwekwa kwenye programu ya kupewa ng'ombe wa kisasa lakini pia Serikali kuanzisha mpango wa kukusanya na kusindika maziwa ili mbuga ifahamike kwa uzalishaji wa maziwa nchini. Wizara itasaidia namna gani tutimize ndoto hii? Nitafurahi kupata mpango wa Wizara kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya ngozi nchi ya Ethiopia imepiga hatua sana katika mazao ya ngozi na mali nyingi, wapo tayari kutusaidia. Wakati wa kuingiza *jackets,* mikoba na viatu toka nje umekwisha, tunaweza kuzalisha vyote hivi hapa nchini. *Please pick up and proceed.* Mungu awabariki sana.

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja hii, pia nampongeza Waziri na timu yake kwa kazi nzuri wanayoifanya kuendeleza sekta hii. Pamoja na pongezi ninayo maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uboreshaji wa mifugo ya asili (Manyoni). Wilaya ya Manyoni na Mkoa wa Singida kwa jumla ufugaji ni moja ya shughuli kubwa ya wananchi wake, lakini ufugaji huo kwa asilimia kubwa ni mifugo ya asili. Changamoto iliyopo ni kuboresha/kubadili mifugo hiyo iwe ya kisasa kwa kuwa kituo cha mifugo ya kisasa kipo Mpwapwa na wananchi wengi hawawezi kwenda kupata huduma hii huko.
Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara inaweza kuweka utaratibu wa huduma za madume ya kisasa na mitamba ya kisasa kusogezwa karibu na wafugaji ili iwe chachu ya kubadilisha ng'ombe wa asili na kupata ng'ombe chotara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu malalamiko ya wajasiriamali wauza chakula cha mifugo nchini Kenya, hivi karibuni yametokea malalamiko ya wajasiriamali wanaouza pumba za mahindi, mpunga na mashudu ya alizeti nchini Kenya. Kuna chakula cha mifugo lalamiko lao ni kwamba huko nyuma Wizara ilikuwa inawapa kibali cha kuuza bidhaa hizo Kenya kwa ada ya shilingi 10,000/= kwa lori moja lakini kuanzia mwezi Machi mwaka huu ada hiyo ya kibali imepanda na kuwa shilingi 10,000/= kwa tani. Hivyo, kwa lori la tani 30 wanatakiwa kulipa shilingi 300,000/= badala ya shilingi 10,000/= za awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badiliko hili ni kubwa mno na limeathiri biashara yao kwani hawawezi kushindana na wenzao wa Uganda na Rwanda ambao nao wanauza bidhaa hizo nchini Kenya. Wizara imeshauriwa kuangalia upya kiwango hicho kuzuia lengo la Serikali ni kuwawezesha Watanzania kupata masoko nje ya nchi na sio kuwawekea vikwazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kusema kwamba, naunga mkono hoja na ahsante.

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kushangazwa na bajeti ndogo shilingi bilioni 66.1. Pamoja na hayo, nachangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu soko la mifugo Mheshimiwa Waziri wafugaji hawana taarifa ya bei ya mifugo Kitaifa na kiulimwengu bado mifugo inauzwa minadani kwa macho na siyo kwa mizani. Nashauri Serikali iwapatie soko la nyama na ngozi na Serikali isisitize elimu ya viwanda vya kusindika nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ruzuku ya mifugo naungana na Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji kwamba elimu itolewe kwa wafugaji kuhusu ruzuku hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya ardhi ya mifugo nashauri Serikali ifanye mpango kabambe kuhusu kupanga matumizi bora ya ardhi baina ya wafugaji na wakulima ili kuzuia ugomvi wa mara kwa mara baina ya jamii hii mpaka kusababisha mauaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maafisa ugani nashauri kuwe na wataalam wa mifugo kila Kata na wasaidizi wao ili kudhibiti magonjwa na mifugo. Aidha, upatikanaji wa dawa na tiba ya mifugo isimamiwe, Maafisa hawa wasikae ofisini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa umuhimu, nachukua nafasi hii kuwapongeza Waziri Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani na Naibu wake Mheshimiwa Kaika Telele, kwa uteuzi wao. Kwa kuwa ni wafugaji tunawategemea sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. DKT. TEREZYA P. L. HUVISA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pamoja na pongezi hizo ni vyema Wizara ikaongeza jitihada katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Ruvuma kwa muda mrefu Wananchi bado hawajaitumia fursa ya ufugaji ili kuleta maendeleo kwa Wananchi. Hata hotuba ya Mheshimiwa Waziri haijatoa kipaumbele cha kuinua shughuli za mifugo Mkoani Ruvuma. Je, ni lini Serikali itachukua mkakati wa makusudi ili kuinua ufugaji kwa Mkoa wa Ruvuma? Mkoa wa Ruvuma una rasilimali ya kutosha kwa ajili ya malisho na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji wa nguruwe ninaipongeza Wizara kwa kuzingatia ufugaji wa nguruwe, kuendeleza shamba la Ngerengere na kuongeza nguruwe wazazi. Je, ni lini tunaweza kupata mbegu ya nguruwe wa kisasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Ruvuma kwa miaka mingi umetegemea zao la nguruwe ili kupata kitoweo, ni lini Wizara itaanzisha shamba la nguruwe Mkoani Ruvuma ili kuwawezesha wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kupata nguruwe wa kisasa na kuboresha ufugaji?

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri dakika 20 na Mheshimiwa Waziri dakika 40. Mngewasaidia Wabunge vilevile, hizi nyavu si ziko madukani, kwa nini msiwakamate wanaouza mnawakamata wanaotumia? *(Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii iliyo mbele yetu leo.

Awali ya yote, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kunifikisha hapa nilipo nikiwa na afya njema, nguvu na uwezo wa kuendelea kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa kusema kwamba, ninaunga mkono hoja hii ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Kabla sijaanza kujibu na kutolea maelezo hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge, naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Viongozi Wakuu mbalimbali wa Taifa hili, kwa kuiongoza nchi yetu kwa busara na hekima, ambayo imeendelea kuleta amani na utulivu na maendeleo. Aidha, nichukue nafasi hii, kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Vilevile, nawapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri wote walioteuliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa na Wananchi hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Waziri wangu, Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani, kwa kunishirikisha kwa karibu sana katika majukumu ya kuongoza Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Aidha, napenda nimpongeze sana Waziri Kamani, kwa jinsi alivyowasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara yetu vizuri sana, amesoma na akamaliza kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, kwa ushirikiano wanaonipa katika utendaji wangu wa kazi ndani na nje ya Bunge. Ninaahidi kwamba, tutaendelea kushirikiana ipasavyo kujenga nchi yetu. Aidha, nawashukuru Katibu Mkuu, Dkt. Charles Nyamrunda, Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Yohana Budeba, Wenyeviti wa Bodi, Wakuu wa Idara, Taasisi zilizo chini ya Wizara na Wafanyakazi wote, kwa ushirikiano wa hali ya juu wanaotupa katika kazi zetu. Nawashukuru Wadau wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi, Wafugaji, Wavuvi, Vyama vya Wafugaji na Vyama vya Wavuvi, kwa ushirikiano wanaotupa katika kutatua matatizo yanayozikabili sekta hizi. Aidha, nasikitika na kutoa pole kwa ndugu na jamaa waliopoteza ndugu zao kutokana na mapigano kati ya Wakulima na Wafugaji; nawaombea wale waliokufa Mwenyezi Mungu awape faraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Ngorongoro ambao walinipa kura zao na kunichagua kuwa mwakilishi wao na kunileta hapa Bungeni. Ninawaahidi kuendelea kuwatumikia kwa uwezo wangu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru kwa dhati familia yangu, mke wangu Catherine na watoto wetu, kwa upendo na uvumilivu na ushirikiano wao kwangu, siku zote katika mambo yote magumu na mepesi wakati wa kutumikia Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo sasa naomba kuchangia hoja na kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, waliopata fursa ya kuchangia kwa kusema au kwa maandishi. Mtoa hoja Mheshimiwa Waziri, atakapokuja kuhitimisha hoja yake, atatoa majibu ya kina kwa michango iliyosalia. Tunathamini sana michango ya Waheshimiwa Wabunge na napenda kuwahakikishia kwamba, tutaendelea kuitolea majibu na kufanya kazi pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana kwa michango yenu na ninaomba nijibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya magonjwa ya mifugo ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete. Majibu ni kama ifuatavyo:-

Wizara itaendelea kushirikiana na Wilaya ya Bagamoyo kufanya tathmini ya gharama za uharibifu zinazohitajika kukarabati majosho yaliyoharibika. Aidha, Wizara inashauri Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo pamoja na Halmashauri nyingine, kuweka makadirio hayo katika bajeti zao. Wakati huo huo Wizara imeomba fedha za chanjo ya mifugo katika bajeti ya mwaka 2014/2015 kwa ajili ya matumizi ya Halmashauri zote nchini.

Napenda kusisitiza kwamba, fedha hizo zikipatikana zitapelekwa katika Wilaya ambazo mara nyingi zinakumbwa na magonjwa ya milipuko ikiwemo Wilaya ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya uendelezaji wa zao la maziwa na Wizara kuendeleza tasnia ya maziwa hapa nchini. Wizara pamoja na Bodi ya Maziwa, kwa kushirikiana na Halmashauri mbalimbali nchini, ziliwaomba wahusika waibue matatizo yanayoikabili tasnia hii ya maziwa ili sisi tuweze kuweka katika utaratibu. Kwa kweli tulikuwa tumeomba fedha ya kuendeleza tasnia hii na bahati nzuri tumepewa fedha kidogo na kwa hiyo, tutashughulikia jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, mtoa hoja atakuja kujibu hoja nyingi zaidi hapa, ndiyo maana siendi ukurasa kwa ukurasa. Hoja nyingine ilikuwa kwamba, Serikali ithamini mifugo pamoja na wafugaji. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa John Momose Cheyo. Wizara inajibu kama ifuatavyo:-

Serikali inawathamini sana wafugaji na mifugo yao, ndiyo maana inajenga majosho, vyanzo vya maji kwa mifugo na minada kwa ajili ya kuhudumia mifugo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja kwamba, katika hii hali ya kupunguza mifugo, wafugaji wakishaelimishwa basi wao watajua namna ya kupunguza mifugo, lakini siyo kuwaambia wapunguze. Waheshimiwa Wabunge pia wameshauri kwamba, mifugo inaweza kujipunguza yenyewe kama tutaweka miundombinu sahihi, kama vile kujenga machinjio, kunenepesha mifugo ili ikinenepa basi wafugaji waipeleke katika machinjio hayo na kujenga viwanda vya kusindika mazao ya mifugo na *automatically* mifugo inaweza ikajipunguza yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishauriwa pia kwamba, Serikali ijenge kiwanda cha maziwa. Hili nalo nimeishalisemea kwamba, ni muhimu sana viwanda vya kusindika maziwa viweze kujengwa. Tutaangalia tumepatiwa fedha kiasi gani ili tuweze kujenga hivi viwanda vya maziwa na kuwahamasisha Watanzania waweze kunywa maziwa. Hali iliyopo sasa ni kwamba, tunasema vijana wa shule wanywe maziwa, lakini pia watu wazima wanatakiwa wanywe maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya kwamba, hakuna taarifa za bei ya mifugo. Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, hutoa taarifa za bei za mifugo katika magazeti ya *Daily News, The Guardian, The Citizen,* Mwananchi na kadhalika. Pia taarifa hizi hupatikana kwa simu za viganjani na kadhalika. Kwa hiyo, hoja kwamba, bei ya mifugo katika minada haijulikani, inajulikana sana ukishafanya hayo ambayo nimeeleza hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya biashara ya mifugo na mazao yake, kwenda kujifunza kutoka huko Ethiopia na Botswana. Nataka niseme kwamba, ni kweli hivi karibuni mimi mwenyewe nilikwenda huko Ethiopia kwa jambo moja la masuala ya samaki, lakini baada ya hapo kwa kujua Ethiopia iko mbele sana katika masuala ya mifugo na hasa mazao ya mifugo, nikawa na *interest* tu kupita pita huko nikauliza uliza, wakanipeleka mahali kwa kweli wako mbele sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara zote nimesikia habari za Botswana ambao nao wako juu katika masuala haya na hasa mazao ya mifugo na hasa nyama. Tutafanya utaratibu ili tuendelee kujifunza zaidi huko Ethiopia na Botswana, ili kuweza kuwahamasisha Wananchi wetu wanenepeshe mifugo yao na tutakapokuwa tumejenga viwanda na machinjio basi waweze kupeleka mazao ya mifugo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya kuunda Wakala wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo na kuandaa Wakala wa Kuendeleza Sekta ya Uvuvi. Huo ulikuwa na ushauri ambao ulitolewa na Mheshimiwa Benedict Ole- Nangoro, Wizara imepokea ushauri huo na tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja mbalimbali sasa kutokana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Maji na Mifugo. Hoja ya kwanza ilikuwa ni Serikali kuimarisha mahusiano ya kikazi kati ya Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Serikali ilishachukua hatua za kuzielekeza Halmashauri kuunda Idara ya Mifugo na Uvuvi, hatua ambayo imeanza kutekelezwa katika baadhi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nyingine kwamba, Serikali itoe umuhimu katika utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo. Jibu ni kwamba, Wizara imetoa mafunzo yanayohusu *TANLITS* kwa Halmashauri zote nchini. Hii *TANLITS* ni Mfumo wa Utambuzi wa Mifugo Kielektroniki. Pia mfumo huo umekamilika na unafanyiwa majaribio katika Wilaya za Kibaha, Muheza na Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilikuwa ni kutenganisha Wataalam wa Mifugo na Kilimo katika Wilaya. Jibu la hoja hii ni kwamba, Wizara imetayarisha na kusambaza mwongozo wa utoaji wa huduma za ugani wa mifugo ambao unaonesha muundo wa huduma za ugani katika ngazi ya Wilaya kwa Mifugo na Uvuvi. Ofisi ya TAMISEMI iliishatoa maelekezo ya kutenganisha Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya migogoro ya ardhi yamezungumzwa sana na Waheshimiwa karibu wote waliochangia hoja ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Nakubaliana na maoni ya Kamati, kwa kuwa utenganishaji wa maeneo ni muhimu sana katika utatuzi wa migogoro. Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, imeagiza Wizara zinazohusika na ardhi, kufanya tathmini ya maeneo ya hifadhi na mashamba ya wanyamapori pamoja na mashamba ya mifugo ili kuona namna gani tunaweza kupata maeneo katika yale maeneo ambayo sasa yamepoteza sifa kama mashamba ya wanyamapori, hakuna digidigi, sungura na kadhalika, yafanyiwe tathmini ili kuweza kupata maeneo ya kuwa-*resettle* hao wafugaji baadae. Vivyo hivyo itafanyika kwa mashamba ya mifugo ambayo yako chini ya *NARCO. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja pia kwamba, kitendo cha kutopima ardhi na kubainisha maeneo ya mifugo na matumizi mengine, imekuwa ni sababu kubwa ya migogoro hapa nchini. Nakubaliana na ushauri wa Kamati kwamba, maeneo yatakayotengwa yawekewe miundombinu ya mifugo kama majosho kwa ajili ya maji, kuchimba malambo, mabwawa, visima virefu na kadhalika ili kuweza kuwaweka hao wafugaji wasiendelee

kuhamahama, kwa sababu wanahama kwa ajili ya kufuata malisho pamoja maji katika maeneo mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kumbe tukiweka miundombinu hii muhimu basi wanaweza wakatulia katika maeneo yao na hivyo kupunguza na kama siyo kumaliza kabisa, tatizo la kuhamahama na kusababisha migogoro katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imeshauriwa ifanye tathmini ya maeneo ambayo yamepoteza sifa na hii nafikiri nimeshaisema, ili kuweza kutoa maeneo hayo kwa ajili ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala haya kwa sababu ni ya kisheria pia, mashamba ya wanyamapori na mifugo yameanzishwa kisheria. Bunge hili ambalo linaweza kutazama na sheria hizo na kama zimepitwa na wakati tuzirekebishe ili kuweza kuwapatia wafugaji maeneo ya kufugia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilikuwa kwamba, Sekta ya Mifugo iongezewe fedha kwa ajili ya kujenga majosho, malambo na kadhalika. Ni kweli Wabunge wengi wamepiga keleke kwamba, bajeti ya Wizara hii ni ndogo sana. Tunawashukuruni sana kwa kelele zenu, *Inshallah,* nadhani wanaohusika wanaweza sasa wakaona umuhimu na kututengea fedha. Habari ya fedha, Mheshimiwa Waziri, anaweza akaielezea baadaye atakapokuwa anahitimisha hoja yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nyingine kwamba, Ranchi walizopewa wawekezaji ambao wameshindwa kuziendeleza zigawiwe sasa kwa wafugaji watakaoweza kuziendeleza. Hoja hii tunaichukua na baada ya Bunge hili tutafanya tathmini na kuangalia kwa makini sana maeneo hayo ili tuweze kutekeleza hayo mnayotushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nyingine kwamba, Serikali itoe elimu ya kitaalam juu ya wafugaji ili kuongeza thamani ya mifugo kabla ya kwenda sokoni. Ni kweli hili jambo lazima tulifanye, kwa sababu kuendelea kuwa na mifugo mingi ambayo haina tija, kwa kweli siyo suala la wakati huu. Serikali inapaswa kuendelea kutoa msukumo kulingana na bajeti ambayo inapata, lakini pia suala la elimu ni muhimu sana kwa sababu tunaweza tukawa tunachunga tu, bila kujali kwamba hiyo mifugo inatuletea tija kiasi gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nyingine ya mwisho katika maoni ya Kamati kwamba, Serikali itoe elimu juu ya uvunaji wa mifugo ili kuongeza pato la mfugaji na Taifa kwa ujumla. Hili nalo nimeshalisemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kwa haraka haraka nieleze mambo ambayo yamesemwa pia na Kambi Rasmi ya Upinzani katika taarifa yao. Kulikuwa na hoja ya kuondoa umaskini katika jamii ya Wafugaji. Serikali itaendelea kutoa elimu kuhusu ufugaji wa kisasa na wa kibiashara, kwa sababu mifugo kwa kweli tukiiboresha ni biashara tosha sana na inaweza ikawaondolea Watanzania umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya umahaji wa mara kwa mara kwa wafugaji. Hili nalo nimelielezea sana kwamba, ni lazima tujenge miundombinu katika maeneo ya wafugaji ili waweze kukaa katika maeneo yao. Vilevile siyo kutenga tu maeneo ya wafugaji, lakini na kuweka Kanuni na Sheria za kuweza kusimamia maeneo yale, ili hawa sasa wasiendelee kuhamahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja pia ya kuhamasisha uanzishwaji wa vyama vya wafugaji na wafanyabiashara wa mifugo. Ni kweli kuna vyama vingi sana sasa vya wafugaji, wamekuja kuona kwamba, kwa kweli bila wao wenyewe wafugaji kuungana na kuwa na vyama vyao, sauti yao inaweza isisikike. Hivi ninavyozungumza, wapo huko juu wamekuja wafugaji na vyama. Niwapongeze kwamba, endeleeni kuungana kwa sababu umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja kwamba, bajeti zizingatie vipaumbele vya wafugaji. Uandaaji wa bajeti umekuwa ukizingatia vipaumbele vya wafugaji ambavyo ni pamoja na upatikanaji wa maji, malisho, minada, udhibiti wa magonjwa, elimu na kadhalika. Kwa hiyo, tutaendelea na elimu hii kulingana na bajeti tutakayokuwa tunapewa.

Kuwepo kwa mpango maalumu wa kupima na kumilikisha wafugaji maeneo ya ufugaji au maeneo yao, nilishalizungumzia jambo hili.

Migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, nimeshalielezea kwamba, Serikali imeandaa mkakati wa kuzuia migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji au watumiaji wengine wa ardhi ambao wameainisha kusimamia uboreshaji wa nyanda za malisho. Katika kuboresha nyanda za malisho, baadhi ya migogoro hii tunaweza tukaitatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaomba niishie hapo, Mheshimiwa mtoa hoja, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, atakuja kuhitimisha na kujibu hoja zilizosalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri mtoa hoja!

NAIBU WAZIRI MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. Ahsante.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu, kwa kuniweka na afya njema hadi jioni hii ya leo wakati tunahitimisha ajenda yetu ya Bajeti yetu ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Namshukuru pia Mheshimiwa Rais, kwa kuniteua kuongoza Wizara hii, mimi na Naibu wangu Mheshimiwa Kaika Saning'o Ole-Telele. Ni kweli kuwa ni Wizara yenye changamoto nyingi, lakini Mheshimiwa Rais amekuwa karibu na mimi katika kuniongoza ili kuona kwamba Wizara hii inaendelea vyema. Vilevile, nimshukuru sana Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kayanza Mizengo Pinda, kwa mwongozo wake muda wake muda wote ambao nimekuwa katika nafasi hii. Mara kwa mara tunapotekeleza kazi zetu, amekuwa ni mshauri wa karibu na hata baadhi ya mambo ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyazungumza hapa, tumekuwa tukishauriana naye na hata kushughulikia baadhi ya migogoro ambayo imejitokeza wakati sisi tumeteuliwa kama kule Kagera na Kilosa; kwa hiyo, ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Serikali inapokuwa inaongozwa kwa misingi ya Utawala Bora, huwezi ukawa unatoa maamuzi na kubadilisha Sheria kwa sababu tu mambo hayaendi vizuri. Kwa hiyo, baadhi ya mambo yanachukua muda kwa sababu ni lazima yaende kwa misingi ya Kisheria na Utawala Bora.

Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, mambo mengi ambayo mmesemea, yanafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sana niwashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao na ushauri wao, nje na ndani ya Bunge. Nilichojifunza ni kwamba, Sekta hizi za Mifugo na Uvuvi zinategemewa na watu wengi sana, ndiyo maana zimeweza kuchangiwa na watu wengi na ninaamini kama kungekuwa na muda, watu wangeweza kuzungumza zaidi. Hii maana yake ni kwamba, Watanzania wengi wana matumaini makubwa na Wabunge wangependa sana kuona kuna tija, kuna amani na kuna maendeleo katika sekta hizi. Kwa hiyoi, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge.

Vilevile, ningependa kuishukuru Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, chini ya Uongozi wa Profesa Peter Msolla. Mimi ninaiona Kamati hii kama ni mlezi, maana yake hata tulipokuwa tunajadili katika hatua mbalimbali za maandalizi ya bajeti hii, wametushauri vizuri sana, lakini hata maoni yao walipotoa hapa, ni ya kutuongoza ambako tunastahili kwenda. Kwa hiyo, ninawashukuru sana na ninaomba tuendelee kushirikiana. Bahati nzuri kwa sababu na mimi nilikuwa hukohuko, kimsingi, mawazo ya Kamati ni mawazo yangu vilevile; kwa hiyo, tutaenda pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile namshukuru Spika na Naibu Spika, kwa kazi nzuri wanayofanya. Kwa namna ya pekee, nikushukuru sana wewe Mwenyekiti, ambaye umesimamia mdahalo wote tangu jana hadi leo, kwa kweli umeongoza mjadala huu vizuri. Kwangu mimi ni kitu cha kihistoria, kwa sababu ni mara ya kwanza ninawasilisha bajeti kama Waziri, lakini umetuongoza vizuri na ninaomba nikuombee kwa Mwenyezi Mungu azidi kukujalia hekima, akili na nguvu ili Wananchi wako wa Ilala waendelee kukuunga mkono. *(Makofi)*

Nipende kuwashukuru Wadau wa Wizara yetu, watu wengi wamefika hapa tangu jana; wapo Wafugaji, Wavuvi, Wawakilishi wao, Wasindikaji, Wanataaluma na Wanachuo. Hii inamaanisha kwamba, kuna matumaini makubwa kwa uongozi na utendaji wa Wizara sasa. Nami ningeomba sana, ushirikiano huu tuuendeleze, kwa sababu Wizara haifanyi biashara, Wizara haifugi, Wizara haivui. Wavuvi ni Wananchi, umaarufu wa Wizara hii utategemea jinsi unavyowezesha Wafugaji, Wavuvi na Wasindikaji wafanye kazi yao vizuri. Kwa hiyo, ninaomba tuendelee kushirikiana vizuri, ninaamini kabisa na Watendaji wa Wizara kokote waliko, wanasikia msimamo wa Waziri; tunataka tuwezeshe Wafugaji, Wavuvi na Wasindikaji wafanye kazi yao vizuri.

Msimamo wangu, sitavumilia Mtendaji wa Wizara anayekwamisha au kucheleweshe wadau wetu kuwekeza au kufanya biashara katika Mifugo, Uvuvi na Mazao yake. Kama kuna Kanuni au Sheria hairuhusu, ni afadhali umpe majibu yule mwombaji kama ni hapana na umshauri hatua gani achukue, siyo kukaa na karatasi na maombi kwa wiki, kwa mwezi, bila kutoa majibu. Lazima biashara inazingatia muda.

Imani yangu kama ninyi Waheshimiwa Wabunge mlivyoonesha kwamba, Sekta hizi ni hazina. Kama Mheshimiwa Nchambi alivyosema, Mifugo ni Dhahabu inayotembea. Mmetoa mifano ya nchi nyingi, mmezungumzia Ethiopia, mmezungumzia Texas kule Marekani, lakini zipo nchi ndogo kama Botswana, uchumi wao umejengwa kwa sababu ya Mifugo, nchi ya Netherlands Mifugo ndiyo shughuli yote ya Uchumi na Nembo yao ya Taifa ni Mifugo. Kwa hiyo, ninaamini kwa hazina ambayo tunato Watanzania, inawezekana sana kubadilisha. Mimi niwaombe tu Wabunge, mimi na Naibu Waziri, tumeteuliwa miezi mitatu, minne iliyopita, bajeti tuliyoomba ni *modest,* tupitishieni tukatende. Bajeti hii itatusaidia kutengeneza misingi ya

kutengeneza bajeti kubwa safari ijayo. Kwa hiyo, ninaombna tushirikiane ili kuhakikisha bajeti hii inapita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninaomba niwashukuru sana wapigakura wangu wa Jimbo la Busega, ambao wameendelea kunitakia heri na kuniunga mkono wakati ninashughulikia masuala haya ya Kitaifa. Bahati nzuri hawakutaka kubaki nyuma, wakiwakilishwa na Mkuu wa Wilaya, kijana mchapa kazi, Paul Mzindakaya, ninawashukuru sana kwa kufika hapa pamoja na Mwenyekiti wa Halmashauri na Viongozi wangu wa Chama, Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na Vijana ambao wana matumaini makubwa; tutazidi kushirikiana, ninawashukuru sana, ninaomba tuendelee kusaidiana.

Kwa namna ya pekee pia naishukuru familia yangu, kwa umuhimu walionipatia wakati ninatekeleza majukumu yangu; Mama Mlengeya, yuko hapa, ninaomba tuendelee kushirikiana. Ninaamini familia yetu itaendelea kuwa imara wakati ninatimiza majukumu ya Kitaifa.

Michango yote ya Waheshimiwa Wabunge ni ya muhimu sana na hoja nyingi zilizotolewa kimsingi ninaafikiana nazo, kuna ushauri, mapendekezo na masuala ya ufafanuzi. Jinsi walivyotoa uzito, imenitia moyo kuwa kwa kweli sekta hizi ni muhimu. Wabunge ishirini na nne wamechangia kwa kuzungumza na Wabunge sitini, kwa kipindi hiki kifupi, wamechangia kwa maandishi. Mawaziri wawili, ninatambua Mheshimiwa Kaka yangu Wasira, Mheshimiwa Mary Nagu, ninawashukuru sana kwa mchango wa mawazo yenu, kunisaidia na kuniongoza jinsi mwelekeo wa Serikali ulivyo katika masuala haya. Vilevile hamkusahau kuwasemea Wananchi wenu, wapigakura wa Majimbo yenu; ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Ninapenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuwa, mimi na Naibu wangu, sisi ni wamoja wenu, sisi ni miongoni mwenu. Kama alivyosema Mheshimiwa Kangi Lugola, tulikuwa wote tunaimba kwaya moja na sasa niwahakikishie tu kwamba, tutaendelea kuiimba hiyo kwaya, msiwe na hofu.

Maswali yaliyoulizwa ni mengi, nitajaribu kujibu baadhi ya hoja, lakini kwa sababu muda una kikomo, basi zingine tutaziwasilisha kwa maandishi. Hoja ambazo sitazijibu hapa haimaanishi kuwa hazikuwa za muhimu, ninaomba muelewe kuwa tunayajali sana maoni yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na hoja za Kamati ya Kudumu ya Bunge, kama nilivyosema awali kwamba, kwa kweli hawa wametupa mwongozo tu kama wazazi na kimsingi hoja zote tunaafikiana nazo. Wamezungumzia habari ya upatikanaji wa fedha kwa bajeti yetu ya mwaka huu unaokwisha, lakini nipende kulijulisha Bunge kwamba, hisia zenu zimesikika na hivyo imewezesha kwa kipindi hiki kifupi tutapewa bilioni kumi nukta tano kutoka Hazina ili kutekeleza Miradi ya Maendeleo ambayo tulikuwa tumeipanga kwa mwa huu unaokamilika.

Ninashukuru sana na Mheshimiwa Waziri Mkuu, alisimamia kidete na ninamshukuru Waziri wa Fedha kwa kuona uwezekano huu unakamilika. Kamati vilevile imezungumzia utendaji hafifu wa *TAFIRI* kwa sababu hakuna rasilimali fedha. Haya yote ni kwa sababu fedha haikuwepo, lakini sasa tutaweza kuboresha kwa sababu kiasi hiki cha fedha zitakwenda kwenye maeneo hayo.

Wamezungumzia habari ya Serikali kutoa ruzuku katika Sekta za Mifugo na Uvuvi. Hili baadaye nitalirudia kwa sababu Wabunge wengi sana wamelizungumzia. Kimsingi, kwa mwaka 2013/2014 Serikali ilitenga shilingi bilioni moja nukta tisa kwa ajili ya ruzuku kwa wavuvi na wafugaji wa samaki. Kwa mwaka huu ambao tunaomba, tumetenga tena shilingi bilioni mbili nukta mbili kwa ruzuku za wavuvi. Katika randama, ukurasa wa 110 mpaka 111, tumeonesha

katika Mradi wa *EAAPP* jinsi wavuvi watakavyoguswa na Mradi huo kwa mfumo wa ruzuku na vifaa vingine.

Vilevile katika chanjo za mifugo, kimsingi, kuna magonjwa ambayo tunaita *public good,* kwa maana kuna umuhimu wa juu Kitaifa na Kimataifa; magonjwa hayo Serikali huwa inagharimia moja kwa moja. Kwa mfano, uogeshaji, Serikali inachangia 40% na mfugaji analipia 60% katika madawa hayo. Katika kumbukumbu inaonesha kuwa, katika mwaka 2006/2007 mpaka mwaka huu wa fedha, shilingi bilioni kumi na sita nukta nane zilishatumika kwa ajili ya kununulia lita milioni moja nukta moja za dawa za kuogeshea. Kwa hiyo, ninachopenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge ni kwamba, Serikali inazingatia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutokomeza uvuvi haramu; Wizara kwa kushirikiana Halmashauri imekuwa ikiunda na kuanzisha vikundi vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Hadi sasa kuna vikundi 721. Vilevile imeanzisha vituo vya doria 23 katika maeneo mbalimbali ya Maziwa kama Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Bahari ya Hindi. Kwa hiyo, vikundi vyote hivi vinasaidia kudhibiti. Nikiri kwamba, uwezo haujafikia kilele, ndiyo maana bado tunasikia matukio hayo. Katika mpango huu wa fedha tunaoomba, tunategemea vilevile tuimaraishe kwa kununua maboti katika vikosi hivi na kuviongezea watendaji ili viweze kufanya kazi yake vizuri. Kwa hiyo, Serikali inalizingatia na inachukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni mtambuka, kwa sababu wakati mwingine vyombo vinavyotumika kushambulia wavuvi vinakuwa ni silaha za kivita na wengine wanatoka nje ya mipaka ya nchi yetu. Kwa hiyo, hapa kuna suala la kiusalama linapaswa lihusishe Vyombo vya Usalama kama Jeshi la Ulinzi, Polisi, Uhamiaji na kadhalika. Tutaangalia Serikali namna tutakavyoweza kutengeneza ulinzi imara kwa kushirikisha taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kulinusuru Ziwa Tanganyika kutokana na kupungua kwa kina, hili litashughulikiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), ambao ndiyo wanaangalia. Kuna Mradi wa pamoja wa nchi zinazozunguka Bonde la Ziwa Tanganyika ambazo zinaangalia ustawi wa Ziwa Tanganyika. Uwepo utaratibu wa kuvua samaki kwa msimu na kusisitza uvuvi wa samaki wa biashara kwa msimu; hili ni wazo zuri tutaliangalia, kwa sababu linapaswa lishirikishe nchi zingine wadau, basi litaangaliwa kwa ujumla wake.

Uwekezaji katika Bahari Kuu na kujenga Viwanda vya kusindika Samaki: Wizara imeandaa andiko la ujenzi wa Bandari ya Uvuvi. Bahati nzuri, kwa bajeti ya mwaka huu ambao tunaendelea kuwa nao, baada ya kupewa hii bilioni kumi, milioni mia tatu zitaelekezwa katika maandalizi ya shughuli hiyo, kwa maana ya kuweka Mhandisi Mwelekezi ili tupate picha ya shughuli yote itakuwaje na wapi itafanyika, ili andiko likishakamilika, tuweze kujua gharama ni kiasi gani kwa ujumla wake na kupata wataalamu wa kufanya hiyo kazi. Kwa hiyo, wazo hilo ni la msingi sana.

Wamezungumzia habari ya *succession plan* ya watafiti; hili ni la msingi sana, tunazo Taasisi za Uvuvi na Utafiti wa Mifugo. Bahati nzuri na Waziri mwenzangu hapa, Mheshimiwa Celina Kombani, ambaye anaangalia masuala ya Utumishi wa Umma atakuwa amelisikia, lakini bado tuna watafiti ambao tayari wako kwenye mafunzo wa *Ph.D*, wa *Masters* na wa Shahada ya Kwanza ambao wapo katika ngazi mbalimbali za mafunzo ambao wakirudi wataingia kwenye shughuli; lakini ni kweli kuwa tuna upungufu mkubwa wa watafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo lilizungumzwa na Kamati ni habari ya minada na masoko ya mipakani kuboreshwa na ikiwezekana kuwekewa mizani. Hili linaendelea kutekelezwa sasa, ni kweli wafugaji wetu wanashindwa kupata bei stahili ya mifugo yao, kwa

sababu inauzwa kwa kuangalia kwa macho bila kujua uzito halisi. Sasa msisitizo wetu kila mnada unapofunguliwa, moja ya vifaa muhimu ni mizani. Kwa hiyo, sasa hivi kwenye minada kumi na mbili tuliyonayo, minada kumi na moja ina mizani. Tunaendelea kusisitiza Wananchi wenyewe Wafugaji wahakikishe hawauzi mifugo yao pembeni bila ya kuingiza minadani ili ipimwe wapate bei stahili. Zao la Ngozi, limezungumzwa sana na ninafahamu na wachangiaji wengine wamezungumza. Kimsingi, tunasisitiza sana uwekezaji na kutosafirisha ngozi ikiwa ghafi. Sasa hivi tunavyo viwanda saba vya kusindika ngozi, lakini viwanda vingi vinasindika kwenye hatua ile ya awali tu, ambayo ni *wet blue;* bado hatua hii haitupatii kama nchi ajira ya kutosha na mapato. Msisitizo wetu sasa ni kuvutia waende hatua zaidi ya usindikaji na hatimaye umaliziaji kabisa. Kuna viwanda viwili vipya vimeanza; ipo Shin'gwa Shinyanga, lakini ipo Meru kule Arusha inategemea kuanza hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kukemea tabia ya wafanyabiashara wa ngozi, wanaotorosha ngozi ghafi kupeleka nje ya nchi. Suala hili hatutaiivumilia kwa sababu linainyima nchi yetu mapato. Wabunge wote tulikuwa tunalalamika hapa habari ya fedha ndogo ya bajeti na wengine wachache wanajaribu kupiga chenga kulipa kodi. Siamini kama kuna mfanyabiashara anaweza kuwa mjanja kuliko Wabunge wote hapa. Kwa hiyo, naomba Wabunge tushirikiane kuwabaini hawa na kutafuta mikakati ya kuhakikisha tunawadhibiti.

Nimezungumza habari ya wavuvi na wafugaji kwa ujumla kujengewa uwezo. Kimsingi, hili tunaendelea nalo na tangu tumeingia tumekuwa na vikao na wadau mbalimbali ili tuhabarishane. Vilevile tuna Kitengo Maalum cha Habari, tunatoa majarida kwa ajili ya elimu ya uvuvi, ufugaji viumbe kwenye maji, ufugaji na unenepeshaji. Nitumie nafasi hii vilevile kuhamasisha wafugaji na wavuvi, elimu itafutwe, wasisubiri kufuatwa. Elimu inatafutwa ili waweze kwenda na wakati na waweze kunufaika vya kutosha kutokana na Sekta hizi za Uvuvi na Mifugo.

Nikija kwenye hoja za Kambi Rasmi ya Upinzani, kama nilivyosema awali, hoja zote kimsingi naafikiana nazo, ukiondoa tu maneno machache ya chokochoko ambayo sikuona kama yalikuwa na haja Mheshimiwa Rose Sukum Kamili kuyasema. Waziri mwenzangu, sikuona kama kulikuwa na ulazima kuyasema baadhi ya maneno, kwa sababu unapokuwa kiongozi wakati mwingine inabidi umezee, siyo kusema mpaka unamkwaza tena hata unayemshauri. Kwa hiyo, hoja ni zilezile, yeye tulikuwa pamoja kwenye Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, malalamiko yake ni hayo hayo ya kwangu, ni mfugaji lakini mimi vilevile pamoja na ufugaji natoka kwa wavuvi. Mimi natoka kandokando ya Ziwa Victoria, kwa hiyo, alivyosema Mheshimiwa Mangungu kwamba siwafahamu wavuvi siyo sahihi, tunategemea sana samaki kule kwetu Busega.

Amezungumzia habari ya ushuru wa mifugo ya ng'ombe. Kimsingi, ni sawa, mtu yoyote asingependa kulipa kodi, lakini tunapodai huduma za mifugo, tutazipataje kama hatuchangii hata kidogo! Wabunge wengi hapa wamechangia wanasema wafugaji siyo maskini, lakini tunajaribu kuwapandikiza mawazo ya kimaskini na wao wanataka kuyakubali kwamba ni maskini. Mtu ana ng'ombe elfu moja, ana ng'ombe mia tano au ana ng'ombe mia mbili unamwitaje maskini!

Mimi naomba sisi Viongozi, tusiwafanye wafugaji wetu wawe wanyonge na kulipa kodi ni wajibu ili uweze kupata huduma, ili waweze kuidai hiyo huduma kwa haki kwa sababu wamelipa. Kwa hiyo, hii kodi iliyopo, mimi nafikiri siyo kubwa sana ya kutisha, naomba tuendelee; ni shilingi elfu moja kwa ng'ombe kusafirisha, kwa mbuzi shilingi mia tano na kondoo. Sasa hii wakati thamani ya ng'ombe ni shilingi laki saba, sasa shilingi elfu moja jamani ndugu zangu naomba tuwajibike kwa manufaa ya nchi yetu. Tukiendelea kuwa wanyonge tunatafuta misaada nje, wakati sisi wenyewe hatujigharimii itakuwa ni hatari. *(Kicheko)*

Limezungumzea suala la msingi la utoaji wa mikopo na bima ya mifugo. Mpango huu uliwahi kujaribiwa haukufanikiwa sana miaka ya tisini, lakini sasa hivi fursa ipo, katika vikao vyangu nilivyokuwa nakutana na wadau nilikuwa nakaribisha Taasisi za Fedha na Taasisi za Bima. Vilevile tutaendelea kuwa na *forum* maalum na taasisi hizi ili tuone namna gani watajielekeza katika Sekta za Mifugo na Uvuvi, kwa sababu bila kuwawezesha kimitaji wafugaji na wavuvi, basi wao watakuwa watazamaji, kwa sababu shughuli kubwa haijengwi kwa fedha ya mfukoni, lazima waingie Taasisi za Fedha.

Kuna Dirisha la Kilimo kwenye Benki ya *TIB* na Benki ya Kilimo ipo katika hatua za kwanza, tunategemea kwamba, zote hizi zitasaidia kuwezesha upatikanaji wa mitaji. Imezungumzwa habari ya kutunga sheria inayotambua maeneo ya wafugaji; kimsingi, Mheshimiwa Waziri mwenzangu sheria hii ipo. Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo Namba 13 ya 2010 inatambua uwepo wa maeneo haya.

Tatizo ni kwamba, imekuwa haifahamiki kwa Wananchi wenyewe na sisi wenyewe labda katika Serikali hatujaisukuma sana. Sheria hii inaenda hatua ya juu zaidi, baada ya Wananchi kubaini maeneo na ya kapimwa, maana ili kuyabaini kuna ushirikishaji mwingi kuanzia ngazi ya Kijiji au Vijiji, Kata, Wilaya, yanatungiwa sheria ndogo. Inaenda hatua zaidi ambapo Waziri mwenye dhamana ya mifugo, anaweza kuyatangaza kama ni maeneo mahususi kwa ajili ya mifugo. Hapo yanapaswa kulindwa kama yanavyolindwa maeneo ya hifadhi na maeneo mengine. Kwa hiyo, nashukuru tu kwamba sasa tunapaswa tusiwe tunaishia kwenye utambuzi wa maeneo katika ngazi zile za chini, twende mpaka hatua ya juu zaidi.

Umezungumzia habari ya mkakati unaotumika kuzalisha Wataalamu wa Ugani. Utaalamu wa Ugani kwa upande wa mifugo unazidi kupanuka, kwa sababu mwaka 2012/2013, vyuo vyetu vilikuwa vinadahiri wanafunzi 949, mwaka huu tumedahiri wanafunzi 2,215. Bahati nzuri kuna vyuo vya binafsi vilevile ambavyo sasa vinadahiri wanafunzi 492. Kwa kweli mahitaji ni makubwa, hatujafikia lengo, lakini dhamira yetu ni kuongeza udahiri walau ufike 5,000. Tunao mpango maalum wa kuongeza udahiri huu, lakini tayari tumeshafungua vyuo viwili vipya kule Kikurula na Chuo cha Mabuki Misungwi, ambavyo navyo vimeanza. Kwa hiyo, nia ni kuendelea kuvipanua ili tuongeze udahili, lakini tunahamasisha hata sekta binafsi iwekeze katika maeneo hayo.

Kwa upande wa Wagani wa Uvuvi, *FETA*, walikuwa 943 mwaka 2012/2013, sasa wamefika 1,073, lakini lengo ni kufikia 1,500.

Umezungumzia habari ya teknolojia duni ya kukaushia samaki. Teknolojia hii inaendelea kufundishwa, tayari kwa mfano, kando ya Ziwa Tanganyika, mwaka huu vinatengenezwa vichanja vinne kwa ajili ya kufundisha maarifa ya kukausha dagaa ili wasiwe na mchanga, wapoteze ubora kwa sababu ya kutokaushwa vizuri. Kwa hiyo, mipango hii inaendelea hata vilevile kwa Ziwa victoria na Bahari ya Hindi.

Umezungumzia habari ya fedha za Miradi ya Idara ya Sera ya Mipango. Hili nafikiri Mheshimiwa Waziri mwenzangu hakuona vizuri, kwa sababu katika Idara ya Sera na Mipango, Kifungu 1003, yale matumizi ya shilingi milioni 59 ni kwa ajili ya programu ya kuendeleza sekta ndani ya Sekta ya Kilimo, lakini mifugo, ambayo inahusu afya na maji kwa mifugo na binadamu, ambacho kinatekelezwa katika Wilaya za Kondoa, Kiteto, Bahi na Chamwino. Hii ni kutokana na ufadhili kutoka Serikali ya Ubilgiji ndani ya Mpango wa Sdp. Shilingi milioni 85 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Idara ya Sera na Mipango. Kwa hiyo, hivi haviingiliani, kwa sababu unapoandika Mradi, Mradi unakuwa na ujumla wake, utakuwa na safari utahitaji mafuta na mitambo ya kudurufu. Kwa hiyo, Mradi hauwezi ukajidondosha bila ya kuwa na vitu vya kuuwezesha uwepo. Kwa hiyo, hayo uliyoyaona ni sehemu ya ukamilishaji wa Mradi wenyewe.

Umezungumza habari ya fedha za utafiti, mafunzo na ugani, kifungu 1004. Mfumo wa utekelezaji Miradi ya Maendeleo unajumuisha matumizi yote kama nilivyosema, nayo majibu yake yanafanana vilevile. Kwa hiyo, naomba Waziri mwenzangu usichanganye na uelewe kabisa kwamba, Mradi unakua, unahitaji vitu vingine vya kuuwezesha ukamilike kama mafuta ambayo unayaona kama ni ya kawaida, lakini ni sehemu ya Mradi.

Umezungumzia eneo linalotosha mifugo yote iliyopo nchini. Kufuatana na Sensa ya Mifugo ya Mwaka 2012, Tanzania inakadiriwa kuwa na *livestock units* milioni 25. Ambapo kila *livestock unit* za nchi za *tropic,* inahitaji takribani hekta mbili kwa mwaka. Hivyo, eneo linalotosha mifugo iliyopo ni hekta milioni 50. Jumla ya hekta milioni 60 ambayo inafaa kwa malisho, inajumuisha maeneo ya hifadhi na misitu. Kwa hiyo, siyo kwamba basi hizo milioni 60 zote zinaachiwa mifugo. Sasa kama Taifa lazima tujue kuipangilia ardhi yetu, hatuwezi tukasema Taifa lote litafuga mifugo, haliwezi Taifa lote likawa hifadhi na misitu na haliwezi Taifa lote likawa kilimo. Mambo yote haya yanategemeana, inabidi tuitumie vizuri ardhi hii ya mifugo ili iweze kutosha. Kiutaalamu unaweza kuongeza uwezo *(carrying capacity)* inaweza ikaongezeka kama yale maeneo yataboreshwa kwa kupanda malisho, kwa kuweka miundombinu ya maji na kadhalika.

Sasa hii ndiyo elimu ambayo tunahitaji kuitoa kwa Wananchi wetu na ndiyo maana tuna vituo vya kuzalisha mbegu za malisho ili Wananchi waweze kupata na baadaye wajifunze vilevile namna ya kuboresha maeneo waliyonayo. *(Makofi)*

Suala la *NARCO* umelizungumza lakini limezungumzwa na Wabunge wengine wengi; *specifically,* umetaka kufahamu wawekezaji wangapi waligaiwa maeneo; ni wawekezaji 105 na takwimu yao ipo kwenye Tovuti ya *NARCO* ambayo ni *www.narco.co.tz* na Tovuti ya Wizara ambayo ni *mifugouvuvi.go.tz.*

Nipende kulisemea hili kwamba, kati ya waliogawiwa kuna ambao wanafanya vizuri na lazima tuwaheshimu, tuwatambue, kwa sababu hatutaki kuwatia hofu wawekezaji wazawa na hata wa nje. Tunapoitisha wawekezaji tunaitisha kotekote, sasa ambao wamewekeza lazima tuwaheshimu, lakini ambao hawafanyi vizuri, nitaendelea kurejea kauli yangu kwamba, maeneo haya tutayaangalia ili yaweze kutumika vizuri.

NARCO inaendelea kukaribisha wawekezaji, naomba Watanzania hata hivi vitaru 105 vilipotangazwa kuna wengine waliogopa kuomba wakafikiri sijui ni akina nani ndiyo wenye sifa. Watanzania tuwe mashujaa, *NARCO* inajitangaza inatafuta wawekezaji *serious*, waje waongee nao, Meneja yupo hapa. Sasa asije akaja Mzungu akaongea na *NARCO* akapewa, tukaanza tena kulalamika kwamba ooh wanapewa wageni tu, kumbe Watanzania tupo. Naomba tuwe mashujaa na mimi naitangaza *NARCO* kwa sababu kazi yetu ni kufanya biashara. *(Makofi)*

Uvuvi haramu na biashara ya magendo ya samaki na mazao yake, hili nimelizungumza kama lilivyozungumzwa na Kamati; mwelekeo ni uleule vitengo vyetu tunaendelea kuviimarisha. Kuna Kitengo cha *MPRU*, Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu, ambayo nayo hata sheria yake tunaipitia upya, ili ipewe mamlaka zaidi na iweze kuangalia hata maeneo kwenye maji baridi.

Mapato katika Bahari Kuu, kuimarisha ukusanyaji wa mapato kutoka Bahari Kuu, kujenga bandari, viwanda na huduma nyinginezo, ni suala la msingi. Nimelizungumza kwamba, katika fedha tulizopewa, hili nalo tutaliangalia ili tuongeze uwezo wa kupata. Kwa kweli tukipata bandari ya uvuvi, itakuwa na mchango mkubwa sana katika mapato ya uvuvi. Nafikiri hata Dkt. Mpango amesikia kilio cha Wabunge na Wabunge hawa ni Wasomi na Wataalamu, wanajua umuhimu. *(Makofi)*

Fedha za kutosha kutoa elimu kwa Maafisa Uvuvi na kutoa elimu kwa wavuvi; kimsingi, katika bajeti yetu mkitupitishia hili eneo limezingatiwa sana, naomba tu Waziri mwenzangu uniunge mkono tupitishe halafu mengine tushauriane wakati tunaendelea kutekeleza. *(Makofi)*

Ufugaji wa samaki ni eneo muhimu sana, kwa kweli kutokana na idadi kubwa ya wavuvi kwenye maji ya asili, sasa namna nyingine ya kutoka hapo ni kuimarisha ufugaji wa samaki. Sisi kujielekeza kwa hilo, tumeunda Idara Maalum, ina Mkurugenzi na Wakurugenzi Wasaidizi na tumepanga bajeti kwa mwaka huu. Bahati nzuri hata kwa hii tuliyoongezewa sasa kuna Miradi na hata kule Lindi kuna kituo kinaanzishwa, Luhila, ambacho kinaendelea kukamilishwa kwa ajili ya kutotolesha vifaranga vya samaki. Kwa hiyo, nafikiri mawazo yenu yote mazuri haya yataimarika tu kama bajeti tutaipitisha ili tukatende kazi. *(Makofi)*

Wabunge wengi wameweka msisitizo katika haya mengi yaliyozungumzwa kwenye Kamati na Waziri mwenzangu. Migogoro ya Wakulima na Wafugaji imezungumzwa na jinsi hii sheria inavyosaidia. Sheria ya Utambuzi, Ufuatiliaji na Usajili wa Mifugo ilipitishwa mwaka 2010, sasa ipo kwenye hatua za majaribio katika Wilaya za Kibaha, Bagamoyo na Muheza. Nina hakika baada ya zoezi hili kwa sababu tulipata fedha kidogo kutoka *FAO*, kwenye bajeti hii tunakusudia kama itapita, mfumo wa *data bank* tayari umeshakamilika ndani ya Wizara ili tuweze kui-*roll-out* sasa kwenye maeneo mengi zaidi iweze kutangulia. Nawashukuru sana Wabunge wote waliochangia kwenye hili.

Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia habari ya ufugaji wa kuku. Nakumbuka Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa na wengine wamezungumzia suala hili. Mimi sipendi kusema kwamba, huu ni Mradi wa Wanawake. Ufugaji kuku ni tasnia imara kabisa na kubwa, inatajirisha watu. Naomba Wabunge wenzangu tuondokane na hii habari ya kesema tuondoe umaskini, ni kutajirika, tuzungumze kutajirika. Unapoondoa umaskini unafanya kidogo kidogo, tuongee habari ya kufanya kwa hatua kubwa, tuweke mashamba makubwa.

Kuku wa kienyeji hata ukianza na watu, katika kipindi cha mwaka mmoja utakuwa na kuku 1,000. Mwaka mmoja na nusu utakuwa na *millions* za kuku. Sasa kusema kwamba hii ni biashara ya wanyonge, siyo sahihi; naomba tufikirie kwa mtazamo chanya zaidi na kwamba inaweza kubadilisha.

Nimezungumza habari ya Zao la Ngozi na Wabunge mmelizungumzia hili. Vilevile kuna hili la unenepeshaji wa mifugo, ambalo Mheshimiwa Mnyika amelizungumza na ubinafsishaji wa Kiwanda cha Maziwa Ubungo. Kwanza, la Kiwanda cha Maziwa ni kwamba, hili lipo kwenye *CHC*. Sisi kama Wizara, Bodi ya Maziwa ilishawaandikia *CHC* ili watupe mwelekeo, kwa sababu tunadhani tuna shughuli ya kufanya na hiki kiwanda. Tunataka tuvutie uwekezaji mkubwa, kwa hiyo, tunasubiri majibu. *(Makofi)*

Suala la unenepeshaji mifugo na hii natoa wito kwa wafugaji wote, hii ndiyo namna ambayo inaweza ikabadilisha wafugaji wetu kama Wabunge wengi walivyochangia. Wilaya ya Longido wamefanikiwa sana. Nafahamu hata kwangu Busega wanafanya, Mwanza wanafanya, lakini Longido wamefanikiwa sana hata kubadilisha *core* safu ya ng'ombe wao. Longido wanafikia hata uzito wa kilo 1,000 na kuendelea. Kwa wafugaji wa kawaida, naomba hata ndugu zangu wengine wa jamii za Wafugaji na Wafugaji wengine binafsi, tubadilishe. Kwa kweli hatutaendelea na utamaduni wa kuhamahama, kwa sababu tunaweza tukajiridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, ninawaahidi Waheshimiwa Wajumbe kwamba, majibu yote tutayatoa kwa maandishi, wote mtapata. Ninawashukuru sana, naomba

mtuunge mkono tukatende kazi. Dhamira tunayo, nguvu tunazo, ninao wataalam tele wa kunisaidia kazi. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo la wageni; tunao wanafunzi 26 kutoka Chuo cha Mifugo cha Mpwapwa na Morogoro, karibuni sana.

Wanafunzi 60 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma na Mwanafunzi mwenzenu Mheshimiwa Juma Nkamia, Naibu Waziri wa Habari na Vijana yupo humu ndani; karibuni sana mmependeza. *(Makofi)*

Katibu, hatua inayofuata!

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 96 – Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi

Kif. 1001 - *Administration and HR Management* … … .... *Shs*. 4,767,936,400

MWENYEKITI: Vipi jamani? Waheshimiwa Wabunge, kama kawaida nina majina ya wachangiaji kutoka kwenye Vyama husika, tunaanza na Mheshimiwa Dunstan Kitandula, hayupo, Mheshimiwa Capt. John Chiligati!

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu wa maandishi, nilimkumbusha Naibu Waziri kwamba, wiki iliyokwisha tulipokea maandamano ya wajasiriamali wanaouza chakula cha mifugo Kenya. Kwanza, niseme sikusudii kushika mshahara wa mtani wangu, nataka ufafanuzi tu.

Tulipowapokea, Mheshimiwa Naibu Waziri aliwapeleka ofisini kwake, wakawa na malamiko kwamba, wanapopeleka Kenya pumba za mahindi na pumba za mpunga na mashudu ya alizeti, awali walikuwa wanatozwa shilingi elfu kumi kwa lori. Sasa mwezi uliopita, wakakuta ile ada ya kibali imebadilika imekuwa shilingi elfu kumi kwa tani, kwa hiyo, lori la tani 30 ambalo awali walikuwa wanavusha kwa ada ya shilingi elfu kumi, sasa wanatakiwa watoe shilingi laki tatu; jambo ambalo limewafanya biashara inakuwa ngumu, lile soko walilolipata sasa linapotea, wenzao wa Uganda na Rwanda sasa ndiyo wananufaika na lile soko. Sasa wameomba Wizara itazame upya hiyo ada ya kibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua je, Wizara malalamiko haya ya Wajasiriamali hawa ambao walishajipatia soko kule Kenya wamelifanyia kazi vipi; kwa sababu lengo la Serikali ni kuwawezesha Watanzania wauze nje, lengo la Serikali siyo kuwawekea vizingiti ili wasiuze nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka maelezo.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anachokisema Mheshimiwa Capt. Chiligati na hata hivyo walishaleta barua ya maandishi. Naibu Waziri alikutana nao. Tunapokea hoja zao, lakini tunakubali kwamba tutaangalia tuone

namna gani. Vilevile ni muhimu watambue kuwa shilingi elfu kumi kwa uzito wote haikuwa sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaliangalia suala hili.

MHE. BEATRICE M. SHELUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilitamani sana nichangie lakini kwa kweli nafasi haikuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ambayo yanaathirika sana katika migogoro ya Wakulima na Wafugaji mojawapo ni Kilindi. Kabla sijasema hoja yangu, napenda niishukuru Serikali kupitia Wizara hii ya Mifugo, kwa kweli wamekuwa wakitupa misaada mbalimbali na hata kwenye Hotuba ya Waziri safari hii amezungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo nyuma miaka takribani kumi na zaidi, kulikuwa na Mradi wa *Handeni Integrated Approach Program (HIAP)*. Huu mradi ulitenganisha maeneo ya malisho na maeneo ya wakulima pamoja na njia. Mradi huu utazingatia kwamba ni miaka mingi, waliokuwa watoto na wajukuu, sasa hivi nao wana mifugo yao, waliokuwa wakulima nao watoto wao wameshakuwa wakubwa na wajukuu wameshakuwa wakubwa nao wanahitaji maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ni mengi sana, hata hivi tunavyoongea migogoro inaendelea kule ya kutisha, mingine ambayo inagharimu hata maisha. Je, Waziri au Naibu Waziri wataniahidi kwamba baada ya Bunge hili la Bajeti, tutaongozana mkono kwa mkono twende kule waweze kuongea na Wananchi na kutatua matatizo yao wakiwa kule?

MWENYEKITI: Jibu sahihi ndiyo au hapana basi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo tutafuatana.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kasma hiyo hiyo.

Kwanza, niseme kwamba, nimefurahishwa sana na ile Sera ya Kunenepesha, basi Waziri ujitahidi utupatie hata nafasi ya kuwakopesha hawa vijana ili hiyo Sera iweze kuendelea. Kilichonifanya nisimame ni migogoro kati ya Wafugaji na Mapori Tengefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri mwenyewe anatoka Lamadi, kweli kuna mantiki gani watu ambao wapo Nyamikoma hawawezi kuchunga karibu na Kijereshi, watu ambao wapo Ng'wang'wali! Mimi nilifikiri kwamba, Mheshimiwa Ole Telele baada ya kutoka Ngorongoro angeweza kutueleza vizuri utaratibu wa Ngorongoro unafanyikaje na kama Ngorongoro imeweza kufanikiwa kwa nini Mapori Tengefu karibu na Rung'wa, karibu na Bukundi Wilaya ya Meatu, karibu na kwako pale utaratibu huu wa kuchunga wanyama pamoja na ng'ombe usifanikiwe? Pawe na sheria, hakuna kuua mnyama, hakuna kukata miti na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea hili jambo angalau lingejibiwa. Sasa kama hatanijibu itabidi nitumie shilingi ili nitoe maelezo zaidi. Ahsante sana.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa maoni ya Mheshimiwa Cheyo. Tumeshalizungumza suala hili chini ya Uongozi wa Waziri Mkuu, Wizara zetu za Kilimo, Mifugo na Maji pamoja na Maliasili na Utalii na TAMISEMI na Ardhi. Moja ya maazimio ambayo tuliafikiana ni kwamba, yataangaliwa baadhi ya maeneo ya hifadhi ambayo yanaweza kuachiwa kwa ajili ya ufugaji. Haya yatakapoachiwa, yatakuwa ni

maalum kwa ajili ya ufugaji, ndiyo maana baadhi ya maeneo tutaya-*gazette* kwa ajili ya ufugaji.

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka mwaka jana katika Wizara hii hii na bajeti yake, nilitaka kuondoa shilingi ili fedha ziongezwe katika Miradi ya Maendeleo ya Wizara hii. Mheshimiwa Spika, alikuwepo akasaidia hili kwa kusema kwamba, Sanya anachotaka ni *commitment* ya Serikali kuhusu hizi fedha. Alikuwepo Mheshimiwa Sitta, akikaimu nafasi ya Waziri Mkuu, akatoa ahadi ya kwamba, zitaongezwa bilioni 20 au hata na ziada ili Wizara hii iweze kupata fedha za kutosha kwa vile ina sekta mbili muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake, shilingi bilioni 20 katika Kitabu hiki cha Hotuba ya Waziri ya mwaka huu, zimeonekana kwamba zipo, pamoja na zile za mwanzo ambazo ziliwekwa kwamba ni bilioni 8.9, lakini zilizotolewa fedha za maendeleo ni bilioni 3.8. Ina maana bilioni 25 hazikupatikana hadi tunakwenda kwenye bajeti ya mwaka huu.

Mwaka huu Waziri huyu anaomba tena fedha bilioni 25 za kuendeleza Miradi yake ya Maendeleo katika Wizara hii. Hii inaonekana kwamba, kama vile anaomba tena zile fedha ambazo mwaka jana hazikutolewa. Ninaomba nipate ufafanuzi wa kutosha kwa hili na nina dhamira ya kuondosha shilingi iwapo nitapata maelezo ambayo hayatatosheleza kiu yangu ya kujua hizi fedha kama zitapatikana kabla ya bajeti hii zitatolewa au zitajumlishwa na hiyo 25 ziwe 45 kwa sababu tusiifanyie Wizara hii mchezo; ni Wizara muhimu yenye sekta mbili muhimu kwa nchi yetu ya Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Wizara hii iliongezewa bilioni 20 na katika kikao ambacho Wizara hii ilikaa na Kamati ya Bajeti na Wizara ya Fedha, ilikubaliwa Miradi 11 ambayo ingegharimiwa na pesa hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hadi hivi sasa katika pesa za maendeleo kwa Wizara hii zilizotoka ni bilioni 4.4 tu, pesa za ndani ni bilioni 2.2 na pesa za nje ni bilioni 2.2. Katika hiyo Miradi 11, juzi tumekaa Wizara ya Fedha, Wizara ya Mifugo na Kamati ya Kilimo, chini ya Uenyekiti wa Profesa Msolla na kwenye kikao hicho tumefanya maamuzi ya haraka, kwa sababu katika mazingira ya sasa hivi zipo Wizara nyingi ambazo bado hazijakamilishiwa fedha zake. Tulichofanya, tumekubaliana kwamba katika Miradi hiyo tisa, kama utaniruhusu kama alivyosema Waziri wa kuhitimisha hoja yake, tumekubaliana kabla ya mwisho wa mwaka tutoe bilioni 10.5 kama ifuatavyo:-

Bilioni moja kati ya bilioni tatu mradi wa kuiwezesha *NARCO* kukamilisha machinjio ya Ruvu; bilioni moja na nusu kati ya bilioni 3.5 kuimarisha miundombinu ya mifugo kwenye baadhi ya Wilaya na Halmashauri; na bilioni 2.3, kuendeleza mfumo wa ruzuku kwa wafugaji kwa kununua chanjo. Hizi ndiyo ilikuwa bajeti ya mwaka mzima, tumekubaliana zitoke zote kwa sababu ya umuhimu wa chanjo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mradi wa kuendeleza mashine zile za Sao Hill na Katavi, katika bilioni 1.2 tumetoa milioni 400. Mradi mwingine ni kudhibiti uvuvi haramu, ambapo pesa zilizokuwemo ilikuwa bilioni 2.8, tumekubaliana zitoke zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi mwingine ni kuweka miundombinu ya ufugaji wa viumbe kwenye maji kwa kujenga vituo vya kuzalisha vifaranga vya samaki. Kuna baadhi ya maeneo

ndani na nje, kwa maana ya Pwani na Bara; Kigoma, Mtwara, Igunga, tumekubaliana milioni 950 zitoke zote. Mradi mwingine ambao tumekubaliana kwamba tuutimize tutafute pesa ni kwa ajili ya wanafunzi kwenye Vyuo vya Ugani wa masuala ya uvuvi na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hizo bilioni 20, tumekubaliana kwamba, kabla ya mwisho wa mwaka zitoke bilioni 10.5; na makubaliano hayo baada ya kutoka hapo mimi na Waziri wa Mifugo, tumekwenda kwa Waziri Mkuu na tumeafikiana kwamba, Serikali itafanya kila linalowezekana ili kabla ya mwisho wa mwaka hizo bilioni 10.5 zitoke.

MHE. MOHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi bado ninaona kuna utata; haiwezekani kwa kipindi cha mwaka mzima zikatoka bilioni 3.8 halafu ukatuambia kwamba, kipindi cha mwaka mmoja yaani mwaka huu mwisho wa mwaka kwa mwezi mmoja zipatikane bilioni kumi, nina wasiwasi na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, hata hizi *figure* alizozitoa kwa matumizi yaliyotoka ni tofauti na *figure* zilizomo ndani ya kitabu. Sasa Mheshimiwa Waziri kama anatuambia kwamba, leo kuna upungufu wa bilioni zaidi ya 20 *plus,* halafu kwa kipindi cha mwezi mmoja kuna ongezeko la bilioni kumi zitapatikana zifidie hii bajeti ya mwaka jana ili tupitishe mwaka huu, itakuwa tunawadanganya Wananchi na tunajidanganya na wenyewe. Kwa hiyo, mimi bado hili lisijatosheka nalo na ninaomba hii shilingi niiondoe ili niwape wenzangu wazidi kuchangia katika hoja hii tupate ufumbuzi wa kina utakaoboresha Wizara hii yenye sekta mbili. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sasa Mheshimiwa Sanya, *with due respect*, unayo hoja ya msingi. Serikali inasema itaongeza *ten billion shillings* za Kitanzania au siyo? Wangesema wanatia bilioni 20 hoja yako ingekuwa hivyo hivyo kwa nini msizitoe siku zote za nyuma. Bajeti hii ina muda wake, mwisho ni tarehe 30 Juni, wanao muda bado wa kuzitoa hizi pesa kuzirudisha kwenye Wizara na ndiyo mpango wa Serikali wanaoutaka.

Sasa ukiendelea kutoa shilingi, mimi ninakushauri, hoja yako hii itakuwa haina nguvu; warudishie shilingi yao, shirikiana na Meza, shirikiana na Kamati ya Bajeti, tuwabane warudishe hii pesa, Wananchi tupate maendeleo tunayoyataka. *(Makofi)*

MHE. MOHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa maelekezo yako. Ninakubali kurejesha shilingi kwa sababu tumezoea kudanganywa na hizi Wizara. Endeleeni kutudanganya na tusizipate hizi pesa, kwa sababu huo mwezi mmoja, mimi nina uhakika hapa hizi hazitapatikana, lakini narejesha shilingi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana na hoja yako sasa ni *valid* na tunaifuatilia wote kwa pamoja, Bunge zima litaifuatilia.

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninachangia mchana nilitaka kujua kutoka kwa Waziri, mikakati mbalimbali katika kushughulikia suala la migogoro ya Wakulima na Wafugaji. Nijielekeza katika eneo moja tu, nilitaka kujua nini mipango ya Serikali katika kuchimba mabwawa na majosho?

Katika hili naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri kuwa sitaki kuchukua shilingi yake, nataka nipate mipango na ikiwezekana tushirikiane na nitamwongezea shilingi katika kutatua tatizo hili.

MWENYEKITI: Sijakusikia unataka kutoa au?

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, sitoi shilingi.

MWENYEKITI: *Okay,* Mheshimiwa Waziri, majibu!

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa hoja ya Mheshimiwa Kalogeris. Alishaniambia hofu yake na matarajio yake kwenye eneo lake, kwa kweli shida yake ni ya Taifa zima kwenye jamii zilizo na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti yetu ambayo tumeomba, tunategemea kama itapitishwa kutakuwa na *component* kubwa ya kuchimba mabwawa kwa ajili ya mifugo na visima virefu kwa ajili ya binadamu na mifugo. Kwa ujumla, fedha hiyo haitatosha mahitaji kwa maeneo yote. Sisi tukipewa muda tuna mpango wa kuangalia namna nyingine ya kuanzisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mahitaji ya mifugo kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi naomba atuunge mkono tupitishe halafu ituwezeshe tukakaye na kutafuta namna tutakavyoshughulikia suala la mabwawa kwa nchi yote.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Msigwa!

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mojawapo ya majukumu ya Wizara hii ni pamoja na kupanga na kusimamia matumizi ya ardhi kwa ajili ya mifugo endelevu. Wizara hii imekuwa ni moja ya Wizara ambazo zimekuwa na shida kwa wananchi hasa wafugaji na wakulima na matokeo yake ni mabadiliko ya Baraza la Mawaziri ambalo lilitokea mwaka jana.

Sasa nilitaka kujua baada ya mabadiliko yale ya Wizara, ni *commitment* gani ambayo Wizara inayo ya kuhakikisha inatoa matatizo haya kati ya wafugaji na wakulima ambayo yameleta matatizo makubwa sana kwa wananchi na ambayo yalisababisha Waziri aliyekuwepo na wengine waondoke? Na nilitaka *commitment* ya Wizara ni kitu gani sasa hivi mmepanga kuhakikisha matatizo haya yanaisha na lini tutaachana na tatizo hili kwamba wakulima watakaa kwa raha na wafugaji watakaa kwa raha? Kama nisipopata maelezo ya kutosha, nakusudia kutoa shilingi ili nipate *commitment* ya Wizara hii. Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *Commitment* ya Wizara ni kwamba kwanza imeshaanza kuchukua hatua, tumeshaitisha Vikao na wadau wafugaji, tulikaa hapa Dodoma, Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji walikuwepo. Tuliongea masuala ya msingi likiwemo hili la migogoro.

Moja ya maazimio tuliyokubaliana ni pamoja na kufikisha kilio hiki kwa ngazi za juu za Serikali kwa maana ya Waziri Mkuu na Mheshimiwa Rais. Kazi hiyo tayari tumeshaifanya na maagizo tumeshapewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba baada ya Bunge hili tutakuwa na kikao maalum ambacho kitashughulikia masuala ya migogoro ya wafugaji na wakulima na kuangalia changamoto zote zinazohusu sekta hii.

Sasa mimi nafikiri wewe tupe muda. Sisi tuna miezi minne tu. Tupe muda nakuhakikisha utaona matokeo.

MWENYEKITI: Kwa nini usikutane nao kabla Bunge halijakwisha? Waziri wa Kilimo hapo kalazimisha kukutana na watu wa pamba, na wewe kutana na hawa wakulima pamoja na wafugaji. *This is a burning issue*. Subiri, ngoja sijamaliza. Hii ni *burning issue* sana, na haiwezekani kila siku inakuwa *postponed, postponed, postponed!*

Alisema Mwalimu kama utakumbuka, "*Mubhisabhisa obhurweri kiriro kiramubhura*". Ee, mficha ficha maradhi mauti yatamuumbua. *(Kicheko)*

Wapeni muda, wambieni kabla ya bajeti haijakwisha tutakaa na ninyi kuli-*solve* hili suala *once and for all*, liishe. Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazingatia ushauri wako.

MWENYEKITI: Lini unakaa nao? Waambie kabla ya bajeti kuisha.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Kabla ya mwisho wa bajeti.

MWENYEKITI: *Specific* au unaondoka kesho?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Ni vigumu kuisema sasa hivi hapa, inahitaji muda.

MWENYEKITI: Basi Mheshimiwa Msigwa, Waziri atakaa na ninyi.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijaridhika bado.

MWENYEKITI: Subiri, ngoja, Mheshimiwa Lukuvi!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kukukumbusha kama Spika wa Bunge hili kwamba jambo hili analouliza Mheshimiwa Msigwa ndilo lililosababisha Bunge likaipa kazi Kamati kutokana na Azimio. Liko Azimio la Bunge linalohusiana na migogoro hii na ndiyo maana Bunge hili likaagiza likaunda Kamati chini ya Mheshimiwa Sendeka na Kamati ile wamekaa kule Kunduchi miezi kadhaa na naamini ripoti hiyo ambayo inazungumzia maalum kwa jambo hili, wenzetu wa Kamati wale wameshakabidhi kwa Spika na itakuja hapa Bungeni na naamini kabisa hadidu za rejea tulizowapa ukikumbuka kwamba waje na *solution* ya kukomesha kabisa mapambano haya kati ya wafugaji na wakulima. Kwa hiyo, ni vizuri tukakumbuka kwamba tayari tunalo agizo la Bunge Zima ambalo tumewapa wenzetu. *(Makofi)*

Mimi nilikuwa naomba Mheshimiwa Msigwa akubali, kwa sababu taarifa ya Kamati ile mimi naamini iko tayari. Wajumbe wa Kamati wako hapa na moja ya hadidu za rejea ni zile. Kwa hiyo, leo ukimtaka Waziri aseme tofauti na alishaitwa na kuhojiwa na ile Kamati, alishasema maneno haya na maelezo ya Serikali yamo kwenye Kamati. Kwa hiyo, tungesubiri wale wenzetu tuliowateua ili waje walete maagizo yale kujibu Azimio la Bunge juu ya jambo hili. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa, nafikiri *the way forward* ni hiyo.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani hapo sikubaliani, kwa sababu Kamati ya Mheshimiwa Ole-Sendeka ni Kamati nyingine ambayo haizuii utendaji wa Wizara wa siku kwa siku. Nategemea Wizara ije na utendaji wake na *plan* yake ya siku kwa siku, hivi ni vitu viwili tofauti. Ndugu zangu Wabunge tukumbuke mwaka jana hapa tulikuwa wakali

kama pilipili wananchi wa Tanzania wengi walikufa, mifugo iliuwawa, wote hapa Wizara zikabadilika. Tusianze na *business as usual.*

Ndugu zangu najua kweli mna miezi mine, lakini itakuwa ni *business as usual.* Leo tukiulizana hapa, baada ya Mheshimiwa Mathayo kuondoka, Mheshimiwa Kagasheki kuondoka, Mheshimiwa Nchimbi kuondoka na yule wa Zanzibar kuondoka, kitu gani tunaona kimebadilika katika Wizara hizo, kama hatutawa-*task* hawa watu kwa kazi walizofanya? Baada ya Mheshimiwa Nahodha kuondoka, yaani nikienda leo kwenye ofisi hiyo nakuta tofauti gani?

Tunachosema Wizara hii imekuwa na matatizo, tunataka hawa watu waoneshe *commitment*. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu katika ripoti yao ukiangalia *land* ambayo wameigawa sasa hivi ni hekta milioni 1.3 ambayo kimsingi ng'ombe milioni 21 tulionao wanatosha hekta milioni 50.4. Lakini kwa kitaalam wanasema ng'ombe mmoja anakula kati ekari 6 mpaka 8 kwa mwaka.

Sasa ukiangalia hekta wanazosema wanaandaa kutenga kwa mwaka ambazo wamezitenga sasa hivi ni hekta ambazo zinatosha karibu ng'ombe 500. Sasa tukiendelea hivi na ng'ombe tulionao hawa itachukua miaka mingapi kutenga hizo hekta kama tutakuja na majibu haya madogo madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema niwaombe Wabunge hebu mniunge mkono tuijadili hoja kwa sababu hili ni tatizo kubwa ambalo lilisababisha wananchi wafe, tukaunda Tume na watu wakapata matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujadili tupate *commitment* ya Serikali ni namna gani tutaliondoa hili tatizo, wafugaji na wakulima watakaa kwa raha. Kwa sababu hii Wizara wamekuja tu na takwimu hapa wanatutajia ng'ombe wangapi…

MWENYEKITI: Sema sasa unatoa shilingi, maana mpaka sasa hivi…

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi.

MWENYEKITI: Sawa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Shilingi natoa. Wamekuja tu na takwimu tuna mbuzi wangapi, kondoo wangapi, *we know those things.* Tunataka mikakati na *plan* yao ni namna gani tutaondokana na tatizo la wafugaji na wakulima na ninawaomba Wabunge wenzangu mniunge mkono hili suala tulijadili kwa pamoja Serikali itoe commitment, *we don't want business as usual.*

MWENYEKITI: Sasa Mheshimiwa Msigwa, Serikali imeshakuambia itakutana na ninyi, itakutana na wadau wote na mpango wao watakuambieni kitu gani wanachokifanya. *What else do you want?*

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuchangie kwa sababu hili ni tatizo nyeti ambalo liliivunja Serikali.

MWENYEKITI: Sawa, basi kaa, kaa chini. Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana mkono hoja ya Mheshimiwa Msigwa. Kazi ya Bunge kwa mujibu wa Kataba Ibara ya 63 ni kuisimamia Serikali na Serikali iko mbele yetu kwenye bajeti ambayo tunapaswa kuisimamia. Haiwezekani kutumia mbinu yoyote kuikwepesha Serikali kuwajibika kwenye jambo hili zito inayohusu maisha ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji tu mambo mawili hapa. Ratiba yetu ya Bunge ina kipindi cha Bunge ambacho kiko huru kwa kazi nyingine za ziada ndani ya Mkutano huu kuanzia tarehe 5 Juni mpaka tarehe 11 Juni wakati Kamati inafanya majumuisho.

Kama Wizara hii haikotayari kutueleza hapa toka ipewe taarifa ya Tokomeza imepanga mkakati gani wa kutekeleza mapendekezo ya Bunge, basi Kiongozi wa Shughuli za Serikali aliyeko hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe *commitment* kwamba katika kipindi hiki Serikali italeta Bungeni taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo ya Operesheni Tokomeza bila kutumia kisingizio cha kuundwa kwa Tume ya Rais. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili la Uongozi wa Bunge. Umwambie Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu anasema Kamati hiyo imekwisha kamilisha kazi yake, ripoti ya Kamati hiyo haijawasilishwa hapa Bungeni, tupangiwe ratiba hapa, ripoti hiyo iletwe Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Msemaji wa Upinzani alisema mwanzoni mwa hotuba yake kwamba tusiendelee kwanza na mjadala huu mpaka tuletewe hiyo ripoti ya Kamati? Hatujaletewa hiyo ripoti. *(Makofi)*

Sasa kwa kuwa tunakaribia kuhitimisha mjadala, tuweke azimio hapa la kwamba kwenye Mkutano huu wa Bunge ripoti hiyo itasomwa. Mheshimiwa Mwenyekiti, la sivyo hatua isipochukuliwa sasa, tutakwenda mpaka kwenye uchaguzi hatujamaliza matatizo ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Msigwa, mambo mawili yafanyike, Serikali ilete ripoti ya utekelezaji ya Operesheni Tokomeza na Uongozi wa Bunge upange ratiba ripoti ya Kamati ya Bunge nayo iletwe ndani ya Mkutano huu. Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Laizer.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naunga mkono kwamba taarifa ya Kamati ya Mheshimiwa Prof. Msola iletwe hapa Bungeni. Kwa sababu hiyo ripoti ilikuwa ni ya migogoro ya wafugaji na wakulima. Wananchi wanatuuliza kila siku kwamba ile ripoti imefikia wapi? Waliohojiwa na wasiohojiwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaomba hiyo ripoti ifike ili tuangalie kama matatizo haya yataisha. Kama alivyosema Mheshimiwa Lukuvi kwamba ipo, kuna ripoti nyingi sana ambazo zimewekwa hazikuletwa hapa. Naomba hiyo ripoti isichelewe, ije katika Bunge hili. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lukuvi, ripoti na *commitment!*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mwenyekiti, nilitaka kwanza kabla sijasema hilo niseme jambo moja kama taarifa tu. Maneno haya yanavutia sana kuzungumza lakini yanachanganya mambo mawili.

Kilichosababisha haya anayopenda kurudia Mheshimiwa Msigwa watu kujiuzulu na nini ni Oparesheni Tokomomeza, siyo migogoro ya wakulima na wafugaji na taarifa iliyokuja hapa ni hiyo na tulitoa maazimio mawili Bungeni hapa. Kwanza, tulitaka Serikali kuunda Tume ya Kimahakama ili ichunguze, iangalie ukweli na uendeshaji bora wa ile oparesheni, ilete taarifa hadharani na wale waliohusika wote na mambo haya tujue kama kuna fidia, kuna nini, hatua zichukuliwe. Sisi ndiyo tuliagiza.

Lakini la pili ndani yetu tukasema tuwateue wenzetu Kamati ya akina Mheshimiwa Mzee Msola wachunguze sasa, watupe jibu, maana migogoro ya wakulima na wafugaji ni ya kudumu nchi hii. Hawa wataalam hawa wenzetu wa Kamati waje watupe tiba. Mwongozo ule utakaotolewa na Kamati ndiyo Serikali kupitia Wizara itekeleze ili kuondoa kabisa migogoro hii ya wakulima na wafugaji. Kwa hiyo, haya mambo mawili tuliazimia hapa ndani.

Nilitaka tu kukumbusha hapa kwamba hili jambo si jipya na lina maazimio mawili ambayo tumetunga wenyewe na Serikali inatekeleza kupitia ile Tume ya Kimahakama ya Tokomeza ambayo imeundwa na sisi tunasubiri ile Tume itatuelekeza mambo ya kurekebisha, hatua za kuchukua ili tuweze kuchukua hiyo hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hili la taarifa, mimi kama sehemu ya watu ambao walitakiwa kutoa taarifa kwenye Kamati ile, siwezi hapa kusimama kwamba lazima itakuja, kwa sababu anayepanga Shughuli za Bunge siyo mimi, ni Spika. Kwa hiyo, siwezi kuji-*commit* ratiba ya Spika na wala siwezi kuripoti hapa mwenendo wa Kamati, siyo kazi yangu. Kwa hiyo naomba jambo hili kwa sababu wenye Kamati wapo na wewe ndiye Spika, sasa labda useme umelichukua utalifanyia kazi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa, hitimisha hoja yako na mimi nakubaliana na Mheshimiwa Lukuvi kuwa tunaipokea na tutamtaarifu Mheshimiwa Spika ili taarifa ile ije Bungeni na ijadiliwe na wananchi wajue ukweli wa mambo yaliyotokea. Mrudishie shilingi yake Mheshimiwa Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, niko tayari kurudisha shilingi, lakini ninachotaka ni *commitment, we are in a serious business.* Samahani Mwenyekiti, *we are in a serious business* ya kuwawakilisha wananchi. Uhai wa wananchi umeondoka.

Kama *commitment* itakuwa kabla ya Bunge hili halijaisha tutapata hiyo ripoti tuamue tunaondoka tunaenda kuwaambia nini wananchi wa Tanzania, *I have got no problem with that.* Nataka *commitment* hiyo, hizi taarifa tutazipata kabla ya Bunge halijaisha na ripoti hizo tutazipata ili tutoke na kitu kinachoeleweka kwa wananchi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa, nimekuelewa kabisa hoja yako na nakuelewa kabisa uchungu ulionao na ukweli ambao unaotaka kuupata. Na mimi vile vile nina kazi hapa Mezani, mimi siyo Spika, mimi ni Mwenyekiti wa Bunge. Lakini ni kazi yangu vile vile ku-*relay information* na kumshauri Spika.

Mimi naona kuna umuhimu kama ripoti ulishaipokea iletwe Bungeni, na hicho ndiyo tutakachokifanya, ndiyo nakuahidi. Sasa maamuzi yanakuwa ya mwenyewe Mfalme, siyo mimi. Lakini mimi nakuhakikishia *I will carry this message with a serious note* ili Spika aone uzito wa hiki kitu. Mrudishie shilingi yake. *(Makofi)*

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, nairudisha shilingi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nashukuru sana. Mheshimiwa Ritta Kabati!

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuleta hoja yangu Mezani. Nilipochangia kwa maandishi nilikuwa nataka kupata ufafanuzi kuhusiana na miradi ya machinjio yanayojengwa hapa nchini. Kwa sababu miradi mingi imekuwa ikichukua muda mrefu sana kukamilika.

Nataka nitoe mfano katika Mkoa wetu wa Iringa kuna machinjio moja iko katika Manispaa yetu ambayo ni ya Ngelewala. Machinjio hii imeanza kujengwa toka mwaka 2008 na mradi huu ili uweze kukamilika unahitaji kiasi cha *1.3 billion*. Lakini tumeona kwamba Serikali imekuwa ikileta pesa kidogo kidogo sana kiasi kwamba hata maana ya huu mradi inakuwa haisaidii.

Tunategemea kwamba kama huu mradi ungeweza kukamilika ungeweza hata kuleta ajira na ungeweza pia kuongeza hata uchumi wa Mkoa wetu na Halmashauri yetu. *(Makofi)*

Sasa nilikuwa nataka kujua, vigezo gani vinatumika kumaliza hii miradi na kwa nini Serikali isiweze kumalize ile miradi ambayo imefikia mwisho? Kwa mfano, huu mradi sasa hivi uko kwenye *finishing,* kutengeneza mabarafu kwa ajili ya nyama na umeme na kuweka uzio na kujenga mabwawa. Sasa tuna imani kwamba kama Serikali ingekuwa inaangalia ile miradi ambayo imefikia mwisho iimalizie ili iweze kusaidia hata ajira kwenye Manispaa zetu. Naomba pia *commitment* ya Serikali kwa mradi huu wa Iringa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu na *commitment*.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli labda nitahitaji uelewa zaidi kuhusu mradi huu. Lakini kimsingi ninachofahamu mradi wa machinjio kule Iringa ulikuwa unajengwa kwa ushirikianio wa *UNIDO* na Halmashauri ya Wilaya na siyo Serikali Kuu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilitegemea kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ambako Mheshimiwa Mbunge ni Diwani ama Manispaa ya Iringa ambapo Mheshimiwa Mbunge ni Diwani angeweza kutusaidia.

Lakini mimi kama Waziri mwenye dhamana nitafuatilia tu kuona kwamba tutashirikiana naye kuhakikisha kwamba huu mradi unatekelezwa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Machali!

MHE. MOSSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru. Ukiangalia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa ule wa 99, ni wazi Serikali kupitia Wizara wametenga shilingi 25,100,190,605. Sasa nilikuwa na swali moja ambalo pengine ningeomba nipate ufafanuzi na kama sikupata ufafanuzi wa kutosha nakusudia kuweza kuondoa shilingi.

Naomba Waziri atusaidie kuweza kujua kati ya fedha hizi ni shilingi ngapi ambazo zimetengwa kuelekeza kwenye sekta ya maendeleo ya uvuvi peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza hivi kwa sababu ukijaribu kuangalia sekta ya uvuvi ni moja ya sekta ambapo kwa kweli kama inaweza kusimama vizuri inaweza ikaisaidia nchi yetu kuweza kupata fedha nyingi ambazo zitatumika kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo.

Kwa mfano, Tanzania kama Taifa ambalo lina bahari, lina maziwa pamoja na mito mikubwa hasa hasa kujielekeza kwenye bahari zetu, hakuna bandari ya uvuvi.

Waziri amesema kwamba kuna fedha kidogo ambazo zimetengwa kwa ajili ya kuanza kufanya upembuzi yakinifu. Lakini huko nyuma tumepata kutaarifiwa kwamba tayari upembuzi yakinifu ulishapata kufanyika.

Sasa kwa kuendelea kutenga fedha ambazo pengine naziona kwamba ni kidogo ili kusudi hata yale mameli makubwa ambayo wakati mwingine yanakuja yanavua na pengine hatuna uhakika kwamba Wizara imekuwa ikifanya ukaguzi ili kuweza kujiridhisha kwamba ni kiasi gani cha samaki ambao wamevuliwa na kisha wanapelekwa. Ndiyo maana naomba Waziri atusaidie kujua ni katika hizi fedha ni kiasi gani ambazo zinaelekezwa kwenye sekta hii ya uvuvi peke yake ili kusudi tuweze ku-*promote* sekta hii na hatimaye iweze kuwa na tija kwa nchi yetu. Kama sikupata ufafanuzi wa kutosha, nakusudia kuweza kutoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu!

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti nishukuru tu Mheshimiwa Machali kutaka ufafanuzi na ningeomba tu asiendelee huko kwenye shilingi, hakuna sababu, kwa sababu utatuchelewesha, tukafanye kazi na wewe nafahamu ni mdau muhimu muhimu sana.

Lakini kwa fedha hii bilioni 25 tuliyoomba, uvuvi umetengewa 8,923,846,000/= ambayo kwa kweli ni karibu asilimia 40 ya mpango wote. Na hilo ulilolizungumzia kuhusu bandari ya uvuvi, unavyoiona wewe ya muhimu wote, ndiyo maana niliizungumzia sana pale. Katika fedha hii, kwanza tulikuwa tumeiomba kwenye mpango huu mwaka huu ambao tunamalizia, na katika pesa ambayo tunapewa sasa kabla ya mwisho wa mwaka, kwa sababu tulikuwa hatujafanya upembuzi yakinifu, milioni 300 inatengwa ili tuweze kubaini ni eneo lipi bandari hii ijengwe, igharimu kiasi gani, kwa manufaa ya maendeleo ya uvuvi katika Bahari Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipango hii ya maendeleo kuna mambo mengi makubwa, kule Ziwa Tanganyika tunaimarisha vikosi vya doria, tunajenga mialo, tunaikamilisha mialo ya Kalando, pale Kibirizi, mialo mine. Lakini vilevile kule Nyasa tunajenga pale *Mbamba Bay* kukamilisha bandari pale na kutengeneza kituo cha ujenzi wa maboti kwa ajili ya uvuvi mzuri pamoja na Ziwa Victoria. Bahari ya Hindi kuna shughuli nyingine nyingi. Kwa hiyo, mimi nafikiri wewe turuhusu tu usitoe shilingi ili tuendelee kufanya kazi.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na majibu ambayo ameyatoa Mheshimiwa Waziri, bado nakusudia kutoa Shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kupitia hata Kitabu hiki cha Maendeleo kwenye *Fisheries Development Division,* hakuna fedha hata shilingi moja ambayo imetengwa. Lakini pia katika maelezo yake anasema kwamba, kiasi cha shilingi bilioni 8.925 ndizo ambazo zimetengwa kwa ajili ya sekta nzima ya maendeleo ya uvuvi. Sasa nilikuwa naomba pengine Waziri atusaidie kuweza kujua hivi anadhani pengine kwamba hiki kiwango kinaweza kikatosha

kuweza ku-*meet* needs za sekta hii na anategemea tuweze kuona kweli kwamba hii sekta ya uvuvi inakua kwa kiwango kile ambacho kimekusudiwa na kama Taifa tukiri kweli, tuweze ku-*feel* kwamba, sekta hii ina mchango mkubwa sana kwenye ukuaji wa uchumi wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia la mwisho, Waziri anazungumzia kwamba, wanataka kule Kigoma, Ziwa Nyasa na kwenye Bahari yetu; naomba utusaidie, hizi bandari ambazo mnakusudia kuweza kuzijenga mnategemea kwamba zitakamilika katika kipindi gani? Ningeomba niweze kupata *timeframe, otherwise* naomba kwa kweli, ku-*declare* kwamba, pengine nitatoa shilingi ili kusudi…

MWENYEKITI: Aahaa, Mheshimiwa Machali, huwezi ukaimba halafu ndiyo unatoa shilingi. Mimi ninavyoamini umeishatoa shilingi.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, *ok.*

MWENYEKITI: Sababu, huwezi ukaanza sasa unafungua mjadala halafu unasema natoa shilingi… mjadala. *We don't go… (Sauti ilikuwa inakatika)* Sasa umeshatoa shilingi, unatoa taarifa yako… umeishaitoa. *(Sauti ilikuwa inakatika)*

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshatoa taarifa. Naomba Wabunge wenzangu waniunge mkono.

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Machali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nikiangalia hiki kitabu cha maendeleo, hii *Subvote* ya *Fisheries Development Division,* na mimi sioni hela yoyote iliyotengwa kwa ajili ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi ni eneo muhimu. Tanzania tuna sehemu nyingi za uvuvi, hususani Bahari Kuu, lakini nchi haipati mapato yoyote kutokana na rasilimali ya bahari tuliyonayo na Mheshimiwa Waziri anasema wana mpango wa kujenga bandari ya uvuvi. Hivi, ili tuweze kupata rasilimali na fedha kutokana na uvuvi ni lazima tujenge bandari ya uvuvi? Na hela zenyewe basi ziko wapi? Kama hizo hela zipo basi Mheshishimiwa Waziri atuoneshe. Na pia, je, kama alivyouliza Mheshimiwa Machali, hizo bilioni nane zinaweza kutosha kujenga bandari ya uvuvi?

MHE. MURATAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Hoja hii kimsingi ina umuhimu wake na umuhimu wake ni kwamba, pamoja na majukumu makubwa ambayo Wizara imetengewa, bado hatujawa na umakini wa kutosha kwenye kuboresha na kuimarisha miundombinu ya Wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wanapata shida. Na hivi sasa limeingia jambo lingine jipya ambalo wavuvi wa Tanzania wanavamiwa na wavuvi wa nchi nyingine jirani. Hili tatizo lipo katika maeneo ya Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na lipo mpaka baharini, kwamba, sasa hivi tunapambana na watu wanaotoka katika nchi nyingine kama Msumbiji, nakadhalika, wanakuja kuwanyang'anya vyombo wavuvi wetu, wanaondoka.

Serikali, lazima iweke umuhimu ili kukuza uchumi wa nchi hii na kufanya wananchi wote wanufaike na uchumi wa nchi yao, ni lazima tuweke miundombinu na bajeti ambazo zinapangwa zisiwekwe tu katika masuala mengine ya matumizi ya Serikali. Unapopeleka hela kwenye huduma ya afya bila kuwaboreshea wananchi hawa kuwa na uchumi, hizo dawa wataenda kununua vipi katika hizo hospitali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaitaka Serikali kwamba, lazima tuhakikishe pesa ambazo zinatengwa katika Wizara hizi ambazo ni za kiuchumi, ziwe zinafika. Hii hoja ya kusema kwamba, Serikali imeahidi kupeleka bilioni 10 kufikia mwishoni mwa mwaka huu, bado hatujakuwa na umakini wa kutosha. Kwa hiyo, Serikali iji-*commit* hapa kwamba pesa zote zilizotengwa kwenye kasma ya bajeti ya mwaka jana zipo na bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Uvuvi, Kamati yetu ya Bajeti ishirikiane na Serikali hela zitengwe ili tuweze kuwainua wavuvi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, hii ni *issue* muhimu, ni *issue* inaisaidia Serikali kupata mapato. Je, mna mpango wowote wa ku-*engage private sector* iwasaidie kujenga? Mifuko hii ya *pension,* wape *commitment* fulani tu, ndiyo mkakati ambao mnao.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nazingatia sana hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa sababu, na mimi zinanigusa, lakini tu kwanza kwenye hii pesa inayotolewa na Hazina, bilioni 10.5, bilioni 2.8 zitakuwa mahsusi kwa ajili ya maendeleo ya uvuvi. Na pesa hizi zinalenga kudhibiti uvuvi haramu, lile ambalo amelisema Mheshimiwa Mangungu, ukaguzi wa mazao ya uvuvi kwa kununua meli ya doria yenye uwezo wa kufanya doria katika Bahari Kuu. Boti nne za doria kwa Ziwa Nyasa, kule itakaa *Mbamba Bay,* Kasanga, kule Ziwa Tanganyika, Ikola na Kigoma. Na kuimarisha hifadhi za Bahari na maeneo tengefu kwa kununua na kuziendesha boti za doria hizo, *HP* 2 ambazo zipo, bilioni 2.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nawaomba Waheshimiwa Wabunge warejee randama, wanaposema kwamba, hakuna fedha ya maendeleo kwa uvuvi. Waangalie randama ukurasa wa 110. Kuna mradi wetu wa *EAP – East African Agriculture Productivity Program.* Huu ni wa kuendeleza ubora wa kuongeza tija katika sekta ya kilimo kwa upana wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Fungu 4495, kuna bilioni 2.2 kujenga bandari ya uvuvi ifikapo 2017, kuna kuwawezesha wavuvi wadogo kwa kuwapatia ruzuku za pembejeo, bilioni 2.2, kuwezesha wafugaji samaki kwa kuwapatia ruzuku milioni 244, kuanzisha kituo kimoja Mtwara na kuimarisha vituo viwili Mbegani ili kuzalisha vifaranga wa maji bahari milioni 3. Kuanzisha vituo vitatu vya Dareda, Hombolo na Kigoma, ili kuzalisha vifaranga vya samaki wa maji baridi milioni 10, kwa kushirikiana na sekta binafsi ambayo umeisema Mwenyekiti, milioni 822. Kuna kujenga na kukarabati miundombinu ya uvuvi, vituo vya ulinzi wa rasilimali za uvuvi, udhibiti wa ubora wa mazao ya uvuvi na kiwanda cha kutengeneza boti za kisasa milioni 220. Kuna kukarabati na kununua vifaa kwa ajili ya maeneo tengefu 15 milioni 174. Kuwezesha ujenzi wa chanja za kisasa za kuanikia samaki katika Mikoa ya Kigoma, Mwanza, Rukwa, Mara, Ruvuma na Lindi, milioni 54, na mambo mengine mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sababu Wabunge walikuwa hawajaliona eneo hili, wavuvi wamezingatiwa sana. Na msidhani kwamba, mimi siguswi, nimewambia wananchi wa Busega wanategemea uvuvi kwa kiasi kikubwa, kwa hiyo siwezi kukubali kuacha hivi. Naomba tu mrejeshe. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali, kubali yaishe? *(Makofi)*

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nisikitike tu kwanza kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri. Namheshimu sana Mheshimiwa Waziri na ni rafiki yangu, huwa tunazungumza mambo mengi tu. Lakini naomba niseme kwamba, Serikali bado haiko *serious* na sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tuna *records* ile meli moja tu ya Wakorea ambayo ilikamatwa ndani ya Bahari ya Hindi. Imekuja na wamevua samaki, tukabahatika Serikali ikawakamata, lakini na hata doria ambazo kwamba, pengine zinafanyika hapa nchini ni wazi bado hatujaweza ku-*invest* kwa kiasi kikubwa kwenye suala la kufanya doria kwenye bahari pamoja na maziwa yetu na hatimaye tukajua kwamba ni kiasi gani cha samaki ambao wanavuliwa kihalali na hata kiharamu vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hata hizi boti ngapi ambazo amesema kwamba, boti nne ambazo pengine watapeleka kwenye maeneo ya Maziwa yetu, bado ni kidogo sana. Ninafikiri Serikali kupitia Kiongozi Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna haja ya kuweza kuangalia suala hili, ili kuhakikisha kwamba, sasa tunatenga bajeti ambayo itakuwa na tija kama alivyosema Mheshimiwa Mwenyekiti kwamba hili ni eneo lingine ambalo tunaweza tukapata fedha nyingi, lakini kwa kuendelea kuleta bajeti ambazo ukiangalia kwamba haziwezi zikatufikisha kule ambako tumetarajia, tunaendelea kupoteza wakati wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nihitimishe kwa kusema kwamba, *this time* narejesha shilingi ya Serikali, lakini *next time* niwaombe Waheshimiwa Wabunge kama kweli tuko *serious,* tufanye tafiti na tuone kwamba kwa kuendelea kutenga bajeti za namna hii tunacheza hapa na wala hatuwezi tukaja tukawa-*liberate* wavuvi pamoja na sekta ya uvuvi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana.

(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko Yoyote)

Kif. *1002 – Finance And Accounts……Tsh.1,255,355,600/=*

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi niko katika *Item 220300 – Fuel, Oils and Lubricants;* mwaka juzi kilipangiwa milioni 27, mwaka jana milioni 28 na mwaka huu ni milioni 48.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba, hii Wizara imepata fedha kidogo, lakini Kitengo kimoja au Idara moja ya *Finance And Accounts* imepangiwa maradufu ya fedha ambazo imepangiwa mwaka jana kwa ajili tu ya mafuta. Naomba maelezo ya Waziri katika hili, kitu gani kimesababisha ongezeko kubwa mara dufu namna hii?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inazo taasisi nyingi na katika udhibiti wa rasilimali fedha ni muhimu wakafika. Tunavyo vyuo vya mafunzo ya mifugo, tunavyo vyuo vya mafunzo ya uvuvi, sasa kama hawasafiri tutafanyaje? Haya ni mahitaji halisi ya ukweli.

MWENYEKITI: Na vyuo vingi vimeongezwa.

(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko Yoyote)

Kif. *1003 – Policy And Planning……Tsh.1,010,412,400/=*

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko Kifungu kidogo 221000 – *Travel in Country*.

MWENYEKITI: Mia mbili, ngoja, mia mbili?

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, *221000 – Travel in Country*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa kwamba, Kitengo hiki cha Sera na Mipango ni kitengo muhimu sana na wote tumeelewa matatizo ya uvuvi na ya mifugo. Kwa hiyo, nikiwa naamini kwamba, kifungu hiki kinawasaidia watumishi kusafiri ndani ya nchi ili waweze kwenda kuangalia jinsi ambavyo sera zao na mipango yao inavyotekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia kuna upungufu wa kama shilingi milioni 58. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kupata ufafanuzi ni kwa jinsi gani watumishi wa Idara hii wataweza kwenda kutembelea maeneo mbalimbali kuona jinsi gani sera zao na mipango inavyotekelezwa? Naomba ufafanuzi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kweli, pamoja na upungufu wa bajeti, lakini Idara hii ina fedha vilevile za miradi ambazo zinaisaidia kuunganisha shughuli. Kwa hiyo, nafikiri tumeangalia ki-Wizara, tunafikiri inaweza ikaendelea kufanya kazi yake.

(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko Yoyote)

Kif. *1004 - Livestock Research and Training Inst*…….....*Tsh.12,558,827,200/=*

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko kwenye Kasma 270300 – *Current Grants to Non-Financial Public Units - (Academic Institutions)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasma hii inahusu kutoa ruzuku kwa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi – *TAFIRI* na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo – *TARIRI*. Mwaka jana zilitengewa bilioni 2.9, mwaka huu imeshuka mpaka bilioni moja. Natambua kwamba, kwenye miradi ya maendeleo huko mbele kumetengwa bilioni 1.6 kwa ajili ya TAFIRI na *TARIRI* kwenye mradi mmojawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini huu mshuko wa matumizi ya kawaida ya taasisi hizi muhimu zinazoongoza utafiti kwenye sekta hii unashtusha. Na Bunge hili, lilishawahi kupitisha makubaliano kwamba, fedha za utafiti tutenge walau 1% ya pato la Taifa na *COSTECH* inaratibu masuala haya ya utafiti na fungu hili la utafiti.

Ningependa kupata ufafanuzi kutoka kwa Waziri, ni kwa nini katika kipindi hiki ambapo kuna nyongeza ya fedha kwa ajili ya utafiti, katika kipindi hiki ambapo kuna matatizo makubwa ya wakulima, wafugaji, n.k. yanayohitaji kufanya utafiti vilevile wa kutafuta ufumbuzi endelevu, katika kipindi hiki ambacho tunalia mapato kwenye Bahari Kuu tunahitaji kufanya utafiti wa mbinu bora za kuongeza mapato, vyombo hivi viwili muhimu vya utafiti katika nchi yetu kwenye sekta ya mifugo na sekta ya uvuvi vimepunguziwa fedha kwa kiwango hiki. Ningependa kupata ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri na ufafanuzi usiporidhisha nitaomba kuondoa shilingi katika hili.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Mnyika ina msingi kwa sababu, kweli, taasisi hizi ni za muhimu hasa katika kipindi

hiki, lakini nataka nimtoe hofu tu kwamba, fedha hizi siyo kwamba hizi taasisi hazipati. Kwanza moja ya *grants* hizi zilikuwa kwa ajili ya malengo ya mshahara, lakini ukiona kile kifungu pale cha kwanza kabisa kwenye Kasma hii 210100, sehemu kubwa ya mshahara imepelekwa pale. Lakini vilevile kuna fedha ambayo itapitia *COSTECH* ambayo sasa wamepewa dhamana ya kuhakikisha kwamba tafiti mbalimbali zinafanyika katika taasisi zote za utafiti. Kwa hiyo, kama wakala wale wa utafiti, hawajapata punguzo. Asante sana.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuondoa shilingi katika hili baada ya ufafanuzi, lakini Kamati ya Bajeti itakapokwenda kufanya mapitio ya Wizara si busara sana kurundika pesa zote za utafiti kwenye taasisi moja ya *COSTECH* wakati kuna *sectorial institutions* za utafiti. Mara nyingi taasisi kama *TAFIRI,* taasisi kama *TARIRI* zinapata uzito kupata pesa kutoka *COSTECH* kwa wakati kufanya utafiti zinapohamishiwa kule *COSTECH.*

Kwa hiyo, hili jambo linahitaji kufanyiwa kazi siyo kwa Wizara hii tu, kwa Wizara mbalimbali ili *think tanks* za Wizara mbalimbali ziwezeshwe kwenda kufanya utafiti katika masuala muhimu kama haya ya mifugo na uvuvi na masuala mengine.

MWENYEKITI: Asante.

(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko Yoyote)

Kif. *1005 - Government Communication Unit…….....Tsh.202,962,000/=*

Kif. *1006 - National Livestock Institute – Mpwapwa.....Tsh.0/=*

Kif. *1007 - Internal Audit Unit……Tsh.254,049,300/=*

Kif. *1008 - Procurement Management Unit.....Tsh.372,714,700/=*

Kif. *1009 - Legal Services Unit…….....Tsh.156,001,900/=*
Kif. *1010 - Information Communication and Technology..Tsh.261,622,900/=*

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu, vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kif. 7001 – *Veterinary Services…….....Tsh. 8,203,878,200/=*

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, niko *program* 220400 - *Medical Supplies and Services.* Fedha hizi ni fedha za dawa za mifugo na chanjo. Mwaka jana walitengewa milioni 823, lakini mwaka huu wametengewa milioni 494. Sasa nilitaka ufafanuzi kwamba kwa nini fedha zimekuwa chache na hali majuzi tu Waziri alitangaza kwamba inawezekana mwaka huu kukawa na ugonjwa wa mlipuko wa *rift valley* pamoja na magonjwa mengine ambayo yapo siku zote. Nataka ufafanuzi kwamba kwa nini zile fedha zimekuwa chache.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuna suala la upungufu wa bajeti, lakini kuna mradi ambao unafadhiliwa na Shirika hili la *Bill & Melinda Gates Foundation* ambao wanachangia katika uagizaji wa dawa. Kwa hiyo, hapa kweli kuna upungufu lakini yale makadirio ya chanjo ambazo tumekusudia kununua,

zinatoshelezwa na fedha ambazo tumekadiria kupitia hiki kifungu na kifungu kile cha Mradi wa Bill & *Melinda Gates Foundation.*

(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko Yoyote)

Kif. 7005 – *Veterinary Council of Tanzania*…….....*Tsh.220,589,500/=*

MHE. SUSAN A. JEROME: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nipo kwenye kifungu 230400 - *routine maintenance and repair of vehicles and transportation equipment*. Nilitaka kujua tu hili baraza kwanza lina magari mangapi kwa sababu ukiangalia fedha iliyotengwa mwaka huu kwa mwaka mzima, *routine maintenance* ni shilingi 1,050,000/=. Sasa nilitaka kupata ufafanuzi je, fedha hizi zitatosha vipi na nimeangalia kwenye kitabu cha maendeleo hakuna kabisa kitengo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba ufafanuzi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kweli eneo hili tukiri upungufu wa bajeti upo kwa sababu kupanga ni kuchagua. Tumejitathmini katika Wizara tukaona eneo hili tulipatie hiki. Lakini kwa sababu hiki kitengo kinalelewa na Idara mama ambayo ni ya *veterinary services* (huduma za mifugo) zitahakikisha kitengo hiki kinafanya kazi.

(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko Yoyote)

Kif. 8001 – *Animal Production*……*Tsh.3,637,819,450/=*

(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko Yoyote)

Kif. 9001 – *Fisheries Development Division*……*Tsh. 7,054,875,550/=*

MHE, JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kasma 270400 - *current grant to non-financial public units (authorities)*. Kifungu hiki kinahusika na utoaji ruzuku kwa chombo kinachohusika na usimamizi wa Hifadhi za Baharini na Majini kwa maana ya *Marine Parks*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana kifungu hiki kilitengewa bilioni 1.3, mwaka huu kimeshuka mpaka milioni 299 peke yake. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili nisipopata ufafanuzi nitaomba kwa kweli kuondoa shilingi, kwa sababu hii idara au wakala au *unit* ya *Marine Park Reserves* ndiyo inahusika na kusimamia *Marine Park Reserves* kwa upande wa Dar es Salaam; *Marine Park reserve* ya Mbudya, Marine Park Reserve ya Bongoyo, *Marine Park Reserve* ya Funguini na *Marine Park Reserves* nyingine. Na kwa upande wa maeneo mengine ya Tanzania inasimamia *Marine Park Reserve* ya Mafia kwa upande wa Mkoa wa Pwani, inasimamia *Marine Reserve* ya Pangani kule Tanga, inasimamia *Marine Reserve* kule Mtwara, inasimamia *Marine Reserve* ya Mnazi Bay kwenye Ruvuma *estuary*.

Zamani *Marine Reserves* hizi zilikuwa zinapewa uzito sana wakati zilipokuwa Wizara ya Maliasili na Utalii kama sehemu ya vivutio vya utalii. Sasa hivi kwa kuwa sehemu ya mifugo na uvuvi, ile *aspect* ya kwamba hivi ni vivutio vya utalii ambavyo vingeingizia nchi yetu mapato mengi haipewi tena uzito na zinatengewa pesa ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri na nitaomba katika hili asitumie hoja ya mishahara kwa maana ya kuongezeka kwa mishahara kutoka bilioni 2.3 mpaka bilioni 4 kwenye *fisheries and development division,* kwa sababu hoja hii ina masuala ya wafanyakazi wa idara na ongezeko la mishahara vile vile, isitumike kama kivuli cha kuficha hii hoja. Nitaomba ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri ni kwa nini eneo hili muhimu ambalo lingekuwa chanzo cha mapato limetengewa pesa kidogo sana namna hii zimeshuka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu Mheshimiwa Mnyika kwanza awe na mtazamo chanya. Unafahamu ukianza kuhisi kwamba kuna sababu ambayo siyo sawasawa siyo vizuri kwa sababu hata jibu ukipewa na malaika hutaridhika. Lakini mimi nikueleze sasa kwa sababu ndiye msimamizi wa Wizara.

Hiki kifungu kimepunguzwa kwa sababu mishahara ya kitengo kile cha MPRU ambacho anakisema Mheshimiwa Mnyika, kimehamia kwenye kifungu kidogo kile cha 210100 na ndiyo maana unaona pale ni dhahiri mishahara imetoka bilioni 2.3 mpaka bilioni nne, hiyo siyo nyongeza ya kawaida tu eti watu wameongezwa, wamepandishwa kazi, bilioni mbili *difference* haiwezekani! Kwa hiyo kubali kwamba ni wale wa MPRU imehamia pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikutoe hofu kwamba eti kitengo hiki au idara ya uvuvi imedharaulika au kunyanyaswa kwa kuunganishwa na mifugo siyo kweli, siyo kweli hata kidogo kwa sababu hizi ni idara mbili kubwa na zina vitengo vingine vingi na zina Wakurugenzi. Ya uvuvi yenyewe ina kurugenzi mbili, kurugenzi ya uvuvi na kurugenzi ya ufugaji wa viumbe baharini. Na hiki kitengo cha bahari kwanza sheria yake sasa inaangaliwa upya ili kitengo hiki kiweze kuwa na mamlaka zaidi ya kujisimamia na kukusanya mapato.

Eneo hilo ulilosema la utalii tunalipa kipaumbele sana na sasa wanatangaza maeneo yao, wanavutia wawekezaji. Labda nitumie na fursa hii kutangaza watu ambao wana nia ya kuwekeza katika maeneo ya visiwa na bahari na fukwe ambazo zinasimamiwa na MPRU niwakaribishe tu. Ahsante sana.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika kwa kweli na maelezo. Mimi niseme kwamba mimi ni mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Kamati ambayo kimsingi inasimamia sekta ya utalii. Katika vikao vya Kamati yetu na Wizara yako haiji kuripoti kwenye Kamati yetu, Wizara ya Maliasili inakuja kuripoti kwenye Kamati yetu. Tuki-*assess performance* ya utalii nchini kwenye *Marine Parks* tunaona kabisa tunatumia vibaya rasilimali zetu kwa sababu hatutoi uzito unaostahili kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitarajia Mheshimiwa Waziri kwa kuwa kasma hii inahusu ruzuku kwenye eneo hili, angetuambia kwamba kwa upande wa mishahara kiwango tulichokiondoa ni hiki na kiwango kilichobaki sasa hivi kiasi hiki kitakuwa cha matumizi ya kawaida, kiasi hiki… na nasema kwa sababu ukifungua kitabu cha maendeleo ukurasa wa 282 kuna kifungu kinaitwa *Fisheries Division,* zamani kifungu hiki na miradi yake pamoja na kifungu cha 902 ambacho kilikuwa kinahusika na masuala ya uendelezaji wa wanyama wa majini, vilikuwa vinatumika kuongeza pesa, kuweka pesa kwa ajili ya miradi ya kuendeleza hizi *Marine Parks.*

Sasa ukiangalia kwenye miradi hakuna pesa, kwenye matumizi ya kawaida hajatuambia ni kiwango gani kinakwenda kuziendeleza hizi *parks*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi siridhiki kabisa na majibu yaliyotolewa na naomba kuondoa shilingi ili Mbunge anayetoka Pangani kwenye *Marine Park* Pangani aweze ku-*share* uzoefu wa namna ambavyo *Marine Parks* hazisimamiwi vizuri zinahitaji rasilimali za ziada, Mbunge wa Mafia, Mbunge wa Ruvuma na Wabunge wa maeneo mengine ili walau safari hii Wizara hii ya Mifugo itoe *commitment* ya kuongeza nguvu kwenye eneo hili. Na kama Wizara hii haioni kipaumbele suala la utalii, hiki chombo kihamishiwe kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii ili nchi itumie vizuri hizi rasilimali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuondoa shilingi na Wabunge wenzangu waweze kuchagia.

MWENYEKITI: Nakushukuru, hakuna anayechangia wala kuunga mkono.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiondoa shilingi Waziri anatakiwa kujibu.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba Mheshimiwa Mnyika afahamu suala la utalii haliko chini ya Wizara ile tu peke yake ya Maliasili na Utalii. Kuna maeneo mengi yanayohusika na utalii ambayo hayako pale, utalii ni uwanda mpana sana kuanzia jamii, wacheza ngoma, sijui utalii wa vyakula, hawa hawako chini ya Wizara ya Maliasili, hawa wako kwenye Halmashauri.

Kwa hiyo ukizungumza kwamba eti kila kitengo kinachohusu pamoja na *Marine Parks* siyo, sahihi hii. Hii yote inaendana na sekta yote ya maliasili za uvuvi na bahari, kwa hiyo pale ilipo ni mahali sahihi. Lakini nakuambia tu kwamba sheria tunaitengeneza ili ipewe mamlaka. Lakini hata sasa hiki kitengo kinapata *retention*, pesa kinazokusanya zinabaki kwa maendeleo yake. Kwa hiyo uelewe kwamba tuna dhamira kuu wala siyo kwa sababu eti kipo Maliasili na Utalii, siyo sahihi.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina tatizo sana na kitengo hiki kuwa kwenye Wizara hii kama Wizara ikitoa kipaumbele kwa kitengo hiki sina tatizo kuwa kwenye eneo hili. Ukiwauliza Watanzania, ungewauliza Watanzania kabla ya mazungumzo haya marefu, ungepita ungewauliza Watanzania kwamba Wizara ya Mifugo na Uvuvi inahusika na utalii kupitia *Marine Parks,* wengi wangekuambia hawafahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko Dar es Salaam pale, ziara za kitalii kutoka mwenye Hoteli za kitalii za Dar es Salaam kwenda Mbudia, Kwenda Bongoyo, kwenda maeneo mengine hazidhibitiwi ipasavyo na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi ninachokiomba katika jambo hili, namrudishia Waziri shilingi yake mwaka huu kwa *commitment* hiyo ya kwamba moja italetwa hiyo sheria irekebishwe ili hiki chombo kifanye kazi ipasavyo, lakini pili, Wizara itatoa kipaumbele kwenye eneo hili kwa sababu ni chanzo kikubwa cha mapato ambacho kingeisaidia hii Wizara kama kingepewa uzito unaostahili.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niko kasma 410700 *sub vote* hiyo hiyo 9001 - *feasibility studies, project preparation and design*. Mwaka 2012/2013 kifungu hiki kimekuwa kikitengewa fedha, kilitengewa milioni 53 na *point,* halafu mwaka jana pia kilitengewa 500,500,000/=, mwaka huu kimetengewa milioni hizo mia.

Nilitaka kujua hii *feasibility studies, project preparation and design* ni aina gani ambayo haiishi?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kwanza ni Idara ya *Fisheries Development*. Unapozungumza maendeleo ina maana kila wakati kuna mawazo mapya yanakuja, kila wakati kuna miradi mipya itakuja. Sasa tukikaa tukasema sasa tuwe kama tulivyo, sasa tutaendeleaje? Kwa hiyo hii ni kazi ambayo itaendelea kuwepo. Ahsante.

(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko Yoyote)

Kif. 9002 – *Aquaculture Development Division…….....Tsh. 994,976,900/=*

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niko kwenye kifungu hicho kasma ndogo 410700 kuhusu *feasibility studies, project preparation and design,* ukizingatia kwamba hii ndiyo sekta mpya inayohusika na kuwaonbdolea makali wananchi ambao samaki wao wote wamevuliwa au Ziwa limeuzwa wakabaki hawana kitu.

Nilitaka kujua hizi *feasibility studies* zinahusisha nini katika kuwaondolea wananchi ambao samaki wote wamechukuliwa na hii *aquaculture* inafanya nini kwenye hii kitu. Soma kifungu hapa.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara hii kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge inahusiana na ufugaji wa viumbe kwenye maji. Wajibu wa Idara hii zaidi ni kuwezesha wananchi waweze kupata vifaranga vya samaki.

Sasa tuna vituo ambavyo tunaendelea na ujenzi na vingine ambavyo vinabuniwa. Kuna orodha ndefu kwenye hotuba yangu lakini na kwenye randama ya vituo hivi ambavyo vinajengwa kule Nyamilembe, Chato, kuna Ruhila, Lindi kule, kuna Kigoma, kuna Mwamapuli kule Igunga viko vingi. Kwa hiyo kazi ya *feasibility studies* kasma hii ndiyo hiyo.

MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipo kwenye kasma 411200 inayohusiana na uzalishaji wa vifaranga. Ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 51 amezungumzia kwamba Wizara imekuwa ikihamasisha wananchi na wamechimba mabwawa kwa wingi na wakaongeza mahitaji ya vifaranga na ndiyo sababu akasema mahitaji ya vifaranga yaliongezeka kutoka 20,134 mpaka 20,493.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa utafiti unaonyesha kwamba samaki wanaendelea kupungua na tunakuwa na ukame wa samaki katika Ziwa Victoria. Sasa tumefika mahali katika mazingira ambayo sasa wananchi wengi kando kando ya Ziwa Victoria wanajihusisha sasa na ufugaji wa samaki kwenye mabwawa. Sasa ukiangalia kwenye hiyo kasma mwaka juzi zilitengwa milioni 17, mwaka jana milioni 14 zikapungua, mwaka huu sasa zinatengwa milioni nane kwa ajili ya uzalishaji wa vifaranga. Sasa mimi nashindwa kuelewa inakuwaje upande mmoja mnaendelea kuhamasisha wananchi na mahitaji yanaongezeka ya vifaranga, lakini upande mwingine mnaendelea kupunguza pesa ili kupunguza uzalishaji wa vifaranga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kwangu mimi kwa sababu suala hili ni muhimu katika Ziwa Victoria, ninakusudia kutoa shilingi endapo Mheshimiwa Waziri rafiki yangu huyu atashindwa kunipa maelezo ya kina kwa sababu suala la kuhamasisha mahitaji yanaongezeka halafu upande mwingine unapunguza uzalishaji wa vifaranga mimi haliniingii akilini. Kwa hiyo

ninaomba ufafanuzi vinginevyo nisiporidhika nitaomba Wabunge wenzangu wanisaidie kujadili jambo hili.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hoja ya Mheshimiwa Lugola ni ya msingi ni kweli wote tunaathirika na upungufu wa samaki kule Ziwa Victoria. Lakini tu nimtoe shaka kwamba fedha japo imepungua kwenye fungu hili na tungependa iwe kubwa lakini ili kupunguza hofu yake ukiangalia randama yetu ukurasa 110 kuna mradi maalum wa IAP, kuna kuwezesha wafugaji samaki kwa kuwapatia ruzuku milioni 244 na ukurasa 111 kuna kupandikiza samaki katika mabwawa ya asili ya Bulenya, Nara, Msenda, Basuto, Nyaluhande na Kitele shilingi milioni 40. Kwa hiyo hiyo milioni mbili iliyopungua kwenye hiyo kasma imefunikwa na mradi huu mzuri ambao unakuja na ninamuhakikishia kwamba tutaendelea kutafuta fedha zaidi.

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ndizo ngonjera ambazo huwa wakati mwingine hapa tunasema kwamba tukiendelea na hizi ngonjera kwa kweli tutafika mahali hilo Ziwa Victoria ambalo ukiliona kwa ukubwa wake kwa juu unaweza ukadhani kwamba bado lina samaki kule ndani.

Sasa mimi nilikuwa namuomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na kwamba hizo fedha zingine zilikuwa zimejifunika katika maeneo mengine na mimi hapa nilikuwa nazungumzia fedha ninazoziona hapa milioni nane, sasa hizi ndizo dalili kwamba tunakuwa hatuna maelezo ambayo yanaeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba niendelee kukamata shilingi ili Wabunge wenzangu na hasa ambao wanatoka Ziwa Victoria ni wathirika wakubwa na sisi tunahitaji vifaranga na hata kule Mwibara kuna mabwawa ya samaki yameshachimbwa tayari, lakini matatizo ni vifaranga na inawezekana hata hivi vifaranga upatikanaji wake ni shida. Kwa hiyo nilikuwa naomba hoja yangu hii Wabunge wengine wapate fursa ya kuichangia ili kieleweke. Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lugola, Mheshimiwa Waziri amekuambia hili suala la mtambuka, pesa hizi zimetengwa kwenye eneo lingine la kuja huko huko *Lake Victoria*, sasa Wabunge wengine tutasimama, mnayo haki ya kusimama ndiyo wajibu wa Wabunge kusimama na kutetea. Lakini majibu ndiyo haya. Mheshimiwa Mwijage!

MHE. CHARLES P. J. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na kaka yangu Mheshimiwa Lugola, maelezo ya Mheshimiwa Waziri anapo-*refer* milioni 240 hayana uhakika, nikitumia lugha ya kibunge. Mimi niliomba nizungumze hapa sikupata fursa na nashukuru ulinisoma *mood* yangu niliyokuwanayo. Ninayo mawasiliano kwenye Wizara, hizi *feasibility study* zinazofanyika ni kwamba kuna mahali kuna *bottleneck*. *Bottleneck* ya ufugaji wa samaki ni chakula. Sasa unapozungumza hapa suala la viranga ile milioni 240 haizungumzi inakwenda kufanya nini, inamaana itapotetea hivyo hivyo kama zile randama zinazoonyesha ofisi zinanunua mafriji, ofisi zinanunua majokofu vitu vya namna hiyo.

Kwa hiyo, hapa kuna hoja, hoja ya msingi ni kwamba hizi namba zinachezewa hatuwezi kuona kitu kinafanyika. Kama angetueleza kwamba milioni 240 zitanunua *peretizer* za kutengeneza chakula tungeweza kujua kwamba hizi zinakwenda kutengeneza *feed stock*. Halafu vifaa vyote vilivyozungumzwa, nimemsikiliza kwa makini, nimesoma kitabu chake Mheshimiwa Waziri, anapozungumza ufugaji wa samaki hazungumzi kule ambako samaki wanapaswa kufugwa, wanaolalamika kwamba Ziwa limebinafsishwa, Ziwa liliuzwa ni Ziwa Victoria. Lakini katika *stock* zako unazozungumza Ziwa Victoria haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga na Mheshimiwa Lugola, haya maelezo hayana *justification,* kuna namba zinachanganywa. Atueleze hizo 240 ni ngapi zinakwenda kununua peretizer na kutengeneza chakula kwa ajili ya wafugaji, tuweze kuelewa, kwa sababu mchakato mzima tunaujua na taarifa ziko ofisini kwako, lakini majibu hayatoki, tulitegemea majibu hayo yatoke kwenye ripoti hii au hotuba uliyoisoma.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipatia na mimi nafasi, japo sikupata pale mwanzo nilikuwa nataka nichangie kitu kizuri zaidi. Lakini sasa hivi nikuambie kilichoko katika jimbo langu, baada ya kuona kwamba Ziwa Victoria hatupati samaki tukawahamasisha vijana kuweza kufuga na wakawa wanauziwa vifaranga, tumetoa hata kwenye mifuko ya vijana kuwapesha vijana. Lakini vifaranga vyenyewe vikawa kama viruwi ruwi yaani hata samaki hawakutokea, vijana hawawezi kurudisha mkopo, matokeo yake ni kwamba inaonekana utafiti haukufanyika vizuri wa kuweza kuuza vile vifaranga. Hivyo, tunataka kujua utaratibu gani utafanyika ili vijana watakapokopa waweza kujikomboa katika umaskini?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yale majibu yangu ya mwanzo ambayo Mheshimiwa Kangi Lugola ambayo aidha, hakutaka kuyakubali wakati yameandikwa na ndiyo njia rasmi ya mawasiliano, sasa sijui nitazungumza na lugha ipi. Lakini hiyo milioni 244 na hiyo milioni 40 zipo kwa shughuli hiyo na sina mashaka kwa sababu mradi huu tayari umeshaanza kazi. Kwa hiyo, sina mashaka anavyosema kwamba sijui ni ngonjera, hakuna ngonjera katika utendaji. Kwanza kazi hii ni ya kisayansi haina ngonjera.

Lakini vilevile kumuongezea kwamba mwaka huu katika fedha hii ambayo bajeti hii tunayokamilisha ambayo tumeongezewa na Hazina tumepewa bilioni 10.5, milioni 950 zinaenda kuweka miundombinu ya ufugaji wa viumbe kwenye maji kwa kujenga vituo vya kuzalisha vifaranga vya samaki ambavyo nilivitaja mwanzo; Mwamapuli, Igunga, Nachingwea, Chihiko – Mtwara, Kibirizi – Kigoma na kupanua vituo vya Kingorwira, Ruhira, Chato, Karanga, Machui, Bukoba, Mwanza, Musoma. Sijui kama yeye hatoki eneo la Musoma, Mbegani Chongorehani na Mtama na kununua na kupandikiza vifaranga vya samaki 500,000 katika mabwawa hayo nilioyasema. *(Makofi)*

Sasa sijui, sina lugha ya kimalaika zaidi ya hapo. Mheshimiwa Kangi kubali tu yaishe, kwa sababu mimi nitasimamia, sina shaka. Wewe unapotoka jimboni kwako unapita kwangu Lamadi, sasa ukikatalia shilingi sasa si utamtesa Waziri wako.

MWENYEKITI: Zima *mic* yako.

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nirekebishe kidogo, mimi sitoki Musoma natoka Bunda, ila Bunda na Musoma sote tuko Mkoa wa Mara. Kwanza kabisa kwa heshima niliyonayo na Mheshimiwa Waziri ambaye alikuwa mwanakwaya mwenzangu huku tukiimba ngonjera, nimhakikishie tu kwamba maelezo yake kwa sababu ni mara ya kwanza, nichukulie kwamba tutakapoendelea na safari aya-*justify* haya yatokee kweli. Lakini kama tutaendelea baadaye zikaonekana zilikuwa ni ngonjera basi nitakapong'ang'ania shilingi, nitaing'ang'ania kweli kweli. Basi kwa heshima hiyo nairudisha shilingi.

(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko Yoyote)

KITABU CHA IV

MIRADI YA MAENDELEO

FUNGU 99 – WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI

Kif. 1003 – *Policy and Planning*……..……*Tsh.1,351,947,000/=*

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwenye kifungu hiki toka mwanzo nilisema hata kwenye hotuba yangu na Waziri hakunijibu vizuri, alisema kwamba sikusoma. Ninaomba kumdhihirisha wazi kwamba nimepitia hii kasma na ninapenda kumueleza kwamba *subvote 1003* wamepitishiwa fedha za kutosha kwa ajili ya OC ambapo waliweza kupata zaidi ya milioni 1.105.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na huku pia kasma hiyo hiyo imepewa bilioni 1,351,974,000/=. Sasa mimi naomba hivi, ni kwanini huku wamepewa safari ya nje, halafu tuendelee kukubali kupitisha wakati tunataka kupata fedha za maendeleo hapa. Sasa kama huku walikuwa wanafuatilia kwenye hii *subvote* wao wanafuatilia je, kwanini na huku wasiweze kufuatilia kwa fedha hizo hizo ambazo wametengewa mwanzoni. Mimi naomba nisiunge mkono, nashika shilingi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUNGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyosema kwamba hakusoma sikumaanisha kwamba hajui kusoma. Kwa hiyo, asije akafikiri kwamba labda nimenyanyapaa, nilimaanisha kwamba hakuliona lile fungu. Sasa katika matumizi ya kawaida, hiki kitengo ni cha *policy and planning* hiki ndiyo ubongo wa Wizara. Sasa unaufanya ubongo hausafiri, sasa huo ubongo utafanya kazi gani! Utaongozaje Wizara.

Kwa hiyo, yale matumizi kule kwenye matumizi ya kawaida ni sahihi lakini vilevile huku kwenye hili fungu la maendeleo kawaida miradi, ule mradi unakuwa na component zote kwa ujumla wake siyo tu ujenzi tu kama jengo linadondoka, linadondoka bila usimamizi, bila kwa hiyo posho lazima ziwepo yaani haiwezi ikaja bila watu kusafiri kuleta vifaa yote ni usafiri, ni mafuta ni usafirishaji, ni sehemu ya mradi.

Kwa hiyo, hii iliyokasimiwa hapa ni sahihi tu. Na nikwambie kwamba kitengo hiki kinaongozwa na mwanamke mahimili ambaye sina mashaka kwa sababu wanawake huwa hawaibi, siyo mchwa, mwanamke mwenzako. Kwa hiyo naomba tuunge mkono turudishie shilingi. *(Makofi)*

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mimi namwamini sana huyo mwanamke anayemsema mahili, lakini ninachozungumza ni kwamba kwa vile tuna shida sana tunasema kwamba kuna matatizo makubwa sana kwa ajili ya wafugaji, hatukuweza kuweka kipaumbele kwa ajili ya kuweza kutenga ardhi kwa ajili ya wafugaji. Lakini kwenye kasma hii wameweza kuweka safari za ndani milioni 104, halafu pia safari za nje 96,300,000/=.

Vivyo hivyo kwenye fedha za maendeleo ambayo kweli wao wanafuatilia, mimi sikatai huko wanafuatilia. Lakini pia wamepewa fedha za safari za ndani tena milioni 212, halafu tena wanapewa fedha za safari za nje.

Sasa mimi sikatai, lakini je, kama sisi tunategemea kwamba hizi ni fedha za maendeleo za ndani, mfuko wa ndani, kwanini basi hizi hela zisibaki ndani kwa ajili ya maendeleo yao wakaendelea kutumia hizi ambazo zimepitishwa kwenye OC mimi sikatai lakini. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Hukusema kama nini, ulikuwa na adhima lakini hukumaliza kutoa shilingi.
MHE. ROSE K. SUKUM: Shilingi si nilishasema kwa hiyo Waziri amalizie.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ni kwenye *basket fund*, kwa hiyo hakuna cha kufanya, zina mazingira yake.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala analozungumza Mheshimiwa Rose Kamili ni kwamba kitabu cha matumizi ya kawaida tulichomaliza kupitisha matumizi ya kawaida kwenye Idara hii ya Sera na Mipango tumepitisha pesa za ufuatiliaji, za safari, za matumizi ya kawaida. Sasa hivi tunajadili kitabu cha maendeleo. Kwenye kitabu cha maendeleo vilevile kuna kiwango kikubwa cha pesa kimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Ni wazi mradi wowote una *component* ya *management* ya mradi, lakini mradi huu namna pesa zilivyotengwa zinachekesha. Kwa mfano, kwenye matumizi ya maendeleo kumetegwa gharama za kutoa *photocopy* shilingi milioni 56, gharama za kutoa *photocopy*, za kulipia gharama za kutoa *photocopy*. Lakini papo hapo zimetengwa gharama za kununua fotokopia milioni 80 na wakati gharama za consumables, yaani kununua *tonner*, wino na nini ziko tayari zimetengwa milioni 3. Yaani matumizi ya kawaida, yaani tungekuwa na muda tungepitia ukiangalia vifungu vya randama kwenye maeneo mbalimbali matumizi ya kawaida kabisa yamerundikwa kwenye sehemu ya miradi ya maendeleo.

Sasa Mheshimiwa Waziri jibu lake linasikitisha zaidi anasema kwamba kwa kuwa ni *basket fund* hatuna cha kufanya, yaani maana yake ni kwamba wahisani wakiweka pesa kwenye *basket fund* wanakuja na masharti mpaka kwa kiwango cha kutupangia matumizi ya kawaida kwenye miradi ya maendeleo kwa kiwango cha kushindwa kuzielekeza hizo kwenye miradi ya maendeleo moja kwa moja. Sasa kama hali ni hiyo anayoizungumza Mheshimiwa Waziri kwamba tukiletewa na *basket fund* hatuna cha kufanya, Bunge la Tanzania linafanyia nini? Bunge linafanya nini kama ukiletewa na *basket fund* huna uwezo wa kufanya mabadiliko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hoja ya Mheshimiwa Rose Kamili ni kwamba Kamati ya Bajeti ikaupitie huu mradi iangalie, matumizi ambayo tayari yamekwishapangiwa pesa kwenye matumizi ya kawaida, hizo pesa zihamishwe zielekezwe kwenye miradi ya maendeleo itakayowanufaisha wafugaji na wavuvi na hilo ndilo jambo ambalo naomba kuliunga mkono ambalo Mheshimiwa amelizungumza.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu kwa sababu hapa tunazungumza kwa ufupi bila kufafanua sana mradi huu unamaanisha nini au unagusa wapi. Mradi huu unatekelezwa katika Halmashauri nne, Halmashauri za Bahi, Kondoa, Kiteto, Chemba. Sasa kila eneo la utekelezaji lina mazingira yake siyo kwamba unatekelezwa kutoka Wizarani kwa hiyo, hata unavyoona hivyo sijui vidurufu na nini zinaenda kule kwenye Halmashauri ndiyo njia za kuziwezesha Halmashauri zetu ziweze kutenda vizuri.

Sasa kama tutakuwa na roho ya namna hii sasa tutafanyaje, yaani Wizara yote imiliki kila kitu, hii D by D tunapeleka shughuli kule, sisi ni waratibu tu. Hata hii kusafiri ni watu kule wanakoenda kusimamia miradi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu umekuwa na manufaa makubwa. Wiki mbili zilizopita wale wahusika wenyewe wa fedha walienda na watu wangu kule kwenye maeneo ya mradi huu unakotekelezwa, wananchi wamefurahi, ni Wilaya kame, huu mradi unatekelezwa kwenye Wilaya kame, wamepata maji kwa ajili ya binadamu ambayo ni muhimu sana kwa afya zao, wamepata kwa ajili ya mifugo. Sasa namna hii nafikiri tuwe wakweli. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rose, hitimisha hoja yako!

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha hoja yangu naomba kumweleza Waziri kwamba sijui na mimi kwamba wewe ni mgeni kwenye hii Wizara, kwa hiyo uliowakuta ni wenyeji wako ambao huna namna ya kufanya kwa sababu mimi nadhani Bahi,

Kondoa, Kiteto, haina ndege za nje. Sasa kama hapa kwenye hela za mradi imepanga safari za nje kwa ajili ya mradi wa Bahi, Kondoa na Kiteto, mimi nikuachie wewe, naondoa shilingi yangu.

MWENYEKITI: Umerudisha shilingi?

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sawa na kumpigia mbuzi gitaa, wakati mimi nimeona kuna hela za kwenda nje ya nchi.

MWENYEKITI: Basi tunakushukuru, tunakushukuru.

(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko Yoyote)

Kif. 1004 – *Livestock Research and Training Inst…….....Tsh.11,364,262,000/=*

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko kwenye kifungu kidogo 4486 - *Agriculture Sector Development Programme*. Naelewa kwamba fungu hili linahusiana na masuala ya utafiti wa mifugo pamoja na vyuo vya mafunzo. Lakini ukiangalia fedha ambazo zimetengwa kwanza zote ni za nje hizo shilingi milioni 200, hakuna *commitment* kabisa ya *local money*. Kwa hiyo, naona ni tatizo kubwa sana hasa ukizingatia kwamba tuna tatizo kubwa sana la utafiti na kama ambavyo Wabunge wengi wamechangia, tuna magonjwa mengi ambayo yananyemelea mifugo. Kwa hiyo, naomba kujua ni kwanini Serikali haijatenga kabisa fedha za ndani, imetenga fedha za nje tu milioni 200 na wote tunajua kwamba mara nyingi fedha hizi za nje huwa zinachelewa sana na ndiyo sababu tunashindwa kufanya shughuli za maendeleo? Nilikuwa naomba ufafanuzi kutoka Serikalini.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli hili suala analolisema Mheshimiwa ni la msingi, lakini hapa japo hajaona fedha ya ndani, kuna fedha ambayo kupitia shughuli zile za kawaida hawa LITA wanapewa fedha, lakini vilevile LITA wamepewa *full retention,* kwa hiyo fedha yote wanayokusanya wanabaki nayo kwa matumizi yao. Kwa hiyo, huu mradi unaongezea tu uwezo wao na siyo kwamba Serikali imewapuuza. Lakini vilevile kwa mfano katika fedha hii bilioni 10.5 ambayo tumepewa na hazina leo, bilioni 1.2 ni maalum kwa ajili ya taasisi hizo. Kwa hiyo, uwe na amani Mheshimiwa.

(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko Yoyote)

Kif. 7001 – *Veterinary Services …….....……Tsh.4,380,319,000/=*

(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko Yoyote)

Kif. 8001 – *Animal Production……..Tsh.8,094,077,000/=*

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye kifungu kidogo cha 4495. Nilitaka kujua kama hizo fedha kuna ujenzi wa mnada alioutaja Mheshimiwa Waziri kwenye kitabu chake kwamba mnada wa Longido utajengwa. Sasa nilitaka kujua kama hizi fedha ziko hapo kwa sababu sikuona popote kwamba ameweka wapi hizo hela.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi kabisa alichosema Mheshimiwa.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiki kifungu kimeshaulizwa, lakini kwa ruksa yako naomba niendeleze hapo hapo katika *item* hiyo hiyo. Najua kwamba mashamba ya NARCO sasa hivi wanajiendeleza wenyewe. Mwaka jana wakati tunachangia katika Wizara hii tulitoa mapendekezo kwamba ni vyema sasa Serikali itenge fedha ili kuwasaidia hawa NARCO. Sasa nilitaka kujua kwamba katika fedha hizi milioni zilizopangwa hapa, je, kuna fedha zozote mmepanga kwa ajili ya kusaidia NARCO hasa tukizingatia kwamba sasa hivi NARCO wanadaiwa hata na mifuko zaidi ya milioni 600 ambazo hawajalipa na kila zinapokaa kila mwaka ile *interest* pamoja na riba inakuwa inaongezeka? Ili kuwasaidia hawa NARCO sijui Mheshimiwa hizi fedha ziko hapo?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, NARCO wametengewa fedha mwaka huu kwa ujumla wao tunategemea pesa kwa ajili ya kuongeza mifugo pamoja na ujenzi wa machinjio ya Ruvu. Mwaka huu wanapata bilioni moja kwa kuanzia. Kwa hiyo, tunazingatia sana ushauri wa Mheshimiwa Mbunge.

(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko Yoyote)
(Bunge Lilirudia)

MWENYEKITI: Tukae. Mtoa hoja!

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia makadirio ya matumizi ya fedha ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kifungu kwa kifungu na kuyaptisha bila mbadiliko. Hivyo, naomba sasa Bunge lako tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi kwa mwaka 2014/2015 Yalipitishwa na Bunge.

MWENYEKITI: Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri uliyoifanya na kwa kipindi kifupi tu umeonyesha weledi wako na majibu yako yalikuwa mazuri na unastahili kupongezwa wewe na Naibu Waziri wako pamoja na watendaji wenu wote.

Lakini vilevile tunapongeza na Wabunge kwa kutoa ushirikiano mzuri kwa meza na kumaliza shughuli hii leo. Naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 01.44 usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumamosi,
Tarehe 24 Mei, 2014 Saa Tatu Asubuhi)